# HUDUMA YA MTU ANAYEMPENDA MUNGU






**Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani**

RohoYaUnabii.org MaarifaMtandaoni.com

RohoYaUnabii.net

***Translated from Christian Service  Book 1925***



Warumi 10:15
Ni Mizuri
miguu yao
wahubirio
habari
Njema
Huduma
Uhamishoni
Ughaibuni
Mtandaoni
Majumbani
MaarifaMtandaoni.africa
RohoYaUnabii.org

***Kitabu hiki kimetafsiriwa  kwaajili ya kila mtu. Habari hizi ni muhimu sana hivyo wewe uko huru kunakili  na kusambaza kwa wengine kama kilivyo, toa typos tu! Usipoteze dhana! Kwa nakala ya kidijitali ya kitabu hiki, tafadhali tembelea RohoYaUnabii.org au RohoYaUnabii.net au MaarifaMtandaoni.Africa au kwa Kingereza  WhiteEstate.org. Kugushi Maandishi ya namna hii au kuyakaba koo yasinene, ni kujiletea taabu kubwa. Yeremia 36:27 na Ufunuo 22:18, 19 na Kumbukumbu la Torati 4:9***

Mwito kwa Mpendwa Msomaji

Jiunge na darasa la Uandishi, Ukalimani, Kutafsiri na  Uhariri WhatsApp, Kujifunza au Kufundisha! Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni Roho Mtakatifu , ushauri, na kisha Maombi yako msomaji maana wale watu wanaoishi nje ya Afrika wanahitaji pia kusoma kwa Lugha ya asili . Kumbuka pia huduma zingine za machapisho kwa kila lugha, taifa na jamaa. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la Mungu limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi 6000 hayajafikiwa, angalia Joshugaproject.org na habari za '1040 window' Sambaza Biblia popote ndiyo kauli mbiu ya muumini, Sambaza Neno la Mungu kote. Jiunge nasi katika kuandika vitabu vya kuboresha watu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ombi letu, ni unapochapa, usibadilishe chochote labda typos tu, tuwasiliane kama kuna kosa la dhana au lugha!  Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa rasilimali, mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Ila hapa Kwetu Afrika Mashariki,  sisi tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu kwenye  mada za afya, lishe, mahusiano kati ya wazazi au ndoa, kilimo na mazao yake,  kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga

makanisa, nyimbo zetu na noti zake, haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandano ya magharibi na ni mema tu, ila kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu, tunabidishwa pia kuwa waandishi kwasababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya na jamii kuliko mtu mwingine. Kwanini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa makini, nyimbo zilizoimbwa miaka 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu na kisha watu waimbe? Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila hata wao wanaendelea kuziongeza vitabu, nasi hapa tuna nyimbo nzuri na zinaendana na utamaduni wetu na mtindo wetu wa kuchukua mafungu na kuelezea kisa chote ni wa pekee yake, kwanini basi tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu vizuri vingine, vikiwemo nyimbo za watoto. Tuna wataalamu wengi wa nyimbo sasa, wanaopenda watoto kufanya kazi hii kwa kushirikiana. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission' Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata, Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Waumini wengi kuliko Amerika ya kusini, na tunajua lugha nyingi kubwa kama Kifaransa na Kingereza, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu na watoto wetu, na wanaona pengine wawe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au wawe na mwenendo kama ule. Mfano mdogo sana utakuwa, wasomomaji wanafikiri sisi ni lazima tule Pizza, Tambi, Kimchi, Taco, Panzit, Empanada, Manicotti, Tortellini, Sushi, au Falafel. Je viwanda vyetu vinatengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila jinsi ya kukitengeneza hupishana, Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk. Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika

maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! Naelewa kwamba si utamaduni wetu kuandika, ila si utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya! Nategemea tunaiga mazuri tu! Na si kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii, wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu, vingine vitakudodea. Kitabu cha Jando na Unyago kwa Waumini ni vizuri tupate watu wa kutusaidia kuandika, kwani jamii inaishi sehemu tofauti, na hii inanya kusiwe na Mafundisho au kujifunza kwa mambo fulani muhimu toka kwa Kabila la mtu kama ilivyokuwa, na wakati huo huo pengine serikali haiwezi kukidhi hitaji hili kwa urahisi. Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio taasisi. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao vya kuboresha jamii mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake. Tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwa mamilioni kwenye ujasiliamali nk. Ukiwa na chochote, hata ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani tafadhali usisite kutufikia na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, tuwasiliane, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa ***Maandishi*** yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku, tunaomba mashauri pia kwa kutumia email UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com au simu -1 -908-343-3022- Bwana atubariki sote ili tukae Ndani Yake

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo BWANA!

Asante kwa Wasomaji, Watafsiri, Wahariri, Washauri, Waombezi, Wanaufundi na wote ambao wanasaidia hii kazi ya Machapisho duniani kote. “Watu 1000 Wote Wataamini Siku moja kwa Ule ujumbe wa Kimya wa Machapisho”. Unabii huu unatimia, Maelfu ya watu duniani kote wanabatizwa kwa siku moja, kwa wazi au kwa faragha. Tafsiri zetu ni kama Wikipedia, ukitaka kuboresha bila kupoteza dhana, boresha tu, ila usipoteze kabisa ujumbe na dhana. Tumeweka Pointers (1T 81.1) na kadhalika ili ujihakikishie mwenyewe na kutafsiri kwa ubora zaidi unapopeda kufanya hivyo, Kiswahili kinazidi

kupanuka, Machapisho ya Wamishenari kama Nuru kwa Kanisa sasa tukiyaona tunashangaa, ila enzi hizo yalikuwa ndiyo yenyewe kabisa kwa uzuri! Na Kurasa zilikuwa 80 hivi tu! Badala ya 5000! Kwa vile Vitabu vya Shuhuda viko kama 12 hivi. Kugushi Maandishi yaliyovuviwa au kuyaziba mdomo yasinene, ni kujiletea taabu kubwa. Vitabu hivi vimekuwa msaada kwa wengi Congo, Msumbiji na hata Nje ya Afrika. Wengi wa nchi hizi wametuandikia kwa vile hawana viwanda vya uchapaji

Grace Momadi-Masaka—New Jersey, Marekani

Emmanuel Nhandi Masunga-Bariadi, Tanzania

Daniel Masaka—Kisii, Kenya

Sandra Barron—Kentucky, Marekani

Musa Budodi—Shinyanga, Tanzania

Niwaeli Mburuja—Suji, Tanzania

Sala Jackson—Kombeo na Umishenari TV

Cindy Tustch—Washington, Marekani

Mbusi Mpagalushu—Bariadi, Tanzania

Mohammed Mboi—Nairobi, Kenya

David Masaka—Pennsylvania, Marekani

Tabori Mugeta-Mara, Tanzania

Ezekiel Ojwang—Kiterere, Tanzania

Judi Mmari Mugane—Siha, Tanzania

John Mugane—Nakuru, Kenya

Faustine Momadi Mkama—Dar Es Salaam, Tanzania

Denis Chilala Momadi—Masasi, Tanzania

Paul Momadi Masaka, New Jersey, Marekani

Isack Msusu-Kigoma, Tanzania

Elias Luwela-Rukwa, Tanzania

Brayson Kuy Junior-Kahama, Tanzania

Gerard Makori Nyafanga—Shirati, Tanzania

—

## SURA YA 1 WITO WA MUNGU KWA HUDUMA

### Kutegemea Mawakala wa Kibinadamu

Kama wawakilishi Wake kati ya wanadamu, Mungu hawachagui malaika ambao hawajaanguka kamwe kufanya kazi ya injili, bali wanadamu, watu wenye tamaa, hulka, na shauku sawa na wale wanawaotafuta ili kuwaokoa. Kristo alichukua ubinadamu ili apate kuufikia ubinadamu. Mwokozi aliye Mungu na Mwanadamu, alihitajika kuleta wokovu kwa ulimwengu. Na wanaume na wanawake wamekabidhiwa dhamana takatifu ya kuwajulisha "utajiri wa Kristo usiochunguzika." — **The Acts of the Apostles, p. 134 . ChS 7.1**

Angalia mandhari hii, tukio lenye kugusa moyo. Tazama, Ukuu wa mbinguni umezungukwa na wale kumi na wawili aliowachagua. Anakaribia kuwatenga kwa kazi yao. Kwa mawakala hawa dhaifu, kupitia Neno na Roho Wake, Yeye hupanga/anadisaini kuweka wokovu ndani ya uwezo wa wote ili kila mtu aweze kuufikia.
**—The Acts of the Apostles, 18. ChS 7.2**

"Tuma watu Yafa ukamwite Simoni." Hivyo Mungu alitoa ushahidi wa kujali Kwake kwa huduma ya injili na kwa kanisa Lake lililopangwa. Malaika hakuagizwa kumwambia Kornelio kisa cha msalaba. Mwanadamu, kama akida mwenyewe, chini ya udhaifu na majaribu ya kibinadamu, ndiye aliyepaswa kumwambia Akida juu ya Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka. — **The Acts of the Apostles, p. 134 . ChS 7.3**

**Malaika aliyetumwa kwa Filipo angeweza kufanya kazi kwa ajili ya Mwethiopia mwenyewe, lakini hii si njia ya Mungu ya kufanya kazi. Ni mpango Wake kwamba Wanadamu wanapaswa kufanya kazi kwa ajili ya wanadamu wenzao, na huu ndiyo mpango Wake Mungu — The Acts of the Apostles, p. 109 . ChS 7.4**

"Tuna hazina hii," mtume huyo akaendelea, "katika vyombo vya

udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu.” Mungu angeweza kutangaza Ukweli Wake kupitia malaika wasio na dhambi, lakini huu si mkakati Wake. Yeye huchagua wanadamu, watu waliozingirwa na udhaifu, kama vyombo vya kufanya kazi ya mipango Yake. Hazina hiyo yenye thamani kubwa imewekwa katika vyombo vya udongo. Kupitia wanadamu baraka Zake zinapaswa kuwasilishwa kwa ulimwengu. Kupitia kwao utukufu Wake uangaze katika giza la dhambi. Katika huduma ya upendo wanapaswa kukutana na wenye dhambi na watu wenye mahitaji, na kuwaongoza hadi msalabani. Na katika kazi zao zote, wanapaswa kumpa utukufu, heshima, na sifa Kwake Yeye aliye juu ya yote na katika yote.— **The Acts of the Apostles, p. 330 .** **ChS 7.5**

Lilikuwa ni kusudi la Mwokozi kwamba baada ya Yeye kupaa mbinguni awe Mtetezi na Mwombezi wa mwanadamu., Wafuasi Wake wanapaswa kuendeleza kazi Aliyokuwa ameianzisha. Je, wakala wa kianadamu hataonyesha shauku maalum katika kutoa nuru ya ujumbe wa injili kwa wale wanaokaa gizani? Kuna wengine ambao wako tayari kwenda hadi miisho ya dunia ili kuibeba nuru ya Ukweli kwa wanadamu, lakini Mungu anadai kwamba kila nafsi inayoijua Kweli ifanye kuwatafuta wengine waipende ile Kweli. Ikiwa sisi hatuko tayari

kutoa kafara ya pekee, ili kuokoa roho zilizo tayari kuangamia, sisi tunawezaje kuhesabiwa kuwa tunastahili kuingia katika mji wa Mungu? **Ushuhuda kwa Kanisa 9:103 . ChS 8.1**

Katika hekima Yake Bwana, Yeye huwaleta wale wanaotafuta Ukweli kuwasiliana na wanadamu wenzao wanaojua Ukweli. Ni mpango wa Mbinguni kwamba wale ambao wamepokea nuru wataisambaza kwa wale walio gizani. Ubinadamu, unapochota ufanisi wake kutoka kwa Chanzo kikuu cha hekima, unafanywa kuwa chombo, na wakala wa kufanya kazi, ambamo injili hutumia nguvu zake za kubadilisha akili na moyo. **— The Acts of the Apostles, p. 134 . ChS 8.2**

Mungu angeweza kufikia lengo Lake katika kuokoa wenye dhambi bila msaada wetu wanadamu; lakini ili sisi tuwe na tabia kama ya Kristo, ni lazima tushiriki kazi Yake. Ili kuingia katika shangwe Yake,—furaha ya kuona roho zikikombolewa kwa dhabihu Yake, ni lazima sisi nasi tushiriki katika kazi Zake kwa ajili ya ukombozi wao. **— The Desire of Ages, p. 142 . ChS 8.3**

Kama wawakilishi wa Mungu kati ya wanadamu, Kristo hawachagui malaika ambao hawajaanguka kamwe, bali wanadamu tu, watu wenye hulka na shauku sawa na wale wanaowatafuta ili waokolewe. Kristo aliutwaa ubinadamu, ili apate kuwafikia wanadamu. Uungu ulihitaji ubinadamu; kwa maana ilihitajika vyote vilihitajika, yaani Uungu na ubinadamu kwa pamoja, ili kuleta wokovu kwa ulimwengu. Uungu ulihitaji ubinadamu, ili kwamba ubinadamu uweze kupata njia/chaneli ya mawasiliano kati ya Mungu na mwanadamu. **— The Desire of Ages, 296 . ChS 8.4**

Malaika hungoja ushirikiano wetu, kwa hamu inayoonekana kukaribia kukosa subira; kwa maana mwanadamu lazima awe mfereji wa kuwasiliana na mwanadamu mwenzake. Na sisi tunapojitoa wenyewe kwa Kristo kwa kuitoa mioyo yetu yote kwa

—

unyofu, malaika hufurahi kwamba wanaweza kusema kupitia sauti zetu ili kufunua upendo wa Mungu. — **The Desire of Ages, p . 297. ChS 9.1**

Inatupasa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu; kwa kuwa Mungu hataikamilisha kazi Yake bila mawakala wa kianadamu. — **The Review and Herald, Machi 1, 1887 . ChS 9.2**

**Wito Kwa Mtu Binafsi**

Kazi iliyo tofauti, na ya kipekee, imetolewa kwa kila Mkristo. — **The Southern Watchman, August 2, 1904. ChS 9.3**

Mungu anamtaka kila mtu awe mtendakazi katika shamba Lake la mizabibu. Kila mtu anapaswa kuichukua na kuianza kazi ambayo imewekwa chini ya usimamizi/uangalizi wake, ile ambayo umeagizwa na uifanye kwa uaminifu. —**The Bible Echo, June 10, 1901. ChS 9.4**

Kama kila mmoja wenu angekuwa mmishenari hai, ujumbe wa wakati huu ungetangazwa upesi katika nchi zote, kwa watu wa kila taifa na lugha na jamaa. —**Shuhuda kwa Kanisa 6:438. ChS 9.5**

Kila mfuasi na mwanafunzi wa kweli amezaliwa katika ufalme wa Mungu kama mmishenari. Yule anayekunywa maji ya uzima, huwa chemichemi ya uzima. Mpokeaji huwa mtoaji. Neema ya Kristo katika nafsi ni kama chemichemi jangwani, ikibubujika ili kuwaburudisha wote, na kuwafanya wale walio tayari kuangamia, wawe na matamanio ya kunywa maji ya uzima. —**The Desire of Ages, 195. ChS 9.6**

Mungu anatarajia huduma binafsi kutoka kwa kila mtu aliyempa ujuzi wa Kweli wa wakati huu. Si wote wanaoweza kwenda kama wamishenari katika nchi za kigeni, bali wote wanaweza kuwa wamishenari wa nyumbani katika familia zao na kwenye ujirani wao. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:30. ChS 9.7**

Kristo alikuwa amesimama hatua chache tu kutoka kwenye kiti cha enzi cha mbinguni alipotoa agizo Lake kwa wanafunzi Wake. Ikiwa ni pamoja na wamishenari wote wanaopaswa kuamini Jina Lake, Naye akasema “Enendeni ulimwenguni kote, na kuihubiri injili kwa kila kiumbe” Nguvu na uwezo wa Mungu ingekuwa pamoja nao. —**The Southern** Watchman, September 20, 1904. **ChS 9.8**

Kuokoa roho inapaswa kuwa kazi ya maisha ya kila mwanadamu anayemwamini na kumkiri Kristo. Sisi ni wadeni katika ulimwengu kwa neema tuliyopewa na Mungu, kwa nuru ambayo inatuangazia, na kwasababu ya ufahamu wa uzuri na nguvu ya Ukweli tuliyoigundua. —**Shuhuda kwa Kanisa 4:53. ChS 10.1**

—

Kila mahali kuna mazoea ya mtu kufanya juhudi ya kuiachia taasisi kufanya kazi ambayo yeye binafsi alipaswa kuifanya. Hekima ya kibinadamu ndiyo huongoza kwenye uimarishaji, utegemeaji, na ujumuishaji wa ujenzi wa makanisa na taasisi kubwa. Wengi huziachia taasisi na mashirika, kazi ya ukarimu na kujitoa wenyewe; wanatoa visingizio ili wasichangamane na ulimwengu, na kisha mioyo yao inaendelea kukua katika hali ya ubaridi (inapoa). Wanakuwa watu wanaojifikiria wenyewe tu na wasiotaka kuguswa mioyo yao. Upendo wa Mungu na mwanadamu hufa taratibu nafsini mwao. Kristo amewaagiza kazi wafuasi Wake, kila mtu amepewa kazi binafsi (iliyo ya pekee kwao kuifanya),- kazi ambayo haiwezi kufanywa na mwakilishi, wakala au mtu mwingine kwa niaba yao. Huduma kwa wagonjwa na maskini, ufikishaji wa injili kwa watu waliopotea, hakupaswi kuachwa mikononi mwa wajumbe, kamati au mashirika na vyama maalumu vinavyojitolea kutoa misaada. Wajibu na majukumu ya mtu mmoja mmoja, juhudi za mtu binafsi, kujitoa kafara kwa mtu mmoja mmoja, ni takwa/hitaji la injili. —**The Ministry of Healing, uk. 147. ChS 10.2**

–

Kila mmoja ambaye amepokea nuru ya mbinguni anapaswa kuangazia njia ya wale wasiojua Nuru ya uzima. —**The Desire of Ages, 152. ChS 10.3**

Kila mmoja amepewa kazi, na hakuna hata mtu mmoja ambaye anaweza kuwa mbadala katika kazi ya mwingine. Kila mmoja ana utume muhimu na tena wa ajabu, ambao hawezi kuupuuza, kuudharau au kuuacha, kwani kwa kufanya utume huo kwa ukamilifu wake, inahusisha ustawi (mafanikio) wa nafsi fulani, na kuipuuzia ni ole kutoka kwa Kristo ambaye alikufa kwa ajili yake. **—The Review and Herald, December 12, 1893. ChS 10.4**

Sote tunapaswa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Hakuna wazembe wanaokubaliwa au kutambuliwa kama watumishi Wake. Washiriki wa kanisa, kila mmoja anapaswa kuhisi kwamba maisha na ustawi (mafanikio) wa kanisa hutegemea (huathiriwa) na utendaji (mwenendo) wao binafsi. **—The Review and Herald, February 15, 1887. ChS 10.5**

Kila nafsi ambayo imeokolewa na Kristo, inaitwa ije kufanya kazi kwa Jina Lake kwa ajili ya kuokoa watu waliopotea. Kazi hii ilidharauliwa katika Israeli. Je, haijapuuzwa na kudharauliwa hata leo na wale wanaojidai kuwa ni wafuasi wa Kristo? **—**
**Christ's Object Lessons, 191. ChS 10.6**

Wote wanaweza kupata kitu cha kufanya. Kila roho ambayo inaamini Ukweli itasimama katika zamu yake na mahali pake, na kusema: Mimi hapa, nitume mimi. **Isaya 6:8. — Ushuhuda kwa Kanisa 6:49. ChS 10.7**

Ni fursa na wajibu wa kila Mkristo, si tu kuingojea kwa hamu siku ya kuja kwa Bwana, bali pia kuharakisha ujio wa Bwana wetu Yesu Kristo. **—Christ's Object Lessons, 69. ChS 11.1**

Kila ambaye amekuwa mtoto wa Mungu anapaswa kujiona mwenyewe kama kiungo/kiunganishi cha mnyororo ulioshushwa chini ili kuokoa ulimwengu, sasa amekuwa mmoja na Kristo

—

katika mpango Wake wa rehema, akienda pamoja Naye kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. **—The Ministry of Healing, 105. CHs 11.2**

Wote wanaweza kupata kitu cha kufanya. Asiwepo hata mmoja mwenye kuhisi kwamba hakuna mahali ambapo anapaswa kufanya kazi kwa ajili ya Kristo. Mwokozi anajitambulisha Mwenyewe kwa kila mtoto wa mwanadamu. **—The Ministry of Healing, p. 104. CHs 11.3**

Wale ambao wameungana na Bwana katika agano la utumishi, wako chini ya vifungo vya kuungana Naye katika kazi kubwa na kuu sana ya kuokoa roho. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:19. CHs 11.4**

Hivyo shamba hili la Bwana ni kubwa sana, na mpango ni wa kina sana, kwamba kila moyo uliotakaswa utaingizwa kwenye utumishi kama chombo cha nguvu cha Bwana. **— Ushuhuda kwa Kanisa 9:47. CHs 11.5**

Watu ni vyombo katika mkono wa Mungu, ambavyo Yeye huvitumia kutimiza makusudi Yake ya neema na rehema. Kila mtu ana sehemu ya kufanya; kila mtu anapewa kiasi fulani cha nuru kinachokidhi mahitaji ya wakati wake, na kinachotosha

Kumwezesha atekeleze kazi ambayo Mungu amempa aifanye. **—The Great Controversy, p. 343. CHs 11.6**

Mungu amesubiri kwa muda mrefu kwa roho ya utumishi kulimiliki kanisa zima, ili kila mtu awe anafanya kazi kwa ajili Yake kulingana na uwezo wake. **—The Acts of the Apostles, p. 111. CHs 11.7**

Alipowatuma wale kumi na wawili na baadaye sabini, kutangaza ufalme wa Mungu, alikuwa akiwafundisha wajibu wao wa kuwapa wengine yale aliyowajulisha. Katika kazi Yake yote, alikuwa akiwafunza kufanya kazi binafsi, ya pekee, kuongezeka kadiri idadi yao ilivyoongezeka, na hatiamye kufikia sehemu za mwisho za dunia. **—The Acts of the Apostles, p. 32. CHs 11.8**

Sio tu watumishi waliowekewa mikono, kwamba ndiyo wana majukumu la kwenda kutimiza agizo kuu la utume wa 'Enendeni'. Kila mtu ambaye amempokea Kristo ameitwa kufanya kazi kwa ajili ya kuwaokoa wanadamu wenzake. **—The Acts of the Apostles, p. 110. CHs 11.9**

Tabia halisi ya kanisa inapimwa, sio kwa taaluma yake ya mdomo au linavyojiita tu, sio kwa majina yaliyoandikishwa kwenye kitabu cha kanisa, bali kwa kile linachokinfaya kwaajili ya Bwana, kwa idadi ya watendakazi wake waaminifu waliojitoa kwa uaminifu. Matakwa ya mtu binafsi na bidii ya kukesha, juhudi binafsi za za mtu, ndiyo zitafanikisha zaidi kazi yaKristo kuliko inavyoweza kufanywa kwa njia ya mahubiri au kanuni za imani. **—The Review and Herald, September 6, 1881. CHs 12.1**

Popote kanisa linapoanzishwa, washiriki wote wanapaswa kushiriki kikamilifu katika kazi ya umishenari. Wanapaswa kutembelea kila familia kwenye ujirani wao na kujua hali yao ya kiroho. **—Ushuhuda kwa Kanisa 6:296. CHs 12.2**

—

Washiriki wa kanisa sio wote wameitwa kufanya kazi katika nchi za kigeni, lakini wote wana sehemu ya kutenda katika kazi kuu ya kutoa nuru kwa ulimwengu. Injili ya Kristo ni ya kwenda upesi na yenye kutawanyika. Katika siku Yake Mungu hakuna hata mmoja atakayeachiliwa kwa kuwa amefungwa na maslahi yake binafsi. Kuna kazi kwa kila akili na kwa kila mkono. Kuna aina mbalimbali ya kazi, iliyoasiliwa kwa akili tofauti na uwezo mbalimbali. **— Historical Sketches, p. 290, 291.**CHs 12.3

Amekukabidhi Ukweli mtakatifu; Kristo anayekaa ndani ya washiriki binafsi wa kanisa ni chemichemi ya maji inayobubujikia uzima wa milele. Una hatia mbele za Mungu kama hutafanya kila juhudi iwezekanayo kusambaza maji haya ya uzima kwa wengine. **— Historical Sketches, p. 291.** CHs 12.4

Kama Wakristo, hatujafanya hata moja ya ishirini ya sehemu ambayo tunapaswa kuifanya katika kuongoa roho kwa ajili ya Kristo. Kuna ulimwengu unaopaswa kuonywa, na kila Mkristo mwaminifu atakuwa ni kielelezo na mfano kwa wengine katika

uaminifu, kubeba msalaba, katika kutenda kwa wepesi na kwa nguvu, katika uaminifu usioyumba kwa ajili ya Ukweli, na kuwa dhabihu na kufanya kazi ili kuendeleza kusudi la Mungu. **—The Review and Herald, August 23, 1881. CH 12.5**

Kadri fursa zinavyoendelea kuwepo, kila mtu ambaye amepokea nuru ya Ukweli, yuko chini ya wajibu huo huo kama ilivyokuwa kwa nabii wa Israeli ambaye Neno lilimjia: "Mwanadamu, nimekuweka kuwa mlinzi kwa nyumba ya Israeli; basi ulisikie Neno hili kinywani Mwangu, na uwape maonyo Yangu. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:19, 20. CHs 12.6**

Kwa kila mtu ambaye anakuwa mshiriki wa neema Yake, Bwana huteua (huweka) kazi kwa ajili ya wengine. Kila mmoja wetu binafsi anapaswa kusimama katika zamu na mahali pake, akisema, “Mimi hapa, nitume mimi”. Kwa mhudumu wa Neno, muuguzi mmisionari, tabibu Mkristo, Mkristo binafsi, awe mfanyabiashara au mkulima, mtaalamu au fundi, -jukumu liko juu ya wote. Ni kazi yetu kuwafunulia wanadamu injili ya wokovu wao. Kila biashara ambayo tunashughulika nayo inapaswa kuwa njia ya kufikia lengo hili. **—The Ministry of Healing, p. 148. CHs 13.1**

Bwana mwenye nyumba alipowaita watumishi wake, alimpa kila mtu kazi yake. Familia nzima ya Mungu imejumuishwa katika jukumu la kutumia mali za Bwana wao. Kila mtu, kutoka kwa yule wa chini kabisa na yule asiyejulikana kabisa hadi aliye mkuu na aliyeinuliwa zaidi, ni wakala mwenye kukubalika aliyejaliwa uwezo ambao anawajibika kwa Mungu.
**—The Bible Echo, June 10,**

**1901. CHs 13.2**

—

**Vikosi vya Kikristo Vilizounganishwa**

Ndugu na dada katika imani, je, swali linatokea mioyoni mwenu, “Mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?” Ikiwa unadai kuwa ni mtoto wa Mungu, wewe ni mlinzi wa ndugu yako. Bwana hulitazama kanisa linaloajibika kwa ajili ya roho za wale ambao wanaweza kuwa njia ya kuokoa. **Historical Sketches, 291 . ChS 13.3**

Mwokozi ametoa maisha Yake ya thamani ili kuanzisha kanisa lenye uwezo wa kuhudumia wale wanaoteseka, wenye huzuni, na wale wanaojaribiwa. Kundi la waumini laweza kuwa maskini, wasio na kisomo cha darasani, na wasiojulikana; walakini katika Kristo wanaweza kufanya kazi nyumbani, katika jamii, na hata katika “nchi za ng’ambo,” ambapo matokeo yake yatakuwa makubwa sana, hata milele.— **The Ministry of Healing, p. 106 . ChS 13.4**

Kanisa linaweza kuonekana kuwa dhaifu, lililoharibika na lenye dosari kadiri linavyoweza kuonekana, lakini bado ndicho chombo ambacho Mungu anakijali kwa namna ya pekee na kukipa heshima Yake kuu. Ni jumba la maonyesho la neema Yake, ambamo Yeye anafurahia kufunua nguvu na uweza Wake ili kutengeneza/kubadilisha mioyo.— **Matendo ya Mitume, 12 . ChS 13.5**

Mtu mmoja lazima atimize utume wa Kristo; lazima mtu aendeleze kazi ambayo Alianza kuifanya duniani; na kanisa limepewa fursa hii. Kwa kusudi hili limeandaliwa/limesimikwa. Kwa nini, basi, washiriki wa kanisa hawajakubali wajibu huo? **Shuhuda kwa Kanisa 6:295 . ChS 14.1**

Anatoa wito kwa kanisa kuchukua jukumu lao lililowekwa, likishikilia kiwango cha matengenezo ya kweli katika eneo lao wenyewe, likiwaacha watenda kazi waliofunzwa na wazoefu kusukuma mbele katika maeneno mapya.— **Shuhuda kwa Kanisa 6:292 . ChS 14.2**

Waumini wa Thesalonike walikuwa wamisionari wa kweli.... Mioyo ilivutwa kwa kweli zilizotolewa, na roho ziliongezwa kwa idadi ya waumini.— **The Acts of the Apostle, 256 . ChS 14.3**

Ilikuwa ni wakati wa kuwekwa wakfu kwa wale kumi na wawili ambapo hatua ya kwanza ilichukuliwa katika kuundwa kwa kanisa kwamba baada ya kuondoka kwa Kristo watu hawa na kanisa waendeleze kazi Yake duniani. — **The Acts of The Apostles, 18 . ChS 14.4**

Kanisa la Mungu ni uwanja wa maisha matakatifu, uliojaa karama mbalimbali, nalo limejaliwa kupewa Roho Mtakatifu. Washiriki wake wanapaswa kupata furaha yao katika furaha ya wale wanaowasaidia na kuwabariki. Bwana anakusudia kufanya kazi ya ajabu na kuikamilisha kupitia kanisa Lake, ili Jina Lake litukuzwe.— **The Acts of the Apostles, 12, 13 . ChS 14.5**

Kazi yetu imewekwa wazi kwa kinagaubaga katika Neno la Mungu. Mkristo anapaswa kuunganishwa na Mkristo, kanisa kwa kanisa, chombo cha kibinadamu kinachoshirikiana na Mungu (mwanadamu), kila chombo kikiongozwa chini ya usimamizi na Roho Mtakatifu, na wote waweze kuunganishwa ili kuupatia ulimwengu habari njema za neema ya Mungu. **—The General Conference Daily Bulletin, February 28, 1893, p. 421.**

Makanisa yetu yanapaswa kushirikiana katika kazi ya kiroho ya kulima, kwa matumaini ya kuvuna siku ile ya mwisho Bwana atakaporudi …… Udongo ambao haujawahi kukatuliwa muda mrefu una ukaidi, ila lazima uvunjwe-vunjwe, mbegu za haki lazima zipandwe. Hebu msitulie wala msisitesite, enyi walimu mnaopendwa na Mungu, kana kwamba mna shaka jinsi kazi itakavyofanywa, itakavyokua, inapoendelezwa. —**Shuhuda za Kanisa 6:420 . ChS 14.7**

—

Kanisa ni wakala aliyeteuliwa na Mungu kwa ajili ya wokovu wa wanadamu. Lilipangwa kwa ajili ya huduma, na dhamira yake ni kupeleka injili ulimwenguni. Tangu mwanzo umekuwa ni mpango wa Mungu kwamba kupitia kanisa Lake utimilifu Wake na utoshelevu Wake utaakisiwa kwa ulimwengu. Washiriki wa kanisa, wale ambao Yeye amewaita kutoka gizani kuingia katika nuru Yake ya ajabu, wanapaswa kudhihirisha utukufu Wake.— **The Acts of the Apostles, 9 . ChS 15.1**

Hebu kanisa lolote lisifikirie kuwa ni dogo sana kuwa na ushawishi na kufanya huduma katika kazi kuu kwa wakati huu. **ChS 15.2**

Nendeni kazini, ndugu. Sio tu mikutano mikubwa ya makambi au makusanyiko na mabaraza pekee ambayo yatakuwa na upendeleo wa pekee wa Mungu; juhudi ya unyenyekevu zaidi ya upendo usio na ubinafsi itavikwa taji ya baraka Zake, na kupokea thawabu Yake kuu. Fanya uwezavyo, na Mungu ataongeza uwezo wako.— **The Review and Herald, Machi 13, 1888 . ChS 15.3**

**Mashahidi**

Sisi ni mashahidi wa Kristo, na hatupaswi kuruhusu masilahi na mipango ya ulimwengu kumeza muda wetu na usikivu wetu. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:53, 54 . ChS 15.4**

Ninyi ni mashahidi Wangu, asema BWANA, na mtumishi niliyemchagua; mpate kujua, na kuniamini, na kufahamu ya kuwa Mimi Ndiye; kabla Yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu Mimi hatakuwapo mwingine **Isaiah 43:10** Mimi, BWANA, nimekuita katika haki, Nami nitakushika mkono, na kukulinda, na kukutoa uwe agano la watu, na nuru ya mataifa; Kuyafunua macho ya vipofu, kuwatoa gerezani waliofungwa, kuwatoa wale walioketi gizani katika nyumba ya kufungwa. **Isaiah 42:6-7 —The Acts of the Apostles, 10 . ChS 15.5**

Watu wa ulimwengu wanaabudu miungu ya uwongo. Wanapaswa kugeuzwa kutoka kwa ibada yao ya uwongo, si kwa kusikia hukumu au kashifa ya sanamu zao, bali kwa kukitazama kitu bora zaidi. Wema wa Mungu unapaswa kujulikana. “Ninyi ni mashahidi Wangu, asema Bwana, kwamba Mimi ni Mungu.”— **Christ's Object Lessons, 299 . ChS 15.6**

Wote ambao wataingia katika mji wa Mungu lazima wakati wa maisha yao duniani wamwonyeshe na kumweka mbele Kristo katika mwenendo na shuguli zao. Hii ndio huwafanya kuwa wajumbe wa Kristo, mashahidi Wake. Wanapaswa kutoa

ushuhuda ulio wazi, ulioamuliwa dhidi ya mazoea yote maovu, wakiwaelekeza wenye dhambi kwa Mwana- Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu. —**Shuhuda za Kanisa 9:23 . ChS 15.7**

Wanafunzi walipaswa kusonga mbele kama mashahidi wa Kristo, kutangaza kwa ulimwengu kile walichokiona na kusikia Kwake. Ofisi yao ilikuwa ya muhimu sana ambayo wanadamu wamewahi kuitwa kwayo, ya pili baada ya ile ya Kristo Mwenyewe. Walipaswa kuwa watendakazi pamoja na Mungu kwa ajili ya kuwaokoa wanadamu.— **The Acts of the Aposles, 19 . ChS 16.1**

—

Mwalimu wa Kiungu/mbingu anasema: "Roho Yangu peke Yake Ndiye ana uwezo wa kufundisha na kuwasadikisha wanadamu dhambi. Watu wengine hutuoa ushawishi wa muda mfupi tu katika roho. Nitaingiza Ukweli katika dhamiri, na watu watakuwa mashahidi Wangu, ulimwenguni kote wakihimiza madai Yangu katika muda wa mwanadamu, pesa zake na akili yake. —**Shuhuda kwa Kanisa 7:159 . ChS 16.2**

Kukiri kwetu kwa uaminifu Wake ni wakala mteule wa Mbinguni kwa ajili ya kumdhihirisha Kristo kwa ulimwengu. Yatupasa kukiri neema Yake kama ilivyodhihirishwa kupitia watakatifu wa kale; lakini kile ambacho kitakuwa na matokeo zaidi ni ushuhuda wa uzoefu wetu wenyewe. Sisi ni mashahidi wa Mungu tunapofunua ndani yetu utendaji wa nguvu ambayo ni ya Bwana. Kila mtu ana maisha tofauti na wengine wote, na uzoefu unaotofautiana kimsingi na wengine. Mungu anatamani kwamba sifa zetu zipae Kwake, zikiwekwa alama na upekee wetu. Makubaliano haya ya thamani kwa sifa ya utukufu wa neema Yake, yanapoungwa mkono na maisha kama ya Kristo, yana nguvu isiyozuilika, inayofanya kazi kwa ajili ya wokovu wa nafsi.— **The Desire of Ages, 347 . ChS 16.3**

Mwenyezi Mungu hawezi kuonyesha ujuzi wa mapenzi Yake na maajabu ya neema Yake miongoni mwa walimwengu wasioamini isipokuwa awe na mashahidi waliotawanyika duniani kote. Ni mpango Wake kwamba wale wanaoshiriki wokovu huu mkuu kupitia Yesu Kristo wawe wamishenari Wake, vyombo vya nuru ulimwenguni kote, wawe kama ishara kwa watu, nyaraka zilizo hai, zinazojulikana na ~~ku~~somwa na watu wote, imani na matendo yao. wakishuhudia kukaribia kwa Mwokozi ajaye na kuonyesha kwamba hawajapokea neema ya Mungu bure. Ni lazima watu waonywe ili kujitayarisha kwa ajili ya hukumu inayokuja.— **Shuhuda kwa Kanisa 2:631, 632 . ChS 16.4**

[Wanafunzi] walipotafakari juu ya maisha Yake safi, na matakatifu, walihisi kwamba hakuna kazi ingekuwa ngumu sana, hakuna

—

dhabihu kubwa sana, ikiwa tu wangeweza kushuhudia katika maisha yao uzuri wa tabia ya Kristo. Lo, kama tu wangaliweza kuishi tena kwa kwenda nyuma miaka mitatu iliyopita, walifikiri, jinsi ambavyo wangalitenda kwa njia tofauti! Laiti wangemwona Bwana tena, jinsi ambavyo wangejitahidi kwa dhati na bidii kumwonyesha jinsi walivyompenda kwa dhati, na jinsi walivyohuzunika kwa dhati kwa kuwahi kumhuzunisha kwa neno au tendo la kutokuamini, walipoishi Naye! Lakini walifarijiwa na wazo kwamba walikuwa wamesamehewa. Na waliamua kwamba, kadiri inavyowezekana, wangefidia kutokuamini kwao kwa kumkiri kwa ujasiri mbele ya ulimwengu.— **The Acts of the Apostles, 36 . ChS 17.1**

Wale watu wawili waliokuwa na pepo na kuponywa, walikuwa wamishenari wa kwanza ambao Kristo aliwatuma wahubiri injili katika eneo la Dekapoli. Kwa muda mfupi tu, wanaume hawa walikuwa na fursa ya kusikia mafundisho ya Kristo. Hakuna hata hotuba moja kutoka kwa midomo Yake iliyowahi kuanguka kwenye masikio yao. Hawakuweza kuwafundisha watu kama vile wanafunzi waliokuwa na Kristo kila siku walivyoweza

—

kufanya. Lakini wao wenyewe walikuwa na uthibitisho wa kwamba Yesu Ndiye Masihi. Wangeweza tu kusema kile wanachojua; ambacho wao wenyewe walikuwa wamekiona na kusikia na kuhisi juu ya uwezo wa Kristo. Hivi ndivyo kila mtu anaweza kufanya ambaye moyo wake umeguswa na neema ya Mungu. Yohana, mwanafunzi mpendwa, aliandika hivi: "Lile lililokuwako tangu mwanzo, ambalo tumelisikia, ambalo tumeliona kwa macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalishika, la Neno la uzima; ... hayo tuliyoyaona na kuyasikia tunayahubiri kwenu." Kama mashahidi wa Kristo, tunapaswa kusema kile tunachojua, kile ambacho sisi wenyewe tumeona na kusikia na kuhisi. Ikiwa tumekuwa tukimfuata Yesu hatua kwa hatua, tutakuwa na kitu kwenye pointi sahihi, ili kufikia hatua ya kusema kuhusu njia ambayo ametuongoza. Tunaweza kueleza jinsi ambavyo tumezionja na kuzijaribu ahadi zake na kujionea wenyewe jinsi ahadi hizo zilivyo za Kweli. Tunaweza kushuhudia yale tuliyoyajua kuhusu neema ya Kristo. Huu ndio ushuhuda ambao Bwana wetu anatuita tuutoe, na ulimwengu unapoukosa huu ushuhuda, matokeo yake ni watu kuangamia.— **The Desire of Ages, p. 340 . ChS 17.2**

### Mifereji ya Nuru na Baraka

Tunapaswa kuwa mikondo iliyowekwa wakfu, ambayo maisha ya mbinguni hutiririka kwenda kwa wengine. Roho Mtakatifu anapaswa kuhuisha na kujaza kanisa lote, akitakasa na kuimarisha mioyo. **Shuhuda Kwa Kanisa 9:20 . ChS 18.1**

Kila mfuasi wa Yesu ana kazi ya kufanya kama mmishenari wa Kristo katika familia, kwa majirani anapoishi, na katika mji au jiji analoishi. Wote ambao wamewekwa wakfu kwa Mungu ni chaneli za nuru. Mungu huwafanya kuwa vyombo vya haki kuwasilisha kwa wengine nuru ya Ukweli.— **Shuhuda kwa Kanisa 2:632 . ChS 18.2.**

Matokeo ya kazi ya Yesu, alipokuwa ameketi, akiwa amechoka

—

na akisikia njaa kisimani, yalizidi kuwa baraka iliyosambaa. Nafsi moja ambayo alitafuta kuisaidia ikawa njia ya kuwafikia wengine na kuwaleta kwa Mwokozi. Hii ndiyo njia endelevu, ambayo kazi ya Mungu imeweza kupiga hatua ya maendeleo duniani. Hebu taa/nuru yako iangaze, na taa (mishumaa) zingine zitawashwa.— **Gospel Workers, p. 195 . ChS 18.3**

Wengi wana wazo kwamba wanawajibika kwa Kristo pekee kwa nuru na uzoefu wao, bila kujihusisha na wafuasi Wake Mungu, wanaotambulika duniani. Yesu ni rafiki wa wenye dhambi; na moyo Wake umeguswa na kilio chao. Yeye Ana uwezo wote, mbinguni na duniani; Lakini anaheshimu njia ambazo Yeyeameziweka kwa ajili ya kutoa elimu/maarifa na wokovu wa wanadamu; Anawaelekeza wenye dhambi kwenye kanisa, ambalo amelifanya kuwa mfereji wa nuru kwa ulimwengu. **— The Acts of The Apostles, 122. ChS 18.4**

Kanisa la kwanza lilikuwa limekabidhiwa kazi iliyoongezeka kila mara,—ile ya kuanzisha vituo vya nuru na baraka popote palipokuwa na watu (nafsi/roho) waaminifu waliokuwa tayari kujitolea kwa huduma ya Kristo.**—The Acts of the Apostles, 90. ChS 18.5**

Kama miale ya jua inavyopenya hadi kwenye pembe za mbali zaidi za dunia, ndivyo Mungu anavyopanga kwamba nuru ya injili itaenea kwa kila nafsi juu ya dunia. Ikiwa Kanisa la Kristo lingetimiza kusudi la Bwana wetu, nuru ingeangazwa juu ya wote waliokaa gizani na katika eneo lililo katika uvuli wa mauti. **—Thoughts from the Mount of Blessing, 42. ChS 18.6**

Ni fursa ya kila mwanadamu kuwa mfereji hai ambao kwa huo Mungu anaweza kuwasiliana na ulimwengu hazina za neema Yake, utajiri usiochunguzika wa Kristo. Hakuna kitu ambacho Kristo anatamani sana, kama mawakala ambao watawakilisha kwa ulimwengu Roho na tabia Yake. Hakuna kitu ambacho ulimwengu unahitaji sana kama udhihirisho kupitia ubinadamu wa upendo wa Mwokozi. Mbingu yote inangojea njia ambazo kupitia hizo mafuta matakatifu yanaweza kumwagwa na kuwa furaha na baraka kwa mioyo ya wanadamu. **— Christ's Object Lessons, 419**. **ChS 19.1**

Utukufu wa Kanisa la Mungu umo katika uchamungu wa washiriki Wake; kwa maana hapo kuna kufichwa kwa nguvu za Kristo. Ushawishi wa watoto wa Kweli wa Mungu unaweza kutambuliwa kama wa thamani ndogo, lakini utahisiwa kwa wakati wote, na kufunuliwa kwa usahihi katika siku ya kupewa tunu/malipo. Nuru ya Mkristo wa kweli, inayong'aa kwa uchamungu thabiti, kwa imani isiyoyumba, itauthibitishia ulimwengu nguvu ya Mwokozi aliye hai. Kupitia wafuasi Wake Kristo atafunuliwa kama chemichemi ya maji, inayobubujika uzima wa milele. Ingawa hawajulikani sana ulimwenguni, wanakubalika kuwa watu wa pekee wa Mungu, vyombo Vyake vilivyochaguliwa vya wokovu, mifereji Yake ambayo inapitisha nuru kuufikia ulimwengu —The Review and Herald, March 24, 1891.**ChS 19.2**

Washiriki wa kanisa, hebu na muiangaze nje nuru yenu. Hebu

—

sauti zenu zisikike katika maombi ya unyenyekevu, katika ushuhuda dhidi ya kutokuwa na kiasi, upumbavu, na anasa za dunia hii, na katika kuitangaza Kweli ya leo. Sauti yako, mvuto wako, wakati wako, vyote hivi ni karama kutoka kwa Mungu na vinapaswa kutumika kuleta roho kwa Kristo. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:38.ChS 19.3**

Nimeonyeshwa kuwa wanafunzi wa Kristo ni wawakilishi Wake duniani; na Mungu amekusudia kuwa watakuwa taa katika giza la kimaadili ya ulimwengu huu, lililotawanyika kote nchini, mijini, vijiji, na miji mikuu, "Tamasha kwa ulimwengu, na kwa malaika, na kwa wanadamu." ”**—Shuhuda kwa Kanisa 2:631. ChS 19.4**

Wafuasi wa Kristo wanapaswa kuwa nuru ya ulimwengu; Lakini Mungu hawaagizi kwamba wajikaze kufanya jitihada ili waweze kuangaza. Yeye Hakubaliani na jitihada zozote za kujiridhisha wenyewe katika kufanya maonyesho (kujionyesha) ya wema wa hali ya juu. Anatamani kwamba nafsi zao zijazwe na kanuni za mbinguni; na ndipo, wanapokutana

na ulimwengu, wataiangaza nuru iliyo ndani yao. Uaminifu wao ulio thabiti katika kila tendo la maisha utakuwa njia ya kuangaza. **—The Ministry of Healing, 36.ChS 19.5**

Wakati, katikati ya upotovu wake wa upofu na ubaguzi, Sauli alipewa ufunuo wa Kristo ambaye alikuwa akimtesa, aliwekwa katika mawasiliano ya moja kwa moja na Kanisa, ambalo ni nuru ya ulimwengu. Katika hali hii, Anania anamwakilisha Kristo, na pia anawawakilisha wahudumu/watumishi wa Kristo duniani, ambao wameteuliwa kutenda kwa niaba (mbadala) Yake. Kwa niaba ya Kristo, Anania anagusa macho ya Sauli, ili yapate kuona. Kwa niaba ya Kristo, anaweka mikono yake juu yake, na anapoomba katika Jina la Kristo, Sauli anapokea Roho Mtakatifu. Yote yanafanywa kwa Jina na kwa Mamlaka ya Kristo. Kristo Ndiye Msingi wa chemchemi; Kanisa ni mfereji/chombo/njia ya mawasiliano. **—The Acts of the Apostles, 122.ChS 20.1**

Makosa yanatawala kila mahali. Adui mkuu wa roho anakusanya nguvu zake. Anaweka kila mbinu inayofanya kazi ili kuchanganya akili za watu kwa makosa yanayoonekana ni sahihi kumbe ni uongo, na hivyo kuiangamiza roho. Wale ambao Mungu amekabidhi hazina za Kweli Yake wanapaswa kuacha nuru iangaze katikati ya giza la kimadili.— **Historical Sketches, 290.ChS 20.2**

Mungu anataka watu Wake waangaze kama nuru katika ulimwengu. Sio wahubiri tu wanaohitajika kufanya hivi, lakini kila mwanafunzi wa Kristo. Mazungumzo yao yanapaswa kuwa ya kimbingu. Na wanapofurahia ushirika na Mungu watatamani kuwa na ushirikiano na wanadamu wenzao ili kuonesha kwa maneno yao na vitendo upendo wa Mungu ambao huhuisha mioyo yao. Kwa njia hii watakuwa nuru katika ulimwengu, na nuru inayopitishwa kutoka kwao ili kuwaangazia wanadamu wengine, haitazimika au kuondolewa. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:122,**

**123. ChS 20.2**

Wafuasi wa Kristo wanapaswa kuwa vyombo vya haki, watendakazi, mawe yaliyo hai, wakitoa nuru, ili kwamba waweze kuhimiza uwepo wa malaika wa mbinguni. Kwa jinsi hii watakuwa nuru kwa ulimwengu kuwa mifereji, kama ilivyokuwa, ambayo kupitia hiyo roho ya Kweli na haki itatiririka. **— Shuhuda kwa Kanisa 2:126, 127.ChS 20.3**

Bwana amefanya kanisa Lake kuwa hazina ya ushawishi wa kimungu. Ulimwengu wa mbinguni unangoja washiriki wawe njia ambazo mkondo wa maisha utatiririka kwa ulimwengu, ili wengi waongoke, na kwa upande wao kuwa njia ambazo neema ya Kristo itatiririka hadi sehemu za jangwa za shamba la mizabibu la Bwana. **—The Bible Echo, August 12, 1901. ChS 21.1**

Kila mtu aliyeunganishwa na Mungu atatoa nuru kwa wengine. Ikiwa kuna wale ambao hawana nuru ya kutoa, ni kwa sababu hawana uhusiano/muungano na chanzo cha nuru. **— Historical Sketches, 291. ChS 21.2**

Mungu amewateua watoto Wake kutoa nuru kwa wengine, na ikiwa watashindwa/watafeli kuifanya, na roho zikaachwa katika giza la upotovu kwa sababu ya kushindwa kwao kufanya kile ambacho wangefanya kama wangehuishwa na Roho Mtakatifu, watu hawa watawajibika kwa Mungu. Tumeitwa kutoka gizani kuingia katika nuru Yake ya ajabu, ili tuweze kuzionyesha sifa za Kristo.— **The Review and Herald, Desemba 12, 1893 . ChS 21.3**

Wote waliowekwa wakfu kwa Mungu watakuwa mikondo ya nuru. Mungu huwafanya kuwa wakala Wake ili kuwasilisha kwa wengine utajiri wa neema Yake… Ushawishi wetu juu ya wengine hautegemei sana kile tunachosema, bali vile tulivyo. Watu wanaweza kupigana nasi na kupinga mantiki yetu, wanaweza kupinga mwito tunaotoa kwao; lakini maisha ya upendo usio na makuu ni hoja ambayo hawawezi kupinga. Maisha yenye uthabiti usioyumbayumba, yenye sifa ya upole wa Kristo, ni nguvu ulimwenguni.— **The Desire of Ages, p. 141, 142 . ChS 21.4**

Wale ambao walipaswa kuwa nuru ya ulimwengu wametoa miale iliyo dhaifu na hafifu. Nuru ni nini? Ni uchamungu, wema, Ukweli, rehema, upendo; ni kuufunua Ukweli katika tabia na mtindo wa maisha. Injili inategemea utauwa binafsi wa waumini wake kwa nguvu yake kali, na Mungu amefanya mpango kupitia kifo cha Mwanawe mpendwa, ili kila roho iweze kutayarishwa kwa kila kazi njema. Kila nafsi inapaswa kuwa nuru angavu na yenye kung'aa, ikionyesha sifa Zake Yeye aliyetuita kutoka gizani kuingia katika nuru Yake yaajabu. "Sisi ni watendakazi pamoja na Mungu." Naam, watendakazi; hiyo inamaanisha kufanya utumishi wa bidii katika shamba la mizabibu la Bwana.—Kuna roho zinazopaswa kuokolewa,—roho kwenye makanisa yetu, katika shule zetu za Sabato, na katika majirani zetu.— **The Review and Herald, Machi 24, 1891 . ChS 21.5**

Ni katika kufanya kazi kwa ajili ya wengine ndipo wanadamu wanaziweka hai nafsi zao. Ikiwa watakuwa watendakazi pamoja

—

na Yesu, tutaona nuru thabiti na endelevu katika makanisa yetu ikizidi kuwaka na kung'aa zaidi na zaidi, ikituma miale yake, na hata kupenya giza na kutoa nuru nje ya mipaka yao wenyewe.— **Historical Sketches, 291 . ChS 22.1**

"Ninyi ni nuru ya ulimwengu." Wayahudi walifikiri kuweka faida za wokovu kwa taifa lao wenyewe; lakini Kristo aliwaonyesha kwamba wokovu ni kama mwanga wa jua. Ni mali ya ulimwengu wote.— **The Desire of Ages, 306 . ChS 22.2**

Mioyo inayoitikia ushawishi wa Roho Mtakatifu ndiyo mikondo ambayo baraka za Mungu hutiririka. Ikiwa wale waliomtumikia Mungu wangeondolewa duniani, na Roho Wake kuondolewa miongoni mwa wanadamu, ulimwengu huu ungeachwa kwenye ukiwa na uharibifu, hilo ndilo tunda la utawala wa Shetani. Ingawa waovu hawajui, wana deni hata la baraka za maisha haya kwa uwepo wa watu wa Mungu katika ulimwengu huu, ambao wao wanawadharau, wanawatesa na kuwaonea. Lakini ikiwa Wakristo ni wapo kwa jina tu, wao ni kama chumvi ambayo imepoteza ladha yake. Hawana ushawishi kwa wema duniani. Kwa njia ya kumwakilisha Mungu vibaya wao ni wabaya zaidi kuliko wasioamini.— **The Desire of Ages, 306 . ChS 22.3**

## Utume wa Mungu

Kazi ambayo wanafunzi walifanya, sisi pia tunapaswa kuifanya. Kila Mkristo anapaswa kuwa mmisionari. Kwa huruma na sikitiko inatupasa kuwahudumia wale wanaohitaji msaada, tukitafuta kwa bidii isiyo na ubinafsi kupunguza taabu za wanadamu wanaoteseka.— **The Ministry of Healing, p. 104 . ChS 22.4**

Kabla ya kupaa mbinguni, Kristo aliwapa wanafunzi Wake utume wao. Aliwaambia kwamba walipaswa kuwa watekelezaji wa mapenzi ambayo kwayo Yeye aliuachia ulimwengu hazina za uzima wa milele.— **The Act of the Apostles, 27 . ChS 22.5**

Katika dhamana waliyopewa wanafunzi wa kwanza, waumini katika kila zama wameshiriki. Kila mtu ambaye amepokea injili amepewa Ukweli mtakatifu ili kuusambaza kwa ulimwengu. Watu waaminifu wa Mungu sikuzote wamekuwa wamishenari wenye ujasiri na bidii kali, wakitoa wakfu rasilimali zao kwa heshima ya Jina Lake, na kutumia kwa hekima talanta zao katika utumishi Wake.— **The Acts of the Apostles, 109 . ChS 22.6**

Utume wa injili ni hati kuu ya umishenari ya ufalme wa Kristo. Wanafunzi walipaswa kufanya kazi kwa dhati na bidii kwa ajili ya nafsi, wakitoa mwaliko wote wa rehema. Hawakupaswa kungoja watu waje kwao; walipaswa kwenda kwa watu na ujumbe wao.—
**The Acts of the Apostles, 28 . ChS 23.1**

Wajumbe wa Mungu wameagizwa kuchukua kazi ileile ambayo Kristo aliifanya alipokuwa hapa duniani. Hawa wanapaswa kujitoa wenyewe kwa kila aina ya huduma aliyoifanya. Kwa bidii na uaminifu wanapaswa kuwaambia watu juu ya utajiri usiochunguzika na hazina ya mbinguni isiyoweza kuharibika. — **Shuhuda za Kanisa 9:130 . ChS 23.2**

Agizo walilopewa wanafunzi limetolewa kwetu pia. Leo, kama ilivyokuwa wakati huo, Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka anapaswa kuinuliwa mbele ya wale wasio na Mungu na wasio na

—

tumaini duniani. Bwana anawaita wachungaji, walimu na wainjilisti. Kutoka mlango kwa mlango (nyumba kwa nyumba), watumishi Wake wanapaswa kutangaza ujumbe wa wokovu. Kwa kila taifa, kabila, lugha na jamaa, habari za msamaha kupitia Kristo zinapaswa kubebwa. Sio kwa kunyamaza, kukosa uhai, bali kwa maneno yaliyo wazi, yaliyoamuliwa na yenye kusisimua. Mamia wanalisuburi onyo ili waepuke kwa ajili ya maisha yao. Ulimwengu unahitaji kuona kwa Wakristo ushahidi wa nguvu ya Ukristo. Si katika sehemu chache tu, bali ulimwenguni pote, jumbe za rehema zinahitajika.— **Gospel Workers, 29 . ChS 23.3**

Yesu alipopaa mbinguni, Alikabidhi kazi Yake duniani kwa wale ambao walikuwa wamepokea nuru ya injili. Hawa walipaswa kuendeleza kazi hiyo hadi ikamilike. Yeye Hajatoa wakala mwingine kwa ajili ya kutangaza Ukweli Wake. “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” "Na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata

ukamilifu wa dahari." Utume huu adhimu unatshuka na kufika kwetu katika zama hizi. Mungu analiachia kanisa Lake jukumu la kuupokea au kuukataa.— **Historical Sketches, p. 288 . ChS 23.4**

Juu yetu kumewekwa wajibu mtakatifu. Tumepewa agizo la utume: "**Basi enendeni , mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi , mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu: na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi: na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari."Mathayo 28:19, 20. Wewe u**mewekwa wakfu kwa kazi ya kuitangaza injili ya wokovu. Ukamilifu wa Mbingu unapaswa kuwa nguvu yako.— **Shuhuda kwa Kanisa 9:20, 21 . ChS 24.1**

**Kuitwa Kutoka Kwenye Shughuli za Maisha**

Watu wa kawaida wanapaswa kuchukua mahali pao kama watendakazi. Wakishiriki huzuni za wanadamu wenzao kama Mwokozi alivyoshiriki huzuni za wanadamu, kwa imani watamwona Yeye akifanya kazi pamoja nao.— **Gospel Workers, 38 . ChS 24.2**

Katika maeneo yote, karibu na mbali, watu wataitwa kutoka kwenye kwenye kilimo cha jembe la plau na kutoka katika biashara za kawaida kabisa ambazo kwa kiasi kikubwa hutawala akili kwa kiasi kikubwa, na watafunzwa kwa kuunganishwa na watu wenye uzoefu. Kadri wanavyojifunza kufanya kazi kwa ufanisi watatangaza Kweli kwa nguvu. Kupitia utendaji kazi wa ajabu wa mipango na majaliwa ya Mungu, milima ya shida itaondolewa na kutupwa baharini. Ujumbe wenye maana sana kwa wakaaji wa duniani utasikiwa na kueleweka. Watu watajua Kweli ni nini. Mbele na mbele zaidi kazi itasonga mpaka dunia yote itakapoonywa, na ndipo ule mwisho utakapokuja. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:96 . ChS 24.3**

Mungu anaweza na atawatumia wale ambao hawajapata elimu kubwa katika shule za wanadamu. Kutilia shaka uwezo Wake wa

—

kufanya hivi, ni ukafiri ulio wazi; ni kuwekea mipaka uwezo mkuu wa Yule ambaye Kwake hakuna lisilowezekana. Oh! Kama kungekuwa na kuweka tahadhari kwa udogo tu, na kutoamini kudogo! Kwani kufanya hivi, huleta nishati kubwa ya kanisa isiweze kutumika; inafunga njia, ili Roho Mtakatifu asiweze kuwatumia wanadamu; inawaweka watu katika kukaa bila kufanya kitu chochote, wale walio tayari kuhangaika na kufanya kazi katika njia za Kristo; inakatisha tamaa wengi kuingia katika kazi hiyo ambayo wangekuwa watendakazi wenye ufanisi pamoja na Mungu, ikiwa wangepewa nafasi inayofaa.— **Gospel Workers, 488, 489 . ChS 24.4**

Ni fursa ya kila nafsi kufanya kuendelea kusonga mbele. Wale waliounganishwa na Kristo watakua katika neema na katika kumjua Mwana wa Mungu, hata kufikia kimo kamili cha wanaume na wanawake. Ikiwa wote wanaodai kuamini Ukweli wangetumia vyema uwezo wao na fursa za kujifunza na kutenda, wangekuwa na nguvu katika Kristo. Haidhuru ni watu wa tasniagani,—iwe walikuwa wakulima, makanika/mafundi, walimu, au wachungaji,—kama wangejiweka wakfu kabisa kwa Mungu wangekuwa watenda kazi wenye ufanisi kwa ajili ya Bwana wa mbinguni. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:423 . ChS 25.1**

Wale katika kanisa ambao wana talanta za kutosha kushiriki katika miito mbalimbali ya maisha, kama vile kufundisha, kujenga, utengenzaji wa vitu viwandani, na kilimo, kwa ujumla wanapaswa kuwa tayari kufanya kazi kwa ajili ya kulijenga kanisa kwa kutumika katika kamati au kama walimu katika kanisa. Shule za Sabato, kufanya kazi ya umishenari, au kujaza ofisi mbalimbali zilizounganishwa na kanisa.— **The Review and Herald, Februari 15, 1887 . ChS 25.2**

Kwa ajili ya kuendeleza kazi Yake, Kristo hakuchagua watu wenye elimu kubwa na ufasaha wa Baraza la Kiyahudi la Sanhedrin, au mamlaka ya Rumi. Alipita kando ya walimu wa Kiyahudi waliojiona kuwa waadilifu, Mfanyakazi Stadi alichagua wanaume wanyenyekevu, wasio na elimu kutangaza zile Kweli ambazo zilipaswa kuuchochea ulimwengu. Watu hawa alikusudia kuwafundisha na kuwaelimisha kama viongozi wa kanisa Lake. Wao nao walipaswa kuwaelimisha wengine na kuwatuma na ujumbe wa injili. Ili wapate kufanikiwa katika kazi yao, walipaswa kupewa nguvu za Roho Mtakatifu. Si kwa uwezo wa kibinadamu au hekima ya kibinadamu ambayo injili ilipaswa kutangazwa, bali kwa uwezo wa Mungu.— **The Acts of the Apostles, 17 . ChS 25.3**

Miongoni mwa wale ambao Mwokozi alikuwa amewapa agizo, "Basi, enendeni, mkafundishe mataifa yote," wengi walitoka katika hali duni za maisha,—wanaume na wanawake ambao walikuwa wamejifunza kumpenda Bwana wao, na ambaowalikuwa wameazimia kumfuata mfano Wake wa huduma isiyo na ubinafsi. Kwa hawa watu wahali ya chini, na vilevile kwa wanafunzi ambao walikuwa pamoja na Mwokozi wakati wa huduma Yake duniani, walikuwa wamepewa dhamana ya thamani. Walipaswa kupeleka ulimwenguni habari njema ya wokovu kupitia Kristo. —**The Acts pf the Apostles, p. 105, 106 . ChS 25.4**

## Maisha Yanayoshinda

Sio tu kwa kuuhubiri Ukweli, sio tu kwa kuyasambaza machapisho, kwamba tunamshuhudia Mungu. Tukumbuke kuwa maisha kama ya Kristo ndiyo hoja yenye nguvu zaidi ambayo

—

inaweza kuendeleza mbele Ukristo, na kwamba tabia isiyokamili ya Kikristo ina madhara mabaya ulimwenguni kuliko tabia ya kiulimwengu. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:21 . ChS 26.1**

Sio vitabu vyote vilivyoandikwa vinaweza kutumika katika kusudi la maisha matakatifu. Watu wataamini, sio kile mhudumu anachohuhubiri, bali kile kanisa linachokiishi. Mara nyingi sana ushawishi wa mahubiri unaohubiriwa kutoka kwenye mimbari huhafifishwa na mahubiri yanayohubiriwa katika mtindo wa maisha ya wale wanaodai kuwa watetezi wa Kweli. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:21 . ChS 26.2**

Maisha ya Kristo yalikuwa yenye ushawishi uliozidi kupanuka kila wakati, mvuto usio na ukingo, mvuto uliomfungamanisha na Mungu na kwa familia nzima ya kibinadamu. Kupitia Kristo, Mungu amewekeza kwa mwanadamu ushawishi unaomfanya asiweze kamwe kuishi kwa nafsi

—

yake mwenyewe. Kila mmoja wetu ameunganishwa na wanadamu mwenzake, sehemu ya mtandao mzima wa Mungu, na tunasimama chini ya wajibu wa pande zote mbili. Hakuna mtu anayeweza kujitegemea bila wanadamu wenzake; kwa ajili ya ustawi wa kila mmoja huathiri wengine. Ni kusudi la Mungu kwamba kila mmoja atahisi kuwa wa lazima kwa ustawi wa wengine, na kutafuta kukuza furaha yao.— **Christ's Object Lessons, p . ChS 26.3**

Dini ya Biblia haipaswi kufungwa kati ya majalada ya kitabu, wala ndani ya kuta za kanisa. Haipaswi kutolewa nje hapa na pale kwa manufaa yetu wenyewe, na kisha kuwekwa kando tena kwa uangalifu. Dini inapaswa kutakasa maisha ya kila siku, kujidhihirisha yenyewe katika kila shughuli ya kibiashara na katika mahusiano yetu yote ya kijamii.— **The Desire of Ages, 306, 307 . ChS 26.4**

Ni kusudi la Mungu kujitukuza kupitia watu Wake kwa ulimwengu. Yeye Anatarajia wale wanaolibeba jina la Kristo kumwakilisha Yeye kwa mawazo, maneno, na matendo. Mawazo yao yanapaswa kuwa safi na maneno mazuri yenye kuinua, na kuwavuta wale wanaowazunguka karibu sana na Mwokozi. Dini ya Kristo inapaswa kusukwa pamoja na yote mtu anayoyatenda na kuzungumza. Kila shughuli yao ya kibiashara inapaswa kuwa na harufu nzuri ya uwepo wa Mungu. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:21 . ChS 26.5**

Hebu mfanyabiashara afanye biashara yake kwa namna ambayo itamtukuza Bwana Wakekwa sababu ya uaminifu wake. Hebu aibebe dini yake katika ~~kila~~ jambo linalofanyika na kuwafunulia watu Roho wa Kristo. Hebu fundi awe mwakilishi mwenye bidii na mwaminifu wa Yeye aliyetaabika katika hali duni za maisha katika miji ya Yudea. Hebu kila mtu analiyetaja jina la Kristo afanye kazi ili mwanadamu kwa kuona matendo yake mema aweze kuongozwa kumtukuza Muumba na Mkombozi wake.— **The Bible Echo, Juni 10, 1901 ( The Review and Herald, May 1, 1888 ). ChS 27.1**

**Wanawake Kama Wamisionari**

Wanawake kama kwa wanaume wanaweza kushiriki katika kazi

—

ya kuuficha Ukweli ambapo unaweza kufanikiwa na kudhihirishwa. Wanaweza kuchukua nafasi yao katika kazi katika zahama hii, na Bwana atafanya kazi kupitia wao. Ikiwa wao watajazwa na hisia za wajibu wao, na kufanya kazi chini ya ushawishi wa Roho wa Mungu, watamiliki uwezo unaohitajika kwa wakati huu. Mwokozi ataakisi kwa wanawake hawa waliojitolea, nuru ya uso Wake, na hii itawapa uwezo ambao utapita ule wa wanaume. Wanaweza kufanya katika familia kazi ambayo wanaume hawawezi kuifanya, kazi inayofikia maisha ya ndani. Wanaweza kuja karibu na mioyo ya wale ambao wanaume hawawezi kuwafikia. Kazi yao inahitajika. Wanawake wenye busara na wanyenyekevu wanaweza kufanya kazi nzuri katika kueleza Ukweli kwa watu katika nyumba zao. Neno la Mungu linaloelezwa hivi litafanya kazi yake ya chachu, na kwa ushawishi wake familia nzima itaongoka. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:128, 129 . ChS 27.2**

—

Wote wanaofanya kazi kwa ajili ya Mungu wanapaswa kuwa na sifa za Martha na Mariamu zilizochangamana-- utayari wa kuhudumu na upendo wa dhati wa Ukweli. Ubinafsi na uchoyo lazima viondolewe machoni. Mungu anawaita wanawake wafanyao kazi kwa bidii, watendakazi walio na busara, wachangamfu, wapole, na waaminifu kwa kanuni. Anawaita wanawake wavumilivu ambao watachukua akili zao kutoka kwa ubinafsi na urahisi wao binafsi, na kuziweka kwa Kristo, wakisema maneno ya Ukweli, wakiomba pamoja na watu ambao wanaweza kupata ufikiaji, wakijitahidi kutendakazi kwa uongofu wa roho. — **Shuhuda kwa Kanisa 6:118 . ChS 27.3**

Akina dada wanaweza kufanya kazi kwa ustadi katika kuwapata wanaojiandikisha kwa ajili ya kununua magazeti/majarida yetu, kwa njia hii wakileta nuru mbele ya akili wengi.— **The Review and Herald, Juni 10, 1880 . ChS 28.1**

Kuna wanawake waungwana na bora ambao wamekuwa na ujasiri wa kimaadili wa kuamua kuunga mkono Ukweli kutokana na uzito wa ushahidi. Wamekubali Kweli kwa dhamiri zao. Wana busara, utambuzi, na uwezo mzuri, na watazalisha watendakazi wenye mafanikio kwa Bwana wao. Wanawake Wakristo wanaitwa.— **The Review and Herald, Desemba 19, 1878 . ChS 28.2**

Dada zetu wanaweza kutumika kama watendakazi makini katika kuandika, na kuchora hisia za kweli za marafiki ambao wamepokea karatasi na vipeperushi vyetu Wanawake
Wenye tabia na kanuni iliyoamuliwa wanahitajika ambao wanaamini

kwamba kweli tunaishi katika siku za mwisho, na kwamba ~~tu~~na ujumbe mzito wa mwisho wa onyo utakaotolewa kwa ulimwengu.... Hawa ndio ambao Mungu anaweza kuwatumia katika vipeperushi na kazi ya umisionari. Hawa wanaweza kwa njia nyingi
kufanya kazi ya thamani kwa ajili ya Mungu katika kusambaza vijuzuu

na kugawanya kwa busara *Ishara za Nyakati.*— **The Review and Herald, Desemba 19, 1878 . ChS 28.3**

Sipendekezi kwamba mwanamke atafute kuwa mpiga kura au mshika ofisi ya siasa; lakini akiwa mmishenari, akifundisha Kweli kwa mawasiliano ya barua, akigawanya vipeperushi na kuomba waliojiandikisha kwa ajili ya magazeti yenye zile Kweli nzito za wakati huu, anaweza kufanya mengi sana.— **The Review and Herald, Desemba 19, 1878 . ChS 28.4**

Ikiwa kungekuwa na wanawake ishirini ambapo sasa kuna mmoja ambao wangefanya utume huu mtakatifu kuwa kazi yao yenye kupendwa sana, tungepaswa kuona wengi zaidi wakiongolewa na Kweli.— **The Review and Herald, Januari 2, 1879 . ChS 28.5**

Wanawake wanaoweza kufanya kazi wanahitajika sasa, wanawake wasiojiona kuwa wa maana, bali wapole na wanyenyekevu wa moyo, ambao watafanya kazi kwa upole wa Kristo popote pale wanapoweza kupata kazi ya kufanya kwa ajili ya wokovu wa roho.— **The Review and Herald. Januari 2, 1879 . ChS 28.6**

Mamia ya dada zetu wanaweza kuwa kazini leo kama wangefanya hivyo. Wanapaswa kujivika wenyewe na watoto wao kwa usahili, mavazi nadhifu na ya kudumu, yasiyo na mapambo, na watoe wakati ambao wametumia katika maonyesho yasiyo ya lazima kwa kazi ya umishenari. Barua zinaweza kuandikwa kwa marafiki walio mbali. Dada zetu wanaweza kukutana pamoja ili kushauriana kuhusu namna bora ya kazi. Pesa zinaweza kuokolewa na kutunzwa ili zitolewe kama sadaka kwa Mungu, na kuwekezwa kwenye karatasi na vipeperushi vya kutuma kwa marafiki zao. Wale ambao sasa hawafanyi chochote wanapaswa kwenda kufanya kazi. Acha kila dada anayedai kuwa mtoto wa Mungu ahisi wajibu wa kusaidia wote walio kwenye ufikiaji wake.— **The Review and Herald, Desemba 12, 1878 . ChS 28.7**

Dada zetu wamekuwa tayari sana kutoa udhuru wa kubeba majukumu ambayo yanahitaji fikra na matumizi ya karibu ya akili; lakini hii ndiyo nidhamu hasa wanayohitaji ili kupata uzoefu wa Kikristo ulio kamili. Huenda wakawa watendakazi katika shamba la umishenari, wakiwa na shauku binafsi katika ugawaji wa vipeperushi na machapisho yanayowakilisha imani yetu kwa usahihi.— **The Review and Herald, Desemba 12, 1878 . ChS 29.1**

Akina dada, msichoke na kazi makini ya umishenari inayohusisha kukesha. Hii ni kazi ambayo nyote mnaweza kushiriki kwa mafanikio, ikiwa tu mtaungana na Mungu. Kabla ya kuandika barua za
Kuulizia watu jambo, daima inua moyo wako kwa Mungu katika maombi, ili uweze kufanikiwa
katika kukusanya baadhi ya matawi ya mwitu ambayo yanaweza kupandikizwa katika mzabibu wa Kweli, na kuzaa matunda kwa utukufu wa Mungu. Wale wote ambao kwa mioyo ya unyenyekevu wanashiriki katika kazi hii watakuwa wakijielimisha wenyewe wakiwa watendakazi katika shamba la mizabibu la Bwana.— **The Review and Herald, Juni 10, 1880 . ChS 29.2**

## SURA YA 2 WITO KWA VIJANA

### Uteuzi wa Bwana

Bwana amewateua vijana kuwa mkono Wake wa msaada/kusaidia. — **Shuhuda za Kanisa 7:64 . ChS 30.1**

Tukiwa na jeshi la watendakazi kama vijana wetu, na wawe wamefunzwa ipasavyo, wangeweza kutoa kwa haraka jinsi gani, ujumbe wa Mwokozi aliyesulubiwa, aliyefufuka, na anayekuja hivi karibuni na kisha Ukweli ungeweza kupelekwa katika ulimwenguni wote!— **Education, 271 . ChS 30.2**

Tuna jeshi la vijana leo ambao wanaweza kufanya mengi ikiwa wataelekezwa na kutiwa moyo ipasavyo. Tunataka watoto wetu waamini Ukweli. Tunataka wabarikiwe na Mungu. Tunataka washiriki katika mipango iliyopangwa vizuri ya kuwasaidia vijana wengine. Hebu wote wazoezwe hivyo ili waweze kuwakilisha Ukweli kwa haki, wakitoa sababu ya tumaini lililo ndani yao, na kumheshimu Mungu katika tawi lolote la kazi ambapo wana sifa za kufanya kazi.— General Conference Daily Bulletin, Januari 29, 1893 , 24. ChS 30.3

### Vijana Katika Kazi ya Kanisa

Vipaji vya ujana, vilivyopangwa vyema na vilivyofunzwa vyema, vinahitajika katika makanisa yetu. Vijana watafanya kitu kwa nguvu zao z~~ina~~zofurika. Nguvu hizi zisipoelekezwa kwenye njia sahihi, zitatumiwa na vijana kwa njia ambayo itadhuru hali yao ya kiroho, na kuthibitisha madhara kwa wale wanaoshirikiana nao.— **Gospel Workers, 211 . ChS 30.4**

—

Vijana wanapotoa mioyo yao kwa Mungu, wajibu wetu kwao haukomi. Ni lazima wawe na shauku ya kazi ya Bwana, na kuongozwa kuona kwamba anawatarajia kufanya jambo fulani ili kuendeleza kazi Yake. Haitoshi kuonyesha ni kiasi gani kinahitajika kufanywa, na kuwahimiza vijana kuchukua sehemu. Lazima wafundishwe jinsi ya kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Ni lazima wafunzwe, wasaidiwe nidhamu, wapewe mazoezi, katika mbinu bora za kuleta roho kwa Kristo. Wafundishe kujaribu kwa utulivu, njia halisi na kweli ya kuwasaidia wenzao wachanga bila ya kujifanya (kutokuwa feki). Acheni matawi mbalimbali ya jitihada ya umishenari yawekwe katika mfumo wenye utaratibu, ambao wanaweza kushiriki, na wapewe maagizo na msaada. Hivyo watajifunza kufanya kazi kwa ajili ya Mungu.— **Gospel Workers, p. 210 . ChS 30.5**

## Katika miaka ya Mapema

Hebu wema na heshima/adabu/uungwana ya mchungaji ionekane kwa jinsi anavyowatendea watoto. Mchungaji anapaswa kukumbuka kuwa wao ni wanaume na wanawake wadogo, washiriki wachanga katika familia ya Bwana. Hawa wanaweza kuwa karibu sana wa kupendwa na

Bwana, na, kama wakielekezwa ipasavyo na kuadibishwa, watamfanyia huduma, hata katika ujana wao. —**Shuhuda za Kanisa 4:397, 398 . ChS 31.1**

Vijana wasipuuzwe; hebu washiriki katika kazi na wajibu. Waache wajisikie kwamba wana sehemu ya kutenda katika kuwasaidia na kuwabariki wengine. Hata watoto wanapaswa kufundishwa kufanya kazi ndogo za upendo na rehema kwa wale ambao hawakubahatika kuliko wao wenyewe. — **Ushuhuda wa Kanisa 6:435 . ChS 31.2**

Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao thamani na matumizi sahihi ya wakati. Wafundishe kwamba kufanya jambo ambalo litamheshimu Mungu na kuwabariki wanadamu ni jambo la maana kujitahidi kulifanya. Hata katika miaka yao ya mapema wanaweza kuwa wamishenari kwa ajili ya Mungu.— **Christ's Object Lessons, p . ChS 31.3**

## Wakati ulio Mbeleni mwa Vijana

Vijana wengi wa siku hizi, waliokua kama Danieli katika nyumba yake ya Yuda, akijifunza Neno la Mungu na kazi Zake, na kujifunza masomo ya utumishi wenye uaminifu, bado watasimama katika mabunge ya kutunga sheria, katika mabunge ya kutunga sheria, au katika vituo vya polisi au mahakamani, na majumba ya kifalme kama shahidi wa Mfalme wa wafalme.— **Education, 262 . ChS 31.4**

## Timotheo Kijana mdogoAlipochaguliwa

Paulo aliona kwamba Timotheo alikuwa mwaminifu, th~~abi~~ti, na wa kweli, na akamchagua kama mshiriki mwenza katika kazi na safari. Wale waliokuwa wamemfundisha Timotheo katika utoto wake walipata thawabu kwa kumwona mwana waliyemlea akihusishwa katika ushirika wa karibu na mtume mkuu. Timotheo alikuwa kijana mdogo alipochaguliwa na Mungu kuwa mwalimu; lakini kanuni zake zilikuwa zimethibitishwa na elimu yake ya awali hivi kwamba alifaa kuchukua nafasi yake kama msaidizi

—

wa Paulo. Na ingawa alikuwa kijana, alibeba majukumu yake kwa upole na unyenyekevu wa Kikristo.— **The Acts of the Apostles, 203, 204 . ChS 31.5**

**Akiba ya Kujaza Nafasi**

Wabeba mizigo miongoni mwetu wanaanguka kwa kifo. Wengi wa wale ambao wamekuwa wa mstari wa mbele katika kutekeleza matengenezo yaliyoanzishwa na sisi kama watu wa imani, sasa wamepita umri wa utu uzima na kuingia uzeeni, na wanapungua nguvu za kimwili na kiakili. Huku kukiwa na mahangaiko makubwa kuhusu jambo hili, swali laweza kuulizwa, Ni nani watakaojaza nafasi yao? Masilahi muhimu ya kanisa yatakabidhiwa kwa nani wakati washika viwango wa sasa wanapoanguka vhini? Hatuwezi ila kuwatazama vijana wa siku hizi kwa wasiwasi kama wale ambao wanapaswa kubeba mizigo hii, na ambao majukumu lazima yawashukie. Hawa lazima waanze kazi ambapo wengine wanaiacha, na mwendo wao ndio utakaoamua ikiwa maadili, dini, na utauwa muhimu utashinda, au ikiwa ukosefu wa maadili na ukafiri

utaharibu na kutia doa kila kitu ambacho ni cha thamani.— **Gospel Workers, 68 . ChS 32.1**

**Waanzilishi Katika Mateso na Kujitoa Dhabihu**

Ni lazima tuonyeshe (kudhihirisha) imani kwa vijana wetu. Wanapaswa kuwa payonia/waanzilishi katika kila shughuli inayohenyesha na kuhusisha mateso na dhabihu, huku watumishi wa Kristo waliolemewa na umri na kazi, wanapaswa kuthaminiwa kuwa washauri, ili kuwatia moyo na kuwabariki wale wazee ambao kwenye enzi zao kazini, walitoa vipigo vikali kwenye kazi ya Mungu.— **The Counsels to Parents, Teachers, and Students, 516, 517 . ChS 32.2**

Vijana wanatakiwa. Mungu anawaita hawa kwenye maeneo umishenari. Kwa vile wangali huru na masumbufu na majukumu, wako katika hali nzuri zaidi ya kushiriki katika kazi hiyo kuliko wale ambao wanapaswa kutoa malezi, mafunzo na msaada wa familia kubwa. Zaidi ya hayo, vijana wanaweza kubadilika na kuendana na mazingira kwa urahisi zaidi katika hali ya hewa mpya na jamii mpya, na wanaweza kustahimili usumbufu na magumu. Kwa busara na ustahimilivu, wanaweza kufikia watu mahali walipo.— **The Counsels to Parents, Teachers and Students, 517 . ChS 32.3**

Vijana wengi walio nyumbani ambao wamekuwa na aina sahihi ya elimu wanapaswa kufunzwa kwa ajili ya huduma na kutiwa moyo kuinua kiwango cha Ukweli katika maeneo mapya kwa kazi iliyopangwa vizuri na ya uaminifu. Kwa kushirikisha pamoja na watumishi wetu na watendakazi wenye uzoefu katika kazi ~~za~~ mijini, watapata aina bora ya mafunzo. Wakitenda kazi chini ya mwongozo wa Mungu na kuungwa mkono na maombi ya watendakazi wenzao wenye uzoefu zaidi, wanaweza kufanya kazi nzuri na yenye baraka. Wanapounganisha utumishi wao na ule wa watendakazi wenye umri mkubwa, kwa kutumia nguvu zao za ujana kwa ubora kabisa, watakuwa na ushirika wa malaika wa mbinguni; na kama watendakazi pamoja na Mungu, ni fursa yao

—

kuimba na kuomba na kuamini, na kufanya kazi kwa ujasiri na uhuru. Ujasiri na imani ambao uwepo wa mawakala wa mbinguni utaleta kwao na kwa watendakazi wenzao utawaongoza kwenye sala na sifa na usahili wa imani ya kweli. —**Ushuhuda kwa Kanisa 9:119 . ChS 32.4**

**Maeneo ya Kazi**

Kuna njia nyingi ambazo vijana wanaweza kupata fursa ya juhudi za kusaidia. Vikosi vinapaswa kupangwa na kuelimishwa kikamili ili kufanya kazi kama wauguzi, watembeaji wa injili nyumba kwa nyumba au mikutanoni au wainjilisti wa vitabu, na wasomaji wa Biblia, wakiwa wahubiri, wahudumu, na wainjilisti wamishenari wa tiba.— **The Counsels to Parents, Teachers and Studentsi, 546 . ChS 33.1**

Tuwaelimishe vijana kuwasaidia vijana; na wanapotafuta kufanya kazi hii watapata uzoefu utakaowawezesha kuwa watendakazi waliowekwa wakfu katika nyanja kubwa zaidi. —**Shuhuda kwa Kanisa 6:115 . ChS 33.2**

—

Vijana wa kiume na wa kike wanapaswa kuelimishwa ili kuwa watendakazi katika maeneo ya ujirani wao na katika maeneo mengine. Hebu wote waweke mioyo na nia zao kuwa na akili kuhusiana na kazi ya wakati huu, wakijistahilisha wenyewe kufanya yale ambayo kwayo wanaendana vyema nayo.— **Shuhuda kwa Kanisa 9:118, 119 . ChS 33.3**

**Siri ya Mafanikio**

Fuateni, enyi vijana, ili kumjua Bwana, nanyi mtajua kwamba "kutokea Kwake ni yakini kama asubuhi." Hosea 6:3. Tafuta kuwa bora mara zote. Tafuta kwa bidii kufanana na Mkombozi na kuwa na utambulisho Wake. Ishi kwa imani katika Kristo. Fanya kazi aliyoifanya. Ishi kwa ajili ya kuokoa roho za watu aliowatolea maisha Yake. Jaribu kwa kila njia kuwasaidia wale unaowasiliana na kukutana nao. Jitahidi kuendelea kuboresha kwa kila njia. Hebu maisha yako yatimize Maneno haya: "Wewe kwa amri zako umenifanya kuwa mwenye hekima kuliko adui zangu." Zaburi 119:98. Zungumza na Kaka yako, ambaye atakamilisha elimu yako, mstari juu ya mstari, amri juu ya kanuni, hapa kidogo na pale kidogo. Uhusiano wa karibu na Yeye aliyejitoa Mwenyewe kuwa dhabihu ili kuokoa ulimwengu unaoangamia atawafanya ninyi kuwa watenda kazi wanaokubalika. — **Shuhuda kwa Kanisa 6:416 . ChS 33.4**

**Kujipanga kwa ajili ya Huduma**

Vijana wa kiume na wa kike, je, hamwezi kuunda vikundi, na, kama askari wa Kristo, kujiandikisha katika kazi, mkiweka busara zenu zote na ustadi na talanta katika utumishi wa Bwana, ili mpate kuokoa roho kutoka kwenye uharibifu? Na kuwe na vikosi vilivyopangwa katika kila kanisa kufanya kazi hii.... Je, vijana wa kiume na wa kike wanaompenda Yesu kweli watajipanga kuwa watenda kazi, si kwa ajili ya wale tu wanaodai kuwa watunza Sabato, bali kwa wale ambao si imani yetu?— **The Signs of the Times, Mei 29, 1893 . ChS 34.1**

—

Hebu vijana wa kiume na wakike na watoto waende kufanya kazi kwa Jina la Yesu. Waache waungane pamoja juu ya mpango fulani na utaratibu wa utekelezaji. Je, hamwezi kuunda kikundi cha watendakazi, na kupanga muda kuomba pamoja na kumwomba Mungu awapatie neema Yake, na kusonga mbele kwa umoja? —
**Youth's Instructor, August 9, 1894.**
**ChS 34.2**

## SURA YA 3 HALI MIONGONI MWA WATU WA MUNGU

### Roho ya Umisionari inakosekana

Kumekuwa na roho kidogo tu ya umishenari miongoni mwa Waadventista wanaoitunza Sabato. Kama wachungaji na watu wangeamshwa vya kutosha, hawangepumzika hivyo bila kujali wakati Mungu amewaheshimu kwa kuwafanya wapokeaji wa sheria Yake kwa kuichapa/kuiandika katika akili zao na kuiandika mioyoni mwao. —**Shuhuda za Kanisa 3:202 . ChS 35.1**

Roho ya Kweli ya umishenari imeyaacha makanisa ambayo hujitukuza kuwa yanajua (wao ni wajuaji); mioyo yao haimeremeti au kung’aa kwa upendo wa roho na hamu ya kuwaongoza watu katika zizi la Kristo. Tunataka watendakazi dhati na wenye bidii. Je, hakuna wa kujibu kilio kilichosikika kutoka kila nyumba: "Njoo ... Utusaidie"? — **Shuhuda za Kanisa 4:156. ChS 35.2**

Nilioneshwa kuwa kama watu tuna upungufu. Kazi zetu hazilingani na imani yetu. Imani yetu inashuhudia kwamba tunaishi wakati wa kutangazwa kwa ujumbe mzito na muhimu sana kuwahi kupewa wanadamu wanaokufa. Walakini kwa mtazamo kamili wa Ukweli huu, jitihada zetu, bidii yetu, ari yetu, na roho yetu ya kujitoa kafara, havilingani na tabia ya kazi. Tunapaswa kuamka toka kwa wafu, na Kristo atatupatia uzima.— **Shuhuda za Kanisa 2:114. ChS 35.3**

Moyo wangu unaumia ninapofikiria jinsi makanisa yetu yanavyohisi kwa udogo uwajibikaji wao mzito kwa Mungu. Sio wachungaji peke yao ndio ambao ni askari, lakini kila mwanamume na mwanamke ambaye amejiandikisha katika jeshi la Kristo; na je, hawa wako tayari kwenda mwendo wa askari, kama vile Kristo alivyowapa kielelezo katika maisha Yake ya kujikana nafsi na kujitoa mhanga? Je, ni hali gani ya kujikana nafsi ambayo makanisa yetu kwa ujumla yamedhihirisha? Wanaweza kuwa wametoa mchango kwa pesa, lakini wamejizuia wenyewe, (hawajajitoa

—

wenyewe ila wametoa pesa)….. **ChS 35.4**

Wengi wa wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo hawahisi mzigo kwa ajili ya roho za watu kama vile ambavyo walimwengu wanavyofanya. Tamaa za macho, na kiburi cha uzima, upendo wa kujionyesha, upendo wa kuridhika, hutenganisha wale wanaojiita Wakristo na Mungu, na roho ya kimishenari kwa uhalisia iko, ila kwa wachache tu. Je, nini kifanyike ili kufungua macho ya watu hawa wenye dhambi katika Sayuni, na hata kuwafanya wanafiki watetemeke?— **The General Conference Daily Bulletin, Februari 4, 1893 , 131, 132. ChS 35.5**

Kuna kikundi ambacho kinawakilishwa na Merozi (Waamuzi 5:23). Roho ya umishenari haijawahi kupata mashiko kwenye roho zao. Wito wa misheni za kigeni haujawachochea kuchukua hatua. Je, watu hawa watatoa hesabu gani kwa Mungu, wakati hawafanyi lolote katika kazi Yake,—hakuna lolote linalofanyika katika kuleta roho kwa Kristo? Hao watalaumiwa hadharani, "Wewe mtumishi mwovu na mvivu."— **Historical Sketches, 290 . ChS 36.1**

Kama kielelezo cha kushindwa kwako kuja kumsaidia kazi Mungu, kama ilivyokuwa
fursa yako, niliekelezwa katika maneno haya; "Ulaanini Merozi, alisema malaika wa

BWANA, muwalaani kwa uchungu wenyeji wake; kwa maana hawakuja kumsaidia Bwana, kumsaidia BWANA juu ya hao wenye nguvu” Waamuzi 5:23. Je, Merozi ilikuwa mefanya nini? Hakuna chochote. Na hii ndiyo ilikuwa dhambi yake. Wao hawakwenda kumsaidia Bwana dhidi ya mashujaa.”— **Shuhuda kwa Kanisa, 2:247.ChS 36.2**

**Kundi la Watu Walioridhika, Wakiona Wamejitosheleza**

Nilioneshwa tabaka la watu wengi waliokuwa wanafahamu kuwa wana misukumo ya ukarimu mioyoni mwao, wenye hisia za uchaji Mungu (ibada), na upendo wa kutenda mema; lakini wakati huo huo wanaishi bila kufanya chochote. Wameridhika kwa njia hasi, wakijipendeza kwamba ikiwa wangekuwa nayo fursa, au upendeleo fulani, basi wangeweza kufanya kazi nzuri sana; ila wameendelea kubungaa tu wakisubiri fursa. Wanawadharu mabahili wenye akili finyu, masikini ambao wanabania visenti vichache kwa ajili ya wahitaji. Wanaona kuwa anaishi kwa ajili ya nafsi yake wenyewe kwa ubahili, kuwa hana wito wa kuwatendea wengine mema, kuwabariki kwa talanta ya ushawishi na mali ambazo zimewekwa kwake azitumie, sio kwa kutumia vibaya, au kuziruhusu kula kutu, au kuzizika chini ardhini. Wale ambao wanajipa wenyewe hali ya ubahili na ubinafsi wanawajibika kwa matendo yao ya uchoyo, wanawajibika kwa talanta walizotumia vibaya. Lakini wanaowajibika zaidi ni wale ambao wana misukumo ya ukarimu na kwa kawaida ni wepesi kutambua mambo ya kiroho, na bado wanabaki bila ya kufanya kazi, wakingojea fursa waliyokuwa wanaitarajia nayo haikupatikana, na huku wanatofautiana na utayari wao wa kutenda kwa kutokuwa na utayari na bahili wanayemcheka, na kupuuzia kwao kwamba hali yao ni nzuri zaidi kuliko ile ya majirani zao wenye roho za ubahili. Hao hujidanganya wenyewe. Umiliki wa sifa ambazo hazitumiwi ni kuongeza majukumu tu; na ikiwa watazitunza talanta za Bwana wao bila kuziendeleza au kuzihifadhi, hali yao haina tofauti na ile ya majirani zao ambao wao wana kawaida ya kuwadharau. Watu hawa wataambiwa, mlijua mapenzi ya Bwana wenu lakini

—

hamkuyatenda. —**Shuhuda kwa Kanisa, 2:250,251.** **ChS 36.3**

## Usingizi wa Kifo Cha Kishetani

Watu wa Mungu lazima wachukue moyoni onyo na kupambanua ishara za nyakati. Ishara za kuja kwa Yesu Kristo ziko wazi kabisa kiasi cha kutotiliwa shaka, na kwa kuzingatia mambo haya kila mtu anayekiri Ukweli anapaswa kuwa Mhubiri Aliye Hai. Mungu anatoa wito kwa wote, wahubiri na watu, kuamka. Mbingu yote inaonesha matukio yanayoendelea. Matukio ya historia ya dunia yanafungwa haraka. Tuko katikati ya maafa ya siku za mwisho.Maafa makubwa yako mbele yetu, na bado hatujaamka. Ukosefu huu wa shughuli na bidii katika kufuata maelekezo ya Mungu ni wa kutisha. Usingizi wa kifo unatoka kwa Shetani. Yeye hudhibiti akili za Watunza Sabato ambao hawajajitakasa, na huwaongoza kuwaonea wivu wenzao, kutafuta makosa baina yao. —**Shuhuda kwa Kanisa, 1:260,261.** **ChS 37.1**

Kutokuamini kumetanda kama wingu linalofunika watu kwa sanda ya mauti, na kuzunguka-zunguka katika makanisa yetu, kwasababu watu hawatumii talanta ambazo Mungu amewapa ili kuwapa nuru wale wasiojua Ukweli wa thamani. Bwana anawataka wale watu ambao tayari wamesamehewa, wale ambao tayari wanaifurahia nuru, kuwajulisha wengine Ukweli. —**The General Conference Bulletin, 1893, 133.** **ChS 37.2**

Shetani sasa anatafuta kuwashikilia watu wa Mungu katika hali ya kutofanya kazi, kuwazuia wasitekeleze sehemu yao katika kueneza Ukweli, ili mwishowe wapimwe katika mizani na kuonekana wamepungua, wana uhitaji/kasoro. —**Shuhuda kwa Kanisa, 1:260. ChS 37.3**

Wanadamu wako hatarini. Umati wa watu unaangamia. Lakini ni wachache kiasi gani kati ya wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wanaolemewa na roho hizi. Hatima ya ulimwengu imening'inia katika mzani; lakini hii haiwagusi hata wale wanaodai kuamini zile Kweli zinazofika mbali, zilizowahi kuwahi kutolewa kwa wanadamu. Kuna ukosefu wa upendo ule ambao ulimfanya Kristo kuondoka kwenye makao Yake ya mbinguni na kuchukua asili ya mwanadamu, ili ubinadamu uweze kugusa ubinadamu, na kuvuta ubinadamu kwa Uungu. Kuna usingizi mkali, kupooza, juu ya watu wa Mungu, ambao unawazuia kuelewa wajibu wa maombi wa saa hii tuliyopo. —**Christ's Object Lessons, 303 . ChS 37.4**

Shetani anatumia uvivu na usingizi wa kizembe kwa wale wanaojidai kuwa Wakristo kwa mdomo tu, ili kuimarisha nguvu zake na kuvuta roho kwenda upande wake. Wengi wanafikiri kwamba ingawa hawafanyi kazi hai kwa ajili ya Kristo, wao bado wako upande Wake, na hakika watu kama hawa wanamwezesha adui kumiliki ardhi na kupata faida (ardhi ya mioyo yao, na kazi). Kwa kushindwa kwao kuwa watendakazi wenye bidii kwa ajili ya Bwana, kwa kuacha majukumu yakiwa hewani bila kutimizwa na maneno wanayopaswa kutamka bila kusemwa, wamemruhusu Shetani apate kuzitawaka/kuzidhibiti nafsi ambazo huenda zingevutwa na kujitoa kwa Kristo kikamilifu.— **Christ's Object Lessons, p . ChS 38.1**

Ninaposoma Maandiko, ninashangazwa na Israeli ya Mungu katika siku hizi za mwisho. Wanaonywa kuikimbia ibada ya sanamu. Ninahofia ~~kw~~amba wamelala fofofo na wamejiunganisha na ulimwengu kiasi kwamba inakuwa vigumu kutofautisha kati ya yule

anayemtumikia Mungu na yule asiyemtumikia. Umbali unazidi kuongezeka kati ya Kristo na watu Wake na kupungua kati yao na dunia. Alama zinazowatambulisha wale watu wanaojidai ni wa Kristo kwa maneno, na ulimwengu ni kama zimepotea zote. Kama Israeli ya zamani wanafuata machukizo ya mataifa yanayowazunguka. —Shuhuda kwa Kanisa, 1:277. ChS 38.2

## Utambuzi wa Kiroho Umefifia

Na sio tu ulimwenguni tunaona matokeo ya kupuuza kwa kanisa kufanya kazi katika nyanja na kusudi la Kristo. Kwa kupuuza huku hali ya mambo imeletwa ndani ya kanisa ambayo imefunika masilahi ya juu na matakatifu ya kazi ya Mungu. Roho ya ukosoaji na uchungu imekuja ndani ya kanisa, na uelewa wa kiroho wa wengi umefifia. Kwa sababu hii kazi ya Kristo imepata hasara kubwa. —Shuhuda kwa Kanisa, 6:297. ChS 38.3

“Nimejawa na huzuni ninapofikiria hali ya watu wetu wa masalio. BWANA hajatufungia mbingu, lakini mwenendo wetu wenyewe ya kurudi nyuma umetutenga na MUNGU. Dhambi za kutisha na zile za kiburi na kuyumkinisha mambo, zimekaa kati yetu. Na bado cha kushangaza ni kuwa maoni ya jumla ya watu, ni kwamba kanisa linashamiri, na kwamba amani na ustawi wa kiroho uko katika mipaka yake yote. "Kanisa limeacha kumfuata Kristo Kiongozi wake na linarudi nyuma kuelekea Misri kwa uhakika. Walakini ni wachache tu wanaochukua waliogutuka na kuchukua tahadhari dhidi ya hitaji lao la nguvu za kiroho. Mashaka na hata kutoziamini shuhuda za Roho wa Mungu, vinatia chachu makanisa yetu kila mahali. Shetani angependa mambo yawe hivi. —Shuhuda kwa Kanisa, 5:217. ChS 38.4

## Hali ya Udhaifu wa Kiroho

Nuru iliyokusanywa imeangaza kwa watu wa Mungu; lakini wengi wamepuuza kuifuata nuru, na kwa sababu hii wako katika udhaifu wa kiroho wa kutisha. Sio kwa kukosa maarifa kwamba watu wa Mungu wanaangamia sasa. Hawatahukumiwa kwa sababu hawajui Njia, Kweli na Uzima. Ukweli ulioufikia uelewa

wao, nuru ilioangaza katika roho, lakini ambayo imepuuzwa, au kudharauliwa au kukataliwa, itawahukumu. Wale ambao kamwe hawakuwa na nuru ya kukataa hawatakuwa katika hukumu. Nini zaidi kingefanyika kwa shamba la mizabibu la Mungu kuliko kilichofanyika? Nuru, nuru ya thamani, inaangaza kwa watu wa Mungu; lakini haitawaokoa isipokuwa wamekubali kuokolewa nayo, kuiishi kulingana nayo kikamilifu, na kuipeleka kwa wengine walio gizani. —**Shuhuda kwa Kanisa, 2:123. ChS 38.5**

### Haja ya Macho ya Kimbingu

Makanisa yanahitaji kuwekewa dawa machoni mwao, dawa ya mbinguni, ili wapate kuona fursa nyingi zinazowahusu kumtumikia Mungu. Mara kwa mara Mungu amewaita watu Wake watoke kwenye njia kuu na viunga, na kuwashurutisha watu waingie, ili nyumba Yake ijae; lakini hata ndani ya kivuli cha milango yetu wenyewe kuna familia ambazo hatujaonyesha nia ya kutosha kuwaongoza watu hawa kufikiri kwamba tulijali nafsi zao. Ni kazi hii iliyo karibu nasi ambayo sasa Bwana analiita kanisa kuifanya. Hatupaswi kusimama tukisema: "Jirani yangu ni nani?" Tunapaswa kukumbuka kwamba jirani yetu ndiye yule anayehitaji sana huruma na msaada wetu. Jirani yetu ni kila nafsi iliyojeruhiwa na kupondwa na adui. Jirani yetu ni kila mtu ambaye ni mali ya Mungu. Katika Kristo, tofauti zilizofanywa na Wayahudi kuhusu nani alikuwa jirani yao zimefagiliwa mbali. Hakuna mistari ya eneo la watu fulani, mipaka, hakuna tofauti za bandia, hakuna tabaka, hakuna ukoo wa kifalme. —**Shuhuda kwa Kanisa, 6:294**

### Ushupavu na Kupoa Kiimani

Shetani sasa anafanya kazi kwa uwezo wake wote wa kudanganya, kuwapendekezea watu wengi kwa ujanja mbaya kutoka kwenye kazi ya ujumbe wa malaika wa tatu, ambao unapaswa kutangazwa kwa nguvu kuu. Adui aonapo kuwa Bwana anawabariki watu Wake, na kuwatayarisha kutambua upotovu wake, atafanya kazi kwa uwezo wake mkuu kuleta ushupavu na kupitiliza, kwa upande mmoja na kwa upande mwingine urasimu wenye ubaridi,

—

ili apate kukusanya katika mavuno ya roho. Sasa ni wakati wa kukesha macho bila kukoma. Tazama kwa tahadhari hatua ya kwanza ya mapema ambayo Shetani anaweza kukanyaga/kufanya miongoni mwetu.— **The Review and Herald, Januari 24, 1893 . ChS 40.1**

Kuna majabali makubwa ya barafu za kimaadili kwenye makanisa yetu (icebergs). Kuna watu wenye wenye urasmi wengi ambao wanaweza kufanya onyesho la kuvutia, lakini

—

hawawezi kuangaza kama taa ulimwenguni (*hawana joto na upendo kwenye mioyo, wamekauka na kila kitu wao wanakifanya kwa urasimu-itifaki, urasmi, ratiba, mapokeo, desturi, mikakati, ni kazi ya kiofisi). —**The Review and Herald, Januari 24, 1893.ChS 40.2**

**Kushushwa Kiwango na Ubinafsi**

Sababu inayowafanya watu wa Mungu kutokuwa na mtazamo imara wa kiroho na kutokuwa na imani zaidi, nimeonyeshwa, ni kwa sababu wamekunjwa mioyo kwa ufinyu wa ubinafsi/uchoyo. Nabii anazungumza na watunza Sabato, siyo wale wasioamini, bali wale wanaojidai sana kuwa wachamungu. Siyo wingi wa mikutano yako ndiyo ambayo Mungu anaikubali. Siyo idadi kubwa ya maombi, lakini kutenda kwa haki, kufanya jambo sahihi na kwa wakati unaofaa. — **Shuhuda kwa Kanisa 2:36. ChS 40.3**

•

**Tamaa**

Hata hivyo wengine wamekataa kuongoka. Hawakuwa tayari kutembea katika njia ya Mungu, na wakati, ili kazi ya Mungu isonge mbele, miito ilitolewa kwa ajili ya matoleo ya hiari, wengine wakazikumbatia kwa ubinafsi mali zao za duniani hapa. Hawa watu wenye choyo, walijitenga na kundi la waaminio. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:126. ChS 40.2**

**Hakuna Hata Mtu mmoja Kati ya Ishirini Aliye tayari**

Ni tamko zito ninaloliambia kanisa, kwamba hakuna hata mtu mmoja kati ya ishirini ambaye jina lake limeandikwa katika vitabu vya kanisa ambaye yuko tayari kufunga historia yake hapa duniani, akiwa upande wa Bwana, wengi ni wale ambao katika ulimwengu huu, hawana Mungu, wala matumaini mioyoni kama ilivyo kwa mdhambi wa kawaida. Wanajidai kusema wanamtumikia Mungu, lakini wanatumikia kwa dhati na bidii mali. Kazi hii ya moyo ulio nusu-nusu ni kuendelea kumkana Kristo, badala ya kumkiri Kristo. Wengi

wameleta ndani ya kanisa roho yao wenyewe isiyojisalimisha kwa Mungu, isiyosafishwa, isiyolainishwa; ladha yao ya kiroho inapotoshwa na kukosa kwao maadili, mmomonyoko wa tabia, ufisadi unaofedhehesha, unaoonyesha ulimwengu katika roho, moyoni, katika kusudi, wakijithibitisha wenyewe katika tamaa kali za ngono chafu, na wamejaa udanganyifu tele katika maisha yao ndani na nje, huku wakikiri kwa mdomo kuwa ni Wakristo. Wakiishi kama watu wenye dhambi, na huku wakidai kuwa Wakristo! Wale wanaodai kuwa Wakristo na wanamkiri Kristo wanapaswa kutoka miongoni mwao na wasiguse kitu kilicho najisi, na wajitenge.…Naiweka kalamu yangu chini, na kuinua roho yangu kwa maombi, ili Bwana awahuishe kwa pumzi Yake, watu wake walioasi na kurudi nyuma, watu walio kama mifupa mikavu, ili wapate kuishi. Mwisho umekaribia, ukinyemelea kwa siri sana, bila sisi kugundua, bila kelele, kama hatua za mwizi wa usiku zinavyokanyaga taratibu, ili kuwashangaza wale wanaolala bila kukesha au kuwa katika ulinzi na kutokuwa tayari. Hebu Bwana na atujalie kumleta Roho Wake Mtakatifu juu ya mioyo ya watu ambayo sasa imestarehe na kujisau/kujiziuka, ili wasilale tena kama wengine, bali wakeshe na kuwa na kiasi.—**The General Conference Daily Bulletin, Februari 4, 1893 , 132, 133. ChS. 41.2**

**Uamsho na Matengenezo Vinahitajika**

Wakristo wanapaswa kujiandaa kwa yale ambayo yatatokea hivi karibuni katika ulimwengu na kuleta mshangao mkubwa, na maandalizi haya wanapaswa kufanya kwa

kujifunza Neno la Mungu kwa bidii, na kujitahidi kuishi maisha yao kulingana na amri Zake.— **Prophets and Kings, 626 . ChS 41.3**

Uamsho wa utauwa wa kweli miongoni mwetu ndilo hitaji kuu, la dharura na haraka zaidi kati ya mahitaji yetu yote. Kutafuta huu uamsho yapasa iwe kazi yetu ya kwanza.— **The Review and Herald, Machi 22, 1887 . ChS 41.4**

Wakati umefika kwa ajili ya matengenezo kamili kufanyika. Matengenezo haya yanapoanza, roho ya maombi itamwamsha kila muumini na itaondoa katika kanisa roho ya mafarakano na ugomvi. —**Shuhuda kwa Kanisa 8:251. ChS 41.5**

Uamsho na matengenezo lazima vifanyike chini ya huduma ya Roho Mtakatifu. Uamsho na matengenezo ni vitu viwili tofauti. Uamsho unaashiria kufanywa upya kwa maisha ya kiroho, kuhuishwa kwa nguvu za akili na moyo, ufufuo kutoka kwa kifo cha kiroho. Matengenezo yanaashiria kuundwa upya, mabadiliko ya mawazo na nadharia, tabia na mazoea. Matengenezo hayatazaa matunda mema ya haki isipokuwa yameunganishwa na uamsho wa Roho. Uamsho na matengenezo yanapaswa kufanya kazi yake iliyoamriwa, na katika kufanya kazi hii lazima vyote viungane pamoja.— **The Review and Herald, Februari 25, 1902 . ChS 42.2**

Je, Maandiko hayahitaji kazi iliyo safi na takatifu zaidi kuliko ile ambayo bado hatujaona? ... Mungu anawaita wale ambao wako tayari kutawaliwa na Roho Mtakatifu, kuongoza katika kazi ya matengenezo kamili. Ninaona shida na mgogoro mbele y~~etu~~, na Bwana anawaita watenda kazi Wake kuingia kwenye mstari wa utumishi. Kila nafsi sasa inapaswa kusimama katika nafasi ya kujiweka wakfu kwa kina zaidi kwa Mungu kuliko miaka ambayo imepita.... Nimevutiwa sana na matukio ambayo yamepita mbele yangu hivi majuzi katika majira ya usiku. Kulionekana kuwa na vuguvugu kubwa—kazi ya uamsho—iliyosonga mbele katika sehemu nyingi. Watu wetu walikuwa

—

wakienda kwenye mstari pamoja, wakiitikia wito wa Mungu.—**The General Conference Bulletin, Mei 19, 1913 , p. 34. ChS 42.3**

Katika maono ya usiku, maono yalipita mbele yangu ya vuguvugu kubwa la matengenezo kati ya watu wa Mungu. Wengi walikuwa wakimsifu Mungu. Wagonjwa waliponywa, na miujiza mingine ikafanyika. Roho ya maombezi ilionekana, kama ilivyodhihirishwa kabla ya siku kuu ya Pentekoste. Mamia kwa maelfu walionekana wakizitembelea familia na kulifunua mbele yao Neno la Mungu. Mioyo ilisadikishwa na hatia kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, na roho ya uongofu wa kweli ikadhihirishwa. Katika kila upande wa milango kuliwekwa wazi kwa ajili ya kuitangaza Kweli. Dunia ilionekana kuangazwa na mvuto wa mbinguni. Baraka kuu zilipokelewa na watu wa Kweli na wanyenyekevu wa Mungu. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:126. ChS 42.4**

Kuna umuhimu mkubwa wa matengenezo kati ya watu wa Mungu. Hali ya sasa ya kanisa inaleta swali hili: Je! Huu ni uwakilishi sahihi wa Yeye aliyeutoa uhai Wake kwa ajili yetu? — **Shuhuda kwa Kanisa 3:474. ChS 43.1**

—

Wakati aibu za uvivu, uzembe, ulegevu na ugoigoi zitakapokuwa zimetupiliwa mbali kutoka kanisani, Roho wa Bwana atatolewa ukarimu mwingi. Nguvu za mbinguni zitafunuliwa. Kanisa litaona utendaji wa mipango na majaliwa ya Bwana wa majeshi. Nuru ya Ukweli itang'aa katika miale iliyo wazi, miale yenye nguvu, ni kama ilivyokuwa nyakati za mitume, nafsi nyingi zitageuka, na kuachana na upotovu na kuugeukia Ukweli. ulimwengu utaangazwa kwa utukufu wa Bwana. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:46. ChS 43.2**

## Kuchelewa ni Uangamivu

Nilioneshwa watu wa Mungu wakingoja badiliko fulani litokee, - nguvu ya kuwahamasisha kuwa pamoja. Lakini watakatishwa tamaa, kwani wamekosea. Lazima wachukue hatua, lazima washike kazi hiyo wenyewe na kumlilia Mungu kwa dhati bidii ili wapate ujuzi wa Kweli wao wenyewe. Matukio ambayo yanapita mbele yetu yana ukubwa wa kutosha kutufanya tuamke na kuuhimiza Ukweli nyumbani kwa mioyo ya wote watakaosikiliza. Mavuno ya dunia yanakaribia kuiva. —**Shuhuda kwa Kanisa 1:261. 43.3**

Kwa upande mwingine, kuna wengine ambao, badala ya kuboresha kwa hekima fursa zilizopo sasa, wanangoja vipindi au majira fulani ya pekee ya kuburudishwa kiroho ambayo kwayo uwezo wao wa kuelimisha wengine utaongezeka sana. Wanapuuza wajibu na fursa za sasa na kuruhusu nuru yao iangaze kwa kufifia, huku wakitazamia kwa hamu kubwa, wakati ambapo, bila jitihada yoyote kwa upande wao, watafanywa wapokeaji wa baraka za pekee, ambazo kwazo watabadilishwa na kufaa kwa ajili ya utumishi. — **The Acts of the Apostles, 54. 43.4**

—

## Sio wazalishaji bali watumiaji tu

Wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo wako kwenye majaribio mbele ya ulimwengu wa mbinguni; lakini ubaridi wa bidii yao na

—

unyonge wa jitihada zao katika utumishi wa Mungu, huwatia alama kuwa wao sio watu waaminifu. Kama wanachofanya kingekuwa bora zaidi ya kile wangeweza kufanya, hukumu isingekuwa juu yao; lakini mioyo yao ingekuwa imeandikishwa kwenye katika kazi, hakika wangeweza kufanya mengi zaidi. Wanajua, na ulimwengu unajua, kwamba wamepoteza kwa kiwango kikubwa roho ya kujikana nafsi (kujinyima) na kubeba msalaba. Kuna watu wengi ambao wanawapinga au wako dhidi yao (hawawathamini nk), ambao majina yao yataonekana yameandikwa katika vitabu vya mbinguni, sio kama wazalishaji, lakini watumiaji*. Ila wengi wanaolibeba Jina la Kristo, utukufu Wake umetiwa giza, uzuri Wake umefunikwa, na heshima Yake imezuiliwa. Kuna wengi ambao majina yao yako kwenye vitabu vya kanisa, lakini ambao hawako chini ya milki au utawala wa Kristo. Hawa hawatii maagizo Yake au kufanya kazi Yake. Kwa hiyo wako chini ya udhibiti wa adui. Hawafanyi chochote chanya, kwa hivyo wanafanya madhara yasiyoweza kuhesabika (hayana idadi). Kwa sababu ushawishi wao sio harufu ya uhai uendao kuleta uzima, bali harufu ya kifo hadi kifo (*Watumiaji wa Neno la Mungu ila hawazai tunda la Roho!*).— **Christ's Object Lessons, 303, 304 . ChS 43.5**

### Utunzaji wa Amri Limekuwa Joho la Kufunika Dhambi

Hatari hiyo hiyo ipo leo kati ya watu wanaojidai kuwa wao wamepewa dhamana ya kutunza sheria ya Mungu (wahifadhi/watunzaji). Wana tabia ya kujidanganya wenyewe, wakiwa na mtazamo kwamba kushika kwao

—

Amri za Mungu, kutawalinda kutoka katika nguvu ya haki ya Mungu. Wanakataa kukemewa kwa uovu wao, na kuwashtaki watumishi wa Mungu kuwa na usongo sana katika kuiondoa dhambi kwenye kambi. Mungu anayechukia dhambi anawataka watu wote wanaodai kushika sheria Yake wakimbie uovu wote. Kupuuza kutubu na kutii Neno Lake kutaleta matokeo ya kuogofya sana kwa watu wa Mungu leo kama vile dhambi ile ile juu ya Israeli ya kale. Kuna kikomo mbele ambapo Yeye hatachelewesha tena hukumu Zake. — **Shuhuda kwa Kanisa 4:166,167.** **ChS 44.1**

**Wafu Katika Makosa na Dhambi**

Leo hii sehemu kubwa ya wale wanaounda washiriki wetu wamekufa katika makosa na dhambi. Wanakuja na kuondoka kanisani kama mlango kwenye bawaba zake. Kwa miaka mingi wamesikiliza kwa moyo mkunjufu Kweli zile nzito, zenye kukoroga na kuamsha moyo sana, lakini hawajaziweka kwenye utendaji. Hivyo mioyo yao imekuwa sugu kuhusiana na thamani ya Ukweli. Ushuhuda wenye kuchochea wa karipio na maonyo hauwaamshi kutubu. Nyimbo tamu zaidi zinazotoka kwa Mungu kupitia midomo ya mwanadamu-- kuhesabiwa haki kwa imani, na haki ya Kristo--haziibui mwitikio wa upendo na shukrani kutoka kwenye mioyo yao. Ingawa Mtendakazi wa mbinguni anaonyesha mbele yao vito vya thamani zaidi vya imani na upendo, ingawa anawaalika wanunue Kwake "dhahabu iliyosafishwa kwa moto," na mavazi meupe" ili wavikwe, na "dawa ya macho" wapate kuona. Watu hawa wanaweka mioyo yao dhidi Yake, na kushindwa kubadilisha uvuguvugu wao kwa upendo na bidii wakifanya taaluma au usanii tu na huku wakikana nguvu ya utauwa (maisha feki ya Laodikia). Wakiendelea katika hali hii, Mungu atawakataa. Wao wenyewe wanajikosesha stahiki ya kuwa washiriki wa familia Yake. —**Shuhuda kwa Kanisa 4:166,167.** **ChS 44.2**

**Wanadamu Wanaofuata Maadili Mazuri ila sio Wakristo**

—

Wengi wanaojiita Wakristo ni watu wenye maadili mema tu ila siyo Wakristo. Wamekataa karama ambayo ndiyo peke yake tu ingewawezesha kumheshimu Kristo kwa kumwakilisha kwa ulimwengu. Kazi ya Roho Mtakatifu kwao ni kazi ngeni kwao. Wao si watendaji wa Neno. Kanuni za mbinguni zinazotofautisha wale walio wamoja na Kristo na wale walio wamoja na ulimwengu hazitofautishwi bayana. Wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo si watu tena waliojitenga na wa kipekee. Mstari wa mpaka haueleweki. Watu hawa wanajiweka chini ya ulimwengu, kwa mazoea yake, desturi zake, ubinafsi wake. Kanisa limeuendea ulimwenguni katika uvunjaji wa sheria, wakati ulimwengu ulipaswa kuja kwa kanisa kwa utii wa sheria. Kila siku kanisa linageuzwa kuwa ulimwengu.— **Christ's Object Lessons, 315, 316 . ChS 45.1**

**Rekodi Yenye Mawaa**

Wengi wana mfano wa utauwa, majina yao yako kwenye vitabu vya ushirika wa kanisa; ila wana rekodi yenye mawaa mbinguni. Malaika wa kurekodi ameandika kwa uaminifu matendo yao. Kila tendo la ubinafsi, kila neno baya, kila jukumu lisilotekelezwa, na kila dhambi ya siri, na kila aina ya ulaghai na ujanja, imeandikwa kwa

uaminifu katika kitabu cha kumbukumbu kilichohifadhiwa na malaika wa anyerekodi mambo. —
**Shuhuda kwa Kanisa 2:442. ChS 45.2**

## Wabeba Mizigo Wanachoka

Kwa sababu wengine hawakunyanyua mizigo ambayo wangeweza kuiinua, au kufanya kazi ambayo wangeweza kuifanya, kazi hiyo imekuwa nzito kupindukia kwa watu wachache tu, watakaojihusisha nayo. Wanaona mengi ya kufanya nao hufanya kazi zinazozidi nguvu zao na kisha huchoka haraka na miili yao huchakaa. —**Shuhuda kwa Kanisa 2:645. ChS 45.3**

## Wasioweza Kuelezea Imani kwa Akili Bora

Wengi wanaodai kuamini Ukweli wa siku hizi za mwisho watakutwa wamepunguka. Watu hawa wamepuuza mambo mazito. Uongofu wao ni wa juu juu tu, sio wa kina, sio wa bidii, na sio kamili. Hawajui ni kwanini wanaamini Ukweli, wanaamini kwasababu tu wengine wameuamini, na wanauchukulia Ukweli kuwa ni wa kawaida tu. Hawawezi kutoa sababu zinazosugua akili kwa nini wanaamini. Wengi wameruhusu akili zao kujazwa na vitu vyenye umuhimu mdogo, na masilahi yao ya umilele hufanywa kuwa namba mbili. Nafsi zao zimedumaa na kulemaa katika kukua kiroho. Wanadamu wengine hawaangaziwi au kujengwa na uzoefu wao au kwa maarifa ambayo ilikuwa fursa yao na wajibu wao kuyapata. Nguvu na utulivu viko pamoja na wale wanaokiri ile Kweli, kwa mioyo ya dhati/unyofu. —
**Shuhuda kwa Kanisa 2:64 - ChS 45.4**

## Wengine Watafuatilia Gombo la Kinabii

Mungu ana watu duniani ambao kwa imani na tumaini takatifu wanafuatilia Gombo la Maandiko ya unabii yanaotimizwa haraka na wanatafuta kutakasa roho zao kwa kutii Ukweli, ili wasikutwe hawana vazi la arusi wakati Kristo atakapotokea mawinguni. —

Shuhuda kwa Kanisa 4:307. ChS 46.1

## Ndoto Yenye Kuvutia

Katika ndoto niliyopewa Septemba 29, 1886, nilikuwa nikitembea na watu wengi ambao walikuwa wakitafuta matunda ya beri, jamii ya maforosadi nk (berries). Kulikuwa na vijana wengi wa kiume na wa kike katika kikundi ambao wangesaidia katika kukusanya matunda. Tulionekana kuwa katika jiji, kwa kuwa kulikuwa na ardhi ndogo sana isiyokuwa na kitu; lakini kuzunguka jiji hilo kulikuwa na mashamba yaliyo wazi, vichaka vya kupendeza, na bustani zilizolimwa. Gari kubwa lililokuwa limesheheni mahitaji ya kikundi chetu lilitangulia mbele yetu. (chakula na maji ya watendakazi nk). ChS 46.2

Punde gari lilisimama, na watu wakatawanyika kila upande kutafuta matunda. Kulizunguka gari kulikuwa na vichaka virefu na vifupi, vilivyosheheni matunda makubwa, mazuri; lakini vikundi vyote vilikuwav inatazama mbali sana hata hawakuweza kuviona hivi vichaka. Nilianza kukusanya matunda yaliyokuwa karibu, lakini kwa uangalifu sana, kwa kuogopa kuokota matunda ya mabichi, ambayo bado kuiva, na ambayo yalikuwa yamechanganyika na matunda yaliyoiva hivi kwamba niliweza kuchuchuma tunda moja au mawili tu kutoka kwenye kichale cha maberi. ChS 46.3







—

Baadhi ya matunda makubwa mazuri yaliyoiva yalikuwa yameanguka chini, na minyoo na wadudu walikuwa wameyala nusu. “Oh!” nilifikiri, “kama shamba hili lingeingiwa hapo awali na kuvunwa, matunda haya yote ya thamani yangekuwa nayo yamehifadhiwa. Lakini sasa hivi tumechelewa mno sasa. Walakini, nitajaribu kuchagua yale yaliyoanguka ardhini, na nione kama kuna matunda mazuri yoyote yaliyopo na niyaweke kwenye kikapu. Hata ikiwa tunda lote la beri limeharibika, ninaweza kuwaonyesha

—

ndugu kile ambacho wangeweza kukivuna endapo wasingechelewa sana. ChS 46.4

Mara watu wawili au watatu wa kikundi chetu walikuja wakizunguka mahali nilipokuwa kwa taratibu kwa starehe (relax), bila haraka wala juhudi . Walikuwa wakizungumza, na walionekana kutekewa na mazungumzo ya kila mmoja. Waliponiona, walisema, "Tumeangalia kila mahali, na hatujaweza kupata matunda." Wakanitazama kwa mshangao kwa wingi wa maberi niliyokuwa nayo kwenye ndoo yangu. Mimi nikasema, "Kuna matunda mengine mengi zaidi ya kukusanywa kutoka kwenye vichaka hivi." Wakaanza kuokota, lakini mara wakaacha, na kusema, "Si haki sisi kuchagua kuchuma matunda mahali hapa; kwani wewe ndiye uliyepapata mahali hapa kwanza, na matunda haya ni yako." Lakini nilijibu, "Hiyo haijalishi. Ninyi kusanyeni maberi popote pale mnapoweza kupata chochote. Hili ni shamba la Mungu, na haya ndiyo matunda yake; ni fursa yako kuyavuna."." ChS 47.1

Lakini haikuchukua muda na nilionekana kuwa peke yangu tena. Kila baada ya muda kidogo nilisikia watu wakizungumza na kucheka kwenye gari. Niliwaita wale waliokuwa pale, "Mnafanya nini?" Walijibu, "Hatukuweza kupata matunda yoyote, na kwa kuwa tulikuwa tumechoka na njaa, tuliona kwamba tungekuja kwenye gari na kula chakula cha mchana. Tutakapomaliza kupumzika kwa muda, tutatoka tena na kwenda tena." ChS 47.2

"Lakini," nikasema , "hamjaleta matunda yoyote bado. Na mnakula chakula chote, bila kuleta matunda, wala chakula kingine.Mimi siwezi kula sasa; kuna matunda mengi sana ya kuchumwa. Ninyi humkupata matunda, kwa sababu hamkutazama kwa umakini wa kutosha. Matunda hayaning'inii kwa wazi nje ya vichaka; ni lazima myatafute vichakani. Ni kweli, hamuwezi kuyachuma kwa wingi na mkono mmoja ujae kwa mchumo mmoja; lakini kwa kutazama kwa uangalifu kati ya matunda ya kijani kibichi yasiyoiva na yale yaliyoiva, kisha mtapata matunda mazuri sana." ChS 47.3

Haikuchukua

—

muda na ndoo yangu ndogo ikawa imejaa maberi, na nikayapeleka kwenye gari. Nikasema, haya ndiyo matunda mazuri kuliko yote niliyopata n a kuchuma, na nimeyachuma hapa karibu, wakati ninyi mmejichosha kwa kutafuta matunda ya mbali bila mafanikio. **ChS 47.4**

Kisha wote walikuja kuona matunda yangu. Wakasema, "Haya ni maberi ya vichaka vya juu, yamekomaa vizuri na si malaini kama yale yanayokaribia kuoza. Hatukufikiri kwamba tungeweza kupata chochote kwenye vichaka virefu, kwa hiyo tulitafuta kwenye matunda ya miti midogo tu, na tukapata haya maberi machache tu." **ChS 47.5**

Kisha nikasema, "Je, mnaweza kutunza haya maberi, kisha mwende nami kutafuta matunda mengi zaidi kwenye vichaka virefu?" Lakini hawakuwa wamejitayarisha kushugulikia matunda hayo. Kulikuwa na sahani na magunia yaliyozagaa kwa wingi, lakini vyombo hivi vilikuwa vimetumika kuwekewa chakula. Nilichoka kusubiri, na hatimaye nikauliza, "Je, hamkuja kuvuna matunda? Kwa nini hamko tayari kuyashugulikia matunda haya basi?" **ChS 47.6**

Mmoja wao alijibu, "Dada White, hatukutarajia kupata matunda yoyote mahali palipokuwa na nyumba nyingi, na mambo mengi yaliyokuwa yakiendelea; lakini kwa vile wewe ulionekana kuwa na hamu ya kukusanya matunda, basi nasi tuliamua kuja pamoja nawe. Tulifikiri kwamba tungeleta chakula cha kutosha, na tungefurahia burudani ya piknik hiyo, ikiwa hatungekusanya matunda yoyote." **ChS 48.1**

Nilijibu, "Sielewi aina hii ya kazi. Nitakwenda kwenye vichaka tena mara moja. Mchana tayari ulikuwa umesogea sana, hivi karibuni usiku utakuja hapa, nasi hatutaweza kukusanya matunda." Wengine walienda nami, lakini wengine walibaki kwenye gari kula" **ChS 48.2**

—

Katika sehemu moja, kundi dogo kilikuwa kimekusanyika, na walikuwa wakizungumza kwa usongo juu ya jambo ambalo walionekana kupendezwa nalo. Nilisogea karibu na kukuta kwamba mtoto mdogo aliyekuwa amebebwa na mwanamke mmoja alikuwa amewavutia. Nikasema kwao, "Mna muda mchache tu, fanyeni kazi kwa ubora zaidi pale mnapoweza." **ChS 48.3**

Umakini wa wengi ulivutiwa na

kijana mmoja na mwanadada waliokuwa wakikimbia mbio za mashindano kuelekea kwenye gari. Walipolifikia gari walikuwa wamechoka sana, hata ikabidi wakae chini na kujipumzisha. Wengine pia walikuwa wamejitupa chini kwenye nyasi na kupumzika. Wengine pia walikuwa wamepumzika hapo kwenye nyasi **ChS 48.4**

Hivyo ndivyo siku ilivyoendelea na kwisha, na kidogo sana kutimizwa. Mwishowe nilisema, “Ndugu, mngeuita huu msafara wa kutokuwa na mafanikio. Ikiwa hivi ndivyo mnavyofanya kazi, mimi sishangai na ukosefu wenu wa mafanikio. Kufanikiwa kwenu au kutofaulu kwenu kunategemea jinsi mnavyoshikilia kazi. Kuna matunda hapa; kwa maana mimi nimeyapata. Baadhi yenu mmekuwa mkisaka matunda kwenye matawi ya chini bure, wengine mmepata maberi machache; lakini vichaka virefu vimepitwa, kwa sababu tu humkutarajia kupata matunda ndani yake. Mnaona matunda niliyokusanya kuwa ni makubwa na yameiva vizuri. Baada ya muda kidogo matunda mengine yataiva, na tunaweza kwenda kuchuma matunda kwenye matawi hayo ya juu tena. Hii ndiyo njia ambayo nilifundishwa kuvuna matunda. Ikiwa mngetafuta matunda karibu na gari, mngeweza kupata matunda kama mimi. **ChS 48.5**

"Somo ambalo unalo leo umewapa wale ambao ndiyo kwanza tu, wanaanza kufanya kazi ya aina hii, na wataliiga. Bwana ameweka vichaka hivi vizaavyo matunda katikati ya maeneo haya yenye watu walioshonana, na anatazamia utawapata na waingie katika ile Kweli. Lakini mmekuwa mkijishughulisha sana katika kula, na kujifurahisha wenyewe. Hamkuja shambani mkiwa na dhamira ya dhati ya kutafuta na kuyapata matunda.**ChS 48.6**

Ni lazima mfanye kazi baada ya hapa kwa dhati, usongo na bidii zaidi, na kwa mtazamo na malengo tofauti kabisa, au kazi yenu haitafanikiwa kamwe. Kwa kufanya kazi kwa njia ifaayo, mtawafundisha watendakazi wachanga kwamba mambo ya kula, matumbuizo na tafrija si ya maana sana. Imekuwa kazi ngumu kuleta gari lenye vifaa, nyenzo na chakula hapa, lakini

—

Ninyi mmefikiria zaidi juu ya vitu hivi mlivyovileta na gari kuliko matunda ambayo mnapaswa kuyabeba nyumbani kama matokeo ya kazi yenu. Mnapaswa kuwa na bidii, kwanza kwa kuyachuma matunda yaliyo karibu nanyi, na kisha mtafute yale yaliyo mbali zaidi; baada ya hapo mnaweza kurudi na kufanya kazi karibu tena, na hivyo mtafanikiwa.” — **Gospel Workers, 136-139 . ChS 49.1**

—

## Mtihani Utakaotolewa

Katika kazi adhimu ya mwisho kabisa ni watu wachache wakuu na wenye vyeo tu ndiyo watashiriki. Hawa wanajitosheleza wenyewe, ni watu wasiomtegemea Mungu, na Yeye hawezi kuwatumia. Bwana ana watumishi waaminifu, ambao wakati wa kupepetwa na pepeto, wakati wa kujaribiwa watafunuliwa wazi kuwatazama. Kuna watu wa thamani wasiompigia magoti Baali ambao kwa sasa wamefichwa. Hawa hawakuwa na nuru ambayo imekuwa ikiwaangazia ninyi kwa moto uliokolea. Lakini inaweza kuwa chini ya uso mkali na usiovutia, mwangaza safi wa tabia halisi ya Kikristo utafunuliwa. Wakati wa mchana tunaangalia kuelekea mbinguni lakini hatuoni nyota. Nyota zipo angani, zimeshikiliwa angani, lakini jicho haliwezi kuzitofautisha. Usiku tunaona mng'ao wao halisi. **49.1**

Wakati hauko mbali sana ambapo kila nafsi itajaribiwa. Chapa ya mnyama itashurutishwa juu yetu. Wale ambao wamejisalimisha hatua kwa hatua katika matakwa ya ulimwengu na kuzifuatisha desturi za ulimwengu hawataona kuwa ni jambo gumu kujisalimisha chini ya mamlaka yatakayokuwepo, kuliko kujiweka katika dhihaka, matusi, vitisho vya kutupwa gerezani, na kifo. Pambano hili ni kati ya amri za Mungu na amri za wanadamu. Katika kipindi hiki dhahabu itatenganishwa na uchafu katika kanisa. Utauwa wa Kweli utatofautishwa wazi kutoka katika mwonekano wa je na ubatili wake. Nyota nyingi ambazo tumezipendeza kwa mng'aro wake zitazima. Makapi kama wingu yatachukuliwa na upepo, hata kutoka mahali ambapo kwa sasa tunaona kuna wingi wa ngano nzuri. Wote wanaojifanya mapambo ya Patakatifu, lakini hawajavaa haki ya Kristo, wataonekana katika aibu ya uchi wao wenyewe. — **Shuhuda kwa Kanisa 5:80,81. ChS 49.2**

# SURA YA 4 HALI ZA ULIMWENGU ZINAZOMKABILI MTENDAKAZI WA KIKRISTO.

## Onesho la Kiulimwengu

Ulimwengu ni ukumbi wa maonesho; wahusika, wakazi wake,

wanajiandaa kuigiza sehemu zao katika onesho kuu la mwisho. Miongoni mwa umati mkubwa wa wanadamu hakuna umoja, isipokuwa pale watu wanapoungana pamoja ili kutimiliza makusudi yao yenye ubinafsi. Mungu anaangalia. Makusudi Yake kuhusu raia waasi yatatimizwa. Ulimwengu haujawekwa mikononi mwa wanadamu, ingawa Mungu ameruhusu matukio makuu ya mwisho kwenye onesho hii kuyumbayumba na kupindishwa kwa kipindi tu - Nguvu kutoka chini inafanya kazi ili kuleta matukio makubwa kwenye drama hii (onyesho hili)- Shetani akija kama Kristo, na kufanya kazi kwa udanganyifu wote wa udhalimu ndani ya wale ambao wanajifunga pamoja katika mashirika ya siri (secret societies). Wale ambao wanaosalimu amri kwa mapenzi makali ya kuwa kwenye shirikisho, wanatekeleza mipango ya adui. Sababu itafuatiwa na athari/matokeo. — **Shuhuda kwa Kanisa 8:27,28. ChS 50.1**

## Igizo la Mwisho Kwenye Drama

Kamwe ujumbe huu haukutumika kwa nguvu kubwa kuliko unavyotumika leo. Ulimwengu unabatilisha madai ya Mungu zaidi na zaidi. Watu wamekuwa hodari katika makosa. Uovu wa wakazi wa ulimwengu karibu ujaze kipimo cha uovu wao. Dunia hii imekaribia kufika mahali ambapo Mungu atamruhusu mharibu ajifanyie mapenzi yake mwenyewe. Kuingizwa kwa sheria za wanadamu katika sheria ya Mungu, kuinuliwa, kwa mamlaka ya kianadamu, ya siku ya Jumapili kuwa mbadala wa Sabato ya Biblia, ni tukio la mwisho katika mchezo huu wa kuigiza (drama). Wakati uingizwaji huu wa mbadala utakapokuwa wa ulimwengu wote, Mungu atajifunua. Atatokea kwa utukufu kuitikisa sana dunia. Atatoka katika kiti Chakeili kuwaadhibu wakazi wa ulimwengu kwa uovu wao, na nchi itadhihirisha damu yake na haitawafunika tena wale waliouawa. — **Shuhuda kwa Kanisa 7:141.ChS 50.2**

## Zahama ya Vizazi Vyote

*Ujumbe wa Mungu kwa wakazi wa dunia leo ni "Ninyi nanyi*

—

*jiwekeni tayari; kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja.” **Mathayo 24:44.** Hali zilizoenea katika jamii, na hasa katika miji mikubwa ya mataifa, zinatangaza kwa sauti ya radi kwamba saa ya hukumu ya Mungu imefika na kwamba mwisho wa vitu vyote vya kidunia umekaribia.* Tunasimama katika kilele cha zahama ya vizazi vyote. Kwa mfuatano wa haraka hukumu za Mungu zitakuja moja baada ya nyingine -moto na mafuriko, na tetemeko la ardhi na vita na umwagaji wa damu. Hatupaswi kushangazwa wakati huu wa matukio ambayo ni makubwa na yaliyoamuliwa wazi; kwani Malaika wa rehema hawezi kukaa muda mrefu zaidi kuwalinda wale wenye mioyo migumu-wasiotubu. — **Prophets and Kings, 278. ChS 51.1**

Zahama inanyemelea taratibu mbele zetu hatua kwa hatua kwa kwa uhakika na ukimya. Jua huangaza mbinguni, likipita juu ya mduara wake wa kawaida, na mbingu bado zinatangaza utukufu wa Mungu. Watu bado wanakula na kunywa, wanapanda mbegu na kujenga, wanaoa na kuolewa. Wafanyabiashara bado wananunua na kuuza. Wanaume wanashindana wao kwa wao, wakipigania nafasi ya juu zaidi. Wapenzi wa ansa starehe bado wanasongamana kwenye kumbi za sinema, mbio za farasi, kuzimu za kamari. Msisimko wa hali ya juu zaidi unatawala, lakini saa ya rehema inaisha haraka, na kila kesi iko karibu kuamuliwa milele. Shetani anaona kwamba wakati wake ni mfupi. Ameweka mawakala wake wote kazini ili watu wapate kudanganywa, kuamini kisicho kweli, kuwa na pilikapilika nyingi, kupumbazwa, mpaka kipindi cha majaribio kiishe na mlango wa ufungwe milele.— **The Southern Watchman, Oktoba 3, 1905 . ChS 51.2**

Uasi umekaribia kufikia kikomo chake. Machafuko yanaujaza ulimwengu, na hofu kuu itawajia wanadamu hivi karibuni. Mwisho umekaribia sana. Sisi ambao tunaoujua Ukweli tunapaswa kujiandaa kwa ajili ya kile kitakachopasuka ulimwenguni na kuleta mshtuko mkubwa wa kulemea na kushangaza watu.— **Shuhuda kwa Kanisa 8:28.** ChS 51.3

—

Katika wakati huu wa uovu ulioenea tunaweza kujua kwamba zahama kuu yaa mwisho imekaribia. Wakati uasi wa sheria ya Mungu unapokuwa karibu ulimwenguni pote, watu

Wake wanapoonewa na kuteswa na wanadamu wenzao, Bwana ataingilia kati.—
**Christ's Object Lessons, p . ChS 51.4**

Tunasimama katika kilele cha cha matukio makubwa na mazito. Unabii unatimia. Historia ya ngeni na ya ajabu, yenye matukio mengi inarekodiwa katika vitabu vya mbinguni. Kila kitu katika ulimwengu wetu kiko katika msukosuko. Kuna vita na matetesi/uvumi wa vita. Mataifa yanakasirikiana, na wakati wa wafu umefika ili wahukumiwe. Matukio yanabadilika ili kuleta siku ya Mungu, ambayo inafanya haraka sana. Ni muda mfupi tu wa wakati, kama ilivyokuwa, bado unabakia. Lakini wakati tayari taifa linainuka dhidi ya taifa, na ufalme dhidi ya ufalme, hakuna sasa ushirikiano wa jumla. Bado zile pepo nne zimeshikiliwa hadi watumishi wa Mungu watiwe muhuri katika vipaji vya nyuso zao. Ndipo mamlaka za dunia zitapanga majeshi yao kwa vita kuu vya mwisho. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:14.** ChS 51.5

**Roho wa Mungu Mwenye Kuzuia Akiondolewa**

Roho wa Mungu azuiaye hata sasa anaondolewa katika ulimwengu. Vimbunga, dhoruba, tufani, moto na mafuriko, majanga ya baharini na nchi kavu, hufuatana kwa haraka. Sayansi inatafuta kueleza haya yote. Ishara zinazozidi kutuzunguka, zikielezea kukaribia kwa Mwana wa Mungu, zinahusishwa na kitu kingine chochote isipokuwa kwa sababu ya kweli. Watu hawawezi kutambua malaika walinzi wanaozuia pepo nne ambazo hazitavuma hadi watumishi wa Mungu wawe wametiwa muhuri; lakini Mungu atakapo waamuru malaika Wake wazifungue pepo, kutakuwa na tukio la ugomvi ambalo hakuna kalamu inayoweza kulielezea. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:408.** ChS 52.1

Siku tunazoishi ni za adhimu na muhimu. Roho wa Mungu taratibu, na hatua kwa hatua lakini kwa hakika anaondolewa duniani. Mapigo na hukumu za Mungu tayari zinawaangukia watu wanaodharau neema ya Mungu. Majanga juu ya nchi kavu na bahari, hali ya jamii kukosa utulivu, tetesi za vita, na matukio

—

ya kutisha, hushangaza. Huonesha zahama ya matukio makubwa yanayokaribia kwa ukubwa. Mawakala wa uovu wanaunganisha nguvu zao na kujizatiti. Wanajiimarisha kwa zahama kuu ya mwisho. Mabadiliko makubwa hivi karibuni yatatokea katika ulimwengu wetu, na harakati za mwisho zitakuwa za kasi sana. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:11**.ChS 52.2

Muda umekaribia ambapo kutakuwa na huzuni ulimwenguni ambayo hakuna zeri ya binadamu inaweza kuiponya. Roho wa Mungu anaondolewa. Maafa baharini na katika nchi kavu hufuatana kwa mfululizo kwa haraka. Ni mara ngapi tunasikia kuhusu matetemeko ya ardhi na vimbunga, kuhusu uharibifu kwa moto na mafuriko, na hasara kubwa ya maisha na mali! Inavyoonekena majanga haya ni milipuko inayokengeuka nguvu za asili ambazo hazina mpangilio, ambazo hazithibitiki, ambazo ziko juu kabisa ya uwezo wa mwanadamu kuweza kutawala, nazo zinakuja kwa ghafla; lakini katika hizo zote, kusudi la Mungu linaweza kusomeka. Hayo ni miongoni mwa mawakala ambao Yeye huwatumia kutaka kuwaamsha wanaume na wanawake kuona hali yao ya hatari. —**Prophets and Kings, 277.**
ChS 52.3

—

**Dunia Hospitali ya Magonjwa ya Maambukizo (Pesthouse-Kolera, ndui, ebola, TB, Corona nk)**

Watu katika upofu wao hujivunia maendeleo ya ajabu na kuelimika au kuwa na mwanganza; lakini walinzi wa mbinguni wanaiona dunia imejaa uharibifu/ufisadi na vurugu. Kwa sababu ya dhambi, anga ya dunia yetu imekuwa kama anga la hospitali yenye magonjwa yenye maambukizo-yanayoletwa na wadudu wa maambukizo. **—Shuhuda Kwa Kanisa 6:10, 11.**

**Janga la Uharibifu**

Tunaishi katikati ya "janga la uhalifu," ambalo watu wenye akli mahiri za kufikiri, wale wanaomcha Mungu kila mahali hushangaa. Ufisadi uliopo, uko nje ya uwezo wa kalamu ya binadamu kuuelezea. Kila siku huleta mafunuo mapya wa ugomvi wa kisiasa, hongo, wizi, uongo na ulaghai. Kila siku huleta rekodi yake mpya yenye kuhuzunisha moyo ya vurugu na uasi wa sheria, na siasa ya kutojali mateso ya wanadamu, ya uharibifu wa kikatili na kutojali maisha ya mwanadamu. Kila siku inashuhudia kuongezeka kwa wazimu, mauaji, na kujiua. Ni nani awezaye kutilia shaka kwamba mawakala wa kishetani wanafanya kazi miongoni mwa wanadamu kwa utendaji/shughuli inayoongezeka ya kuvuruga na kupotosha akili, na kuchafua na kuharibu mwili?— **The Ministry of Healing, 142, 143 . ChS 53.2**

Roho ya machafuko, na ya kutotaka kusimamiwa au kuongozwa inaenea katika mataifa yote, na milipuko ambayo mara kwa mara huibua hofu ya ulimwengu ni dalili tu za mioto ya hasira na uasi wa sheria, na tamaa ambazo, ikiwa zimekwepa kudhibitiwa, zitaijaza dunia ole na ukiwa. Picha ambayo uvuvio umetoa ya ulimwengu wa kabla ya gharika, inawakilisha kwa kweli hali ambayo jamii ya kisasa inaharakisha kufikia. Hata sasa, katika karne hii, na katika nchi zinazodai kuwa za Kikristo, kuna uhalifu unaotendwa kila siku, mbaya na wa kutisha kama ule ambao wenye dhambi wa ulimwengu wa kale waliangamizwa. Kabla ya gharika, Mungu alimtuma Nuhu

—

kuuonya ulimwengu, ili watu waweze kuongozwa kwenye toba, na hivyo kuepuka uharibifu uliokuwa ukitishia. Wakati wa kutokea kwa Kristo mara ya pili unapokaribia, Bwana anatuma watumishi Wake na maonyo kwa ulimwengu ili kujitayarisha kwa tukio hilo kuu. Watu wengi wamekuwa wakiishi katika uvunjaji wa sheria ya Mungu, na sasa Yeye kwa rehema anawaita kutii kanuni Zake takatifu. Wote ambao wataondoa dhambi zao kwa kutubu kwa Mungu na imani katika Kristo, wanapewa msamaha.. —**Patriarchs and Prophets, 102. ChS 53.3**

Hali ya mambo katika ulimwengu inaonyesha kwamba nyakati za taabu ziko mbele yetu. Magazeti ya kila siku yamejaa dalili za migogoro mibaya katika siku za usoni. Ujambazi wa wazi na ujasiri mwingi, hutokea mara kwa mara. Migomo ni ya kawaida. Wizi na mauaji hufanywa kila upande. Watu waliopagawa na pepo wanachukua uhai wa wanaume, wanawake, na watoto wadogo. Watu wamependezwa na uovu na kuwa na mawazo ya kufikirika kuhusu uovu, na kila aina ya uovu hutawala. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:11.ChS 54.1**

## Mdanganyifu Mkuu Kazini

Wakati huu, wakati mwisho wa vitu vyote vya kidunia unakaribia upesi, Shetani anajitahidi kwa bidii nyingi kuunasa ulimwengu. Anapanga mipango mingi ya kushikilia akili, na kugeuza fikira kutoka kwenye Kweli zilizo muhimu kwa wokovu. Katika kila mji

mawakala wake wanajishughulisha sana katika kuwapanga katika vikundi wale wanaoipinga sheria ya Mungu. Mdanganyifu mkuu yuko kazini kuanzisha vipengele vya uharibifu na uasi, na watu wanachemka kwa juhudi katika Mungu lakini si katika maarifa (Warumi 10:2).— **Matendo ya Mitume, 219 . ChS 54.2**

Shetani ni mwanafunzi wa Biblia mwenye bidii. Anajua kuwa wakati wake ni mfupi, na anatafuta kila namna kukabiliana na kazi ya Bwana juu ya dunia hii. **—Shuhuda Kwa Kanisa 9:16. ChS 54.3**

Shetani sasa anatafuta kuwashikilia watu wa Mungu katika hali ya kutofanya kazi, kuwazuia wasitekeleze sehemu yao katika kueneza Ukweli, ili mwishowe wapimwe katika mizani na kuonekana wamepungua (kuanguka kiroho). **—Shuhuda Kwa Kanisa 1:260. ChS 54.4**

### Ulimwengu Ukichochewa na Roho ya Vita

Ulimwengu unachochewa na roho ya vita. Unabii wa Danieli sura ya kumi na moja karibu unafikia utimilifu wake kamili. Hivi karibuni matukio ya taabu yaliyosemwa katika unabii yatatokea. —**Shuhuda Kwa Kanisa 9:14. ChS 54.5**

Nilioneshwa wakazi wa dunia wakiwa katika kuchaganyikiwa kukubwa. Vita, umwagaji wa damu, ufukara, uhitaji, njaa, na tauni vilitapakaa nchi yote. *Wakati mambo haya yakiwazingira watu wa Mungu, walianza kujongeleana pamoja, na kutupilia mbali shida zao ndogo. Hali ya kujijali wenyewe haikuwatawala tena; na badala yake unyenyekevu wa kina ulichukua nafasi yake. Mateso, kuchanganyikiwa, na ufukara vilisababisha akili kuanza tena kukaa kwenye kiti chake cha enzi, na yule mtu mwenye shauku na asiye na busara akapata tena akili timamu, na akafanya kwa busara na hekima.* Usikivu wangu ulivutwa utoke kwenye eneo la tukio. Kulionekana kuwa na wakati mdogo wa amani. Kwa mara nyingine tena wakazi wa dunia waliwasilishwa mbele yangu; na kwa mara nyingine kila kitu kilikuwa katika machafuko makubwa. Mizozo, vita, na umwagaji damu, na njaa na tauni,

—

vilikuwa vimejaa kila mahali. Mataifa mengine yalikuwa yakishiriki katika vita hivi na machafuko. Vita vilisababisha njaa. Uhitaji/umasikini na umwagaji damu vilisababisha tauni. Na ndipo mioyo ya wanadamu wakivunjia mioyo kwa hofu (Luka 21:26), "na kwa kutazamia mambo yatakayoupata ulimwengu." **— Shuhuda kwa Kanisa 1:268. ChS 55.1**

•

## Giza la Kiroho

Huu ni wakati wa giza la kiroho katika makanisa ya ulimwengu. Kutokujua mambo ya Bwana kumemficha Mungu na Ukweli usionekane. Nguvu za uovu zinajikusanyika kwa nguvu. Shetani huwasifu watendakazi wenzake kwamba atafanya kazi ambayo itauteka ulimwengu. Wakati usingizi umelijia kanisa, Shetani na majeshi yake wako macho. Makanisa yanayodai kuwa ya Kikristo hayauongoi ulimwengu; kwani wao wenyewe wamepotoshwa na ubinafsi na kiburi, na wanahitaji kuhisi nguvu ya Mungu inayoongoa miongoni mwao kabla ya kuwaongoza wengine kwenye kiwango safi au cha juu zaidi. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:65.**

**ChS 55.2**

Katika wakati wetu, kama ule wa zamani, Kweli muhimu za Neno la Mungu zimewekwa kando ya nadharia na mawazo ya wanadamu. Watu wengi wanaodai kuwa watumishi wa Mungu hawaikubali Biblia nzima kuwa ni Neno lililovuviwa. Mtu mmoja kwa hekima yake anakataa sehemu moja, na mwingine anahoji juu ya sehemu nyingine. Wanaweka hukumu na maamuzi yao kuwa ndiyo yenye mamlaka kuliko Neno. Na maandiko wanayoyafundisha yanakuwa na mamlaka juu yao wenyewe. Uhalisi wake wa Kiungu unaharibiwa. Hivyo mbegu za ukafiri hupandwa; kwa maana watu huchanganyikiwa, na hawajui la kuamini. Kuna imani nyingi kiasi na akili haina haki kutumbuiza mambo kama haya. —**Christ's Object Lessons, 39. ChS 55.2**

—

Uovu unafikia kilele ambacho hakijawahi kufikiwa, na bado watumishi wengi wa injili wanalia, “amani na usalama.” Lakini wajumbe waaminifu wa Mungu wanapaswa kusonga mbele kwa kasi na kazi yao. Wakiwa wamevikwa silaha za kimbingu, wanapaswa kusonga mbele bila woga na kwa ushindi, kamwe wasiache vita vyao mpaka kila nafsi iliyo ndani ya ufikiaji wao iwe imepokea ujumbe wa Ukweli wa wakati huu. — **The Acts of the Apostles, 220. ChS 55.3**

Kuna sababu ya kuwa na tahadhari katika hali ya ulimwengu wa kidini leo. Rehema ya Mungu imepuuzwa. Wengi wanabatilisha sheria ya Yehova, “Wanafundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.” **Mathayo 15:9** Ukafiri umeshamiri katika makanisa mengi katika nchi yetu; si ukafiri katika maana yake pana zaidi, yaani kuikataa Biblia waziwazi, lakini ukafiri ambao umevishwa vazi la Ukristo, wakati huohuo ukidhoofisha kidogo-kidogo imani katika Biblia kama ufunuo kutoka kwa Mungu. Uchaji wa dhati na utauwa wa kweli umetowekana badala yake kuna desturi tu isiyokuwa na maana. Matokeo yake, ukengeufu na ufisadi hutawala. Kristo alitangaza, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ... ndivyo itakavyokuwa katika siku atakapofunuliwa Mwana wa Adamu.” Rekodi ya kila siku ya matukio yanayopita inashuhudia utimizwaji wa maneno Yake. Ulimwengu kwa haraka unaiva kwa ajili ya kuangamizwa. Hivi karibuni hukumu za Mungu zitamwagwa, na dhambi na wenye dhambi wataangamizwa. **—Patriarchs and Prophets, 166. ChS 56.1**

## Kuitenganisha Ngano Kwenye Magugu

Wakati wa hukumu za Mungu za uharibifu ni wakati wa rehema kwa wale ambao hawakuwa na nafasi ya kujifunza ni nini iliyo Kweli. Bwana atawatazama kwa huruma nyororo-upole Moyo Wake wa rehema umeguswa; Mkono Wake bado umenyooshwa

ili kuokoa, wakati mlango ukiwa umefungwa kwa wale ambao hawakutaka kuingia. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:97. ChS 56.2**

Hivi karibuni pambano kali litainuka dhidi ya wale wanaomtumikia Mungu na wale wasiomtumikia. Hivi karibuni kila kitu kinachoweza kupepetwa kitapepetwa, ili vile yasivyoweza kupepetwa vibaki. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:15, 16. ChS 56.3**

Katika nyakati za dhiki na kuchanganyikiwa kwa mataifa kutakuwa na wengi ambao

hawakujitoa kikamilifu kwa mivuto potofu ya ulimwengu na kazi za Shetani, ambao watajinyenyekeza kwa Mungu na kumrejea Yeye kwa mioyo yao yote na kupata ukubali na msamaha. **—Shuhuda kwa Kanisa 1:269. ChS 55.4**

Kuna wengi wanaosoma Maandiko ambao hawawezi kuelewa maana yake ya Kweli. Ulimwenguni kote wanaume na wanawake wanatazama mbinguni kwa matamanio makubwa. Maombi na machozi na maswali hupanda juu kutoka kwa roho zinazotamani nuru, neema, na Roho Mtakatifu. Wengi wako kwenye ukingo wa ufalme, wakingoja tu kukusanywa.— **Matendo ya Mitume, ukurasa wa 109 . ChS 57.1**

## Masomo Kutoka kwa Uzoefu wa Eliya

Kutokana na uzoefu wa Eliya katika siku hizo za kukatishwa tamaa kulikoonekana kuwa ni kushindwa dhahiri, kina masomo mengi yanayopaswa kuchukuliwa,—masomo yenye thamani sana kwa watumishi wa Mungu katika zama hizi, yanayotambulishwa na mkengeuko wa jumla kutoka katika uadilifu. Uasi ulioenea leo ni sawa na ule ambao katika siku za nabii ulienea Israeli. Katika kumwinua mwanadamu juu ya Mungu, katika kuwasifu viongozi mashuhuri, katika ibada ya fedha, na katika kuyaweka mafundisho ya sayansi juu ya Ukweli wa ufunuo, watu wengi leo wanamfuata Baali. Mashaka na kutoamini yanatenda kwa ushawishi wao mbaya juu ya akili na moyo, na wengi wanazifanya nadharia za wanadamu kuchukua nafasi ya Mausia ya Mungu. Inafundishwa hadharani kwamba tumefikia wakati ambapo mawazo ya kibinadamu yanapaswa kuinuliwa juu ya mafundisho ya Neno la Mungu na Sheria Yake. Sheria ya Mungu ambayo ni kiwango cha Kiungu cha haki, inatangazwa kuwa haina maana. Adui wa Ukweli wote anafanya kazi kwa nguvu za udanganyifu kuwafanya wanaume na wanawake waweke taasisi za kibinadamu mahali ambapo Mungu anapaswa kuwa, na kusahau yale yaliyowekwa kwa ajili ya furaha na wokovu wa wanadamu. Walakini uasi huu, ulioenea kama ulivyokuja kuwa, sio wa ulimwengu wote. Si wote duniani ni waasi na wenye

—

dhambi; sio wote wamechukua upande wa adui. Mungu ana maelfu mengi ambao hawajapiga goti kwa Baali, wengi wanaotamani kuelewa kikamilifu zaidi kuhusu Kristo na sheria, wengi ambao wanaendelea kutarajia ingawa matumaini hayapo kwamba Yesu atakuja hivi karibuni kukomesha utawala wa dhambi na kifo. Na kuna watu wengi ambao wamekuwa wakimwabudu Baali bila kujua, lakini Roho wa Mungu angali anafanya kazi pamoja nao. — **Prophets and Kings, 170, 171.**
**ChS 57.2**

## SURA YA 5 KANISA KITUO CHA MAFUNZO

### Hitaji la Saa Hii

Kinachohitajika sasa kwa ajili ya ujenzi wa makanisa yetu ni kazi nzuri ya watenda kazi wenye busara ili kutambua na kukuza talanta katika kanisa, talanta ambazo zinaweza kuelimishwa kwa ajili ya kutumiwa na Bwana. Kuwe na mpango uliopangwa vizuri wa kuwaajiri watendakazi kwenda katika makanisa yetu yote, wakubwa kwa wadogo, kuwaelekeza washiriki jinsi ya kufanya kazi kwa ajili ya kulijenga kanisa na pia kwa ajili ya wale wasioamini. Ni mafunzo, na elimu, ambavyo vinahitajika. Wale wanaofanya kazi katika kutembelea makanisa wanapaswa kuwapatia ndugu na akina dada mafundisho katika njia za vitendo za kufanya kazi ya umishenari. **—Shuhuda Kwa Kanisa 9:117. ChS 58.1**

Mungu anatarajia kanisa Lake kuadabisha na kuwafanya washiriki wake kufaa kwa kazi ya kuangazia ulimwengu. Elimu inapaswa kutolewa, hilo lingetokeza kuwapa mamia ambao wangetoa kwa wabadilishanaji talanta zenye thamani. Kwa kutumia talanta hizi, watu wangekuzwa ambao wangetayarishwa kujaza nafasi za uaminifu na ushawishi, na kudumisha kanuni safi, zisizoharibika. Hivyo basi mambo makuu yaliyo mema/mazuri yangetimizwa kwa ajili ya Mwalimu. **—Shuhuda Kwa Kanisa 6:431, 432. ChS 58.2**

Kila mfanyakazi anapaswa kuwa na uelewa mzuri wenye ufanisi. Halafu kwa hali ya juu na pana anaweza kuwasilisha Ukweli kama ulivyo katika Yesu. **— Shuhuda Kwa Kanisa 7:70. ChS 58.3**

Haipaswi kuwa na uchelewesho katika juhudi hii iliyopangwa vizuri ya kuwaelimisha washiriki wa kanisa. **— Shuhuda Kwa Kanisa 9:119. ChS 58.4**

Msaada mkubwa zaidi ambao unaweza kutolewa kwa watu wetu ni kuwafundisha kufanya kazi kwa ajili ya Mungu, na kumtegemea Yeye, na sio wachungaji..— **Shuhuda Kwa Kanisa 7:19. ChS 58.5**

—

Ni dhahiri kwamba mahubiri yote ambayo yamehubiriwa hayajakuza tabaka kubwa la watenda kazi wanaojikana nafsi zao. Somo hili linapaswa kuzingatiwa kuwa linahusisha matokeo makubwa na mazito zaidi. Mustakabali wetu wa umilele uko hatarini. Makanisa yananyauka kwa sababu yameshindwa kutumia talanta zao katika kueneza nuru. Mafundisho makini yanapaswa kutolewa ambayo yatakuwa kama somo kutoka kwa Bwana, ili wote waweze kutumia nuru yao kwa vitendo. — **Shuhuda Kwa Kanisa 6:431. ChS 58.6**

Watu wamekuwa na mahubiri mengi sana; lakini je, wamefundishwa jinsi ya kufanya kazi kwa ajili ya wale ambao Kristo alikufa kwa ajili yao? Je, mstari wa kazi umebuniwa na kuwekwa mbele yao kwa namna ambayo kila mmoja ameona ulazima wa kushiriki katika kazi hiyo? — **Shuhuda Kwa Kanisa 6:431. ChS 59.1**

Ni kwa njia ya elimu na mazoezi kwamba ndio watu wawe na sifa za kukidhi dharura yoyote inayoweza kujitokeza; na mipango ya busara inahitajika ili kumweka kila mmoja katika sehemu yake sahihi, ili aweze kupata uzoefu ambao utamfaa kubeba

jukumu/kuwajibika. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:221. ChS 59.2**

## Mtaala wa Umishenari wa Kanisa

Wengi wangekuwa tayari kufanya kazi ikiwa wangefundishwa jinsi ya kuanza. Wanahitaji kufundishwa na kutiwa moyo. Kila kanisa linapaswa kuwa shule ya mafunzo kwa watenda kazi Wakristo. Washiriki wake wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuendesha darasa la usomaji wa Biblia (Bible class, Bible Reading), jinsi ya kuendesha na kufundisha madarasa ya shule ya Sabato, jinsi bora ya kuwasaidia maskini na kutunza wagonjwa, jinsi ya kufanya kazi kwa ajili ya watu wasioongoka. Kunapaswa kuwa na shule za afya, shule za upishi, na madarasa katika safu mbalimbali za kazi ya usaidizi wa Kikristo. Haipaswi kuwa na ufundishaji tu, bali kazi halisi chini ya waalimu wenye uzoefu. Hebu walimu waongoze njia katika kufanya kazi kati ya watu, na wengine, wakiungana nao, watajifunza kutokana na mfano wao. Mfano mmoja una thamani zaidi kuliko maagizo mengi.— **The Ministry of Healing, 149 . ChS 59.3**

## Mafunzo Maalumu

Juhudi kubwa zaidi zinapaswa kuwekwa kuwaelimisha watu katika kanuni za matengenezo ya afya. Shule za upishi zinapaswa kuanzishwa, na mafundisho ya nyumba kwa nyumba yatolewe katika sanaa wa kupika chakula bora. Wazee na vijana wanapaswa kujifunza jinsi ya kupika kwa urahisi zaidi. Popote ukweli unapowasilishwa, watu wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuandaa chakula kwa njia rahisi, lakini kwa namna iletayo ladha nzuri. Wanapaswa kuonyeshwa kwamba lishe bora inaweza kutolewa bila kuwa na matumizi ya vyakula vya nyama (vegeterian au mbogamboga). —**Shuhuda Kwa Kanisa 9:161. ChS 59.4**

Katika kila mahali palipo na kanisa, mafundisho yanapaswa kutolewa kuhusiana na utayarishaji wa vyakula rahisi, vyema, kwa ajili ya matumizi ya wale wanaotaka kuishi kulingana na kanuni za afya. Na washiriki wa kanisa wanapaswa kuwapa watu kwenye ujirani wao, nuru wanayopokea kuhusu somo hili.— **Gospel Workers, p. 362 . ChS 60.1**

—

## Kuendana na Maelekezo

Ni watenda kazi wangapi wenye manufaa na wenye kuheshimika katika kazi ya Mungu wamepata mafunzo katikati ya majukumu ya unyenyekevu ya nyadhifa za chini sana maishani! Musa ndiye aliyekuwa mtawala mtarajiwa wa Misri, lakini Mungu hangeweza kumchukua kutoka katika ikulu ya mfalme ili kufanya kazi aliyomteua. Ni pale tu alipokuwa amekaa kwa miaka arobaini kama mchungaji mwaminifu ndipo alipotumwa kuwa mkombozi wa watu wake. Gideoni alichukuliwa kutoka kwenye uwanja wa kupuria na kuwa chombo mikononi mwa Mungu kwa ajili ya kuwakomboa majeshi ya Israeli. Elisha aliitwa kuacha jembe na kufanya agizo la Mungu. Amosi alikuwa mkulima, mkulima wa udongo, Wakati Mungu alipompa ujumbe wa kutangaza. Wote wanaokuwa watendakazi wenza pamoja na Kristo watakuwa na kazi ngumu sana, isiyo ya kawaida kuifanya, na masomo yao ya mafundisho yanapaswa kuchaguliwa kwa hekima, na yenye kuendana na sifa zao za kipekee za tabia, na kazi wanayopaswa kushiriki.— **Gospel Workers. 332, 333 . ChS 60.2**

## Jukumu la Kutoa Mafunzo

Wakati watu wenye mafanikio na uwezo walipoongoka, kama ilivyokuwa kwa Timotheo, Paulo na Barnaba walitafuta kwa bidii kuwaonyesha ulazima wa kufanya kazi katika shamba la mizabibu. Na mitume walipoondoka kwenda mahali pengine, imani ya watu hawa haikupunguka au kufeli, bali iliongezeka. Walikuwa wamefundishwa kwa uaminifu katika njia ya Bwana, na walikuwa wamefundishwa jinsi ya kufanya kazi bila ubinafsi, kwa dhati, kwa bidii, kwa uvumilivu wa kudumu kwa ajili ya wokovu wa wanadamu wenzao. Mafunzo haya makini ya waongofu wapya yalikuwa jambo muhimu katika mafanikio ya ajabu ambayo waliyafanya Paulo na Barnaba walipokuwa wakihubiri injili katika nchi za kipagani.— **The Acts of the Apostles, 186, 187 . ChS 60.3**

Makanisa yanapoanzishwa, inapaswa kuwekwa mbele yao kwamba hata kutoka miongoni mwao ni lazima watu wachukuliwe ili kupeleka Ukweli kwa wengine na kuinua makanisa mapya; kwa hiyo ni lazima wote wafanye kazi, na kusitawisha kwa ukamilifu kwa kadari iwezekanavyo, talanta ambazo Mungu amewapa, na kuwazoeza akili zao kushiriki katika utumishi wa Bwana wao. **— Shuhuda kwa Kanisa Church 3:205. ChS 61.1**

Shughuli za umishenari huumbuka kila mara kwa kukosa watenda kazi wenye mawazo sahihi,—wafanyakazi walio na upendo na uchaji Mungu ambao utawakilisha imani yetu kwa usahihi. Kuna wengi ambao wanaopaswa kuwa wamishenari, lakini hawaingii kamwe shambani kwa sababu wale waliounganishwa nao katika nyanja ya kanisa au katika vyuo vyetu hawahisi mzigo wa kufanya kazi pamoja nao, ili kufungua mbele yao madai ya Mungu juu ya uwezo Wake wote, na hawaombi pamoja nao na kwa ajili yao.— **Counsels to the Parents, Teachers and Students, 500, 501 . ChS 61.2**

Wale walio na uangalizi wa kiroho wa kanisa wanapaswa kubuni mbinu na njia ambazo kwazo nafasi zinaweza kutolewa kwa kila

—

mshiriki wa kanisa kutenda sehemu fulani katika kazi ya Mungu. Mara nyingi sana siku za nyuma hili limekuwa halifanyiki. Mipango haijawekwa wazi na kutekelezwa kikamilifu ambapo karama za wote zinaweza kuingizwa katika utendaji wa huduma. Ni wachache tu wanaotambua ni upotevu gani unaotokana na hili. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:116. ChS 61.3**

Katika kila kanisa washiriki wanapaswa kufundishwa ili watoe muda wa kuleta roho kwa Kristo. Inawezaje kusemwa juu ya kanisa, "Ninyi ni nuru ya ulimwengu," pasipo washiriki wa kanisa kuwa wanatoa nuru? Hebu wale ambao wanasimamia kundi la Kristo waamke kwa wajibu wao na kuandaa roho nyingi kufanya kazi. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:436.ChS 61.4**

## Chagua Maofisa Wenye Sifa za Kutoa Mafunzo

Uangalifu mkubwa unapaswa kutekelezwa katika kuchagua maafisa wa makanisa mapya. Hebu na wawe wanaume na wanawake walioongoka kabisa. Hebu wachaguliwe watu wanaostahili zaidi kufundisha, wale wanaoweza kuhudumu kwa Neno na kwa vitendo. Kuna hitaji la kina la kufanya kazi katika kila mstari. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:85. ChS 61.5**

—

Wazee na wale walio na nafasi za kuongoza kanisani wanapaswa kufikiria zaidi mipango yao ya kuendesha kazi. Wanapaswa kupanga mambo ili kila mshiriki wa kanisa awe na sehemu ya kutenda, ili kwamba asiwepo yeyote awezaye kuishi maisha yasiyo na malengo, bali kwamba wote watimize wawezavyo kulingana na uwezo wao mbalimbali.... Ni muhimu sana kwamba elimu kama hiyo itolewe kwa washiriki wa kanisa ili kwamba waweze kuwa watenda kazi wasio na ubinafsi, waliojitolea, na wafanisi kwa ajili ya Mungu; na ni kupitia njia hiyo pekee ndipo kanisa linaweza kuepushwa na kutozaa matunda na a kufa Hebu kila mshiriki wa kanisa awe mtenda kazi,—jiwe lililo hai, likitoa nuru katika hekalu la Mungu.— **The Review and Herald, Septemba 2, 1890 . ChS 62.1**

## Washiriki wa Kanisa Kujielimisha Wenyewe

Washiriki wa kanisa lazima wafanye kazi; lazima wajielimishe wenyewe, wakijitahidi kufikia kiwango cha juu kilichowekwa mbele yao. Jambo hili Bwana atawasaidia kukifikia kama watashirikiana Naye. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:140.**

Hatupaswi kuruhusu kupoteza hata fursa moja ya kujipatia stahiki kiakili ili kumtumikia Mungu.— **Christ's Object Lessons, p. 334 . ChS 62.3**

## Kiwango cha Kimungu

Bwana anatamani sisi tupate elimu yote iwezekanayo, kwa lengo la kutoa maarifa yetu kwa wengine. Hakuna anayeweza kujua ni wapi au jinsi gani wanaweza kuitwa kufanya kazi au kusema kwa niaba ya Mungu. Baba yetu wa mbinguni pekee ndiye anayeona kile anachoweza kumfanya mwanadamu awe. Kuna uwezekano mbele yetu ambao imani yetu dhaifu haitambui. Akili zetu zapaswa kuzoezwa ili kwamba ikibidi tuweze kuwasilisha Kweli za Neno Lake mbele ya mamlaka kuu za kidunia kwa njia ya kutukuza Jina Lake.— **Christ's Object Lessons, 333, 334 . ChS 62.4**

Ni nani wamekuwa wakijitayarisha kwenda kufanya kazi katika shamba Lake la mizabibu? Mungu hapendezwi na wasio na uzoefu.

—

Anataka tutumie kwa njia iliyo bora zaidi na ya juu zaidi iwezekanayo, talanta ambazo Ametupa.— **The Review and Herald, Aprili 2, 1889 . ChS 62.5**

**Kielelezo**

Nikawa nimeota kwamba mtu alinileteа jora la kitambaa cheupe, na akaniambia nishone nguo kwa watu wa viwango vyote na ufafanuzi wa kila tabia na hali za maisha mbali mbali. Niliambiwa nivikate na kuvitundika vyote ili viwe tayari wakati wake utakapofika kuvishona. Nilikuwa na mawazo kwamba wengi ambao nilihitajika kuwashonea nguo hawakustahili. Nikauliza ikiwa hicho kilikuwa kipande cha mwisho cha nguo nilichopaswa kushona, na nikaambiwa kwamba sivyo; kwamba mara tu ninapomaliza hiki, kulikuwa na vingine vya kuvifanyia kazi. **ChS 63.1**

Nilihisi kukatishwa tamaa na kiwango cha kazi iliyokuwa mbele yangu, na nikasema kwamba nilikuwa nimehusika katika kushona nguo kwa wengine kwa zaidi ya miaka ishirini, na kazi yangu haikuthaminiwa, na wala

sikuona kwamba kazi yangu ilikuwa imetimiza mazuri mengi. Nilizungumza na mtu aliyeniletea kitambaa, cha mwanamke mmoja haswa, ambaye alikuwa ameniambia nimshonee nguo yake. Nilisema kuwa hataithamini, na kwamba itakuwa ni kupoteza muda kumpatia kitambaa yeye. Alikuwa maskini sana, mwenye akili duni, fukara, asiye nadhifu na mchafu kwa tabia, na punde ataishia kuichafua tu hiyo nguo. Mtu huyo akajibu: "Shona nguo. Huo ni wajibu wako. Hasara sio yako, bali ni yangu. Mungu haoni kama vile mtu anavyoona. Yeye Anaweka wazi kazi ambayo angependa kuifanya, na haujui ni ipi itakayofanikiwa, hii au ile. Itashangaza kwamba roho nyingi kama hizo maskini zitaingia katika ufalme, wakati wengine, ambao wamependelewa na baraka zote za maisha, wakiwa na akili nzuri na mazingira mazuri, wakipewa fursa zote za kuwa bora zaidi, wataachwa nje. — **Shuhuda kwa Kanisa 2:10, 11. ChS 63.2**

Kwa muda wa saa nyingi, askari huandaliwa kwa zoezi la kubeba mizigo yao wao wenyewe kwenye shanta zao (begi la mgongoni), na kuiiweka kwa haraka tena juu ya mtu. Wanafundishwa zoezi la kuweka/panga mikono yao, na jinsi ya kuishusha kwa haraka. Wanapewa mazoezi ya kukabiliana dhidi ya adui, na wamefunzwa katika kila aina ya mbinu. Hivyo zoezi linaendelea, kuwandaa watu kwa dharura yoyote. Na je, wale wanaopigana vita kwa ajili ya Emmanuel Mkuu wasiwe na bidii na umakini mkubwa katika kujitayarisha kwa ajili ya vita vya kiroho? — **Gospel Workers, 75 . ChS 63.3**

—

**SURA YA 6**

# WANAFUNZI KUFANYA KAZI YA KIMISHENARI WAKIWA KWENYE MAFUNZO

## Kusudi la Elimu

Elimu ya kweli ni mafunzo ya kimishenari. Kila mwana na binti wa Mungu anaitwa kuwa mmishenari; tunaitwa kumtumikia Mungu na wanadamu wenzetu; na ili kutufaa kwa huduma hii inapaswa kuwa lengo la elimu yetu.— **The Ministry of Healing, p. 395 . ChS 64.1**

Ni kuwatia nguvu/kuwaimarisha vijana dhidi ya vishawishi vya adui kwamba tumeanzisha shule ambapo wanaweza kustahili kupata manufaa katika maisha haya na kwa ajili ya utumishi wa Mungu milele.—**The Counsels to Parents, Teachers and Students, 495 . ChS 64.2**

Anayejitahidi kupata maarifa ili afanye kazi kwa ajili ya wajinga na wanaoangamia, anatenda sehemu yake katika kutimiza kusudi kuu la Mungu kwa wanadamu. Katika

utumishi usio na ubinafsi kwa ajili ya baraka za wengine anafikia kiwango cha juu kabisa cha elimu ya Kikristo.— **The Counsels to Parents, Teachers, and Students, 545 . ChS 64.3**

Bwana anawaita vijana wa kiume na wa kike wenye nguvu, waliojitoa wakfu, wenye kujitoa dhabihu, ambao watasonga mbele, na ambao, baada ya muda mfupi wa kukaa shuleni, watatoka wakiwa tayari kutoa ujumbe kwa ulimwengu.— **The Counsels to Parents, Teachers and Students, 549 . ChS 64.4**

**Kujifunza kwa Kutenda**

Ni muhimu kwa elimu yao kamili kwamba wanafunzi wapewe muda wa kufanya kazi ya umisionari—wakati wa kufahamiana na mahitaji ya kiroho ya familia katika jumuiya inayowazunguka. Hawapaswi kulemewa na masomo yaliyosheheni, kiasi kwamba hawana muda wa kutumia ujuzi walioupata. Wapaswa kutiwa moyo kufanya jitihada ya umishenari yenye bidii kwa ajili ya wale walio katika makosa, kujuana nao, na kuwapelekea Ukweli. Kwa kufanya kazi kwa unyenyekevu, kutafuta hekima kutoka kwa Kristo, kusali na kukesha kwenye sala, wanaweza kuwapa wengine ujuzi ambao umeboresha maisha yao.**— The Counsels to Parents, Teachers and Students, 5545, 546. ChS 64.**

Popote inapowezekana wanafunzi wanapaswa kusonga mbele mwaka wa shule unapoendelea, kushiriki katika kazi ya misheni ya jiji. Wanapaswa kufanya kazi ya umishenari katika miji na vijiji vinavyowazunguka. Wanaweza kujipanga wenyewe katika vikundi vya kufanya kazi ya usaidizi ya Kikristo. Wanafunzi wanapaswa kuwa na maoni mapana kuhusu wajibu wao wa sasa kwa Mungu. Hawapaswi kutazamia kwa hamu wakati muhula wa unaisha na shule kufungwa, kwamba ndiyo watafanya kazi fulani kubwa kwa ajili ya Mungu, bali wanapaswa kujifunza jinsi, wakati wa maisha yao ya uanafunzi, watie nira pamoja na Kristo katika utumishi usio na ubinafsi kwa ajili ya wengine.— **The Counsels to Parents, Teachers and Students, 547. ChS 65.1**

Haitoshi kujaza akili za vijana na masomo yenye umuhimu

—

mkubwa; lazima wajifunze kutoa kile ambacho wamepokea.— **The Counsels to Parents, Teachers and Students, 545. ChS 65.2**

Kutoka katika vyuo vyetu na shule za mafunzo wamishenari wapaswa kutumwa nchi za mbali. Wakiwa shuleni, hebu wanafunzi waboreshe kila fursa ili kujitayarisha kwa ajili ya kazi hii. Hapa wanapaswa kujaribiwa na kuthibitishwa, ili ionekane jinsi kuendana kwao na majukumu kulivyo, na kama wana mshiko unaopaswa na mbingu, juu.— **The Counsels to Parents, Teachers and Students, 549. ChS 65.3**

**Himiza Roho ya Umishenari**

Walimu na wanafunzi katika shule zetu wanahitaji mguso wa Bwana. Mungu anaweza kufanya mengi zaidi kwa ajili yao kuliko ambavyo amefanya, kwa sababu zamani njia

Yake ilikuwa imezuiliwa. Roho ya umishenari ikitiwa moyo, hata ikichukua saa kadhaa kutoka kwa programu ya mafunzo ya kawaida, baraka nyingi za Mbingu zitatolewa, mradi tu kutakuwa na imani zaidi na bidii ya kiroho, zaidi ya ufahamu wa yale ambayo Mungu atafanya.— **The Counsels to Parents, Teachers and Students, 546. ChS 65.4**

## Shule Inapofunga

Shule inapofunga, kuna fursa kwa wengi kwenda shambani kama wahubiri wa wainjilisti wa vitabu. Muuzaji mwaminifu wa machapisho ya injili, anaingia katika nyumba nyingi, ambako anaacha habari za kusoma zenye Kweli za wakati huu. Wanafunzi wetu wanapaswa kujifunza jinsi ya kuuza vitabu vyetu. Kuna haja ya watu wenye uzoefu wa kina wa Kikristo, watu wenye akili timamu, watu wenye nguvu, waliosoma vizuri, kushiriki katika tawi hili la kazi. Wengine wana talanta, elimu, na uzoefu ambao ungewawezesha kuwaelimisha vijana kwa ajili ya kazi ya kutembelea watu kwa njia ambayo mengi zaidi yangetimizwa kuliko yanayofanywa sasa. Wale walio na uzoefu huo wana wajibu wa kipekee wa kufanya katika kufundisha wengine. — **The Counsels to Parents, Teachers and Students, 546, 547, . ChS 65.5**

## Huduma ya Wimbo



Wanafunzi ambao wamejifunza kuimba nyimbo tamu za injili kwa melodi na kutofautisha maneno kwa uwazi, wanaweza kufanya mengi mazuri kama waimbaji wainjilisti. Watapata fursa nyingi za kutumia talanta ambayo Mungu amewapa katika kubeba nyimbo na kuangaza katika sehemu nyingi za upweke zilizotiwa giza na huzuni na taabu, wakiwaimbia wale ambao ni mara chache tu ndiyo wana upendeleo wa kuwa kanisani. **ChS 66.1**

Wanafunzi, Tokeni nje mwende barabarani na mipakani penye

vichochoro. mjitahidi kufikia tabaka la juu na la chini. Ingia katika nyumba za matajiri na maskini, na unapopata nafasi, uliza, “Je, ungependa kuwa na sisi kuimba baadhi ya nyimbo za injili?” Kisha mioyo inapolainika, njia inaweza kufunguka kwako kutoa maneno machache ya maombi kwa ajili ya baraka za Mungu. Si wengi watakataa kusikiliza. Huduma hiyo ni kazi ya umisionari ya dhati na yenye moyo ulio safi.— **The Counsels to Parents, Teachers and Students, 547, 548. ChS 66.2**

## SURA YA 7 —USHIRIKIANO WA WACHUNGAJI NA WALEI

### Kwa Umoja Ingia Eneo la Huduma

Hebu wahudumu na washiriki waende kwenye mashamba (maeneo) yanayoiva. Watapata mavuno yao popote pale wanapotangaza kweli zilizosahaulika za Biblia. Watapata wale ambao watakubali Ukweli, na ambao watajitolea katika maisha yao kuleta roho kwa Kristo.— Australasian Signs of the Times, Agosti 3, 1903 **( The Review and Herald, Julai 14, 1903 ). ChS 67.1**

Sio kusudi la Bwana kwamba wachungaji waachwe wafanye sehemu kubwa zaidi ya kazi ya kupanda mbegu za Ukweli. Watu ambao hawajaitwa kwenye huduma ya kichungaji wanapaswa kuhamashwa/kuhimizwa kufanya kazi ya Bwana kulingana na uwezo wao. Mamia ya wanaume na wanawake waliokaa kizembe bila ya kitu cha kufanya sasa, wangeweza kufanya huduma inayokubalika. Kwa kubeba Ukweli ndani ya nyumba za marafiki na majirani zao, wangeweza kufanya kazi kubwa kwa Bwana..—**Shuhuda kwa Kanisa 7:21. ChS 67.2**

Mungu amewapa watumishi Wake ujumbe wa Kweli wa kutangaza. Haya makanisa yanapaswa kupokea na kwa kila njia iwezekanayo kuwasiliana, na kukamata miale ya kwanza ya nuru na kuisambaza..—**Shuhuda kwa Kanisa 6:425. ChS 67.3**

Watu lazima wainue pale mchungaji anapoinua, hivyo kuunga mkono juhudi zake na kumsaidia kubeba mizigo yake, na hapo hatakuwa na kazi nyingi zilizopitiliza na kukata tamaa. Hakuna ushawishi uwezao kuletwa juu ya kanisa litakalodumu isipokuwa watu wasogee kwa akili, kutoka kwa kanuni, kufanya yote wawezayo ili kuendeleza kazi hiyo.— **The Review and Herald, Agosti 23, 1881 . ChS 67.4**

**Muunganiko unaoshawishi**

Ulimwengu utashawishika, sio kwa kile kinachofundishwa katika mimbari, bali kile kanisa linaishi kwacho. Mchungaji mimbarani hutangaza nadharia ya injili; uchaji wa vitendo wa kanisa huonyesha kwa vitendo nguvu yake. —**Shuhuda kwa Kanisa 7:16. ChS 67.5**

Kazi ya Mungu katika dunia hii haiwezi kumalizika hadi wanaume na wanawake wanaojumuisha washiriki wetu wa kanisa wakusanyike kwa kazi, na kuunganisha juhudi zao na zile za wahudumu na maofisa wa kanisa.— **Gospel Workers, 352 . ChS 68.1**

Kuhubiri ni sehemu ndogo ya kazi inayofanyika kwa wokovu wa roho. Roho wa Mungu huwasadikisha wenye dhambi Ukweli, na huwaweka mikononi mwa kanisa. Wachungaji wanaweza kufanya

—

sehemu yao, lakini hawawezi kamwe kufanya kazi ambayo kanisa linapaswa kufanya. — **Shuhuda kwa Kanisa 4:69**. **ChS 68.2**

Usambazaji wa Kweli ya Mungu haifungwi tu kwa wachungaji wachache waliowekwa wakfu. Ukweli unapaswa kutawanywa na wote wanaodai kuwa wanafunzi wa Kristo. Ni lazima upandwe kando ya maji yote.— **The Review and Herald, Agosti 22, 1899** . **ChS 68.3**

Wachungaji wanaweza kuhubiri hotuba za kuvutia na za kulazimisha, na kazi nyingi inaweza kufanywa ili kulijenga na kulifanya kanisa kustawi; lakini ikiwa washiriki wake binafsi watafanya sehemu yao kama watumishi wa Yesu Kristo, kanisa litakuwa gizani na bila nguvu. Katika ulimwengu mgumu na ulio gizani kama huu tulionao, ushawishi wa mfano ulio thabiti utakuwa nguvu ya wema. —**Shuhuda kwa Kanisa 4:285, 286**. **ChS 68.4**

**Kosa la Kufisha**

Ni kosa baya sana kudhani kwamba kazi ya kuokoa roho inategemea huduma pekee. Muumini mnyenyekevu, aliyejiweka wakfu ambaye juu yake Bwana wa shamba la

mizabibu amemwekea mzigo wa roho, anapaswa kutiwa moyo na watu ambao Bwana ameweka juu yao majukumu makubwa zaidi. Wale wanaosimama kama viongozi katika kanisa la Mungu wanapaswa kutambua kwamba agizo la Mwokozi limetolewa kwa wote wanaoamini katika Jina Lake. Mungu atatuma katika shamba Lake la mizabibu wengi ambao hawajawekwa wakfu kwa ajili ya huduma kwa njia ya kuwekewa mikono.— **The Acts of the AApostles, p. 110 . ChS 68.5**

Wazo la kwamba mchungaji lazima abebe mizigo yote na kufanya kazi yote ni kosa kubwa. Akiwa amefanya kazi kupita kiasi na kuishiwa nguvu, anaweza kwenda kaburini, wakati, kama mzigo ungeshirikishwa kama Bwana alivyopanga, angaliishi. Ili mzigo huo usambazwe, elimu lazima itolewe kwa kanisa na wale wanaoweza kuwafundisha watenda kazi kumfuata Kristo na kufanya kazi kama alivyofanya kazi. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:435. ChS 68.6**

Mchungaji hapaswi kuhisi kuwa ni wajibu wake kufanya mazungumzo yote na kazi zote na maombi yote; anapaswa kuelimisha wasaidizi katika kila kanisa. Hebu watu mbalimbali wabadilishane katika kuongoza mikusanyiko/mikutano, na katika kuongoza usomaji wa Biblia au darasa la Biblia; kwa kufanya hivyo watakuwa wanazitendea kazi talanta ambazo Mungu amewapa, na wakati huohuo watakuwa wakipokea mafunzo kama watenda kazi.— **Gospel Workers, 197 . ChS 69.1**

Wachungaji hawapaswi kufanya kazi ambayo ni ya kanisa, hivyo kujichosha, na kuwazuia wengine kutekeleza wajibu wao. Wanapaswa kuwafundisha washiriki jinsi ya kufanya kazi katika kanisa na katika jumuiya.— **Historical Sketches, p. 291 . ChS 69.2**

Jitihada inapofanywa ili kuwasilisha imani yetu kwa watu wasioamini, washiriki wa kanisa mara nyingi sana husimama nyuma, kana kwamba wao sio washiriki wanaopendezwa, na kuacha mzigo wote uwe juu ya mchungaji. Kwa sababu hii kazi ya wachungaji wetu wenye uwezo sana nyakati fulani imekuwa

—

na matokeo yenye mafanikio kidogo.— Gospel Workers, p. 196 . ChS 69.3

### Wajibu wa Mchungaji

“Msaada bora zaidi ambao viongozi wanaweza kuwapatia washiriki wa makanisa yetu si kuhubiri, bali kupanga kazi kwa ajili yao. Mpe kila mmoja kitu cha kufanya kwa ajili ya wengine. Wasaidie wote kuona hilo kama wapokeaji wa neema ya Kristo wako chini ya wajibu wa kumfanyia kazi. Na wote wafundishwe jinsi ya kufanya kazi. Haswa wale walio wapya katika imani waelimishwe kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. — **Shuhuda kwa Kanisa 9:82. ChS 69.4**

Wachungaji, hubirini Kweli zitakazopelekea utendaji binafsi kwa wale walio nje ya Kristo. Himiza juhudi binafsi kwa kila namna iwezekanayo. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:124. ChS 69.5**

Hebu wachungaji wawafundishe washiriki wa kanisa kwamba ili kukua kiroho, ni lazima wabebe mzigo ambao Bwana ameweka juu yao,—mzigo wa kuongoza roho

kwenye Ukweli. Wale ambao hawatimizi wajibu wao watembelewe, waombewe, washughulikiwe. Msiwaongoze watu wawategemee ninyi kama wachungaji; wafundishe badala yake kwamba wanapaswa kutumia talanta zao katika kutoa Ukweli kwa wale walio karibu nao. Katika kufanya kazi hivyo watakuwa na ushirikiano wa malaika wa mbinguni, na watapata uzoefu ambao utaongeza imani yao, na kuwapa mshikamano wenye nguvu na Mungu.— **Gospel Workers, 200 . ChS 69.6**

Katika kufanya kazi mahali ambapo tayari kuna baadhi walio katika imani, mchungaji kwa mara ya kwanza hapaswi kutaka sana kuwaongoa wasioamini, bali kuwazoeza washiriki wa kanisa kwa ajili ya ushirikiano unaokubalika. Hebu afanye kazi kwa ajili yao binafsi, akijitahidi kuwaamsha kutafuta uzoefu wa ndani zaidi wao wenyewe, na kufanya kazi kwa ajili ya wengine. Wanapotayarishwa kumtegemeza mchungaji kwa sala na utendaji wao, mafanikio makubwa zaidi yatakuja kwa jitihada zake.— **Gospel Workers, 196 . ChS 70.1**

Katika baadhi ya mambo mchungaji anashikilia nafasi sawa na ile ya msimamizi wa kundi la wafanyakazi wa kazi au nahodha wa wafanyakazi wa meli. Wanatarajiwa kuona kwamba watu waliowekwa juu yao, wanafanya kazi waliyopewa kwa usahihi na mara moja, na katika kesi ya dharura tu ndio watekeleze kwa undani. Mmiliki wa karakana kubwa aliwahi kumkuta msimamizi wake katika gurudumu ambalo lilitumika kama injini kwa wakati, alikuwa hapo akifanya matengenezo rahisi, huku wafanyakazi nusu dazeni (6) kwenye kibarua hicho, wakiwa wamesimama kando bila kazi na wakitazama kivivu. Mmiliki, baada ya kujua ukweli wa kile kilichokuwa kinaendelea, ili kuhakikisha kuwa hakuna dhuluma iliyofanywa, alimwita msimamizi ofisini kwake na kumpa malipo yake kamili na karatasi la maandishi ya kumwachisha kazi. Kwa mshangao msimamizi akaomba ufafanuzi. Maelezo yalitolewa kwa maneno haya: “Nilikuajiri wewe kuhakikisha unawafanya watu hawa sita kufanya kazi. Nilipata watu sita wamekaa kivivu bila kazi, na wewe

—

ukifanya kazi ya mmoja wao tu. Kazi yako ingeweza kufanywa vyema na yeyote kati ya watu hao sita. Sina uwezo wa kulipa mishahara saba ili tu uwafundishe hao sita jinsi ya kukaa kivivu bila kazi.” **ChS 70.2**

Tukio hili linaweza kutumika katika hali zingine, na kwa zingine sio. Lakini wachungaji wengi hushindwa kwa kutojua jinsi gani, au kwa kutojaribu, kupata washiriki kamili wa kanisa wanaoshiriki kikamilifu katika idara mbalimbali za kazi ya kanisa. Ikiwa wachungaji wangezingatia zaidi kupata na kutunza kundi lao kuwa lenye bidii kazini, wangetimiza mema zaidi, wangepata wakati mwingi zaidi wa kujifunza na kutembelea mambo ya kidini, na pia waepuke visababishi vingi vya msuguano.— **Gospel Workers, 197, 198 . ChS 70.3**

**Mfano Mzuri**

Mtume [Paulo] alihisi kwamba aliwajibika kwa kadiri kubwa kwa ajili ya hali njema ya kiroho ya wale walioongoka chini ya kazi yake ngumu. Shauku yake kwao ilikuwa kwamba waongezeke katika ujuzi wa Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo, aliyemtuma. Mara nyingi katika huduma yake alikutana na makundi madogo ya

wanaume na wanawake waliompenda Yesu, na kupiga magoti pamoja nao katika sala, akimwomba Mungu awafundishe jinsi ya kudumisha uhusiano ulio hai Naye. *Mara nyingi alishauriana pamoja nao kuhusu mbinu bora za kuwapa wengine nuru ya ukweli wa injili* . Na mara nyingi, alipotengwa na wale ambao alikuwa amejitaabisha hivyo kwa ajili yao, alimsihi Mungu awaepushe na uovu, na kuwasaidia wawe wamishenari hodari, wenye bidii.— **The Acts of the Apostles, p. 262 . ChS 71.1**

**SURA YA 8— KUUNGANISHA JUHUDI ZA KIKRISTO**

Muda ni mfupi, na juhudi zetu lazima ziunganishwe ili kufanya kazi kubwa zaidi. —
**Shuhuda kwa Kanisa 9:27. ChS 71.2**

Uundaji wa makundi madogo madogo kama msingi wa juhudi za Kikristo umewasilishwa kwangu na Yule ambaye hawezi kukosea kamwe. —**Shuhuda kwa Kanisa 7:21, 22. ChS 72.1**

Katika makanisa yetu hebu makundi yaundwe kwa ajili ya huduma. Hebu watu tofauti waungane katika kazi kama wavuvi wa watu. Hebu watafute kukusanya roho kutoka katika uharibifu wa ulimwengu kwenda kwenye usafi wa kuokoa wa upendo wa Kristo.—Shuhuda kwa Kristo 7:21. **ChS 72.2**

Na kuwe na katika kila kanisa, vikundi vya watenda kazi vilivyopangwa vizuri kufanya
kazi katika ujirani wa kanisa hilo.— **The Review and Herald, Septemba 29, 1891 . ChS 72.3**

Katika kila mji kunapaswa kuwa na kikosi cha watenda kazi waliopangwa na wenye nidhamu; si kimoja au viwili tu, bali utendaji wa kila mmoja unapaswa kutekelezwa.— **The General Conference Daily Bulletin, Januari 30, 1893 , 37. ChS 72.4**

Kanisa la Kristo duniani lilipangwa kwa madhumuni ya kimisionari, na Bwana anatamani kuona kanisa zima likibuni njia na mbinu ambazo kwazo wakubwa na wa chini, matajiri na maskini, wapate kusikia ujumbe wa Ukweli. Sio wote wameitwa

kufanya kazi ya kibinafsi katika nyanja za kigeni, lakini wote wanaweza kufanya kitu kwa sala zao na karama zao kusaidia kazi ya umisionari. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:29. ChS 72.5**

Ikiwa kuna idadi kubwa ya watu kanisani, hebu washiriki wapangwe katika makundi madogo madogo, kufanya kazi sio tu kwa ajili ya washiriki wa kanisa, bali kwa ajili ya wasioamini. Ikiwa katika sehemu moja wapo wawili tu au watatu ambao wanaujua Ukweli, hebu wajiunge katika kikundi cha watenda kazi. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:22.ChS 72.6**

Ikiwa nidhamu na utaratibu ni muhimu kwa kila mafanikio kwenye uwanja wa vita, ndivyo hivyo hivyo vinavyohitajika zaidi katika vita ambavyo tunahusika ndani yake kwani kitu kitakachopatikana ni cha thamani kubwa na kimeinuliwa zaidi katika tabia, zaidi kuliko yale ambayo vikosi vya wapinzani vinashindana nayo katika uwanja wa vita.

Katika mzozo tunaohusika nao, masilahi ya milele yako hatarini. —**Shuhuda kwa Kanisa 1:649. ChS 72.7**

Mungu ni Mungu wa utaratibu. Kila kitu kilichounganishwa na mbingu kiko katika mpangilio kamili; utii na nidhamu kamili huashiria mienendo ya jeshi la malaika. Mafanikio yanaweza tu kutendendeka kwa utaratibu na hatua ya usawa. Mungu anahitaji utaratibu na mfumo katika kazi Yake sasa sawa na siku za Israeli. Wote wanaofanya kazi kwa ajili Yake wanapaswa kufanya kazi kwa akili, si kwa njia ya ovyo na ya kubahatisha. Angetaka kazi Yake ifanywe kwa imani na usahihi, ili atie muhuri wa kibali Chake juu yake.— **Patriarchs and Prophets, p. 376 . ChS 73.1**

Kazi iliyopangiliwa vizuri lazima ifanywe kanisani, ili washiriki wake waweze kuelewa jinsi ya kuwapa wengine nuru na hivyo kuimarisha imani yao wenyewe na kuongeza ujuzi wao. Wanapotoa yale waliyopokea kutoka kwa Mungu watathibitishwa katika imani. Kanisa linalofanya kazi ni kanisa lililo hai. Tumejengwa kama mawe yaliyo hai, na kila jiwe linapaswa kutoa mwanga. Kila Mkristo anafananishwa na jiwe la thamani linaloshika utukufu wa Mungu na kuuangaza/kuakisi. — **Shuhuda kwa Kanisa 6:435. ChS 73.2**

## Masomo Katika Muundo Kamili

Na anakusudia kwamba tujifunze masomo ya utaratibu na mfumo kutoka katika mpangilio kamili ulioanzishwa katika siku za Musa kwa faida ya wana wa Israeli. — **Shuhuda kwa Kanisa 1:653.ChS 73.3**

## Hatua ya Kwanza Katika Muundo wa Kanisa

Ilikuwa ni wakati wa kuwekwa wakfu kwa wale kumi na wawili ambapo hatua ya kwanza ilichukuliwa katika kuundwa kwa kanisa kwamba baada ya kuondoka kwa Kristo ilikuwa kuendeleza kazi Yake duniani.— **The Acts of the Apostles, 18 . ChS 73.4**

Mpangilio wa kanisa la Yerusalemu ulipaswa kutumika kama kielelezo kwa ajili ya upangaji wa makanisa katika kila mahali

—

ambapo wajumbe wa ukweli wanapaswa kuwavuta waongofu kwa injili.... Baadaye katika historia ya kanisa la kwanza, wakati katika sehemu mbalimbali za ulimwengu makundi mengi ya waamini yalikuwa yameundwa kuwa makanisa, muundo wa kanisa ulikamilishwa zaidi, ili utaratibu na utendaji wenye upatanifu uweze kudumishwa. Kila mshiriki alihimizwa kutenda vyema sehemu yake. Kila mmoja alipaswa kutumia kwa hekima talanta alizokabidhiwa.— **The Acts of the Apostles, 91, 92 . ChS 73.5**

**Kuweka Kila Mmoja Mahali Pake**

Kila mtu anapaswa kuwa tayari kuwa au kufanya chochote katika vita hivi.—**Shuhuda kwa Kanisa 7:30.ChS 74.1**

Mungu hahitaji taasisi nyingi, majengo makubwa, au maonyesho makubwa, bali upatanifu wa kipekee wa matendo ya watu, watu waliochaguliwa na Mungu na wenye thamani. Kila mtu anapaswa kusimama katika sehemu yake na mahali pake, akiwaza,

—

akizungumza, na kutenda kwa kupatana na Roho wa Mungu. Kisha, na sio kabla ya wakati huo, kazi itakuwa kamili, yenye ulinganifu. —**Shuhuda kwa Kanisa 6:293.ChS 74.2**

Nguvu ya jeshi hupimwa kwa kiasi kikubwa na ufanisi wa watu katika safu. Kamanda mwenye busara anawaagiza maafisa wake kumfundisha kila askari kwa ajili ya utumishi imara. Anatafuta kukuza ufanisi wa hali ya juu kwa upande wa wote. Kama angewategemea maafisa wake pekee hangeweza kutarajia kufanya kampeni yenye mafanikio. Anahesabu utumishi mwaminifu na usiochoka kutoka kwa kila mtu katika jeshi Lake. Wajibu unawategemea zaidi watu walio katika safu. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:116.ChS 74.3**

Bwana anawaita watenda kazi wa injili. Je, nani atakaitika? Sio wote wanaoingia jeshini wanapaswa kuwa majenerali, wakuu, maofisa, au hata koplo. Sio wote wana uangalizi na wajibu wa viongozi. Kuna kazi ngumu ya aina nyingine ya kufanywa. Wengine lazima wachimbe mitaro na kujenga ngome; wengine watasimama kama walinzi; wengine kubeba ujumbe. Ingawa kuna maafisa wachache, inahitaji askari wengi kuunda safu na kupanga jeshi; lakini mafanikio yake yanategemea uaminifu wa kila askari. Woga au hila ya mtu mmoja inaweza kuleta msiba juu ya jeshi lote.— **Gospel Workers, 84, 85 . ChS 74.4**

## Siri ya Mafanikio

liii

Siri ya mafanikio yetu katika kazi ya Mungu itapatikana katika utendakazi mzuri wa watu wetu. Lazima kuwe na utendaji mmoja mahususi. Kila kiungo cha mwili wa Kristo lazima kitekeleze sehemu yake katika kazi ya Mungu, kulingana na uwezo ambao Mungu amempa. Ni lazima tusonge pamoja dhidi ya vizuizi na matatizo, bega kwa bega, moyo kwa moyo.— **The Review and Herald, Desemba 2, 1890 . ChS 75.1**

Ikiwa Wakristo wangetenda kwa pamoja, wakisonga mbele kama kitu kimoja, chini ya uongozi wa Nguvu moja, kwa ajili ya kutimiza kusudi moja, wangeupindua ulimwengu.
**—Shuhuda kwa Kanisa 9:221. ChS 75.2**

Malaika hufanya kazi kwa maelewano. Utaratibu kamili unatawala harakati zao zote. Kadri tunavyoiga kwa ukaribu maelewano na utaratibu wa jeshi la malaika, ndivyo juhudi za mawakala hawa wa mbinguni zitakavyofanikiwa zaidi kwa niaba yetu. Ikiwa hatuoni ulazima wa hatua ya maelewano, na ni wavivu, wasio na nidhamu, na wasio na mpangilio katika mwenendo wetu, malaika, ambao wamepangwa vizuri na wanafanya kwa utaratibu kamili, hawawezi kufanya kazi kwa ajili yetu kwa mafanikio. Wanageuka kwa huzuni, kwa maana hawajaruhusiwa kubariki mikanganyiko, usumbufu, na kukosekana kwa mpangilio. Wote wanaotamani ushirikiano wa wajumbe wa mbinguni lazima wafanye nao kazi kwa umoja. Wale ambao wametiwa mafuta kutoka juu katika juhudi zao zote wanahimiza utaratibu, nidhamu, na umoja wa vitendo, ndipo malaika wa Mungu wanaweza kushirikiana nao. Lakini kamwe, kamwe hawa wajumbe wa mbinguni hawataweka idhini yao mahali pasipo na utaratibu, pasipo na mipangilio na

—

penye machafuko. **—Shuhuda kwa Kanisa 1:649, 650.ChS 75.3**

**Onyo la Wakati**

Kuna haja ya kazi ya utaratibu; lakini pale ambapo baadhi yenu wana muda mrefu sana katika kufikiri, na kupanga, na kujitayarisha kwa ajili ya kazi, Shetani hushughulika na shamba kwa hadithi za uchawi, na uangalifu wa wanadamu unaingizwa katika udanganyifu wa mdanganyifu mkuu.— The Review and Herald. Machi 13, 1888 . ChS 75.4

Jinsi Shetani angefurahi ikiwa angeweza kufaulu katika juhudi zake za kuingia miongoni mwa watu hawa, na kuharibu kazi wakati ambapo utaratibu kamili ni muhimu, na atakuwa mamlaka kuu zaidi ya kuzuia maasi ya uwongo, na kukanusha madai ambayo hayajaingizwa kwa Neno la Mungu! Tunataka kushikilia mistari kwa usawa, ili kusiwe na kuvunjwa kwa mfumo wa mpangilio na utaratibu ambao umejengwa na kazi ya busara, makini. Leseni haipaswi kutolewa kwa watu wasio na utaratibu ambao wanataka kudhibiti kazi wakati huu.— **Gospel Workers, 487 . ChS 75.5**

## SURA YA 9 WITO WA KUAMKA

—

### Mahubiri

Hebu kengele ya ujumbe wa injili isikike kupitia makanisa yetu, na kuwaita kwenye utendaji duniani kote. Hebu washiriki wa kanisa wawe na imani inayoongezeka, wakipokea ari na nguvu kutoka kwa washiriki wa mbinguni, wasioonekana kwa macho ya kibinadamu, kutoka kwa ujuzi wa rasilimali zao zisizoisha, kutoka kwa ukubwa wa kazi wanayoifanya, na kutoka katika nguvu ya Kiongozi wao. Wale wanaojisalimisha chini ya uongozi wa Mungu, wakikubali kuongozwa na kuelekezwa Naye, watafunuliwa mpangilio wa matukio yaliyopangwa kutokea duniani na Yeye Mwenyewe. Wakiwa wamevuviwa na Roho

—

Wake na Yeye aliyetoa uhai Wake kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu, Hawataweza kusimama tena bila nguvu au uwezo utokao Kwake, hawatatazama tazama tu yale wasiyoweza kuyafanya. Bali watajivika silaha za mbingu, kisha watasonga mbele vitani wakiwa tayari kutenda na kuthubutu kwa ajili ya Mungu, wakijua kwamba uweza Wake usio na kikomo unatosha kuwatimizia mahitaji yao yote. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:14.ChS 77.1**

Hebuna tuamke! Vita vinaendelea kwa ukali sana. Ukweli na makosa yanakaribia pambano lake la mwisho. Hebu tutembee chini ya bendera iliyotiwa damu ya Mfalme Emmanueli (Mwana wa Mfalme), na tupigane vita vizuri vya imani, na kushinda heshima za milele; kwa maana Kweli itashinda, nasi twaweza kuwa washindi na zaidi kwa Yeye aliyetupenda. Saa za thamani za majaribio zinafungwa. Hebu tufanye kazi kwa uhakika kwa ajili ya uzima wa milele, ili tuweze kumtukuza Baba yetu wa mbinguni, na kuwa njia ya kuokoa nafsi

ambazo Kristo alikufa kwa ajili yake. — **The Review and Herald, Machi 13, 1888 . ChS 77.2**

### Maagizo ya Kuandama

Wakati fulani, Mkuu wa Wellington (Duke of Wellington) alikuwepo mahali ambapo chama cha wanaume Wakristo kilikuwa kikijadili uwezekano wa kufaulu katika jitihada ya umishenari miongoni mwa watu wapagani. Wakamwomba ushauri kiongozi huyo kutoa maoni ikiwa kwa fikra zake juhudi kama hizo zinaweza kuthibitisha mafanikio kulingana na gharama. Yule askari mzee akajibu: "Waheshimiwa, Je, maagizo kuondoka kwenda vitani ya Kiongozi wenu mkuu wa Jeshi ni yapi? (Marching orders) au Kauli mbiu yenu ni ipi? Yule kiongozi wa Wellington alijibu- Mafanikio ya misheni hiyo sio suala la ninyi kujadili. Kama nimeyasoma vyema maagizo yako uliyopewa na Jemedari wako wa vita ni haya, 'Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.' Mabwana, yatiini maagizo yenu ya vita mliyopewa." (Jibu lapaswa kuwa Nitakwenda-I will go! Na siyo kujadili, twende au tusiende.)— **Gospel Workers, 115 . ChS 77.3**

### Hakuna Muda wa Kuchelewa

"Hiyo siku ya Bwana iliyo kuu i karibu; I karibu, nayo inafanya haraka sana." **Sefania 1:14.** Hebu tuvae viatu vya injili, tayari kupiga gwaride la vita hata kwa tangazo na amri ya muda mfupi. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:48. ChS 78.1**

Washiriki wa kanisa wanapaswa kuweka mbele juhudi endelevu, za kudumu ambazo Yeye aliziweka. Wanapaswa kuchangamka na kuruka kwa utayari siku zote, kuanza kwa kutenda wanapoisika amri ya Bwana. Popote tunapoona kazi inayongoja kufanywa tunapaswa kuichukua na kuifanya, tukimtazama Yesu daima. Kama washiriki wa kanisa letu wangetii agizo hili na kuwa wamishenari hai, mamia ya roho zingevutwa kwa Yesu. Kama kila mshiriki wa kanisa angekuwa mmishenari aliye hai, injili ingetangazwa kwa

—

kasi katika nchi zote, kwa watu wote. mataifa, na jamaa. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:32. ChS 78.2**

Tunakaribia mwisho wa historia ya dunia hii. Tunayo kazi kubwa mbele yetu, kazi inayohusu kufunga kazi, na kutoa ujumbe wa mwisho wa onyo kwa ulimwengu wenye dhambi. Kuna watu ambao watakaochukuliwa kutoka kwenye jembe la plau-taaluma ya kilimo, kutoka katika shamba la mizabibu, kutoka katika matawi mengine ya kazi, na kutumwa na Bwana kutoa ujumbe huu kwa ulimwengu. —**Shuhuda kwa Kanisa 7:270. ChS 78.3**

Piga kengele ya tahadhari kote kwa urefu na upana wa dunia. Waambie watu kwamba siku ya Bwana i karibu na inafanya haraka sana kuja. Hebu mtu yeyote asiachwe bila kuonywa. Huenda tukawa katika nafasi za watu masikini walio katika upotofu na makosa. Huenda tuliwekwa miongoni mwa watu wasio wastaarabu (washenzi). Kulingana na Ukweli tuliopokea kuliko watu wengine wowote, sisi tu wadeni wa kuueneza sawia kwao. —**Shuhuda kwa Kanisa 6:22.ChS 78.4**

Ndugu na dada zangu, mmechelewa sana kuutoa muda na nguvu zenu kujitumikia wenyewe. Hebu siku ya mwisho isikukute umepungukiwa na hazina ya mbinguni. Tafuteni kuendelea kuutangaza kwa msukumo mkali ushindi wa msalaba, tafuta kuziangaza roho, jitaabisheni kwa ajili ya wokovu wa wenzenu, na kazi yenu itastahimili kujaribiwa kwa moto unaopima watu. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:56.ChS 78.5**

—

Lazima tuutoe ujumbe huu haraka, mstari juu kwa mstari, amri juu kwa amri. Hivi karibuni watu watalazimika kufanya maamuzi mazito, na ni wajibu wetu kuona kwamba wanafanya hivyo kwa kupewa nafasi ya kuuelewa Ukweli, ili waweze kuchukua msimamo wao wakiwa na akili timamu, katika upande sahihi. Bwana anawaita watu Wake kufanya kazi—kufanya kazi kwa dhati, bidii na kwa hekima—wakati rehema ingalipo-wakati mlango wa rehema bado uko wazi. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:126, 127. ChS 79.1**

Hatuna muda wa kupoteza. Mwisho u karibu. Njia kutoka mahali hadi mahali ili kueneza Kweli hivi karibuni itazungukwa na hatari kwenye mkono wa kuume na wa kushoto. Kila kitu kitawekwa ili kuzuia njia ya wajumbe wa Bwana, ili wasiweze kufanya kile ambacho kinawezekana kwao kufanya sasa. Lazima tuikabili kazi yetu kwa uzito na kipaumbele na kusonga mbele haraka iwezekanavyo katika vita hivi vikali. Kutoka kwa nuru niliyopewa na Mungu najua kwamba nguvu za giza zinafanya kazi kwa nguvu nyingi kutoka chini, na kwa kukanyaga hatua kwa siri Shetani anasonga mbele kuwachukua wale ambao sasa wamelala, kama mbwa-mwitu anayekamata mawindo yake. Tuna maonyo sasa ambayo tunaweza kutoa, kazi ambayo tunaweza kuifanya sasa; lakini hivi karibuni itakuwa ngumu zaidi kuliko tunavyoweza kufikiria. Mungu atusaidie kushika mkondo wa nuru, kufanya kazi huku macho yetu yakiwa yamekazia/yamekodoa kwa Yesu Kiongozi wetu, na kwa subira, tukisonga mbele kwa ustahimilivu ili kupata ushindi. **— Shuhuda kwa Kanisa 6:22. ChS 79.2**

Kuna hatari katika kuchelewa. Roho hiyo ambayo huenda ungeipata, nafsi hiyo ambayo huenda ungeifungulia Maandiko, inapita nje ya uwezo wako. Shetani ametayarisha wavu kwa ajili ya miguu yake, na kesho anaweza kuwa anafanyia kazi mipango ya adui mkuu wa Mungu. Kwa nini kuchelewa siku moja? Kwa nini usiende kazini mara moja? **— Shuhuda kwa Kanisa 6:443.ChS 79.3**

Uangalifu na uaminifu vinahitajika kwa wafuasi wa Kristo katika

—

kila kizazi; lakini kwa kuwa sasa tumesimama kwenye ukingo wa ulimwengu wa milele, tukishikilia Kweli tulizonazo na tuzitendazo, tukiwa na nuru kubwa, na kazi muhimu sana, ni lazima tuongeze bidii zetu maradufu. Kila mtu anapaswa kufanya kazi kwa uwezo wake wote. Ndugu yangu, unahatarisha wokovu wako ikiwa utasitasita sasa. Mungu atakukuleta hukumuni ikiwa utashindwa kufanya kazi aliyokupatia. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:460, 461.ChS 79.4**

**Maswali ya Muhimu**

Umilele unasimama mbele yetu. Pazia linakaribia kuinuliwa. Je, tunafikiria nini, kwamba tutang'ang'ania upendo wetu wenye ubinafsi wenye kupenda maisha rahisi/bwerere, wakati roho zinazotuzunguka pande zote zinaangamia? **ChS 80.1**

Je, mioyo yetu imekuwa imeota sugu na kuwa migumu kabisa? **ChS 80.2**

Je, hatuwezi kuona na kuelewa kwamba tuna kazi ya kufanya kwa ajili ya wengine? **ChS 80.3**

Ndugu zangu, Je, ninyi ni miongoni mwa wale ambao, wana macho, lakini hawaoni, na wana masikio, lakini hawasikii? **ChS 80.4**

Je, ni kazi bure Mungu kukupa wewe ujuzi wa mapenzi Yake? **ChS 80.5**

Je, haina maana yoyote kwa Yeye kukutumia onyo baada ya onyo juu ya kukaribia kwa wakati wa mwisho? **ChS 80.6**

Je! unaamini matamko ya Neno Lake juu ya mambo yanayoujia ulimwengu? **ChS 80.7**

Je, unaamini kwamba hukumu za Mungu zinaning’inia juu ya wakazi wa dunia? **ChS 80.8**

Baada ya kusikia haya yote, wewe unawezaje kukaa ukitulia kizembe tu, kwa kutojali na kupuuzia? **– Shuhuda kwa Kanisa 9:26, 27. ChS 80.9**

—

**Wito wa Kuamka**

Kazi inafungwa kwa kasi, na kila upande uovu unaongezeka. Tuna muda mfupi tu wa kufanya kazi. Hebu na tuamke kutoka katika usingizi wa kiroho, na tuweke wakfu yote tuliyo nayo na sisi wenyewe tulivyo kwa Bwana. Roho Yake itadumu pamoja na wamishenari wa kweli, akiwapa uwezo wa utumishi.— **The Southern Watchman, Aprili 9, 1903 . ChS 80.10**

Amka, akina ndugu na dada, amka. Msilale tena. "Kwa nini unasimama hapa mchana kutwa bila kazi?" Yesu anakuita, akisema, "Nendeni mkafanye kazi leo katika shamba Langu la mizabibu." Yeyote aliyempokea Roho Mtakatifu, atadhihirisha; kwa kuwa nguvu zake zote zitatumika katika huduma imara zaidi. Wote wanaompokea Kristo kwa imani, huwa wanafanya kazi. Wanahisi mzigo wa roho. Mungu sasa anamwita kila mtu aliye na ujuzi wa ile Kweli, ambaye ni hazina ya Kweli takatifu, ainuke na kuwapa wengine nuru ya mbinguni.— **The Review and Herald, Desemba 5, 1893 . ChS 80.11**

Amka, ndugu; kwa ajili ya nafsi yako, amka. Bila neema ya Kristo huwezi kufanya lolote. Fanya kazi uwezavyo, wakati unaweza kufanya kazi bado.—**The Southern Watchman, Julai 17, 1906 . ChS 80.12**

Ikiwa macho yetu yangeweza kufunguliwa kutambua_malaika walioanguka wanavyofanya kazi kwa wale ambao wanahisi kwamba mambo ni rahisi na wanajiona wako salama, tusingeweza kujisikia salama. Malaika waovu wako njiani mwetu kila wakati. **— Shuhuda kwa Kanisa 1:302. ChS 81.1**

Mungu anatoa wito kwa wote, wahubiri na walei, kuamka. Mbingu yote inaonesha matukio yanayoendelea. Matukio ya historia ya dunia yanafungwa haraka. Tuko katikati ya maafa ya siku za mwisho. Hatari na maafa makubwa viko mbele yetu, na bado sisi hatujaamka. Ukosefu huu wa utendaji na bidii katika kufuata maelekezo ya Mungu ni jambo la kutisha. Usingizi wa kifo unatoka kwa Shetani. **—Shuhuda kwa Kanisa 1:260, 261.**

—

**ChS 81.2**

Niseme nini ili kuwaamsha watu wa Mungu waliobaki? Nilioneshwa kuwa matukio ya kutisha yako mbele yetu; Shetani na malaika zake wanaleta nguvu zao zote juu ya watu wa Mungu. Anajua kwamba ikiwa wanadamu watalala kidogo kidogo ana uhakika kuwa kuangamizwa kwao ni hakika. **—Shuhuda kwa Kanisa 1:263.ChS 81.3**

Katika saa hizi za mwisho kabla ya mlango wa rehema kufungwa kwa wana wa wanadamu, ambapo hivi karibuni hatima ya umilele ya kila nafsi itakapoamuliwa upesi sana, Bwana wa mbingu na dunia anatarajia kanisa Lake kuamsha na kutenda kuliko wakati mwingine wowote. Wale ambao wamewekwa huru katika Kristo kupitia maarifa ya Ukweli wa thamani, wanachukuliwa na Bwana Yesu kuwa wateule Wake, waliopendelewa zaidi ya watu wengine wote juu ya uso wa dunia; Naye amewahesabu kutangaza sifa Yake Yeye aliyewaita kutoka gizani waingie katika nuru ya ajabu. Baraka ambazo zimetolewa kwa wingi, zinapaswa

kuwasilishwa kwa wengine. Habari njema ya wokovu inapaswa kwenda kwa kila taifa, kabila, lugha, na jamaa.— **Prophets and Kings, 716, 717 . ChS 81.4**

Hakuna hata mmoja, miongoni wa watu mia kati yetu ambaye anayefanya lolote zaidi ya kujihusisha na pilikapilika za kawaida za kidunia. Hatujaamka hata nusu, ili kuona thamani ya roho ambazo Kristo alizifia. **—Shuhuda kwa Kanisa 8:148. ChS 81.5**
Ikiwa wafuasi wa Kristo wangekuwa macho kufanya kazi, kungekuwa na maelfu mahali ambapo kuna mmoja leo, wakitangaza injili katika nchi za kipagani. Na wote ambao hawakuweza kujishughulisha binafsi na kazi hiyo, bado wangeitegemeza kwa mali zao, huruma zao, na maombi yao. Na kungekuwa na kazi ya bidii zaidi kwa ajili ya nafsi katika nchi za Kikristo.**— Steps to Christ, 81 . ChS 81.6**

Maelfu wanafurahia nuru kubwa na fursa za thamani, lakini hawafanyi chochote kwa ushawishi wao au pesa zao ili kuwaangazia wengine. Hawachukui hata jukumu la kuziweka roho zao wenyewe katika upendo wa Mungu, ili wasiwe mzigo kwa kanisa. Watu kama hao wangekuwa mzigo na kuziba mbingu kama bomba linavyoziba na kuzuia wengine kuingia. Kwa ajili ya Kristo, kwa ajili ya ile Kweli, kwa ajili yao wenyewe, hao wapaswa kuamka na kufanya kazi yenye bidii kwa ajili ya umilele.— **The Review and Herald, Machi 1, 1887 . ChS 82.1**

Kanisa la Kristo linaweza kulinganishwa vyema na jeshi. Maisha ya kila askari ni magumu, yenye kazi za kuhenyesha na yenye shida na hatari. Katika kila mkono kuna maadui walio macho, wakiongozwa na mkuu wa nguvu za giza ambaye hasinzii kamwe na haachi kamwe kituo chake cha ulinzi. Wakati wowote Mkristo anapojiziuka/anapojisahau na kuacha kituo chake cha ulinzi, adui huyu hodari hufanya shambulio la ghafla, yenye vurugu na ya kikatili. Pasipo washiriki wa kanisa kufanya kazi bila kukoma kwa kuwa macho na kukesha, watashindwa na hila zake.**Shuhuda kwa Kanisa 5:394. ChS 82.2**

—

Je, ingekuwaje ikiwa nusu ya wanajeshi ndani ya jeshi walikuwa wamelala au wamekaa kizembe wakati wameagizwa kuwa macho na makini kazini; matokeo yake yatakuwa kushindwa, kufungwa, au kifo. Je! Kama mwanajeshi wa namna hii, angefanikiwa kutoroka kutoka mikono mwa adui, Je, anapofika kwenye upande wa jeshi analolipigania angefikiriwa kustahili tuzo kweli? Hapana; wangepokea hukumu ya kifo haraka. Na ndivyo, kanisa la Kristo lilivyo halijali na wala si aminifu dhidi ya matokeo yanayoweza kulikumba. Jeshi lililolala la askari wa Kikristo — ni kitu gani kichoweza kuwa kibaya zaidi ya hiki! Je! Ni maendeleo gani yanaweza kufanywa dhidi ya ulimwengu, ambao uko chini ya udhibiti wa mkuu wa giza? Wale ambao husimama nyuma bila kujali siku ya vita, kana kwamba hawakuwa na nia au shauku yoyote na hawakuhisi jukumu lolote kuhusu shindano, wangeweza kubadilisha mwelekeo wao au kuacha safu mara moja. **Shuhuda kwa Kanisa 5:394. ChS 82.2**

## Lazima kuwe na Vitendo

Nilioneshwa watu wa Mungu walikuwa wakisubiri mabadiliko yatokee - nguvu zenye ushawishi zitawashikilia. Lakini watakatishwa tamaa, kwani wamekosea. Lazima wachukue hatua, lazima washike kazi hiyo wenyewe na wamlilie Mungu kwa bidii kupata maarifa ya Kweli juu yao. Matukio ambayo yanapita mbele yetu yana ukubwa wa kutosha kutusababisha kuamka na kusisitiza Ukweli nyumbani kwa mioyo ya wote watakaosikiliza. Mavuno ya dunia yamekaribia kuiva. **—Shuhuda kwa Kanisa 1:261.ChS 82.4**

Kila kitu katika ulimwengu kinawataka wale wanaoijua Kweli kujitakasa wao wenyewe bila kusita au kujibakiza, kwa ajili ya kuutangaza Ukweli kama ilivyojulishwa kwao katika ujumbe wa Malaika wa tatu. Kile tunachokiona na kukisikia hutuita kwenye wajibu wetu. Utendaji kazi wa mawakala wa Shetani huita kila Mkristo kusimama katika nafasi yake. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:25, 26. ChS 83.1**

—

Ujumbe wa kuja kwa Kristo upesi utatolewa kwa mataifa yote ya dunia. Juhudi za kukesha, zisizochoka zinahitajika ili kushinda nguvu za adui. Sehemu yetu si kukaa kwa kutulia na kulia na kukunja mikono yetu, bali kuinuka na kufanya kazi kwa ajili ya sasa na umilele.— **The Southern Watchman, Mei 29, 1902 . ChS 83.2**

Fanya kitu!, kifanye upesi, kwa nguvu zako zote;
Mbawa za Malaika zingeshuka kwa kudhoofika, ikiwa zingepumzika kwa muda mrefu; Na Mungu mwenyewe, asingembariki asiyefanya kazi. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:308. ChS 83.3**

Mtu asifikiri kwamba yuko huru kukunja mikono yake na asifanye lolote. Uwezekano wa mwanadamu yoyote kuokolewa katika uvivu na kutofanya kazi ni jambo lisilowezekana kabisa. Fikiria kile ambacho Kristo alitimiza wakati wa huduma Yake duniani. Jinsi juhudi Zake zilivyokuwa za dhati, na zisizochoka! Yeye Hakuruhusu chochote kumtenga na kazi aliyopewa. Je, tunazifuata nyayo Zake?— **The Colporteur Evangelist, 38 . ChS 83.4**

Mawakala wa Kiungu na wa kianadamu wameunganishwa katika kazi ya kuokoa roho. Mungu amefanya sehemu Yake, na utendaji wa Kikristo unahitajika sasa. Mungu anatoa wito kwa jambo hili. Yeye Anatarajia watu Wake washiriki katika kuwasilisha nuru ya Ukweli kwa mataifa yote. Ni nani watakaoingia katika ubia huo pamoja na Bwana Yesu Kristo?— **The Review and Herald, Machi 1, 1887 . ChS 83.5**

Kanisa lazima liwe kanisa linalofanya kazi kama lingekuwa kanisa hai. Halipaswi kuridhika tu na kupigwa gwaride na kukaa mahali ili kushugulika dhidi ya nguvu zinazopingana za dhambi na makosa, halipaswi kuridhika kutembea polepole, linapaswa kuweka bidii, kubeba nira ya Kristo, na kusonga mbele kwa bidii na Kiongozi wake, na kuhamasika katika kuleta watenda kazi wapya njiani, watenda kazi ambao watafundishwa kazi (kanisa halipaswi kuridhika kukaa mahali bila kusonga mbele kwa bidii)— **The Review and Herald, Agosti 4, 1891 . ChS 83.6**

Tuna muda kidogo tu wa kuhimiza vita; kisha Kristo atakuja, na tukio hili la uasi litafungwa. Ndipo juhudi zetu za mwisho zitakuwa zimefanywa kufanya kazi na Kristo na kuendeleza

—

ufalme Wake. Wengine ambao wamesimama mstari wa mbele katika vita, wakipinga kwa bidii uovu unaokuja, huanguka kwenye nafasi ya kazi kwa kifo; wengine huwatazama kwa huzuni mashujaa walioanguka, lakini hawana wakati wa kusitisha au kuacha kazi. Ni lazima wasogee pamoja na kuziba nafasi zilizoachwa wazi kwenye safu, washike bendera iliyoanguka kwenye mkono uliopooza kwa kifo, na kwa nguvu mpya waitetee na kuithibithisha Kweli na heshima ya Kristo. Sasa, kuliko hata hapo awali, upinzani lazima ufanywe dhidi ya dhambi,—dhidi ya nguvu za giza. Wakati unahitaji shughuli yenye nguvu na iliyodhamiriwa kwa upande wa wale wanaoamini Ukweli wa sasa. Wanapaswa kufundisha Kweli kwa kanuni na mifano.— **The Review and Herald, Oktoba 25, 1881 . ChS 84.1**

Bwana anawaita sasa Waadventista wa Sabato, katika kila eneo mahalia kujiweka wakfu Kwake na kufanya yote wawezayo, kulingana na hali zao, kusaidia katika kazi Yake. Kwa ukarimu wao katika kutoa talanta, zawadi na sadaka, Yeye anataka waonyeshe kuthamini kwao baraka Zake na shukrani zao kwa rehema Zake. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:132.**

Uvivu na dini haviendani pamoja; na ni sababu ya upungufu wetu mkubwa katika maisha ya Kikristo na uzoefu ni kutotenda kazi katika kazi ya Mungu. Misuli ya mwili wako itakuwa dhaifu na isiyoweza kufanya kitu chochote, ikiwa haitawekwa katika mazoezi, na ni hivyo kwa asili ya kiroho. Kama unataka kuwa na nguvu, lazima utumie uwezo wako.— **The Review and Herald, Machi 13, 1888 . ChS 84.3**

—

Tunapaswa kuwa watenda kazi wenye bidii; mtu asiye na kazi ni kiumbe duni. Lakini ni kisingizio gani kinaweza kutolewa kwa uvivu katika kazi kuu ambayo Kristo aliyatoa maisha Yake ili kuiamilisha? Nguvu za kiroho zitakoma kuwapo kama hazitatumika, na ni mpango wa Shetani kwamba zitaangamia. Mbingu yote inashiriki kikamilifu katika kazi ya kuwatayarisha watu kwa ajili ya ujio wa pili wa Kristo katika ulimwengu wetu, na "sisi ni watenda kazi pamoja na Mungu." Mwisho wa mambo yote umekaribia. Sasa ndiyo fursa yetu ya kufanya kazi.— **The Review and Herald, Januari 24, 1893 . ChS 84.4**

Wanahitajika wamishenari wenye moyo. Jitihada za ulegevu na za kushtukiza hapa na pale kama kifafa, hazitafanya vizuri sana. Ni lazima tuwe na umakini. Lazima tuwe dhati kabisa. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:45.ChS 85.1**

Kuna baadhi yetu ambao, kama wangechukua muda kufikiria, wangechukulia nafasi yao ya kufanya kwao sifuri kuwa ni dhambi ya kupuuzia na kutojali talanta zao walizopewa na Mungu. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:425. ChS 85.2**

Je! Nafasi yetu ni ipi duniani? Tuko katika wakati wa kungojea. Lakini kipindi hiki hakitakiwi kutumiwa katika mawazi ya kufikirika na maombi tu. Kungojea, kukesha, na kufanya kazi kwa bidii vyote vinapaswa kuunganishwa kwa pamoja. Maisha yetu hayapaswi kujaa pilikapilika zenye makelele na kuendeshwa katika kupanga juu ya mambo ya ulimwengu, kiasi cha kupuuza utauwa binafsi na utumishi ambao Mungu anautaka. Wakati hatupaswi kuwa wavivu katika biashara au shuguli, tunapaswa kuwa na bidii katika roho, tukimtumikia Bwana. Taa ya roho yapaswa irekebishwe utambi wake kwa kutoa sehemu nyeusi iliyoungua, na lazima tuwe na mafuta ya neema kwenye vyombo vyetu na taa zetu. Kila tahadhari lazima itumike kuzuia anguko la kiroho, na kurudi nyuma kimaadili, siku ya Bwana isije ikatujia kama mwizi. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:276.ChS 85.3**

Tunaishi katika zama ambazo hazipaswi kuwa na uvivu wa kiroho.

Kila nafsi inapaswa kuchajiwa na mkondo wa umeme wa Mbinguni wa maisha. **— Shuhuda kwa Kanisa 8:169. ChS 85.4**

Jaza matendo mema na kazi zote nzuri, unazoweza kuzibabanisha kwa kadri uwezavyo katika kapu la maisha haya. **— Shuhuda kwa Kanisa 5:488. ChS 85.5**

Yesu angependa wote wanaolikiri Jina Lake wawe watenda kazi wenye bidii. Ni muhimu kwamba kila mshiriki ajenge juu ya Mwamba, Kristo Yesu. Dhoruba inakuja ambayo itawavuta watu na kuleta maumivu makali na kupima msingi wa kiroho wa kila mtu kwa kiwango cha juu sana. Kwa hivyo jiepusheni na msingi wa mchanga; jengeni juu ya mwamba. Chimbeni kina kirefu; wekeni imara msingi wenu. Jengeni, oh, jengeni kwa ajili ya umilele! Jengeni kwa machozi, na sala za kutoka moyoni. Hebu kila mmoja wenu kuanzia sasa, aanze maisha yake mazuri kwa matendo mema. Watu kama Kalebu ndiyo wanaohitajika zaidi katika siku hizi za mwisho. **— Shuhuda kwa Kanisa 5:129, 130. ChS 85.6**

KIPIMO CHA BWANA

Kuna kipimo cha tabia kinachoendelea kila wakati. Malaika wa Mungu wanakadiria thamani yako ya maadili, na kuhakikisha mahitaji yako, na kupeleka kesi yako kwa Mungu.— **The Review and Herald, Aprili 2, 1889 . ChS 85.7**

Sisi binafsi tutawajibika kwa kufanya yodi moja chini ya uwezo wetu wa kufanya. Bwana hupima kwa usahihi kila uwezekano wa huduma. Uwezo ambao haujatumiwa huzingatiwa sana kama tu, ule ulioboreshwa. Kwa yote tunayoweza kuwa kupitia matumizi sahihi ya talanta zetu Mungu anatuwajibisha. Tutahukumiwa kulingana na yale tuliyopaswa kufanya, lakini hatukutimiza kwa sababu hatukutumia nguvu zetu kumtukuza Mungu. Hata kama hatupotezi nafsi zetu, tutatambua milele matokeo ya talanta zetu ambazo hazijatumiwa. Kwa ujuzi na uwezo wote ambao

—

tungeweza kupata na hatukupata, kutakuwa na hasara ya milele.— **Christ's Object Lessons, p . ChS 86.1**

## Hichi Ndicho Kingepaswa Kuwa

Ikiwa kila askari wa Kristo angefanya kazi yake, kama kila mlinzi wa kuta za Sayuni, angepiga tarumbeta kwa sauti fulani, ulimwengu ungekuwa umesikia ujumbe wa onyo tayari. Lakini kazi ipo nyuma miaka nenda rudi. Wakati watu wamelala, Shetani amepiga hatua juu yetu kwa kunyata. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:29. ChS 86.2**

Hebu sasa na tuichukue kazi tuliyoitiwa na kuutangaza ujumbe ambao utawaamsha wanaume na wanawake kuhisi hatari yao. Ikiwa kila Mwaadventista Msabato angefanya kazi iliyowekwa juu yake, idadi ya waumini ingekuwa kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa. Katika miji yote ya [Marekani] kungekuwa na wale ambao wangekuwa wameongozwa kutii ujumbe wa kuitii Sheria ya Mungu. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:25.ChS 86.3**

Kama kusudi la Mungu lingetekelezwa na watu Wake katika kuupa ulimwengu ujumbe wa rehema, Kristo angekuja duniani kabla ya haya, na watakatifu wangepokelewa na kukaribishwa katika mji wa Mungu. **—Shuhuda kwa Kristo 6:450.ChS 86.4**

## Kitabu cha Mbinguni

Ulimwengu unahitaji wamishenari, wamishenari wa nyumbani waliowekwa wakfu, na hakuna yeyote atakayeandikishwa katika vitabu vya mbinguni kuwa Mkristo ambaye hana roho ya umishenari.— **The Review and Herald, Agosti 23, 1892 . ChS 86.5**

Ikiwa washiriki wa kanisa hawatafanya kazi hii, basi wanaonyesha kuwa hawana uhusiano wowote na Mungu wao. Majina yao yanasajiliwa kama watumishi wavivu. **— Shuhuda kwa Kanisa 5:462, 463. ChS 87.1**

Katika kila vuguvugu la kidini kuna watu ambao, ingawa hawawezi

—

kukana kwamba kazi ni ya Mungu, bado wanajiweka kando, wakikataa kufanya juhudi yoyote ya kusaidia. Ingekuwa vyema kwa watu kama hao kukumbuka taarifa iliyohifadhiwa juu,—kitabu kile ambacho ndani yake hakina mapungufu, hakina makosa, na katika hicho watahukumiwa. Hapo kila nafasi iliyopuuzwa ya kufanya huduma kwa Mungu

imeandikwa; na huko pia, kila tendo la imani na upendo huwekwa katika ukumbusho wa milele.— **Prophets and Kings, 639 . ChS 87.2**

Asubuhi ya tarehe 23 Octoba mwaka 1879, majira ya saa nane usiku, Roho wa Bwana alinijilia, na tazama nikaona matukio yahusuyo hukumu ijayo. Ninakosa lugha ya kuelezea kwa utoshelevu kuhusu mambo yaliyooneshwa mbele yangu na athari iliyoletwa, na mambo hayo akilini mwangu. Siku kuu, ile ya kuanza kwa hukumu ya Mungu ilionekana kuwa imewadia. Elfu kumi mara elfu kumi wakasimama mbele ya kiti cha enzi kikubwa, ambapo juu yake alikuwa ameketi Yule Mwenye mwonekano wenye utukufu Mkuu. Vitabu mbalimbali vilikuwa mbele Yake, na juu ya majalada ya kila kitabu palikuwa pameandikwa kwa herufi za dhahabu, zikionekana kama mwali wa moto uwakao: "Kitabu cha Mbinguni." Kimoja kati ya vitabu hivi, kilichokuwa na majina ya wale wanaodai kuiamini Kweli, kikafunguliwa. Ghafla nikapoteza uoni wa watu mamilioni, watu wasiohesabika katika kiti cha enzi, na umakini wangu ukawa kwa wale waliodai kuwa ni watoto wa nuru na wa ile Kweli. *Watu hawa walipoitwa, mmoja baada ya mwingine, na matendo yao mema kuorodheshwa, nyuso zao zingeliangaza kwa furaha takatifu ambayo ingeliakisiwa kila upande. Lakini hili halikuonekana kubakia akilini mwangu kwa msukumo mkubwa.* **ChS 87.3**

Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ndani yake zimenakiliwa dhambi za wale wanaoijidai waufuata Ukweli na kuukiri kwa midomo yao tu. Chini ya kichwa kikuu cha ubinafsi imeorodheshwa kila dhambi. Kulikuwa pia kulikuwa na vichwa juu ya kila safu, na chini ya hivi, pembeni ya kila jina, pameandikwa katika kila safu zake, dhambi ndogo. Chini ya kutamani ulionekana uongo, wizi, unyang'anyi, ulaghai na ubadhirifu: chini ya tamaa kilionekana kiburi na ufujaji wa mali; wivu ulikuwa juu ya mawazo maovu, husuda, na chuki; na kutokuwa na kiasi kulikuwa juu ya orodha ndefu ya uhalifu wa kutisha, kama vile

—

ulegevu, uzinzi, anasa iliyojawa shauku ya *kinyama, n.k. Nilipokuwa nikitazama nilijawa na uchungu na kushangaa: "Nani awezaye kuokoka? Nani ataonekana yu ana haki mbele za Mungu? Nani mwenye mavazi yaliyo safi? Akina nani hawana makosa mbele za Mungu aliye safi na mtakatifu?" Kwa kadri Mtakatifu aliyeko kwenye kiti cha enzi alipozifungua kurasa za kitabu, na macho Yake kuwatazama watu hao kwa kitambo, mtazamo Wake ulizichoma nafsi zao, na kwa wakati huohuo kila neno na tendo walilolifanya katika maisha yao vilipitishwa akilini mwao kwa wazi kama kupitishwa katika njozi yao kwa herufi ziwakazo moto. Watu wakatetemeka, na nyuso zao zikajawa hofu. Mwonekano wao wa awali walipokizunguka kiti cha enzi ulikuwa ni wa kutokujali. Lakini badiliko lililoje la mwonekano wao sasa! Hisia ya kuwa salama ilikuwa imetoweka, na mahala pake kukaliwa na hofu kuu isiyotamkika. Hofu na majuto i kwa kila mtu, asije akaonekana miongoni mwao waliopungua. Kila jicho limeuelekea uso Wake Yeye aliyeketi katika kiti cha enzi; na kwa kadri jicho Lake makini, lichunguzalo linapoliangalia kundi lile, mioyo inadundadunda; kwa kuwa wanajitia hatiani wao wenyewe pasi na neno lolote kuzungumzwa kwao. Kwa uchungu nafsini kila mtu anadhihirisha hatia yake mwenyewe na kwa uwazi wa kutisha anaona kuwa ameitupilia mbali tunu thamani ya uzima wa milele.* Kundi moja lilisajiliwa kama watu waharibuo/waichoshao ardhi (Luka 13:7-9). Kwa kadri jicho lichomalo

la Hakimu lilipowatazama hawa, dhambi zao za kupuuza ziliwekwa wazi. Kwa midomo ya hofu na kutetemeka wakatambua kuwa walikuwa wasaliti kwa tumaini lao takatifu. Walipewa maonyo na fursa/fadhila, lakini hawakuyazingatia wala kuboresha. Sasa waliona kuwa walizitumia vibaya fadhila ya Mungu. Ni kweli, hawakuwa na ungamo kwamba walikuwa watu waliofanya uovu mbaya na ufisadi; lakini kama mtini wakalaaniwa kwa kutozaa matunda, kwa sababu hawakuzitumia talanta walizopewa. Kundi hili lilifanya jitihada binafsi na kuu za kiutendaji kazi kwa ajili tu ya kujipatia manufaa yao wenyewe (wachoyo). Hawakuwa matajiri kwa Mungu katika matendo yao katika chochote kile, kwani hawakuonesha mwitikio kwa madai Yake kwao. Ingawa wanadai kuwa watumishi wa Kristo, hawakupeleka nafsi zozote Kwake Bwana. Kama kazi ya Mungu ingelitegemea jitihada zao, ingelidhoofika; kwa kuwa sio tu walizuia vipato walivyopewa na Mungu, bali walijizuia/walijibakiza na wao wenyewe. Lakini hawa wanaweza kuona na kuhisi kuwa kwa kutowajibika kwao katika kazi ya Mungu wamejiweka wenyewe katika upande wa mkono wa kushoto. Walikuwa na fursa, lakini hawakuzifanyia kazi waliyopaswa kuifanya na iliyotakiwa kufanyika. Majina ya wote wanaoikiri Kweli yaliorodheshwa. Baadhi wakakemewa kwa kutokuamini kwao, na wengine kwa kuwa watumishi wazembe/wavivu. Waliwaachia watu wengine wafanye kazi katika shamba la mzabibu la Bwana, wabebe majukumu mazito, na ilihali wao wakitumika nafsi zao, kwa manufaa yao wenyewe ya kitambo tu. *Kama wangelikuza uwezo ambao walipatiwa na Mungu, wangelikuwa wabeba mizigo madhubuti, watendao kazi kwa ajili ya Bwana*. ………**ChS 87.4**

Anasema Hakimu: "Wote watahesabiwa haki kwa imani yao na kuhukumiwa kwa matendo yao." Ni dhahiri kiasi gani kupuuzia kwao kunavyoonekana, na una busara kiasi gani, mpango wa Mungu katika kumpatia kila mtu kazi ya kufanya kusaidia na kuwaokoa wanadamu wenzake. Kila mmoja alipaswa

—

kudhihirisha imani iliyo hai katika familia yake na majirani zake, kwa kuonesha wema kwa walio masikini, kwa kuwahurumia watesekao, kujihusisha katika kazi ya utume, na kuitegemeza kazi ya Mungu kwa mapato yake. Lakini, kama Merozi, laana ya Mungu ilikuwa juu yao kwa kile ambacho hawajakifanya. Waliipenda kazi ile ambayo ingeliwapatia faida kubwa katika maisha haya; na hivyo pembeni ya majina yao katika kitabu cha waliotenda mema palikuwa na uwazi wenye kuhuzunisha. —Shuhuda kwa Kanisa 4:384-386. ChS 88.1

## Inahitajika Zaidi Kwetu Kuliko Baba Zetu

Nuru kubwa huangaza juu yetu kuliko ilivyoangaza kwa baba zetu. Hatuwezi kukubalika au kuheshimiwa na Mungu kwa kutoa huduma hiyo hiyo, au kufanya kazi zile zile, ambazo baba zetu walifanya. Ili Kukubaliwa na Kubarikiwa na Mungu kama walivyokuwa, lazima tuige uadilifu na bidii yao, - tuboreshe Nuru yetu kama walivyoiboresha yao, - na tufanye kama ambavyo wangefanya ikiwa wangeishi katika siku zetu. Lazima tutembee katika Nuru ambayo inatuangazia, vinginevyo Nuru hiyo itakuwa giza. —Shuhuda kwa Kanisa 1:262. ChS 88.2

## Wito kwa Kanisa Lenye Uvivu

Ni fumbo kwamba hakuna mamia kazini mahali ambapo sasa kuna mtu mmoja tu. Ulimwengu

wa mbinguni inashangazwa na kutojali, ubaridi, kutozingatia kwa wale wanaodai kuwa wana na binti za Mungu. Katika Kweli kuna nguvu iliyo hai. Nendeni kwa imani, na muitangaze Kweli kana kwamba mliiamini. Hebu wale unaowafanyia kazi waone kwamba kwako hakika ni Kweli iliyo hai. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:42. ChS 88.3**

Hatuwezi kamwe kuokolewa katika uvivu na kutofanya kazi. Hakuna kitu kama mtu aliyeongoka kikweli na anaishi maisha ya hovyo, yasiyo na maana, yasiyofaa na yasiyo na msaada. Haiwezekani mtu ajipate ameteleza tu kiajabu hadi akafika mbinguni. Hakuna mvivu anayeweza kuingia humo.... Wale wanaokataa kushirikiana na Mungu duniani, hawataweza kushirikiana Naye mbinguni. Haingekuwa salama kuwapeleka mbinguni-mbingu ingekuwa hatari kuwa na watu kama hao.— **Christ's Object Lessons, p. 280 . ChS 89.1**

Mbingu yote inatazama kanisa kwa hamu kubwa, ili kuona kile ambacho washiriki wake mmoja-mmoja wanafanya ili kuwatia nuru wale walio gizani.— **The Review and Herald, Februari 27, 1894 . ChS 89.2**

Unatakiwa kuchukulia kwa uzito kwamba unashughulika na MUNGU Mkuu na daima lazima ukumbuke kwamba Yeye siyo mtoto wa kuchezewa au kucheza Naye. Huwezi kujihusisha katika huduma Yake kama upendavyo au kwa kujifurahisha na starehe zako mwenyewe. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:221.ChS 89.3**

Mawakala wa mbinguni wamekuwa wakingoja kushirikiana na mawakala wa kianadamu, lakini hatujatambua uwepo Wake. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:297.ChS 89.4**

Malaika wa mbinguni kwa muda mrefu wamekuwa wakingojea mawakala wa kianadamu - washiriki wa kanisa - kushirikiana nao katika kazi kubwa inayopaswa kufanywa. Hawa waanakungoja wewe. **—Suhuda kwa Kanisa 9:46, 47.ChS 89.5**

Wengi, wengi sana, wanakaribia siku ya Mungu bila kufanya lolote, wakikwepa majukumu, na matokeo yake ni mbilikimo wa kiroho.

—

Kwa kadiri kazi ya Mungu inavyohusika, kurasa za historia ya maisha yao zinajaza sufuri au nafasi tupu zenye kuleta vilio tu na huzuni. Wao ni miti katika bustani ya Mungu, lakini ni wasumbuaji tu wa lishe ya ardhi, wanaotia giza kwa matawi yao yasiyozaa matunda, ingelikuwa heri kama miti yenye kuzaa matunda ingemiliki hiyo ardhi.— **The Review and Herald, Mei 22, 1888 . ChS 89.6**

Kuna hatari kwa wale wanaofanya kidogo au kutofanya chochote kwa ajili ya Kristo. Neema ya Mungu haitadumu kwa muda mrefu ndani ya nafsi ya yule ambaye, akiwa na upendeleo mkubwa na fursa nyingi, anabaki kimya tu.— **The Review and Herald, Agosti 22, 1899 . ChS 89.7**

Hakuna wakati wa kulala sasa, - hakuna wakati wa kuendekeza katika majuto yasiyo na maana. Mtu anayethubutu kusinzia sasa atakosa fursa za thamani za kufanya mema. Tumepewa upendeleo wenye baraka wa kukusanya miganda katika kipindi cha mavuno makubwa; na kila nafsi iliyookolewa itakuwa nyota ya ziada katika taji ya Yesu, Mkombozi wetu mwema na Anayependeza na tunayemwabudu. Ni nani aliye na hamu ya kuweka silaha chini wakati kwa kuendelea vita kwa muda mrefu kidogo, atapata ushindi mpya na kukusanya nyara mpya za roho kwa umilele?— **The Review and Herald, Oktoba 25, 1881 . ChS 90.1**

Wajumbe wa mbinguni wanafanya kazi yao; Lakini sisi tunafanya nini? Ndugu na dada, Mungu anawaita ninyi kukomboa wakati. Mkaribie Mungu. Amsha karama iliyo ndani yako. Hebu wale ambao wamepata fursa ya kufahamiana na sababu za imani yetu, watumie sasa ujuzi huu kwa kusudi fulani.— **Historical Sketches, 288 . ChS 90.2**

Je, mnawezaje kurudia sala ya Bwana, "Ufalme wako uje, Mapenzi Yako yatimizwe hapa duniani kama mbinguni," na kuketi kwa utulivu katika nyumba zenu bila kusaidia kubeba mwenge/tochi ya mwanga wa Ukweli kwa wengine? Unawezaje kuinua mikono yako mbele za Mungu na kuomba baraka Zake Bwana juu yako na familia zako, wakati unafanya kidogo sana kusaidia wengine?— **Historical Sketches, 288 . ChS 90.3**

Kuna baadhi yetu ambao, kama wangechukua muda kufikiria, wangechukulia nafasi yao ya kufanya kwao sifuri kuwa ni dhambi ya kupuuza talanta zao walizopewa na Mungu. Ndugu na dada, Mkombozi wako na malaika wote watakatifu wanahuzunishwa na ugumu wa moyo wako. Kristo alitoa maisha Yake Mwenyewe ili kuokoa roho, na bado ninyi ambao mmejua upendo Wake mnafanya juhudi ndogo sana kutoa baraka za neema Yake kwa wale aliowafia. Kutojali huko na kupuuzia wajibu ni jambo linaloleta mshangao kwa Malaika. Katika hukumu siku ile, lazima ukutane na roho ulizozipuuza. Katika siku hiyo kuu utajihukumu na kujishutumu mwenyewe. Hebu Bwana na akuongoze sasa kwenye toba. Hebu na awasamehe watu Wake kwa kupuuza kazi katika shamba Lake la mizabibu ambalo amewapa kufanya. —**Shuhuda kwa Kanisa 6:425, 426. ChS 90.4**

Je, tunaweza kusema nini kwa mshiriki wa kanisa mvivu/mtegeaji ili kumfanya atambue umuhimu wa kuibua talanta yake na kuitoa kwa wabadilishanaji? Hakutakuwa na mvivu, mzururaji wala mtegeaji, atakayepatikana ndani ya ufalme wa mbinguni. Laiti Mungu angeweka jambo hili katika umuhimu wake wote mbele ya makanisa yaliyo lala! Laiti Sayuni angesimama na kuvaa mavazi yake mazuri! Oh, kwamba angeweza kuangaza! —

—

**Shuhuda Kwa Kanisa 6:434. ChS 90.5**

Kuna kazi ya kufanywa kwa wale wasioijua Kweli, kazi kama ile iliyofanywa kwako ulipokuwa gizani. Umechelewa sana kulala sasa, si wakati wa kulala yrms, umechelewa sana kuwa mvivu na kutofanya kitu. Kwa kila mmoja, Mwenye Nyumba amempa kazi. Hebu twende mbele, na sio kurudi nyuma. Tunataka wongofu wapya kila siku. Tunataka upendo wa Yesu udunde kwa nguvu, mioyoni mwetu, ili tuwe chombo muhimu katika kuokoa roho nyingi.— **The Review and Herald, Juni 10, 1880 . ChS 91.1**

Bwana Yesu anahitaji kwamba kila nafsi inayodai kuwa mwana au binti wa Mungu, haipaswi tu kuacha maovu yote, bali iwe na wingi wa matendo ya upendo, kujinyima, kujikana nafsi na unyenyekevu. Bwana amewasilisha utendaji kazi wa sheria fulani ya akili na matendo, ambayo inapaswa kutuonya kuhusiana na kazi yetu. Anasema: "Yeyote asiye na kitu, hata kile anachoonekana kuwa nacho, atanyang'anywa." Wale wasioboresha fursa zao, ambao hawatumii neema ambayo Mungu huwapa, wana mwelekeo mdogo wa kufanya hivyo, na hatimaye kwa uchovu wa usingizi, hupoteza kile walichokuwa nacho hapo awali. Hawafanyi maandalizi kwa ajili ya wakati ujao wa uhitaji, katika kupata uzoefu

mkubwa, katika kupata ujuzi ulioongezeka wa mambo ya Kiungu, ili kwamba mitihani na majaribu yanapowajia, waweze kusimama. Mateso au majaribu yanapokuja, tabaka hili hupoteza ujasiri na imani yao, na msingi wao unafagiliwa mbali, kwa sababu hawakuona haja ya kufanya msingi wao kuwa thabiti. Hawakuelekeza nafsi zao kwa Mwamba wa milele.— **The Review and Herald, Machi 27, 1894 . ChS 91.2**

Itakuwa kitu cha kuogofya jinsi gani katika siku kuu ya mwisho kupata kwamba wale ambao tumekuwa tukishirikiana nao na kuwajua vyema, wametenganishwa nasi milele; kuona washiriki wa familia zetu, labda watoto wetu wenyewe, hawajaokolewa; kupata wale ambao wametembelea nyumba zetu, na kula kwenye meza zetu, kati ya watu waliopotea. Kisha tutajiuliza swali hili, Je! ni kwa sababu kutokuwa na ustahimilivu, je, ni kwasababu mwenendo wangu haukufanana na Kristo? Je, ni kwasababu sikuweza kuutawala ubinafsi na uchoyo wangu, hivyodini ya Kristo ikawa isiyo na ladha na chukizo kwao? **ChS 91.3**

Ulimwengu lazima uonywe juu ya ujio wa Bwana upesi. Tuna muda kidogo tu wa kufanya kazi. Miaka imepita katika umilele ambao ungeweza kuboreshwa katika kutafuta kwanza ufalme wa Mungu na haki Yake, na katika kueneza nuru kwa wengine. Mungu sasa anawaita watu Wake walio na nuru kuu na wameimarishwa katika Ukweli, wakiwa wamepewa kazi nyingi sana, wafanye kazi kwa ajili yao wenyewe na kwa ajili ya wengine, jinsi ambavyo hawajapata kufanya hapo awali. Tumia kila uwezo; kuleta katika mazoezi kila nguvu, kila talanta iliyokabidhiwa; tumia nuru yote ambayo Mungu amekupa kuwatendea wengine mema. Msikazane kuwa wahubiri, bali kuwa wahudumu wa Mungu.— The Southern Watchman, Juni 20, 1905 **( The Review and Herald, Machi 18, 1902 ). ChS 92.1**

**Vielelezo vya Nguvu**

Upendo wa Mungu umeamka kwa kina Chake kisichoweza

—

kueleweka, au kuchunguzika kwa ajili ya wanadamu, na malaika wanashtuka kuona wapokeaji wa upendo mkuu wa namna hii wakiwa na shukrani ya juu juu tu. Malaika wanashangaa mno jinsi mwanadamu anavyothamini upendo wa Mungu kwa udogo sana. Mbingu inasimama kwa hasira kwa kupuuzwa na kutojali kunakoonyeshwa kwa roho za wanadamu. Je, tunajua kweli jinsi Kristo anavyozichukulia roho za watu? Baba na mama wangejisikiaje, kama wangejua kwamba mtoto wao, aliyepotea kwenye baridi na theluji, alikuwa amepitwa, na kuachwa aangamie, na wale ambao wangeweza kumuokoa? Je, hawangehuzunika na na hata kukasirika sana kwa vitendo vya watu hawa wasiojali? Je, hawangeshutumu wauaji hao kwa hasira kali kama machozi yao, kali kama upendo wao? Mateso ya kila mwanadamu ni mateso ya mtoto wa Mungu, na wale wasionyoosha mkono, wasio na msaada kwa wanadamu wenzao wanaoangamia huchochea hasira Yake ya haki.— **The Desire of Ages, 825 . ChS 92.2**

Nimesoma juu ya mtu ambaye, baada ya kusafiri siku ya majira ya baridi kali kupitia theluji yenye kina kirefu, akaanza kugandishwa na theluji, alizidiwa na baridi kali, ambayo ilikuwa karibu kumaliza nguvu zake muhimu. Na alipokuwa karibu kufa kwa kukumbatiwa na mapande ya barafu, na akiwa karibu kuacha mapambano ya maisha, alisikia

maombolezo ya ndugu msafiri, aliyekuwa analalamika kwa baridi iliyokuwa inakaribia kumwangamiza. Unyenyekevu (na ubinadamu) wake uliamshwa ili kumwokoa. Aliisugua miguu iliyokaa kwenye mapande ya barafu yaliyokuwa miguuni mwake yule mtu aliyepatwa na bahati mbaya (janga) ili apate joto, na, baada ya juhudi kubwa, alimwinua na kumsimamisha kwa miguu yake; na kwa vile hakuweza kusimama, alimbeba kwa mikono yake yenye huruma na kutembea kupitia upepo ule-ule wa theluji aliodhani hangeweza kamwe kufanikiwa kupita akiwa peke yake. Na alipomchukua msafiri mwenzake hadi mahali pa usalama, ndipo uhalisia ulimwangazia mawazoni mwake kwamba katika kumwokoa jirani yake alikuwa amejiokoa mwenyewe pia. Jitihada zake za dhati za kuokoa mwingine zilihuisha na kuyeyusha damu iliyokuwa ikiganda kwenye mishipa yake mwenyewe, na kuunda joto lenye afya katika maeneo yaliyokaribiana na sehemu za nje za mwili wake. Masomo haya lazima yasukumwe kwa waamini wachanga sikuzote, si kwa kanuni tu, bali kwa mfano, ili katika uzoefu wao wa Kikristo waweze kupata matokeo sawa. —**Shuhuda kwa Kanisa4:319, 320. ChS 92.3**

Hampaswi kujifungia wenyewe, na kuridhika kwa sababu mmebarikiwa na ujuzi wa Ukweli. Ni nani aliyeleta Ukweli kwako? Ni nani aliyekuonyesha nuru ya Neno la Mungu? Mungu hakukupa nuru Yakeile iwekwe chini ya pishi. Nimesoma juu ya msafara ambao ulitumwa kumtafuta Sir John Franklin. Watu hawa jasiri waliacha nyumba zao, na kutanga- tanga katika Bahari ya Kaskazini, wakiteseka kwa ufukara, njaa, baridi, na dhiki. Na yote yalifanywa kwa ajili ya nini?—Kwa ajili tu ya heshima ya kugundua maiti za wavumbuzi, au, ikiwezekana, kuwaokoa baadhi ya wahusika wa safari kutoka katika kifo kibaya ambacho lazima kingewajia, isipokuwa msaada uwafikie kwa wakati. Kama wangeweza kumwokoa hata mtu mmoja tu asiangamie, wangehesabu mateso yao kuwa yamefidiwa vizuri. Hii ilifanyika kwa kujitolea kwa faraja na furaha yao yote. **ChS 93.1**

Fikiria hili, na kisha fikiria jinsi tusivyo tayari kujitolea kwa ajili

—

ya wokovu wa roho za thamani zinazotuzunguka hata kwa udogo tu. Hatulazimishwi kwenda mbali na nyumbani, kwa kufanya safari ndefu na ya kuchosha ili kuokoa maisha ya mwanadamu anayeangamia. Milangoni mwetu, kila upande wetu, kila mahali, kushoto na kulia, kuna roho za kuokolewa, roho zinazoangamia, wanaume na wanawake wanaokufa bila tumaini, bila Mungu, na bado sisi tunajisikia kupuuzia na kutojali, kwa kweli tunasema kwa matendo yetu, kama si kwa maneno yetu, "Je, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?" Wanaume hawa waliopoteza maisha katika kujaribu kuokoa watu wengine wanasifiwa na ulimwengu kama mashujaa na wafia dini kwenye maneno ya tanzia. Je, sisi tulio na tazamio la uzima wa milele tunapaswa kuwa na hisia za namna gani, ikiwa hatutoi dhabihu hata ndogo ambazo Mungu anataka kutoka kwetu, kwa ajili ya wokovu wa nafsi za wanadamu?— The Review and Herald, Agosti 14, 1888 . ChS 93.2

Katika mji mmoja huko New England, kisima kilikuwa kikichimbwa. Kazi ilipokaribia kumalizika, mtu mmoja alipokuwa angali chini, ardhi ilizama na kumzika. Mara moja yowe/kengele ikapigwa ili kuwaita watu, na mafundi, wakulima, wafanyabiashara, wanasheria, waliharakisha wakihema ili kumwokoa. Kamba, ngazi, jembe, na majembe vililetwa kwa mikono yenye shauku na iliyo tayari. "Mwokoe, Ee umwokoe!" kilikuwa kilio. ChS 94.1

Wanaume walifanya kazi kwa nguvu isiyokata kukata tamaa, hadi matone ya jasho yakasimama kwenye nyuso zao na mikono yao ikatetemeka kwa bidii wakati wanafanya shime hii. Boma refu lilitupwa chini, ambalo wakalitumia kupiga kelele kwa mtu huyo ali ajibu ikiwa bado yuko hai. Jibu lilikuja, "Hai, lakini fanyeni haraka, panatisha humu ndani." Kwa kelele za furaha walifanya upya juhudi zao, na mwishowe akafikiwa na kuokolewa, na uchangamfu uliopanda ulionekana kuzipenya mbingu zile zile. “Ameokolewa!” ilisikika katika kila barabara mjini. **ChS 94.2**

Je, hii haikuwa bidii na shauku kubwa sana, shauku kubwa mno, ya kumwokoa mtu mmoja tu? Hakika haikuwa hivyo; lakini ni hasara gani ya maisha ya muda ukilinganisha na kupoteza roho za watu milele? Ikiwa hatari ya kupoteza maisha itaamsha mioyoni mwa wanadamu hisia kali sana kama hizo, je, hasara ya nafsi haipaswi kuamshawasiwasi wa ndani zaidi kwa wanadamu wanaodai kutambua hatari ya wale walio mbali na Kristo? Je! watumishi wa Mungu hawataonyesha ari/usongo mkubwa katika kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa nafsi kama ilivyoonyeshwa kwa ajili ya uhai wa mtu mmoja aliyezikwa kisimani?— **Gospel Workers, 31, 32 . ChS 94.3**

**Kusema kwa mdomo Dhidi ya Kuonekana kwa Macho**

Kila Ukweli muhimu unaopokelewa moyoni lazima udhihirishwe maishani. Ni kwa kadiri ya mapokezi ya upendo wa Kristo ambapo wanadamu hutamani kutangaza uwezo wake kwa wengine; na kitendo chenyewe cha kuitangaza, huongeza na kuimarisha thamani yake kwa nafsi zao wenyewe.— **The Review and Herald, Februari 19, 1889 . ChS 94.4**

Imani yetu inapaswa kuzaa matendo mema, kwani imani bila matendo imekufa. — **Shuhuda kwa Kanisa 4:145. ChS 95.1**

Wote wanaopokea ujumbe wa injili ndani ya mioyo yao watatamani kuutangaza. Upendo wa mbinguni unaobebwa na

kutolewa na Kristo lazima uonekane.— **Christ's Object Lessons, p. 125 . ChS 95.2**

Tunapaswa kumsifu Mungu kwa utumishi unaoonekana na kuleta matokeo, kwa kufanya yote tuwezayo kuendeleza utukufu wa Jina Lake.— **Christ's Object Lessons, 300 . ChS 95.3**

Imani yetu kwa wakati huu lazima isiishie kwenye dhana tu, au imani katika nadharia ya ujumbe wa malaika wa tatu. Ni lazima tuwe na mafuta ya neema ya Kristo ambayo yatakayotumika kwenye taa na kuifanya nuru ya uzima iangaze, ikionyesha njia kwa wale walio gizani.
— **Shuhuda kwa Kanisa 9:155. ChS 95.4**

Nguvu zako za kiroho na baraka zitakuwa sawia na kazi ya upendo na matendo mema unayoyafanya. **—Shuhuda kwa Kanisa 3:526. ChS 95.5**

Mengi zaidi yangeweza kufanywa kwa ajili ya Kristo ikiwa wote walio na nuru ya Kweli wangeweka Ukweli kwenye mazoezi ya vitendo. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:40. ChS 95.6**

Nilioneshwa kuwa kama watu tuna upungufu. Kazi zetu hazilingani na imani yetu. Imani

yetu inashuhudia kwamba tunaishi wakati wa kutangazwa kwa ujumbe mzito na muhimu sana kuwahi kupewa wanadamu wa kufa. Walakini kwa mtazamo kamili wa Ukweli huu, jitihada zetu, bidii yetu, roho yetu ya kujitoa kafara, havilingani na tabia ya kazi. Tunapaswa kuamka toka kwa wafu, na Kristo atatupatia uzima. —**Shuhuda kwa Kanisa 2:114. ChS 95.7**

Nendeni kwa imani, na muitangaze Kweli kana kwamba mnaiamini. Hebu wale unaowafanyia kazi waone kwamba kwako hakika ni Ukweli ulio hai. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:42.ChS 95.8**

Tukumbuke kuwa maisha kama ya Kristo ni hoja yenye nguvu zaidi ambayo inaweza kuendelezwa ili kuuthamini Ukristo. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:21. ChS 95.9**

Kuna wengi wanaokiri Jina la Kristo ambao mioyo yao haijashughulika na huduma Yake. Wamejivika tu joho la utauwa, na kwa tendo hili hili wamefanya hukumu yao kuwa kubwa zaidi, na wamekuwa wadanganyifu zaidi na wenye mafanikio zaidi mawakala wa Shetani katika uharibifu wa nafsi.— **The Review and Herald, Machi 27, 1888 . ChS 95.10**

Wale wanaomngojea Bwana, wanasafisha nafsi zao kwa kuitii Kweli. Kwa kukesha kwa bidii, wanachanganya kufanya kazi kwa dhati na juhudi. Kwa sababu wanajua kwamba Bwana
Yuko mlangoni, bidii yao inahuishwa ili kushirikiana na mawakala wa Kiungu katika kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa roho. Hawa ndio watumishi waaminifu na wenye hekima ambao huwapa nyumba ya Bwana "fungu lao la chakula kwa wakati wake." Wanatangaza Ukweli ambao sasa unatumika na kuhusika haswa. Kama vile Henoko, Nuhu, Ibrahimu, na Musa walivyotangaza Ukweli kwa wakati wake, ndivyo watumishi wa Kristo sasa watatoa onyo la pekee kwa kizazi chao.— **The Desire of Ages, 634 . ChS 96.1**

Kusimama kwetu mbele za Mungu hakutegemei kiasi cha nuru ambayo tumepokea, bali kunategemea jinsi tunavyotumia kile tulicho nacho. Kwa hiyo hata wapagani wanaochagua haki kadiri

—

wawezavyo kuitofautisha, wako katika hali nzuri zaidi kuliko wale ambao wamekuwa na nuru kuu, na wanadai kumtumikia Mungu, lakini wanaipuuza na kudharau ile nuru, na kwa maisha yao ya kila siku wanapingana na kujua kwao.— **The Desire of Ages, 239 . ChS 96.2**

Ni fursa ya kila Mkristo, si tu kutazamia, bali kuharakisha ujio wa Bwana wetu Yesu Kristo. Kama wote wanaokiri Jina Lake wangezaa matunda kwa utukufu Wake, jinsi ulimwengu wote ungepandwa mbegu na injili upesi. Kwa upesi mavuno makubwa ya mwisho yangeiva, na Kristo angekuja kukusanya nafaka ya thamani.— **Christ's Object Lessons, 69 . ChS 96.3**

Wakristo wanapaswa kujiamsha wenyewe, na kuchukua majukumu yao yaliyopuuzwa; kwa maana wokovu wa nafsi zao wenyewe hutegemea jitihada zao binafsi.— **The Review and Herald, Agosti 23, 1881 . ChS 96.4**

—

Ibada ya kweli inajumuisha kufanya kazi pamoja na Kristo. Maombi, mawaidha/maonyo, na mazungumzo ni matunda ya thamani ndogo, ambayo mara nyingi hufungwa; lakini matunda yanayodhihirishwa katika matendo mema, katika kutunza wenye uhitaji, yatima, na wajane, ni matunda ya dhati, ya kweli, na hukua kiasili juu ya mti mzuri.— **The Review and Herald, Agosti 16, 1881 . ChS 96.5**

Acha washiriki binafsi wa kanisa wachukue kazi yao iliyoteuliwa ya kueneza na pia kupokea nuru. Hakuna hata mmoja anayesamehewa kwa kuwa mvivu katika shamba la mizabibu la Bwana.— **The Review and Herald, Februari 19, 1889 . ChS 96.6**

Kanuni *ya kutenda* ni tunda ambalo Kristo anatuhitaji tuzae; kufanya matendo ya wema, kusema maneno ya fadhili, ukarimu na kuonyesha upole kwa maskini, wenye uhitaji, walioteseka.— **The Review and Herald, Agosti 16, 1881 . ChS 97.1**

Mwanamke Msamaria ambaye alizungumza na Yesu kwenye kisima cha Yakobo, punde alipompata Mwokozi punde tu aliwaleta wengine Kwake. Alijidhihirisha kuwa mmishenari mwenye ufanisi zaidi kuliko wanafunzi Wake Yesu Mwenyewe. Wanafunzi hawakuona chochote katika Samaria chenye dalili ya kuonyesha kwamba lilikuwa shamba lenye kutia moyo. Mawazo yao yaliwekwa juu ya kazi kubwa ambayo ingefanywa katika siku zijazo. Hawakuona kwamba karibu nao kulikuwa na mavuno ya kukusanywa. Lakini kupitia kwa yule mwanamke waliyemdharau, mji mzima uliletwa kumsikiliza Yesu. Huyu mwanamke alibeba Nuru mara moja kwa watu wa nchi yake. Mwanamke huyu anawakilisha utendaji wa imani ya vitendo katika Kristo.— **The Ministry of Healing, p. 102 . ChS 97.2**

Waadventista Wasabato wanasonga mbele wakifanya maendeleo, wakiongeza idadi yao maradufu, wanaanzisha misheni, na kuinua bendera ya Ukweli katika sehemu zenye giza za dunia; na bado kazi inasonga polepole zaidi kuliko vile Mungu

—

angetaka. [Kwa nini?] Kila mshiriki mmoja mmoja hachochewi kuweka juhudi za dhati anazoweza kufanya, na kila tawi la kazi limelemazwa na ukosefu wa uchaji wa dhati, na watenda kazi waliojitolea, wanyenyekevu, wanaomcha Mungu. Askari wa msalaba wa Kristo wako wapi? Hebu wale wamchao Mungu, watu waaminifu, walio na moyo mmoja, wanaotazama kwa uthabiti utukufu wa Mungu, wajitayarishe kwa vita dhidi ya makosa. Kuna mioyo mingi sana iliyozimia, yenye hofu na woga katika saa hii ya mzozo wa kiroho. Laiti hawa wangefanywa kuwa na nguvu kutokana na udhaifu, na kuwa hodari katika vita, na kuyakimbia majeshi ya wageni!— **Historical Sketches, 290 . ChS 97.3**

Ni kanuni ya ulimwengu wote kwamba wakati wowote mtu anapokataa kutumia nguvu zake alizopewa na Mungu, nguvu hizi huharibika na kupotea. Ukweli ambao mtu hauishi, ambao hautolewi au kupewa kwa watu wengine, hupoteza nguvu zake za uzima, nguvu yake ya uponyaji.— **The Acts of the Apostles, p. 206 . ChS 97.4**

Hakuna kitakachoipa mifupa na nyama uchamungu wako kama kufanya kazi ili kuendeleza jambo unalodai kulipenda, badala ya kulifungia kwenye leso. **— Shuhuda kwa Kanisa**

—

**4:236.ChS 98.1**

Wale wanaojitahidi kudumisha maisha ya Kikristo kimyakimya tu, na kwa kukubali tu baraka zinazokuja kwa njia ya neema, na kutofanya lolote kwa ajili ya Kristo, wanajaribu tu kuishi kwa kula bila kufanya kazi. Na katika ulimwengu wa kiroho kama katika ulimwengu wa asili, jambo hili daima husababisha kuzorota na kuoza. — **Steps to Christ, 80, 81 . ChS 98.2**

**Hatari Inayoambatana na Shughuli ya Umishenari**

Tusisahau kwamba kadiri shughuli zinavyoongezeka, na kupata mafanikio katika kufanya kazi ambayo lazima itimizwe, kuna hatari ya kuamini mipango na mbinu za wanadamu. Kutakuwa na tabia ya kusali kidogo, na kuwa na imani ndogo. Tutakuwa katika hatari ya kupoteza hisia zetu za kumtegemea Mungu, ambaye peke yake Ndiye anayeweza kufanikisha kazi yetu; lakini ingawa huu ndio mwelekeo, mtu asifikirie kuwa chombo cha ubinadamu kinapaswa kufanya kidogo tu. La, hatakiwi kufanya pungufu/machache, bali kufanya mengi zaidi kwa kukubali karama ya kimbingu, Roho Mtakatifu.— **The Review and Herald, Julai 4, 1893 . ChS 98.3**

Kutakuja nyakati ambapo kanisa litachochewa na nguvu za Bwana, na utendaji wa bidii utakuwa matokeo; kwa maana nguvu ya Roho Mtakatifu itiayo uzima itawatia moyo washiriki wake kwenda mbele na kuleta roho kwa Kristo. Lakini utendaji huu utakapodhihirika, watendakazi walio na bidii zaidi watakuwa salama pale tu wanapomtegemea Mungu, na kupitia maombi ya kudumu na ya dhati. Watahitaji kuomba kwa bidii ili kwa neema ya Kristo waokolewe kutokana na kujivunia kazi yao, na kuifanya kazi hiyo kuwa mwokozi wa utendaji wao. Ni lazima wamtazame Yesu daima, ili watambue kwamba ni uweza Wake ndio unaofanya kazi hiyo, na hivyo waweze kutoa utukufu wote kwa Mungu. Tutaitwa kufanya jitihada nyingi zilizoamuliwa kupanua kazi ya Mungu, na sala kwa Baba yetu wa mbinguni itakuwa muhimu zaidi. Itakuwa lazima kushiriki katika sala chumbani, katika familia, na

—

kanisani.— **The Review and Herald, Julai 4, 1893 . ChS 98.4**

Katika makadirio ya marabi, jumla ya dini ilikuwa pilikapilika zilizosongamana daima. Walitegemea utendaji fulani wa nje ili kuonyesha uchaMungu wao mkuu. Hivyo walitenganisha nafsi zao na Mungu, na kujijenga katika kujitosheleza. Hatari sawa bado zipo. Shughuli inapoongezeka, na watu kufanikiwa katika kufanya kazi yoyote kwa ajili ya Mungu, kuna hatari ya kutumainia mipango na mbinu za wanadamu. Kuna tabia ya kuomba kidogo, na kuwa na imani ndogo. Kama wanafunzi wa Yesu, tuko katika hatari ya kupoteza mtazamo wa kumtegemea Mungu, na kutafuta kufanya matendo yao kuwa ndiyo mwokozi. Tunahitaji kumwangalia Yesu kila mara, tukitambua kwamba ni uweza Wake ndio unaofanya kazi hiyo. Wakati tunapaswa kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya wokovu wa waliopotea, ni lazima pia tuchukue muda kwa ajili ya kutafakari, kwa ajili ya maombi, na kwa ajili ya kujifunza Neno la Mungu. Ni kazi tu inayotimizwa kwa sala nyingi, na kutakaswa kwa wema wa Kristo, ndiyo mwishowe itathibitika kuwa yenye matokeo mazuri.— **The Desire of Ages, 362 . ChS 98.5**

**Faraja kwa Wanaoanza Kazi Katika Huduma ya Kikristo**

Watenda kazi waliofanikiwa zaidi ni wale wanaochukua kwa uchangamfu kazi ya kumtumikia Mungu katika mambo madogo. Kila mwanadamu anapaswa kufanya kazi na uzi wa maisha yake, akiufuma kwenye kitambaa ili kusaidia kukamilisha muundo/pateni. **— Shuhuda kwa Kanisa 6:115.ChS 99.1**

Tunapaswa kufanya kazi zetu za kila siku kuwa matendo ya ibada, tukizidi kuongezeka katika manufaa, kwa sababu tunaiona kazi yetu katika nuru ya umilele. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:150. ChS 99.2**

Bwana anayo nafasi kwa kila mtu katika mpango Wake mkuu. Talanta ambazo hazihitajiki huwa hazitolewi. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:37. ChS 99.3**

Kila mmoja anayo nafasi yake katika mpango wa umilele wa mbinguni. Kila mmoja anapaswa kufanya kazi kwa ushirikiano na Kristo kusaidia watu wengine ili waweze kupata wokovu. Kila mwanadamu ana mpango na nafasi ya pekee aliyopewa kufanya katika kazi ya Mungu, kwaajili ya wokovu wa watu hapa duniani. Kama vile tulivyo na nafsi maalum mbinguni, basi tuna kazi maalum ya kufanya hapa Duniani. (Yeye anataka tuifanye kazi yetu ya kuongoa watu kwa umuhimu sawa na nafasi inayotayarishwa kwa ajili yetu katika makao makuu ya mbinguni.)**— Christ's Object Lessons, 326, 327 . ChS 99.4**

Bwana ameweka jicho Lake juu ya kila mmoja wa watu Wake; Yeye Anayo mipango Yake kuhusu kila mmoja. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:12.**

Wote wanaweza kufanya kitu katika kazi. Hakuna atakayetangazwa kuwa hana hatia mbele za Mungu isipokuwa amefanya kazi kwa bidii na bila ubinafsi kwa ajili ya wokovu wa roho nyingi kwa Kristo. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:395.ChS 100.1**

Wajibu wako hauwezi kuhamishika na kwenda kwa mtu mwingine. Hakuna mtu isipokuwa wewe mwenyewe unayeweza

—

kufanya kazi yako. Ukizuia au kubania nuru yako, lazima kuna mtu ataachwa gizani kupitia upuuziaji wako, au kudharau kwako (wajibu wa mtu hauwezi kuhamishika kwenda kwa mwingine). **—Shuhuda kwa Kanisa 5:464. ChS 100.2**

Mtendakazi mnyenyekevu anayeitikia mwito wa Mungu kwa utiifu anaweza kuwa na uhakika wa kupata msaada wa Mungu. Kule kukubali jukumu hili kubwa na takatifu sana, kwenyewe kuna hali ya kuiinua tabia ya mtu kuwa bora. Inaamsha mawazo na nguvu za juu zaidi za kiakili na kiroho, na huimarisha na kutakasa akili na moyo. Kupitia njia ya imani katika uwezo wa Mungu, inastajabisha jinsi ambavyo mtu dhaifu anavyoweza kuwa na nguvu, jinsi juhudi zake zinavyoweza kufanyiwa maamuzi bora, jinsi matokeo ya kazi yake yanavyokuwa makubwa na mengi. Mtu anayeanza na maarifa kidogo, kwa unyenyekevu, na kuelezea kile anachokijua, huku akitafuta kwa bidii kuelewa maarifa mengine zaidi, atapata hazina zote ya mbinguni zikingojea kukutana na mahitaji yake. Kadiri anavyotafuta namna ya kutoa nuru yake kwa watu wengine, ndivyo atakavyopokea nuru zaidi. Kadiri mtu anavyojaribu kulielezea na kulifafanua Neno la Mungu kwa wengine, akibubujika kwa upendo kwa nafsi hizo, ndivyo Neno linavyokuwa wazi zaidi kwake mwenyewe. Kadiri tunavyoendelea kutumia ujuzi wetu na kutumia nguvu zetu, ndivyo tutakavyozidi kupata ujuzi na uwezo zaidi.— **Christ's Object Lessons, p. 354 . ChS 100.3**

Hebu kila mtu na afanye kazi kwa ajili ya Mungu na kwa ajili ya nafsi; kila mtu na aonyeshe hekima, wala asionekane katika uvivu, akingojea mtu aje kumbandikia kwenye kazi fulani ya kufanya. "Mtu fulani" ambaye angeweza kukuweka kazini, hakika yeye mwenyewe ana majukumu mengi kupita kiasi, na wakati

unapotea katika kungoja maagizo yake. Mungu atakupa hekima katika kufanya matengenezo au kurekebisha mambo mara moja; kwa maana wito bado unatolewa, “Mwanangu, nenda ukafanye kazi leo katika shamba Langu la mizabibu.” "Leo kama mtaisikia sauti Yake, msifanye migumu mioyo yenu." Waebrania 3:7, 8 . Bwana anatanguliza hitaji hilo kwa neno la kupendeza “mwana.” Jinsi neno hili linavyoonyesha huruma, sikitiko, lakini pamoja na hili neno kuna mtazamo wa kufanya mambo kwa uharaka! Mwaliko Wake pia ni amri (NENDA au ENENDENI!).— **Testimonies for Parents, Teacher and Students, 419 . ChS 100.4**

Nguvu ya kupinga maovu hupatikana vyema kwa utumishi wenye mkali- wenye upendo na ujasiri.— **The Acts of the Apostles, 105 . ChS 100.5**

Kila tendo, kila tendo la haki na rehema na wema, huleta muziki mbinguni.— **The Review and Herald, Agosti 16, 1881 . ChS 100.6**

Roho ya Kristo ni roho ya kimishenari. Msukumo wa kwanza kabisa wa moyo uliofanywa upya ni kuwaleta wengine pia kwa Mwokozi.— **The Great Controversy, 70 . ChS 101.1**

Njia pekee ya kukua katika neema ni kupendezwa kufanya kazi ileile ambayo Kristo ametuagiza tuifanye.— **The Review and Herald, Juni 7, 1887 . ChS 101.2**

Hupaswi kungojea matukio makubwa au kutarajia uwezo usio wa kawaida kabla ya kufanya kazi kwa ajili ya Mungu.— **Steps to Christ, 83 . ChS 101.3**

Mtu anayeibariki jamii, na kufanikiwa maishani, ndiye ambaye, awe amesoma au hana elimu, anatumia nguvu zake zote katika utumishi wa Mungu na wanadamu wenzake.— **The Southern Watchman, Aprili 2, 1903 . ChS 101.4**

Wengi ambao Mungu amewastahilisha kufanya kazi bora hutimiza machache sana, kwa sababu wanafanya/wanajaribu

kidogo sana.— **Christ's Object Lessons, p. 331 ChS 101.5**

Ikiwa unashindwa mara tisini na tisa kati ya mara mia katika kazi hii ya kuokoa roho, lakini ukafanikiwa kuokoa roho moja tu, kutoka kwenye uharibifu, wewe umefanya tendo zuri katika kusudi la Bwana. —**Shuhuda kwa Kanisa 4:132. ChS 101.6**

Mahusiano kati ya Mungu na kila nafsi ni tofauti na yamesheheni kana kwamba hakuna nafsi nyingine duniani inayoshikiri utunzaji na kujali Kwake, kana kwamba hakuna mtu mwingine duniani ambaye Yeye alimtoa Mwanawe mpendwa afe kwa ajili yake.— **Steps to Christ, 100 . ChS 101.7**

Bwana anaona na kufahamu, Naye atakutumia, licha ya udhaifu wako, ikiwa utatoa talanta yako kama zawadi iliyowekwa wakfu kwa ajili ya huduma Yake; kwa kuwa katika huduma hai, isiyopendelea wale walio dhaifu wanapata nguvu na hufurahia hongera kutoka Yake yenye thamani kuu. Furaha ya Bwana ni pointi yenye nguvu. Ikiwa wewe ni mwaminifu, amani ile ipitayo ufahamu wote itakuwa ni thawabu yako katika maisha haya, na katika maisha ya baadaye utaingia katika raha ya Bwana wako. —**Shuhuda kwa Kanisa 8:34. 101.8**

Watu wenye talanta ndogo, ikiwa ni waaminifu katika kuweka mioyo yao katika upendo

wa Mungu, wanaweza kuleta roho nyingi kwa Kristo. Harlan Page alikuwa fundi duni mwenye uwezo wa kawaida na elimu ndogo; lakini kazi ya kuendeleza kusudi la Mungu mtu huyu aliifanya kuwa jukumu lake kuu, na juhudi zake ziliweka alama kwa mafanikio makubwa sana. Alifanya kazi kwa wokovu wa wanadamu wenzake katika mazungumzo ya faragha na kwa maombi ya dhati. Alianzisha mikutano ya maombi, akapanga shule za Jumapili, na akasambaza vipeperushi na vitabu vingine vya kidini. Na wakati akiwa juu ya kitanda chake cha mauti, na kivuli cha umilele kikiwa juu ya uso wake, aliweza kusema: "Najua kuwa yote ni neema ya Mungu, na siyo kupitia sifa ya chochote ambacho nimefanya, lakini nadhani nina ushahidi kwamba zaidi ya roho mia moja zimeongolewa kwa Mungu kupitia mimi. — **Shuhuda kwa Kanisa 5:307, 308.ChS 101.9**

Ulimwengu huu siyo mbingu ya Mkristo, lakini ni karakana tu ya MUNGU, mahali ambapo tunatengenezwa kufaa ili kuungana na malaika wasio na dhambi katika mbingu takatifu. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:187.ChS 102.1**

Wanafunzi wanyenyekevu na maskini zaidi wa Yesu wanaweza kuwa baraka kwa wengine. Huenda wasitambue kwamba wanafanya wema wowote wa pekee, lakini kwa ushawishi wao wasiouelewa wanaweza kuanza mawimbi ya baraka ambayo yatapanuka na kuwa na kina, na hawataweza kamwe kujua matokeo yenye baraka hadi siku ya thawabu ya mwisho. Watu hawa wajisikii na hawajui kuwa wanafanya jambo lolote kubwa. Hawatakiwi kujichosha na wasiwasi juu ya mafanikio. Inawabidi tu kwenda mbele kimya kimya, wakifanya kwa uaminifu kazi ambayo usimamizi wa Mungu unawapa, na maisha yao hayatakuwa bure. Nafsi zao wenyewe zitakuwa zikikua zaidi ~~na~~ zaidi katika kufanana na Kristo; wao ni watenda kazi pamoja na Mungu katika maisha haya, na hivyo wanastahilisha kwa kazi ya juu zaidi na furaha isiyo na kivuli ya maisha yajayo.— **Steps to Christ, p . ChS 102.2**

Kuna wengi ambao wamejitoa kwa Kristo, ilhali hawaoni nafasi ya kufanya kazi kubwa au kujitolea kafara katika huduma Yake.

—

Hawa wanaweza kupata faraja katika wazo kwamba si lazima kujitoa nafsi mhanga, au kufa kama mfia dini ndiyo kunakubalika na kumpendeza Mungu zaidi; inaweza kuwa si mmishenari ambaye kila siku anakabiliana na hatari na kifo, ndiye ambaye anasimama katika ngazi ya juu zaidi katika vitabu vya mbinguni. Mkristo aliye hivyo katika maisha yake ya faragha, pale watu hawamwangalii, ambaye, katika kujisalimisha kila siku, katika unyofu wa kusudi na usafi wa mawazo, katika upole hata anapochokozwa, katika imani na utauwa, katika uadilifu hata katika lililo dogo zaidi, yule ambaye hata nyumbani, maisha yake yanawakilisha tabia ya Kristo,—mtu wa namna hiyo ndiyo yawezekana hata machoni pa Mungu anaweza kuwa wa thamani zaidi kuliko hata mmishenari hodari ajulikanaye duniani au mfia dini mashuhuri duniani.— **Christ's Object Lessons, p. 403 . ChS 102.3**

Sio kiasi cha kazi iliyofanywa, au matokeo yake yanayoonekana, bali roho ambayo kazi hiyo inafanywa, ndiyo huifanya iwe yenye thamani pamoja na Mungu.— **Christ’s Object Lessons, p. 397 . ChS 103.1**

Idhini ya Mwalimu/Bwana haitolewi kwa sababu ya ukubwa wa kazi iliyofanywa, au kwa sababu ya vitu vingi vilivyopatikana, bali kwasababu ya uadilifu katika hata hivyo vitu vichache.

—

Sio kwa matokeo makubwa tunayopata, bali kwa nia ambazo tunakuwa nazo katika kile tunachotenda, hizo zina uzito kwa Mungu. Yeye Anathamini wema na uadilifu kuliko ukubwa wa kazi iliyokamilishwa. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:510, 511.ChS 103.2**

Usivipite vitu vidogo, na huku ukitazamia kazi kubwa. Unaweza kufanya kazi ndogo kwa mafanikio, lakini ukashindwa kabisa hata katika kujaribu kuanza kazi kubwa na ukakatishwa tamaa. Shikilia popote unapoona kuna kazi ya kufanya. Uwe tajiri au maskini, mkubwa au mdogo, Mungu anakuita ufanye kazi ya huduma imara na hai kwa ajili Yake. Itakuwa kwa kufanya kwa nguvu zako kile ambacho mikono yako itaweza kufanya ndivyo utaendeleza karama na uwezo wa kufanya kazi. Na ni kwa kupuuza na kudharau fursa zako za kila siku ndipo unakuwa usiye na matunda na uliyedumaa. Ndiyo maana kuna miti mingi isiyo na matunda katika bustani ya Bwana. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:129.ChS 103.3**

Bwana anatamani tutumie kila karama tuliyo nayo; na tukifanya hivi, tutakuwa na karama kubwa zaidi za kutumia. Yeye hatujalii kwa njia isiyo ya kawaida sifa ambazo hatuna; lakini tunapotumia kile tulicho nacho, Yeye atafanya kazi nasi kuongeza na kuimarisha kila kitivo. Kwa kila dhabihu ya moyo wote na yenye bidii kwa ajili ya utumishi wa Bwana-mkubwa, nguvu zetu zitaongezeka.— **Christ's Object Lessons, p . ChS 103.4**

Moyo wa Kristo unachangamshwa kwa kuwaona wale ambao ni maskini katika kila maana ya neno hili; anachangamshwa na mtazamo Wake juu ya watu wanaotumiwa vibaya na kuonewa, ambao ni wapole; anachangamshwa na wenye njaa ya haki, kwa kutoweza kuanza kwa wengi. Yeye Anakaribisha, ni kana kwamba, hali ileile ya mambo ambayo yangevunja moyo wahudumu wengi.— **Gospel Workers, 37 . ChS 103.5**

Hatuhitaji kwenda katika nchi za kipagani, au hata kuondoka kwenye mduara mwembamba wa nyumbani, ikiwa ni pale ambapo

—

wajibu wetu uko, ili kufanya kazi kwa ajili ya Kristo. Tunaweza kufanya hivi katika mduara wa nyumbani, na kanisani, miongoni mwa wale tunaoshirikiana nao, na ambao tunafanya nao biashara au tuna mahusiano nao ya kikazi.— **Steps to Christ, p.81. ChS 103.6**

Ikiwa tunayafanya maisha na mafundisho ya Kristo kuwa somo letu, kila tukio linalopita litatoa fungu kwa ajili mazungumzo ya kuvutia, hubiri la kusisimua, au hotuba ya kupendeza. — **Shuhuda kwa Kanisa 9:63. ChS 104.1**

Maisha ya duniani ni mwanzo wa maisha ya mbinguni; elimu ya duniani ni uanzishwaji wa kanuni za mbinguni; maisha-kazi ya hapa ni mafunzo kwa ajili ya maisha-kazi huko. Kile tulicho sasa, katika tabia na utumishi mtakatifu, ndicho kielelezo hakika cha vile tutakavyokuwa.— **Education, p. 307 . ChS 104.2**

Wale wanaokataa fursa ya upendeleo ya ushirika na Kristo katika huduma Yake, wanakataa mafunzo ya pekee ambayo yanampa mtu stahiki/kufaa kwa ajili ya kushiriki Naye katika utukufu Wake. Wanakataa mafunzo ambayo katika maisha haya yanatoa nguvu na heshima ya tabia.— **Education, 264 . ChS 104.3**

Mtu yeyote asidhani kwamba anaweza kuishi maisha ya ubinafsi/uchoyo, halafu, akiwa ametumikia maslahi yake binafsi, aingie katika furaha ya Bwana wake. Katika furaha ya upendo usio na ubinafsi hakuweza kushiriki. Mtu huyu asingefaa katika nyua za mbinguni. Hawakuweza kuthamini na kufahamu mazingira safi ya upendo ambayo yameenea mbinguni. Sauti za malaika na muziki wa vinubi vyao havitawaridhisha watu kama hao. Kwa akili zao sayansi ya mbinguni ingekuwa ni fumbo au kitendawili tu.— **Christ's Object Lessons, 364, 365 . ChS 104.4**

Kristo anatuita tufanye kazi kwa uvumilivu na subira kwa ajili ya maelfu wanaoangamia katika dhambi zao; watu waliotawanyika katika nchi zote, kama masalio/mabaki ya ajali, kwenye ufuo wa jangwa. Wale wanaoshiriki katika utukufu wa Kristo lazima washiriki pia huduma Yake, ya kuwasaidia watu walio dhaifu, wanyonge, na waliokata tamaa. **—Shuhuda kwa Kanisa Church 9:31.ChS 104.5**

Watu wa kawaida wanapaswa kuchukua nafasi zao kama watendakazi. Kwa kushiriki huzuni za wanadamu wenzao kama Mwokozi alivyoshiriki huzuni za wanadamu, kwa imani watamuona Mwokozi akifanya kazi nao. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:272. ChS 104.6**

Kristo amesimika picha Yake kwa kila mfuasi. Kila mmoja ambaye Mungu amemchagua tangu awali "afanane na mfano wa Mwanawe." Katika kila mmoja upendo wenye ustahimilivu wa Kristo, utakatifu Wake, upole, rehema, na Ukweli Wake, vyapaswa kudhihirishwa kwa ulimwengu.— **The Desire of Ages, p . ChS 104.7**

Wito kwa ajili kuweka yote kwenye madhabahu ya huduma huja kwa kila mmoja. Hatujaalikwa sote kutumika kama Elisha alivyotumika, wala hatujaagizwa kuuza kila kitu tulicho nacho; lakini Mungu anataka sisi tuuweke utumishi Wake kwenye nafasi ya kwanza katika maisha yetu, tusiruhusu siku yoyote kupita bila kufanya jambo la kuendeleza kazi Yake duniani. Yeye Hatarajii

—

kutoka aina moja ya huduma. Mtu anaweza kuitwa kuhudumu katika nchi ya kigeni; mwingine anaweza kuombwa atoe mali yake kwa ajili ya kusaidia kazi ya injili. Mungu hukubali sadaka ya kila mmoja. Cha muhimu, ni kuyatoa maisha wakfu a na masilahi yake yote. Wale wanaojiweka wakfu kwa jinsi hii, watausikia na kuutii wito wa Mbingu.— **Prophets and Kings, 221 . ChS 105.1**

Mtu mwenye hekima ya kidunia, ambaye anatafakari na kupanga, na ambaye shughuli zake huwa akilini mwake, anapaswa kutafuta kuwa na hekima katika mambo ya manufaa ya milele. Ikiwa angeweka nguvu nyingi kadiri hiyo ili kupata hazina ya mbinguni na maisha ambayo yanapimwa na urefu wa maisha ya Mungu kama anavyofanya ili kupata faida ya ulimwengu, ni nini ambacho hangeweza kutimiza? **— Shuhuda kwa Kanisa 6:297. ChS 105.2**

Mungu atahamisha kazi Yake ya kutangaza ujumbe wa Ukweli wa sasa juu ya watu walio katika nafasi za unyenyekevu. Wengi wao wataonekana wakikimbia huku na kule, wakibidishwa na Roho wa Mungu kuwapa nuru wale walio gizani. Ukweli ni kama moto katika mifupa yao, ukiwajaza shauku inayowaka ya kuwaangazia wale waliokaa gizani. Wengi, hata kati ya wale wasio na elimu, watatangaza Neno la Bwana. Watoto watasukumwa

na Roho Mtakatifu kwenda kutangaza ujumbe wa mbinguni. Roho atamwagwa juu ya wale ambao hujitoa kwa maongozi Yake. Wakiziondoa sheria za mwanadamu zinazowafunga na kwa harakati za tahadhari, watajiunga na jeshi la Bwana. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:26, 27. ChS 105.3**

## Maisha ya Kikristo Katika Mazingira

Moyo unaopokea Neno la Mungu si kama dimbwi linalokauka maji, si kama birika lililovunjika linalopoteza hazina yake. Ni kama mkondo wa kijito kilicho katika mlima, unaolishwa na chemchemi zisizokoma, ambazo maji yake baridi, yanayometa-meta huruka kutoka mwamba hadi mwamba, na kuburudisha wale waliochoka, wenye kiu, wenye kulemewa na mizigo. Ni kama mto unaotiririka kila mara, na unaposonga mbele, unazidi kuwa na kina zaidi na zaidi, na kupanuka zaidi, mpaka maji yake ya uzima yatakapoenea juu ya dunia yote. Kijito kinachoimba kinapokuwa kikisonga mbele, huacha nyuma zawadi yake ya upya, mimea iliyonawiri na kuzaa matunda. Nyasi kwenye kingo zake ni kijani kibichi mno, miti kando yake imenawiri kwa rangi nzuri, maua ni mengi zaidi. Wakati ardhi iko wazi kama jangwa na kahawia chini ya joto kali linalochoma vitu kwenye majira ya joto, mstari wa kijani kibichi na kunawiri, huashiria mkondo wa mto. **ChS 105.4**

Ndivyo ilivyo kwa mtoto wa Mungu wa kweli. Dini ya Kristo inajidhihirisha yenyewe kama kanuni yenye uhai, inayoenea, yenye uzima, inayofanya kazi, na nishati ya kiroho. Moyo unapofunguliwa kwa mvuto wa kimbingu wa Ukweli na upendo, kanuni hizi zitatiririka tena kama vijito jangwani, na kusababisha kuzaa/matunda yaonekane mahali ambapo sasa ni tasa na kuna upungufu.— **Prophets and Kings, 233, 234 . ChS 106.1**

## Maneno ya Kikristo

Kuna maneno matatu katika kaulimbiu ya maisha ya Kikristo, ambayo yanapaswa kuzingatiwa ikiwa hatungekuwa na

—

msukumo wa shetani juu yetu; yaani, Kesha, omba, fanya kazi. —**Shuhuda kwa Kanisa 2:283.ChS 106.2**

Kila nafsi iliyomkiri Kristo imeahidi kutii na kufanya yote yanayowezekana kuwa mtendakazi wa kiroho, kuwa hai, kuwa na bidii/ari, na ufanisi katika utumishi wa Bwana wake. Kristo anatarajia kila mtu kufanya wajibu wake; hebu hii iwe ndiyo kaulimbiu na mtindo wa maisha katika safu zote za jeshi la wafuasi wa Mungu. —**Shuhuda kwa Kanisa 5:460. ChS 106.3**

## Kupooza Kiroho

Nguvu huja kwa jitihada za mazoezi. Wote wanaotumia uwezo ule ambao Mungu amewapa watakuwa na uwezo ulioongezeka wa kujitolea kwa ajili ya huduma Yake Bwana. Wale ambao hawafanyi chochote katika kazi ya Mungu watashindwa kukua katika neema na katika ujuzi wa Kweli. Mtu ambaye angelala chini na kukataa kutumia viungo vyake hivi karibuni angepoteza nguvu zake zote. Kwa hivyo Mkristo ambaye hatumii nguvu alizopewa na Bwana na kuzifanyia mazoezi, sio tu anashindwa kukua na kuwa kama Kristo, lakini pia anapoteza nguvu ambazo tayari anazo; na anakuwa mlemavu wa kiroho. Ni wale ambao wana upendo

kwa Mungu na ndugu zao, wanaojitahidi kuwasaidia wengine ili waweze kuimarishwa na kutulia katika Ukweli. Mkristo wa Kweli hufanya kazi ya Mungu, si kwa sababu ya msukumo/mihemko, bali ni kwa sababu ya Kanuni ya Mungu; na wala si kwa siku au mwezi, lakini wakati wote wa Maisha yake. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:393.ChS 106.4**

**Dawa ya Uhakika**

Kwa waliokata tamaa kuna dawa ya uhakika,-imani, sala, kazi. Imani na utendaji vitatoa uhakikisho na kuridhika moyo ambako kutaongezeka siku baada ya siku. Je, unashawishiwa kuacha hisia za wasiwasi au kukata tamaa kabisa? Katika siku za giza, wakati mwonekano unaogofya au sio wa kirafiki zaidi, wewe usiogope. Uwe na imani kwa Mungu. Yeye Anajua hitaji lako. Yeye Ana uwezo wote. Upendo na huruma Zake zisizo na kikomo hazichoki. Usiogope kwamba Yeye atashindwa kutimiza ahadi Yake. Yeye ni Ukweli wa milele. Kamwe hatabadili agano alilofanya na wale wanaompenda. Naye atawapa watumishi Wake waaminifu kipimo cha ufanisi ambacho uhitaji wao unadai.— **Prophets and Kings, 164, 165 . ChS 106.5**

Kuna tiba moja tu ya kweli ya uvivu wa kiroho, nayo ni kazi - kufanya kazi na roho zinazohitaji msaada wako. **—Shuhuda kwa Kanisa 4:236.ChS 107.2**

Hiki ndicho kichocheo ambacho Kristo ameagiza kwa ajili ya nafsi iliyokata tamaa, yenye mashaka, na inayotetemeka. Hebu wenye huzuni, waendao kwa machozi mbele za Bwana, wainuke na kumsaidia mtu yule anayehitaji msaada. **— Shuhuda kwa Kanisa 6:266.ChS 107.3**

Wakristo wanaoendelea kukua katika unyofu, bidii, ari, shauku, upendo—Wakristo hao hawarudi nyuma kamwe (no backsliding).— **The Review and Herald, Juni 7, 1887 . ChS 107.4**

Ni wale ambao hawajishughulishi na kazi hii isiyo na ubinafsi ambao wana uzoefu ulio na ugonjwa, na huchoka kwa kuhangaika, mashaka, manung'uniko, kutenda dhambi, na kutubu, mpaka

—

wanapoteza akili kabisa kuhusu nini kinaunda dini ya kweli. Wanahisi kwamba hawawezi kuurudia ulimwengu, na kwa hivyo wananing'inia kwenye upindo wa Sayuni, wakiwa na viwivu vidogo-vidogo, kijicho, kukatishwa tamaa, na majuto. Wamejaa kutafuta makosa, na kujilisha makosa na mapotofu ya ndugu zao. Wana uzoefu usio na tumaini, usio na imani, usio na jua, usio na uchangamfu katika maisha yao ya kidini.— **The Review and Herald, Septemba 2, 1890 . ChS 107.5**

**Visingizio Visivyo na Msingi**

Yesu alipoondoka, Alimwachia kila mtu kazi Yake, na "jamani hakuna la kufanya" ni kisingizio kisicho na msingi. "Hakuna la kufanya" ndiyo sababu ya majaribu miongoni mwa ndugu; kwa maana Shetani atajaza mawazo ya wavivu na mipango yake mwenyewe, na kuwaweka kazini. "Hakuna la kufanya" huleta ushuhuda mbaya dhidi ya ndugu, na mafarakano katika kanisa la Kristo. Yesu anasema, "Yeye asiyekusanya pamoja Nami hutawanya."— **The Review and Herald, Machi 13, 1888 . ChS 108.1**

Ndugu na akina dada, wengi wenu mnatoa udhuru kwamba hamtaweza kufanya kazi

kwa ajili ya wengine. Lakini je! Mungu alikuumba ukiwa huna uwezo kabisa namna hiyo? Je! Kutokuwa na uwezo huu hakukuzalishwa na kutofanya kazi kwako mwenyewe na kuendelezwa na chaguo lako la makusudi? Je! Mungu hakukupa angalau talanta moja uliyopaswa kuiboresha, sio kwa faida yako mwenyewe, au starehe na kujiridhisha, lakini kwa ajili Yake? Je! Umetambua wajibu wako, kama mtumishi Wake aliyeajiriwa, kumwingizia mapato kwa kutumia busara na ustadi wa mtaji huu uliokabidhiwa? Je! Haujapuuza na kudharaufursa za kuboresha nguvu zako kufikia upande huu -duniani? Ni kweli kwamba ni wachache ambao wametambua uhitaji wa uwajibikaji wao kwa ajili ya Mungu. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:457. ChS 108.2**

Wengi wamekuwa na fikra kama watafanikiwa biashara zao, hawawezi kufikiria kufanya chochote kwa ajili ya wokovu wa roho zinazopotea, wala hawafikiri kundeleza kazi aliyoianziasha Mwokozi wao. Wanasema hawawezi kufanya mambo nusu-nusu hivyo wameachana na wajibu wao wa mambo ya kidini,na kujizamisha katika mambo ya dunia. Wanafanya biashara zao kuwa kipaumbele cha kwanza na kumsahau Mungu, na Yeye hafurahishwi nao. Ikiwa kama kuna mtu yeyote anayefanya biashara ambayo haiwezi ikamfanya akue na kusonga mbele kiroho na utakatifu kamili katika kumcha Mungu, imempasa abadili na kufanya biashara ambayo atakuwa na Yesu kila wajatu.— **Shuhuda kwa Kanisa 2:233, 234.ChS 108.3**

### Lenga Kujipatia Taji iliyosheheni nyota, Taji nzito

Hatupaswi kuchoka au kukata tamaa. Ingekuwa hasara mbaya sana kubadilishana utukufu unaostahimili kwa urahisi, usahili, na starehe, au kwa ajili ya anasa za kimwili. Zawadi kutoka kwa mkono wa Mungu inamngoja mshindi. Hakuna hata mmoja wetu anayestahili; ni bure, imetolewa bila gharama kwa upande wetu. Zawadi hii itakuwa ya ajabu na ya utukufu, lakini tukumbuke kwamba “nyota moja hutofautiana na nyota nyingine kwa utukufu.” Lakini tunapohimizwa kujitahidi kwa ustadi, hebu na

—

tulenge, kwa nguvu za Yesu, kuwa taji nzito ya nyota. “Wale walio na hekima watang’aa kama anga, na wale waletao wengi kwenye haki kama nyota milele na milele.”— **The Review and Herald, October 25, 1881 . ChS 108.4**

**Huduma Imelipwa**

Bwana katika kuja Kwake atachunguza kila talanta; atahitaji faida kwa mtaji aliotukabidhi. Kwa kudhililishwa na uchungu Wake, kwa maisha Yake ya taabu na kifo cha aibu, Kristo amelipa kwa ajili ya huduma ya wote ambao wamelibeba Jina Lake na kukiri kuwa watumishi Wake. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:104. ChS 109.1**

Wote wako chini ya wajibu wa dhati wa kuboresha kila uwezo wa kazi ya kuleta roho Kwake. “Ninyi si mali yenu wenyewe,” Anasema; "maana mlinunuliwa kwa thamani;" sasa basi mtukuzeni Mungu kwa maisha ya huduma ambayo yatawaleta wanaume na wanawake kutoka katika dhambi hadi kwenye haki. 1 Wakorintho 6:19, 20. Tumenunuliwa kwa bei ya uzima wa Kristo Mwenyewe, tumenunuliwa ili tumrudishie Mungu yalio Wake katika utumishi wa uaminifu. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:104.ChS 109.2**

Mungu amenipa ujumbe kwa watu Wake. Lazima watu waamke, watandaze hema zao, na kupanua mipaka yao. Ndugu na dada zangu, mmenunuliwa kwa bei, na vyote mlivyo navyo na mlivyo ni vya kutumiwa kwa utukufu wa Mungu na kwa faida ya wanadamu wenzenu. Kristo alikufa msalabani kuokoa ulimwengu unaoangamia dhambini. Yeye Anaomba ushirikiano wako katika kazi hii. Wewe unapaswa kuwa mkono Wake wa msaada. Kwa bidii isiyochoka, ukijitahidi kutafuta kuokoa waliopotea. Kumbuka kwamba ni dhambi zako ambazo zilifanya msalaba uwe wa lazima. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:9.ChS 109.3**

Wafuasi wa Kristo wamekombolewa kwa ajili ya huduma. Bwana wetu anafundisha kwamba lengo la kweli la maisha ni huduma. Kristo Mwenyewe alikuwa mtenda kazi, na kwa wafuasi Wake wote anawapa sheria ya utumishi,—huduma kwa Mungu na kwa wanadamu wenzao.... Sheria ya utumishi inakuwa kiungo kinachotuunganisha sisi kwa Mungu na kwa wanadamu wenzetu. **— Christ's Object Lesson, p. 326 . ChS 109.4**

**Songa Mbele**

Mara nyingi maisha ya Kikristo yamezingirwa na hatari, na wajibu unaonekana kuwa mgumu kutekeleza. Picha za mawazo zinazokaribia uharibifu mbele, na utumwa na kifo nyuma. Ila sauti ya Mungu hunena waziwazi, Songa mbele. Hebu na tuitii amri, ingawa macho yetu hayawezi kupenya giza. Vikwazo vinavyozuia maendeleo yetu kamwe havitatoweka mbele ya roho ya kusitisha, ya mashaka. Wale wanaoahirisha utii hadi kila hali ya kutokuwa na uhakika itoweke, na hakuna hatari ya kushindwa au kufeli, hawatatii kamwe. Imani hutazama zaidi ya magumu, na hushikilia yale yasiyoonekana, hata Uweza wa yote, kwa hiyo haiwezi kutatanishwa. Imani ni kuukumbatia mkono wa Kristo katika kila dharura.— **Gospel Workers, p. 262 . ChS 110.1**

Mawazo yetu ni finyu sana. Mungu anatoa wito wa kuendelea mbele katika kazi ya kueneza nuru. Ni lazima tujifunze njia na mbinu zilizoboreshwa za kuwafikia watu. Tunahitaji kusikia kwa masikio ya imani Kapteni mkuu wa jeshi la Bwana akisema,

—

“Songa mbele.” Ni lazima tutende, na Mungu hatatuangusha. Yeye Atafanya sehemu Yake wakati sisi kwa imani tunafanya yetu. Akina kaka na akina dada ambao mmekaa katika Ukweli kwa muda mrefu, hamjafanya kazi ambayo Mungu anawaita ninyi kufanya. Je, Upendo wako kwa nafsi uko wapi?— **Historical Sketches, 289, 290 . ChS 110.2**

Ilikuwa ni furaha ya Kristo kuokoa roho. Hebu hii iwe kazi yako na furaha yako. Tekeleza majukumu yote na utoe dhabihu zote kwa ajili ya Kristo, Naye atakuwa msaidizi wako daima. Nenda mbele moja kwa moja ambapo sauti ya wajibu inaita; usiruhusu magumu yanayoonekana yakuzuie. Chukua madaraka yako uliyopewa na Mungu, na unapobeba mizigo yako mizito nyakati fulani, usiulize, “Mbona ndugu yangu amesimama bila kazi, mbona hajawekwa nira juu yake? Fanya wajibu ulio karibu nawe zaidi, na uufanye kikamilifu na vizuri, bila kutamani sifa, bali umfanyie kazi Bwana-mkubwa kwa sababu wewe ni Wake.— **The Southern Watchman, Aprili 2, 1903 . ChS 110.3**

Njia ya watu wa Mungu inapaswa kuwa ya kuelekea juu na kwenda katika ushindi. Yeye Aliye

—

mkuu kuliko Yoshua anayaongoza majeshi ya Israeli. Mmoja Yuko katikati yetu, tena ni Kiongozi Mkuu wa wokovu wetu, aliyesema kwa ajili ya kutiwa moyo kwetu: “Na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” “Jipe moyo; nimeushinda ulimwengu.” Yeye Atatuongoza kwenye ushindi wa hakika. Kile Mungu anachoahidi, Anaweza wakati wo wote kufanya. Na kazi anayowapa watu Wake kuifanya, Yeye Anaweza kuitimiza kupitia kwao. Tukiishi katika maisha ya utii mkamilifu, ahadi Zake zitatimizwa kwetu. ___**Shuhuda kwa Kanisa 2:122. ChS 110.4**

Kwa nini hatuwi na hatuchangamshi na kuwa na ari yaRoho ya Kristo? Kwa nini mioyo yetu haisukumwi hata kidogo na vilio vya kusikitisha vya ulimwengu unaoteseka? Je, tunazingatia fursa yetu kuu ya kuongeza nyota kwenye taji ya Kristo - roho iliyofunguliwa kutoka kwa minyororo ambayo Shetani ameliifunga, roho iliyookolewa katika ufalme wa Mungu? Kanisa lazima litambue wajibu wake wa kupeleka injili ya Ukweli wa sasa kwa kila kiumbe. Ninakusihi usome sura ya tatu na ya nne ya Zekaria. Sura hizi zikieleweka, zikipokelewa, kazi itafanywa kwa wale walio na njaa na kiu ya haki, kazi ambayo inamaanisha kwa kanisa: "Songa mbele na juu." **—Shuhuda kwa Kanisa 6:296. ChS 111.1**

Idadi kubwa ya wakaaji wa dunia hii wametoa utii wao kwa adui. Lakini hatujadanganyika. Licha ya ushindi dhahiri wa Shetani, Kristo anaendeleza kazi Yake katika Patakatifu pa mbinguni na duniani. Neno la Mungu linaonyesha uovu na ufisadi ambao ungekuwepo katika siku za mwisho. Tunapoona utimilifu wa unabii, imani yetu katika ushindi wa mwisho wa ufalme wa Kristo inapaswa kuimarisha; nasi twapaswa kwenda tukiwa na ujasiri mpya wa kufanya kazi yetu iliyowek~~wa~~.— **Gosple Workers, 26, 27 . ChS 111.2**

## Tukio la Kuvutia

Katika maono ya usiku tukio la kuvutia sana lilipita mbele yangu.

—

Niliona mpira mkubwa wa moto ukianguka miongoni mwa baadhi ya majumba mazuri, na kusababisha uharibifu wa ghafla. Nilimsikia mtu akisema: “Tulijua kuwa hukumu za Mungu zilikuwa zikija juu ya dunia, lakini hatukujua kwamba ingekuwa mapema kiasi hiki." Wengine, kwa sauti za uchungu, walisema: "Mlijua!? Kwa nini basi hamkutuambia? Sisi hatukujua." Kila upande nilisikia maneno kama hayo ya kulaumu yakisemwa. Kwa huzuni kubwa nikaamka. Nikalala tena, na nilionekana kuwa kwenye kusanyiko kubwa. Moja ya mamlaka ilikuwa Akihutubia mkusanyiko, ambaye mbele yake ilitandazwa ramani ya dunia. Alisema kwamba ramani ilifananishwa na shamba la mizabibu la Mungu, ambalo ni lazima lilimwe. Kama vile nuru kutoka mbinguni imulikavyo kila mtu, hiyo ilipaswa kuakisi nuru kwa wengine. Taa zilipaswa kuwashwa mahali pengi, na kutoka kwenye hizi taa bado taa zingine zilipaswa kuwashwa. Maneno hayo yalirudiwa: "Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu. Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru

yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni. " Mathayo 5:13-16. Nikaona Mihilimili mikubwa ya nuru ikiangaza kutoka mijini na vijijini, na kutoka mahali pa juu na mahali pa chini pa dunia. Neno la Mungu likatiiwa, na matokeo yake yalikuwa ni kumbukizi Lake katika kila mji na kijiji. Ukweli Wake ulitangazwa ulimwenguni kote. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:28, 29. ChS 111.3**

## SURA YA 10 MBINU

Kwa umuhimu sawa na mahubiri ya hadhara ni kazi ya nyumba kwa nyumba katika nyumba za watu. Katika miji mikubwa kuna makundi fulani ambayo hayawezi kufikiwa na mikutano ya hadhara. Hawa lazima watafutwe nje kama mchungaji anavyowatafuta kondoo wake waliopotea. Bidii, na juhudi kibinafsi lazima ziwekwe kwa niaba yao. Wakati kazi ya binafsi inapopuuzwa, fursa nyingi za thamani zinapotea, ambazo kama zingelifikwa, zingeendeleza kazi bila kusita. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:111. ChS 113.1**

Matendo, pamoja na maneno, ya huruma yanahitajika. Kristo alitanguliza kutoa ujumbe Wake kwa matendo ya upendo na wema. Hebu watendakazi hawa waende nyumba kwa nyumba, wakiwasaidia watu pale ambapo msaada unahitajika na, kama fursa itapatikana, waeleze kisa cha msalaba Kristo Ndiye anayepaswa kuwa maandiko yao. Hawana haja ya kusimamia masomo ya mafundisho makuu; hebu wazungumze juu ya kazi na dhabihu ya Kristo. Hebu waishikilie haki Yake, katika maisha yao wakiudhihirisha usafi Wake. **— Shuhuda kwa Kanisa 7:228. ChS 113.2**

Mungu hana upendeleo.Atatumia Wakristo wanyenyekevu, waliojitoa, hata kama hawajapata elimu nyingi ya darasani kama wengine. Hebu watu kama hawa washiriki katika kumtumikia Yeye kwa kufanya kazi ya nyumba kwa nyumba. Wakikaa kukota moto kwa mazungumzo, wanaweza—wakiwa wanyenyekevu,

—

wenye busara, na wacha Mungu— kufanya zaidi kukidhi mahitaji halisi ya familia kuliko mchungaji aliyewekewa mkono. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:21. ChS 113.3**

Miongoni mwa washiriki wa makanisa yetu kunapaswa kuwa na kazi zaidi ya nyumba kwa nyumba katika kuisoma Biblia na kusambaza vitabu (madara ya Biblia nyumbani Bible Study). **—Shuhuda kwa Kanisa 9:127. ChS 113.4**

Wale wanaoshiriki katika kazi ya nyumba kwa nyumba watapata fursa za huduma katika Nyanja nyingi. Wanapaswa kuwaombea wagonjwa na wanapaswa kufanya yote wawezayo kuwaondolea mateso. Wanapaswa kufanya kazi kati ya watu wa hali ya chini, maskini, na waliokandamizwa. Tunapaswa kuwaombea na kuomba nao wanyonge ambao hawana nguvu ya kutaka kudhibiti tamaa za mwili na matamanio ambayo yameshusha hadhi zao. Jitihada ya bidii na ya kudumu lazima ifanywe kwa ajili ya wokovu wa wale ambao shauku ya moyo inaamshwa. Wengi wanaweza kufikiwa tu kupitia matendo ya wema/ukarimu usiojifikiria binafsi. Matakwa yao ya kimwili lazima kwanza yatimizwe ili yasiwepo tena.

—

Wanapoona uthibitisho wa upendo wetu usio na ubinafsi, itakuwa rahisi kwao kuamini katika upendo wa Kristo. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:83, 84.ChS 113.5**

Hebu watenda kazi waende nyumba kwa nyumba, wakiifungua Biblia kwa watu, wakiyasambaza machapisho wakiwaambia wengine juu ya nuru ambayo imebariki roho zao wenyewe. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:123. ChS 114.1**

Mwokozi wetu alienda nyumba kwa nyumba, akiwaponya wagonjwa, akiwafariji waombolezaji, akiwatuliza walioteseka, akinena amani kwa waliokata tamaa. Aliwachukua watoto wadogo mikononi Mwake na kuwabariki, na kusema Naneno ya matumaini na faraja kwa akina mama waliochoka. Kwa upole na upole na huruma nyororo isiyokoma, Alikutana na kila aina ya ole na mateso ya mwanadamu. Sio kwa ajili Yake Mwenyewe, bali kwa ajili ya wengine alifanya kazi. Alikuwa mtumishi wa wote. Ilikuwa ni chakula na kinywaji Chake kuleta tumaini na nguvu kwa wote aliokutana nao. — **Gospel Workers, 188 . ChS 114.2**

Uwasilishaji wa Ukweli, kwa upendo na urahisi, kutoka nyumba hadi nyumba, yanapatana na maagizo ambayo Kristo aliwapa wanafunzi Wake alipowatuma kwenda katika safari yao ya kwanza ya umishenari. Kwa nyimbo za sifa, kwa sala za unyenyekevu, za kutoka moyoni, wengi watafikiwa. Mtendakazi wa mbingu atakuwepo ili kuisadikisha mioyo. "Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote," ni ahadi Yake. Pamoja na uhakikisho wa uwepo wa kudumu wa msaidizi kama huyo tunaweza kufanya kazi kwa imani na matumaini na ujasiri. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:34.**

Watendakazi wa nyumba kwa nyumba wanahitajika. Bwana ataka jitihada zilizoamuliwa ziwekwe mahali ambapo watu hawajui lolote kuhusu Kweli ya Biblia. Kuimba na maombi na usomaji wa Biblia unahitajika katika nyumba za watu. Sasa, sasa hivi, ndio wakati wa kutii agizo, "Mkiwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi." Wale wanaofanya kazi hii lazima wawe na ujuzi tayari wa Maandiko. "Imeandikwa" itakuwa silaha yao ya

—

ulinzi.— **Counsels to Parents, Teachers, and Students, 540 . ChS 114.4**

Ndugu na dada zangu, watembeleeni wale wanaoishi karibu nanyi, na kwa huruma na wema tafuta kufikia mioyo yao. Hakikisha unafanya kazi kwa namna ambayo itaondoa chuki na ubaguzi badala ya kuvitengeneza vitu hivyo. Na kumbuka kwamba wale wanaojua Ukweli kwa wakati huu na bado wanafungia juhudi zao kwenye makanisa yao wenyewe, wakikataa kufanya kazi kwa ajili ya majirani zao ambao hawajaongoka, wataitwa kutoa hesabu ya majukumu ambayo hawakuyatekeleza. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:34.ChS 115.1**

Katika safari hii ya kwanza wanafunzi walipaswa kwenda tu mahali ambapo Yesu alikuwa ametangulia kuwa hapo mbele yao, na alikuwa amepata marafiki. Maandalizi yao kwa ajili ya safari yalikuwa yawe ya aina sahili zaidi. Hakuna kitu kilichoruhusiwa kugeuza mawazo yao kutoka kwa kazi yao kuu, au kwa njia yoyote kuchochea upinzani miongoni mwa watu na kufunga mlango kwa kazi zaidi kutendeka. Hawakupaswa kuigiza mavazi ya walimu wa dini, wala kutumia mavazi yoyote yatayowatofautisha na wakulima wanyenyekevu. Hawakupaswa kuingia katika masinagogi na kuwaita watu pamoja kwa ajili ya ibada ya hadhara au umma; jitihada zao

zilipaswa kufanywa katika kazi ya nyumba kwa nyumba. Hawakupaswa kupoteza wakati katika salamu zisizo na lazima, au katika kwenda nyumba kwa nyumba kwa ajili ya kutumbuizwa au kujipatia burudani. Lakini katika kila mahali walipaswa kukubali ukarimu wa wale waliostahili, wale ambao wangewakaribisha kwa moyo kana kwamba wanamkaribisha Kristo Mwenyewe. Walipaswa kuingia kwenye makao hayo kwa salamu nzuri, "Amani iwe kwenye nyumba hii." Nyumba hiyo ingebarikiwa kwa sala zao, nyimbo zao za sifa, na ufunguzi wa Maandiko katika mzunguko wa familia.— **The Desire of Ages, 351, 352 . ChS 115.2**

Tembelea majirani zako kwa njia ya kirafiki, na kuzoeana nao.... Wale ambao hawachukui kazi hii, wale wanaotenda kwa kutojali ambako wengine wamedhihirisha, hivi karibuni watapoteza upendo wao wa kwanza, na wataanza kulaani; kuchambua, na kushutumu ndugu zao wenyewe.— **The Review and Herald, Mei 13, 1902 . ChS 115.3**

Juhudi za mtume hazikuishia katika kuhubiri/kuzungumza hadharani; kulikuwa na wengi ambao hawakuweza kufikiwa kwa njia hiyo. Alitumia muda mwingi katika kazi ya nyumba kwa nyumba, hivyo kujinufaisha na kuwa na mahusiano ya kawaida na watu wa nyumbani. Aliwatembelea wagonjwa na wenye huzuni, aliwafariji walioteseka, na kuwainua walioonewa. Na katika yote aliyosema na kufanya, alililitukuza Jina la Yesu. Hivyo alijitaabisha, "katika udhaifu, na katika hofu, na katika kutetemeka sana." Alitetemeka isije mafundisho yake yangefichua mambo ya kibinadamu badala ya yale ya Mungu/mbingu.—
**The Acts of the Apostles, 250 . ChS 115.4**

Nenda kwa jirani zako mmoja baada ya mwingine, na uje karibu nao hadi mioyo yao ifurahishwe na kupendezwa na upendo wako usio na ubinafsi. Wahurumie, omba nao, angalia fursa za kuwatendea mema, na kadiri uwezavyo, wakusanye watu wachache pamoja na kulifungua Neno la Mungu kwa akili zao

zilizotiwa giza. Endeleeni kutazama, kama yule ambaye lazima atoe hesabu kwa ajili ya nafsi za watu, na kutumia vyema mapendeleo ambayo Mungu anakupa ya kufanya kazi pamoja Naye katika shamba Lake la mizabibu la kiadili. Usizembee kusema na jirani zako, na kuwatendea wema wote ulio katika uwezo wako, ili "kwa njia zote upate kuwaokoa wengine." Twahitaji kutafuta roho iliyomsukuma mtume Paulo kwenda nyumba kwa nyumba akiomba kwa machozi, na kufundisha "toba kwa Mungu, na imani kwa Bwana wetu Yesu Kristo."— **The Review and Herald, Machi 13, 1888 . ChS 116.1**

Bwana amewasilisha mbele yangu kazi inayopaswa kufanywa katika miji yetu. Waumini katika miji hii wanapaswa kufanya kazi kwa ajili ya Mungu katika ujirani wa nyumba zao. Wafanye kazi kwa utulivu na unyenyekevu, wakibeba pamoja nao popote waendako angahewa la mbinguni. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:128. ChS 116.2**

## Hadhira ya Nafsi Moja

Kazi ya Kristo kwa kiasi kikubwa iliundwa na mahojiano na mtu mmoja mmoja.

—

Kwa uaminifu aliheshimu usikilizaji wa nafsi moja, Kutoka kwa nafsi hiyo moja mawazo yaliyopokelewa akilini yalichukuliwa hadi kwa maelfu. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:115.ChS 116.3**

Alikuwa amezimia na amechoka; hata hivyo hakupuuza fursa ya kuzungumza na mwanamke mmoja (Yohana 4), ingawa alikuwa mtu baki, mgeni kutoka Israeli, na kuishi katika dhambi ya wazi.— **The Desire of Ages, 194 . ChS 116.4**

Mwokozi hakungoja makutaniko makubwa yakusanyike. Mara nyingi Alianza masomo Yake na watu wachache tu waliokusanyika karibu Yake, lakini mmoja baada ya mwingine waliokuwa wapita-njia walitulia ili kumsikiliza, mpaka umati uliposikia kwa mshangao na hofu maneno ya Mungu kupitia kwa Mwalimu aliyetumwa mbinguni. Mtendakazi wa Kristo hapaswi kuhisi kwamba hawezi kusema kwa bidii wakati ambapo anakuwa na wasikilizaji wachache sawa na anapokuwa na kundi kubwa. Kunaweza kuwa na mmoja tu wa kusikia ujumbe; lakini ni nani awezaye kujua mvutowake utakuwa wa mbali kiasi gani? Ilionekana kuwa jambo dogo, hata kwa wanafunzi Wake, kwa Mwokozi kutumia wakati Wake juu ya mwanamke Msamaria. Lakini alijadiliana naye kwa bidii na kwa ufasaha zaidi kuliko wafalme, washauri, au makuhani wakuu. Masomo Aliyompa mwanamke huyo yamerudiwa hadi kwenye mipaka ya mbali zaidi ya dunia.— **The Desire of Ages, 194 . ChS 116.5**

## Mguso Binafsi wa Karibu

Kuna haja ya kuja karibu na watu kwa juhudi binafsi. Ikiwa wakati mdogo ungetolewa kwa mahubiri, na wakati mwingi zaidi ukatumiwa katika huduma binafsi, matokeo makubwa yangeonekana.— **The Ministry of Healing, p. 143 . ChS 117.1**

Bwana anatamani kwamba Neno Lake la neema liletwe nyumbani kwa kila nafsi. Kwa kiwango kikubwa hii lazima itimizwe na kazi ya kibinafsi. Hii ilikuwa mbinu ya Kristo.— **Christ's Object Lessons, 229 . ChS 117.2**

Wale ambao wamefaulu zaidi katika kupata roho walikuwa wanaume na wanawake ambao hawakujivunia uwezo wao, lakini ambao kwa unyenyekevu na imani walitafuta kuwasaidia wale waliowazunguka. Yesu alifanya kazi hii hii. Yeye Alikuja karibu na wale aliotamani kuwafikia.— **Gospel Workers, 194** . **ChS 117.3**

Katika huruma kama ya Kristo tunapaswa kuja karibu na watu binafsi, na kutafuta kuamsha shauku yao katika mambo makuu ya uzima wa milele. Mioyo yao inaweza kuwa migumu kama njia kuu iliyopitiwa na watu wengi, na inaonekana inaweza kuwa juhudi isiyo na matunda kumleta Mwokozi kwao; lakini ingawa mantiki inaweza kushindwa kusonga, na hoja zisiwe na nguvu za kusadikisha, upendo wa Kristo, unaofunuliwa katika huduma ya kibinafsi, yaweza kulainisha moyo wa jiwe, ili mbegu ya Ukweli iweze kuota mizizi.— **Christ's Object Lessons, 57** . **ChS 117.4**

**ChS 117.5**

Kwa kazi binafsi fikia wale walio karibu nawe. Fahamiana nao. Kuhubiri hakutafanya kazi inayohitajika kufanywa. Malaika wa Mungu huandamana nawe kwenye makazi ya wale

—

unaowatembelea. Kazi hii haiwezi kufanywa na mwakilishi au mtu mwingine. Pesa iliyoagizwa au iliyotolewa haitaweza kuitimiza. Mahubiri hayataifanya. Kwa kuwatembelea watu, kuzungumza nao, kuomba nao, kuwahurumia, utaileta mioyo kwa Kristo. Hii ndiyo kazi ya juu zaidi ya umishenari unayoweza kufanya Ili kuifanya, utahitaji ujasiri,I mani idumuyo, uvumilivu usiokoma, na upendo wa kina kwa roho. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:41. ChS 117.5**

Kwa kuitwa kwa Yohana na Andrea na Simoni, Filipo na Nathanaeli, msingi wa kanisa la Kikristo ulianza. Yohana aliwaelekeza wanafunzi wake wawili kwa Kristo. Ndipo mmoja wa hao, Andrea, akamkuta ndugu yake, naye akamwita aje kwa Mwokozi. Filipo aliitwa wakati huo, na akaenda kumtafuta Nathanaeli. Mifano hii yapasa itufundishe umuhimu wa jitihada binafsi za kutoa mwito wa moja kwa moja kwa jamaa zetu, marafiki, na majirani. Kuna wale ambao kwa maisha yao yote wamedai kuwa wanamfahamu Kristo, walakini hawajawahi kufanya jitihada binafsi ya kuleta hata nafsi moja kwa Mwokozi. Wanamuachia mchungaji kazi zote. Mhudumu anaweza kuwa na sifa za kustahili wito wake, lakini hawezi kufanya kile ambacho Mungu amewaachia washiriki wa kanisa wafanye. **ChS 118.1**
Kuna wengi wanaohitaji huduma ya mioyo ya Kikristo yenye upendo. Wengi wameingia kwenye uharibifu ambao wangeweza kuokolewa, ikiwa majirani zao, wanaume na wanawake wa kawaida, wangeweka juhudi binafsi kwa ajili yao. Wengi wanasubiri kushughulikiwa kibinafsi. Katika familia yenyewe, ujirani, mji tunamoishi, kuna kazi ya sisi kufanya kama wamishenari kwa ajili ya Kristo. Ikiwa sisi ni Wakristo, kazi hii itakuwa furaha yetu. Mara tu mtu anapoongoka ndipo inazaliwa ndani yake hamu ya kuwajulisha wengine ni rafiki wa thamani gani amepata katika Yesu. Ukweli unaookoa na utakaso hauwezi kufungiwa moyoni mwake.— **The Desire of Ages, 141 . ChS 118.2**

Mojawapo ya njia zenye matokeo zaidi ambazo mwanga unaweza

—

kuwasilishwa ni kwa juhudi binafsi. Katika mduara wa nyumbani, kando ya moto na jirani yako (mkiwa mmetulia kwa mazungumzo mnapokota moto), kando ya kitanda cha wagonjwa, kwa njia ya utulivu unaweza kusoma Maandiko na kusema Neno kwa ajili ya Yesu na Ukweli. Hivyo unaweza kupanda mbegu ya thamani ambayo itachipuka na kuzaa matunda. **— Shuhuda kwa Kanisa 6:428, 429. ChS 118.3**

Chumvi lazima ichanganywe na dutu/kitu ambacho inaongezwa humo ndani yake; ni lazima ipenye na kusambaa ili kuhifadhi kitu mfano, chakula. Hivyo ni kwa njia ya mawasiliano binafsi na ushirika ndiyo ambavyo watu wanafikiwa na uwezo wa kuokoa wa injili. Watu hawaokolewi kwa makundi, bali kama mtu binafsi. Ushawishi binafsi ni nguvu. Tunapaswa kuwa karibu na wale ambao tunatamani kufaidika.— **Thoughts From the Mount of Blessing, 36 . ChS 119.1**

Yesu aliona katika kila nafsi mtu ambaye lazima apewe mwito wa ufalme Wake. Alizifikia nyoyo za watu kwa kwenda miongoni mwao akiwa ni mwenye kuwatakia mema. Aliwatafuta katika barabara za umma, katika nyumba za watu binafsi, kwenye mashua, katika sinagogi, kando ya ziwa, na kwenye karamu ya ndoa. Alikutana nao kwenye kazi na shuguli zao za kila siku, na akadhihirisha kupendezwa na mambo yao ya kidunia. Alibeba mafundisho Yake ndani ya nyumba, akileta familia katika nyumba zao wenyewe chini ya ushawishi wa uwepo Wake mtakatifu. Huruma Yake ya kibinafsi yenye nguvu ilisaidia kuvutia mioyo.— **The Desire of Ages, 151 . ChS 119.2**

Mbinu ya Kristo pekee ndiyo itatoa mafanikio ya kweli katika kuwafikia watu. Mwokozi alichangamana na wanadamu kama mtu aliyewatakia mema. Alionyesha huruma Yake kwao, alihudumia mahitaji yao, na akapata ujasiri na imani yao. Kisha Akawaambia, “Nifuateni.”— **The Ministry of Healing, 143 . ChS 119.3**

Tunapaswa kufanya kama Kristo alivyofanya. Popote alipokuwa, katika sinagogi, kando ya njia, ndani ya mashua iliyosogezwa nje kidogo kutoka nchi kavu, kwenye karamu ya Mafarisayo au meza ya mtoza ushuru, alizungumza na watu mambo yahusuyo maisha ya juu zaidi. Mambo ya asili, matukio ya maisha ya kila siku, yaliunganishwa Naye kwa Maneno ya Ukweli. Mioyo ya wasikilizaji Wake ilivutwa Kwake; kwa maana alikuwa amewaponya wagonjwa wao, alikuwa amewafariji walio na huzuni yao, na alikuwa amewachukua watoto wao mikononi Mwake na kuwabariki. Alipofungua midomo Yake kunena, fikira zao zilielekezwa Kwake, na kila Neno lilikuwa kwa nafsi fulani harufu ya uzima iendayo uzima. **ChS 119.4**

Hivyo nasi tunapaswa kuwa hivyo. Popote tulipo, tunapaswa kuangalia fursa za kuzungumza na wengine kuhusu Mwokozi. Tukifuata kielelezo cha Kristo katika kutenda mema, mioyo itatufungukia kama ilivyomfungulia Yeye. Si kwa kushtukiza ghafla, bali kwa busara iliyotokana na upendo wa Mungu, tunaweza kuwaambia watu juu yake Yeye ambaye ni "mkuu kati ya elfu kumi," na Yule "Mwenye kupendeza kabisa." Hii ndiyo kazi ya juu kabisa ambayo tunaweza kutumia talanta ya usemi. Ilitolewa kwetu ili tumtoe Kristo kama Mwokozi Mwenye kusamehe dhambi.— **Christ's Object Lessons, p. 338, 339 . ChS 119.5**

Uwepo Wake ulileta angahewa safi zaidi nyumbani, na maisha Yake yalikuwa kama chachu yakifanya kazi katikati masuala ya jamii. Alikuwa asiye na madhara na asiye na unajisi, Akitembea kati ya wasiojali mawazo ya wengine, wasio na adabu, watu jeuri, wale wasio waungwana; miongoni mwa watoza ushuru wasio waadilifu, wapotevu, wazembe, Wasamaria wasio waadilifu, askari wapagani, wakulima rafu-rafu, na kundi la watu waliochanganyika. Alizungumza Neno la huruma hapa na Neno pale, alipowaona watu waliochoka, lakini wanalazimika kubeba mizigo mizito. Alishiriki mizigo yao, na kurudia kwao masomo aliyokuwa amejifunza kutoka kwa asili, ya upendo, fadhila, na

—

wema wa Mungu. **ChS 120.1**

Aliwafundisha wote kujiona kuwa wamejaliwa talanta za thamani, ambazo kama zikitumiwa ipasavyo zingewahakikishia utajiri wa milele. Alipalilia ubatili wote kutoka kwa maisha, na kwa mfano wake mwenyewe alifundisha kwamba kila dakika ya wakati imejaa matokeo ya milele; kwamba inapaswa kutunzwa kama hazina, na kutumiwa kwa makusudi matakatifu. Hakumpita mwanadamu yoyote njiani na kufikiria hana thamani, bali alitafuta kutumia tiba dawa ya kuokoa kwa kila nafsi. Katika kundi lolote alilojipata, Aliwasilisha somo ambalo lilifaa kwa wakati na mazingira. Alitafuta kuwatia moyo kwa tumaini wale wabaya sana na wasio na matumaini, akiweka mbele yao uhakikisho wa kwamba wangeweza kuwa watu wasio na lawama, na wasio na madhara, wakipata tabia kama hiyo ambayo ingewadhihirisha kuwa wana wa Mungu. Mara nyingi alikutana na wale ambao walikuwa wamepeperushwa chini ya udhibiti wa Shetani, na ambao hawakuwa na uwezo wa kutoka kwenye mtego wake. Kwa mtu kama huyo, aliyevunjika moyo, mgonjwa, aliyejaribiwa, na aliyeanguka, Yesu angezungumza Maneno ya huruma nyororo, maneno ambayo yalihitajiwa na yangeweza kueleweka. Wengine alikutana nao ambao walikuwa

wakipigana vita vya ana kwa ana na adui wa roho. Hawa aliwatia moyo kuvumilia, akiwahakikishia kwamba hakika watashinda; kwa maana malaika wa Mungu walikuwa upande wao, na hakika wangewapa ushindi.— **The Desire of Ages, 90 . ChS 120.2**

### Muunganiko wa Uamsho wa Kiroho na Kazi Binafsi

Wakati makanisa yanapopata uamsho (yanapofufuliwa), ni kwa sababu mtu fulani anatafuta kwa bidii baraka za Mungu. Ana njaa na kiu ya Mungu, na anaomba kwa imani, na anapokea ipasavyo. Anaenda kufanya kazi kwa dhati bidii, akihisi utegemezi wake mkuu juu ya Bwana, na nafsi zinaamshwa kutafuta baraka kama hiyo, na majira ya kuburudishwa yanaanguka juu ya mioyo ya wanadamu. Kazi kubwa na pana haitapuuzwa. Mipango mikubwa itawekwa kwa wakati ufaao; lakini juhudi binafsi, za kipekee na maslahi kwa marafiki na majirani zako, zitatimiza mengi zaidi ya yanayoweza kukadiriwa. Ni kwa ajili ya kukosekana kwa aina hii ya kazi ndipo roho ambazo Kristo alizifia zinaangamia. **ChS 121.1**

Nafsi moja ina thamani isiyo na kikomo; kwa maana Kalvari inazungumza thamani yake. Nafsi moja, iliyovutwa kwenye Ukweli, itakuwa muhimu katika kuzipata zingine, na daima kutakuwa na matokeo yanayoongezeka ya baraka na wokovu. Kazi yako inaweza kutimiza mema zaidi kuliko mikutano mingi zaidi iliyoenea kote-kote, ikiwa inakosa jitihada za kibinafsi. Yote mawili yanapounganishwa, kwa baraka ya Mungu, kazi kamilifu zaidi na inayogusa kila kitu inaweza kufanywa; lakini ikiwa tunaweza kufanya sehemu moja tu, basi hiyo sehemu iwe kazi ya mtu binafsi ya kufungua Maandiko majumbani mwa watu, kutoa wito binafsi kwa watu, na kuzungumza na washiriki wa familia kwa ufahamu wa yale ambayo tayari wanayajua na kwa upendo , na sio juu ya mambo ya maana ndogo-ndogo, bali juu ya mada kuu za ukombozi. Hebu waone kwamba moyo wako umelemewa na mzigo kwa ajili ya wokovu wa nafsi.— **The Review and Herald, Machi 13, 1888 . ChS 121.2**

—

## Waendee watu

Hatupaswi kungoja watu waje kwetu; lazima tuwatafute pale walipo. Wakati Neno limehubiriwa mimbarani, hapo ndiyo tu kazi imeanza. Kuna umati ambao hautafikiwa kamwe na injili isipokuwa iwe imepelekwa kwao.— **Christ's Object Lessons, 229 . ChS 121.3**

Utume wa injili ni hati kuu ya umishenari ya ufalme wa Kristo. Wanafunzi walipaswa kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya nafsi, wakitoa mwaliko wote wa rehema. Hawakupaswa kungoja watu waje kwao; walipaswa kwenda kwa watu na ujumbe wao.— **The Acts of the Apostles, 28 . ChS 121.4**

## Alika Watu Nyumbani Kwako Usomaji wa Biblia

Alika jirani zako nyumbani kwako, na usome pamoja nao kutoka katika Biblia yenye thamani na kutoka katika vitabu vinavyoeleza Kweli zake. Waalike kuungana nawe katika wimbo na sala. Katika mikusanyiko hii midogo, Kristo Mwenyewe atakuwepo, kama

alivyoahidi, na mioyo itaguswa na neema Yake.— **The Ministry of Healing, p. 152, 153 . ChS 122.1**

Alipokuwa Efeso, Apolo “alianza kusema kwa ujasiri katika sinagogi.” Miongoni mwa wasikilizaji wake walikuwa Akila na Prisila, ambao, waliona kwamba alikuwa bado hajapokea nuru kamili ya injili, “wakamchukua kwao, na kumfafanulia njia ya Mungu kwa ukamilifu zaidi.” Kupitia mafundisho yao alipata ufahamu ulio wazi zaidi wa Maandiko, na akawa mmoja wa watetezi hodari wa imani ya Kikristo. — **The Acts of the Apostles, 270 . ChS 122.2**

### Kuwa Mtu Mwenye Roho ya Urafiki na kuchangamana na watu (social)

Kwa wote wanaofanya kazi pamoja na Kristo ningesema, Popote unapoweza kupata ufikiaji wa watu nyumbani kwao, kama vile pale wanapokota moto wakati wa baridi, boresha fursa yako. Chukua Biblia yako, na ufungue mbele yao Kweli zake kuu. Mafanikio yako hayatategemea sana maarifa na mafanikio yako, bali juu ya uwezo wako wa kutafuta njia yako ya moyo. Kwa kuwa mtu mwenye moyo wa kirafiki, unayechangamka na kufurahi watu (social) na kuja karibu na watu, unaweza kugeuza mkondo wa mawazo yao kirahisi zaidi kuliko hotuba/hubiri lenye uwezo zaidi. Uwasilishaji wa Kristo katika familia, nyumbani kwao, na katika mikusanyiko midogo katika nyumba za watu binafsi pale wanapokota moto au katika kusanyiko lao dogo, mara nyingi hufaulu zaidi katika kuleta roho kwa Yesu kuliko mahubiri yanayotolewa hadharani, kwa umati unaosonga, au hata kwenye kumbi au makanisa. – **Gospel Workers, 193 . ChS 122.3**

Mfano wa Kristo katika kujiunganisha Mwenyewe na maslahi ~~ya~~ wanadamu unapaswa kufuatwa na wote wanaohubiri Neno Lake, na wote waliopokea injili ya neema yake. Hatupaswi kukataa ushirika wa kijamii (social gathering). Hatupaswi kujitenga kutoka kwa watu wengine. Ili kufikia matabaka yote, lazima tukutane na watu pale walipo. Ni mara chache sana wao

watatutafuta sisi kwa hiari yao wenyewe. Sio tu kutoka kwenye mimbari ndiyo ambapo mioyo ya wanadamu imeguswa na Ukweli wa Mungu. Kuna uwanja mwingine wa kazi, haijalishi ni wenye unyenyekevu kiasi gani, lakini unatoa matumaini mazuri sana ya watu kukubali injili. Inapatikana katika nyumba ya watu wa hali ya chini, na katika makao ya wakuu; kwenye baraza la ukaribishaji-wageni, na katika mikusanyiko ya starehe za kijamii zisizo na hatia au zisisohusisha dhambi.— **The Desire of Ages, 152 . ChS 122.4**

Kristo hakuwa na tabia ya kubagua watu fulani kuwa Naye na watu fulani kuwa mbali naye, na kwa tabia hii, Yeye alikuwa amewachukiza Mafarisayo kwa kutoka kwenye sheria zao ngumu za kutenga watu. Alikuta eneo la dini likiwa limezungushiwa ukuta mrefu uliotenganisha watu, kama ndilo jambo takatifu sana katika maisha ya kila siku. Kuta hizi za kizigeu Yeye Alizipindua. Katika kuwasiliana Kwake na wanadamu hakuuliza, Imani yako ni ipi? Je, wewe ni wa kanisa gani? Yeye Alitumia uwezo Wake wa kusaidia kwa niaba ya wote waliohitaji msaada. Badala ya kujitenga Mwenyewe katika jumba la mtawa ili kuonyesha tabia Yake ya mbinguni, Alifanya kazi kwa bidii kwa ajili ya wanadamu. Alikazia kanuni kwamba dini ya Biblia haijumuishi kuudhalilisha mwili. Alifundisha kwamba dini safi na isiyo na unajisi haikukusudiwa tu kwa nyakati zilizowekwa na matukio maalum. Nyakati zote na

mahali pote Alionyesha upendo wenye shauku kwa wanadamu, na kuwaangazia watu, nuru Yake yenye uchamungu wa uchangamfu.— **The Desire of Ages, 86 . ChS 123.1**

Akikabiliana uso kwa uso na chuki zao, Yeye alikubali ukarimu wa watu hawa waliodharauliwa. Alilala chini ya paa zao, alikula pamoja nao kwenye meza zao,—akishiriki chakula kilichotayarishwa na kupakuliwa, kuletwa mezani na mikono yao,—aliyefundishwa katika barabara zao, na kuwatendea kwa fadhili na adabu nyingi zaidi.— **The Desire of Ages, 193 . ChS 123.2**

## Dhihirisha Moyo ya Huruma

Wale ambao wanapigana vita vya maisha katika hali mbaya sana wanaweza kuburudishwa na kuimarishwa kupewa umakini mdogo ambao hauna gharama yoyote. Maneno ya ukarimu yanayosemwa kwa njia ya kawaida, na usikivu mdogo tu unaooneshwa, vitafagilia mbali mawingu ya majaribu na mashaka yanayoijaza nafsi. Udhihirisho wa dhati/kweli wa moyo wa huruma kama ya Kristo, ukitolewa kwa usahili, una uwezo wa kufungua mlango wa mioyo inayohitaji mguso mwepesi na wa upole wa roho ya Kristo.

—Shuhuda kwa Kanisa 9:30. **ChS 123.3**

Maelfu ya mioyo yaweza kufikiwa kwa njia rahisi zaidi na ya unyenyekevu. Watu wenye akili mahiri zaidi, wale wanaotazamwa na kusifiwa kuwa ni wanaume na wanawake wenye vipawa vingi zaidi ulimwenguni, mara nyingi huburudishwa na maneno rahisi yanayotiririka kutoka moyoni mwa mtu anayempenda Mungu na anayeweza kuzungumza juu ya upendo huo kwa usahili na kwa njia ya kawaida kama walimwengu wanavyozungumza mambo ambayo akili zao huyawaza na kujilisha kwa kawaida. Mara nyingi maneno ambayo mtu amejifunza, ameyasoma na kuyatayarishwa vyemahuwa na ushawishi mdogo. Lakini maneno ya dhati, halisi, na yenye uadilifu ya mwana au binti wa Mungu,

—

yanayozungumzwa kwa usahili wa asili, yatafungua mlango kwa mioyo ambayo imefungwa kwa muda mrefu. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:115. ChS 124.1**

**Shiriki Uzoefu Binafsi**

Wale waliomvaa Kristo watasimulia uzoefu wao, wakifuatilia hatua kwa hatua miongozo ya Roho Mtakatifu,—njaa yao na kiu ya kumjua Mungu na Yesu Kristo ambaye amemtuma, matokeo ya kuyachunguza Maandiko, maombi yao, uchungu wa mioyo yao, na Maneno ya Kristo kwao  "Umesamehewa dhambi zako." Sio jambo la kawaida kwa yeyote kuficha mambo haya, na wale ambao wamejazwa na upendo wa Kristo hawatafanya hivyo. Kwa kadiri ambavyo Bwana amewafanya wahifadhi wa Ukweli mtakatifu,b asi itakuwa nia yao kwamba wengine wapate baraka sawa. Na wanapofanya hazina nyingi za neema ya Mungu zijulikane kwa wengine, neema zaidi na zaidi ya Kristo itatolewa kwao.— **Christ's Object Lessons, 125 . ChS 124.2**

Amsha kila nguvu ya kiroho iwe katika utendaji. Waambie wale unaowatembelea kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia. Bwana Yesu Kristo atafungua milango ya mioyo yao na atatengeza ndani ya nia ya mwanadamu mvuto wa kudumu. Jitahidi kuwaamsha wanaume na wanawake kutoka katika kupoa kwao kiroho. Waambie jinsi ulivyompokea Yesu na jinsi ulivyobarikiwa tangu upate uzoefu katika huduma Yake. Waambie ni baraka gani

huja kwako kadri unavyoketi miguuni pa Yesu na kujifunza masomo ya thamani kutoka katika Neno Lake. Waambie juu ya furaha na shangwe iliyopo katika maisha ya Kikristo. Maneno yako ya uchangamfu, yenye bidii yatawasadikisha kwamba umeipata lulu ya thamani kubwa. Hebu maneno yako ya uchangamfu na yenye kutia moyo yaoneshe kwamba hakika umeipata njia iliyo ya juu. Hii ni kazi ya Kweli ya umishionari, na kadri inavyofanywa, wengi wataamka kama watokao katika ndoto. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:38. ChS 124.3**

Wale ambao Mungu huwaajiri kama vyombo Vyake watu wengine wanaweza kuwachukuliwa kama wale wasio na ufanisi; lakini ikiwa wanaweza kuomba, ikiwa kwa usahili wanaweza kuzungumza Ukweli kwa sababu wanaupenda, wanaweza kuwafikia watu kupitia nguvu za Roho Mtakatifu. Wanapowasilisha Ukweli kwa namna rahisi, wakisoma kutoka katika Neno au kukumbuka matukio ya uzoefu wao, Roho Mtakatifu hufanya msukumo kwenye akili na tabia. Mapenzi yao yanakuwa chini ya mapenzi ya Mungu; Ukweli ambao haujaeleweka huja moyoni ukiwa na usadikisho ulio hai na huwa Ukweli wa kiroho. **— Shuhuda kwa Kanisa 6:444. ChS 125.1**

## Vielelezo Huwa Vina Ufanisi

Jumbe Zake Kristo za rehema zilitofautiana ili kuendana na hadhira Yake. Alijua "kunena Neno kwa wakati kwake yeye aliyechoka; kwa maana neema ilimiminwa midomoni Mwake, ili apate kuwafikishia wanadamu kwa njia ya kuvutia sana, hazina za Kweli. Alikuwa na busara ili kukutana na akili zenye ubaguzi, na kutenga watu na kuwashangaza kwa vielelezo ambavyo vilivutia usikivu wao. Kwa njia ya fikra/mawazo Alifikia moyo. Vielezi vyake vilichukuliwa kutoka katika mambo ya maisha ya kila siku, na ingawa vilikuwa sahili, vilikuwa na maana ya ajabu na kina ndani yake. Ndege wa angani, maua ya kondeni, mbegu, mchungaji na kondoo,—kwa vitu hivi Kristo alionyesha Ukweli usioweza kufa; na baadaye, wasikilizaji Wake walipopata kuona

—

mambo haya katika asili, walikumbuka Maneno Yake. Vielezi vya Kristo vilirudia mara kwa mara masomo Yake.— **The Desire of Ages, p. 254 . ChS 125.2**

Mitume walijitahidi kuwapa waabudu sanamu hao ujuzi wa Mungu Muumba, na Mwanawe, Mwokozi wa jamii ya kibinadamu. Kwanza walielekeza fikira kwenye kazi za ajabu za Mungu,—jua, mwezi, na nyota, mpangilio mzuri wa majira yanayorudiwa-rudiwa, milima mikubwa iliyofunikwa na theluji, miti mirefu, na maajabu mengine mbalimbali ya asili, ambayo yalionyesha ujuzi unaopita ufahamu wa mwanadamu. Kupitia kazi hizo za Mweza-Yote, mitume waliongoza akili za wapagani kwenye tafakari ya Mtawala mkuu wa ulimwengu wote mzima.— **The Acts of the Apostles, 180 . ChS 125.3**

**Shughulika na Misingi ya Vitendo**

Paulo alikuwa mzungumzaji fasaha. Kabla ya kuongoka kwake, mara nyingi alikuwa akijaribu kuwavutia wasikilizaji wake kwa mazungumzo mengi yenye kupendeza ya umbuji. Lakini sasa aliweka haya

yote kando. Badala ya kujihusisha na maelezo ya kishairi na maonyesho ya kuwaziwa au kufikirika, ambayo yangeweza kufurahisha hisia na kulisha mawazo, lakini ambayo hayangegusa uzoefu wa kila siku, Paulo alitaka kwa kutumia lugha rahisi kuleta nyumbani Kweli zilizo muhimu sana. Uwakilishi wa kufikirika wa Ukweli unaweza kusababisha msisimko wa hisia; lakini mara nyingi, Uweli zinazotolewa kwa njia hii hazitoi chakula kinachohitajika ili kuimarisha na kuimarisha muumini kwa ajili ya vita vya maisha. Mahitaji ya mara moja, majaribu ya sasa, ya nafsi zinazotaabika, --haya lazima yatimizwe na mafundisho ya kweli na ya vitendo katika kanuni za msingi za Ukristo.— **The Acts of the Apostles, 251, 252 . ChS 126.1**

### Shikilia Ukweli Uliothibitika

Mara nyingi, tunapotafuta kuuwasilisha Ukweli, upinzani utaamshwa; na ikiwa tutatafuta kukabiliana na upinzani kwa hoja, tutauzidisha tu upinzani, na hivyo hatutakuwa na uwezo wa kuukabili. Angalieni kwenye uthibitisho. Malaika wa Mungu hututazama wanadamu, na wanaelewa jinsi ya kuwashawishi wale ambao tunaacha kukutana nao kwa hoja. Tusing'ang'anie kwenye hoja hasi za maswali yanayojitokeza, bali tupeleke akili zetu kwenye zile Kweli zenye uthibitisho, na kuzielekeza huko kwa kusoma sana na maombi ya dhati na moyo ulio wakfu. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:147, 148. ChS 126.2**

### Wawakilishi Katika Njia za Usafiri

Wale ambao kwa kuitikia wito wa saa, walioingia katika huduma ya Mtendakazi Mkuu, ni lazima wajifunze vema mbinu Zake za kazi. Wakati wa huduma Yake duniani Mwokozi alitumia fursa zilizopatikana kando ya njia kuu za usafiri. Yesu alikaa Kapernaumu katika vipindi vya safari Zake kwenda huko na kule, na ukaja kujulikana kama "mji Wake Mwenyewe". Mji huu ulikuwa mzuri na ulichukuliwa kuwa kitovu cha kazi ya Mwokozi. Ukiwa kwenye barabara kuu kutoka Dameski kwenda Yerusalemu na Misri, na hadi Bahari ya Mediterania, hapa ndiyo palikuwa na njia

—

kuu ya usafiri (highway). Watu kutoka nchi nyingi walipita katikati ya jiji hili au walisubiri kupumzika katika safari zao za kwenda huku na huko. Hapa Yesu aliweza kukutana na watu wote, wa nyadhifa zote, matajiri kwa wakuu, pia maskini na watu wa hali ya chini; na mafundisho Yake yangebebwa kwenda nchi nyingine na katika familia nyingi. Hivyo Uchunguzaji wa unabii ungesisimua; usikivu wa wasafiki, na ungeelekezwa kwa Mwokozi, na utume Wake na kupelekwa ulimwenguni kote. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:121.ChS 126.3**

Katika vituo vya afya maarufu duniani kote na vituo vya watalii wanaosafiri, vilivyojaa maelfu ya watu wanaotafuta afya na starehe, hebu pawepo na watumishi na waombezi walio na uwezo wa kuukamata umakini wa watu. Hebu watendakazi hawa wawe macho kwa nafasi yao ya kuwasilisha ujumbe wa wakati huu, na kufanya mikutano kadiri wanavyopata fursa. Hebu wawe wepesi katika kuikamata fursa ya kuzungumza na watu. Wakisukumwa na nguvu za Roho Mtakatifu, hebu wakutane na watu wakiwa na ujumbe uliotolewa na Yohana Mbatizaji: "Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia."Mathayo 3:2. Neno la Mungu linapaswa kuwasilishwa kwa uwazi na nguvu, ili wale walio na masikio ya kusikia waweze kuusikia Ukweli. Hivyo injili ya Ukweli wa

sasa itawekwa katika njia ya wale ambao hawaijui, na itakubaliwa na watu wengi, na kupelekwa nao hadi majumbani mwao katika sehemu zote za nchi za dunia. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:122.ChS 127.1**

Vitabu vya Huduma ya Uponyaji (Ministry of Healing) na Vielelezo vya maisha ya Kristo (Christ's Object Lesson) vina upekee katika kuendana na matumizi ya vituo vya utalii, na kwa kila namna iwezekanayo kufanyika, ziwekeni nakala za kazi hizi katika mikono ya wale ambao wana muda ambao hawana kitu cha kufanya, au wako katika mapumziko na wana mwelekeo wa kusoma. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:85. ChS 127.2**

Migahawa ya afya (Hygeine Restaurants) na vyumba vya tiba/matibabu (Sanitarium) vinapaswa kuanzishwa. Jitihada zetu katika nyanja hii zinapaswa kujumuisha vituo vingi kwenye fukwe za bahari. Kama sauti ya Yohana Mbatizaji ilivyosikika nyikani, "Tengenezeni njia ya Bwana," ndivyo sauti ya wajumbe wa Bwana inapaswa kusikiwa katika vituo vingi vya watalii na maeneo ya kutalii kando ya bahari. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:55, 56.**

**Watendakazi Walitumwa Wawili Wawili**

Yesu akawaita wale Thenashara wakamzunguka, akawaamuru watoke wawili wawili katika miji na vijiji. Hakuna waliotumwa peke yao, lakini ndugu alihusishwa na ndugu, rafiki na rafiki. Hivyo wangeweza kusaidiana na kutiana moyo, wakishauriana na kusali pamoja, nguvu za kila mmoja ikijaliza na hivyo kufidia udhaifu wa mwingine, na hivyo kuboreshana na kuongeza ufanisi. Vivyo hivyo baadaye Kristo akawatuma wale sabini, ilikuwa ni kusudi la Mwokozi kwamba wajumbe wa injili wanapaswa kuhusishwa kwa njia hii. Katika zama zetu wenyewe kazi ya uinjilisti ingefaulu zaidi ikiwa mfano huu ungefuatwa kwa ukaribu zaidi.**— The Desire of Ages, 350 . ChS 127.4**

**Ziara za Uinjilisti wa Tiba (Medical Missionary Tour)**

—

Kutoka kwenye maagizo ambayo Bwana amenipa mara kwa mara, najua kwamba kunapaswa kuwa watendakazi wanaofanya ziara za uinjilisti wa tiba, katika ya miji na vijiji. Wale wanaofanya kazi hii watakusanya mavuno mengi ya roho kutoka kwenye matabaka ya juu na ya chini. Njia ya kazi hii itaandaliwa kwa ubora zaidi na juhudi za mwinjilisti wa vitabu mwaminifu, anayezungumza akishawishi watu. —Shuhuda kwa Kanisa 9:172. **ChS 128.1**

**Wamishenari wa Injili wa Tiba (Gospel Medical Missionaries)**

Watendakazi - wamishenariwa tiba - wanahitajika sasa. Hamwezi kufanikiwa kwa kuendelea kutumia miaka mingi katika maandalizi. Hivi karibuni milango iliyofunguliwa kwa Ukweli itafungwa milele. Pelekeni ujumbe sasa. Msikawie, mkamruhusu adui kumiliki mashamba ya injili yaliyofunguliwa sasa mbele yenu. Hebu makundi madogo yaende kufanya kazi ambayo Kristo aliwapa wanafunzi Wake. Waache watu hawa wafanye kazi kama wainjilisti, wakitawanya machapisho yetu na kuzungumza juu ya Kweli kwa wale wanaokutana nao. Hebu wawaombee wagonjwa, wakiwahudumia watu mahitaji yao, si kwa kutumia dawa za hospitali, lakini kwa tiba za asili, na kuwafundisha jinsi ya kuirejesha afya na kuepuka magonjwa (Tiba ya asili Lishe bora, Maji Safi ndani na nje, Kupumzika, Kumwamini Mungu, Kiasi, Jua, Hewa Bora, na Mazoezi). —**Shuhuda kwa Kanisa 9:172.ChS 128.2**

Ndugu na dada zangu, jitoeni wenyewe kwa Bwana kwa ajili ya utumishi. Usiruhusu fursa kupita bila kuitumia. Tembelea wagonjwa na watu wenye shida, na uonyeshe shauku na wama kwao. Ikiwezekana, fanya kitu kuwafanya wajisikie vizuri zaidi. Kwa njia hii unaweza kuifikia mioyo yao na kuzungumza Neno kwa ajili ya Kristo. Ni Umilele pekee ndio utakaofunua jinsi aina hii ya kazi inavyofanya kazi kubwa. Mistari mingine yenye kunufaisha itakuwa wazi mbele ya wale ambao wako tayari kufanya kazi iliyo karibu nao. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:36. ChS 128.2**

## Elimu ya Tasnia au Stadi Mbalimbali

Kuna familia nyingi maskini ambazo hakuna kazi bora zaidi ya umishenari ingeweza kufanywa miongoni mwao kuliko ile ya kuwasaidia kupata eneo na kuwafundisha jinsi ya kuifanya ardhi iwapatie riziki kwa kilimobora.Hitaji la msaada na mafunzo kama hayo haliko mijini tu. Hata vijijini, pamoja na uwezekano wake wote wa maisha bora, umati wa watu masikini huko, ni wahitaji mno. Jamii nzima haina elimu katika masuala ya tasnia, stadi za kazi, afya na usafi. Familia huishi katika nyumba za kimasikini, zilizo na samani/fanicha na nguo duni, bila zana za kazi, bila elimu, bila vitabu, bila faraja na vitu ambavyo ni muhimu kuendesha maisha ya kila siku, na hawana utamaduni unaokuwa msaada kwao. Watu walioshushwa chini kimaadili na kuwa kama wanyama,wana miili dhaifu na ulema, haya yote hufichua matokeo ya urithi mbaya na tabia mbaya kutoka kwenye mazingira yao na wazazi. Watu hawa lazima waelimishwe tangu kwenye msingi kabisa. Wameishi maisha ya ugoigoi bila kazi, uvivu na ufisadi, na wanahitaji kuzoezwa, na kufundisha kukarabati mazoea mabaya **—The Ministry of Healing, 192 . ChS 129.1**

Tahadhari iangaliwe juu ya uanzishwaji wa shuguli za tasnia na stadi mbalimbali familia maskini zipate ajira. Mafundi seremala, wahunzi, na kwa kweli kila mtu anayeelewa kazi fulani yenye manufaa, anapaswa kuhisi wajibu wa kuwafundisha na kuwasaidia watu wajinga wasio na stadi yoyote ya kazi, wasio na bidii ya kazi na wasio na kazi.— **The Ministry of Healing, p . ChS 129.2**

Wakulima Wakristo wanaweza kufanya kazi halisi ya umishenari katika kuwasaidia maskini kujenga nyumba katika ardhi, na katika kuwafundisha jinsi ya kulima udongo na kuufanya uzae-Kilimo bora. Wawafundishe watu jinsi ya kutumia zana za kilimo, na

kulima mazao mbalimbali inavyotakiwa, jinsi ya kupanda mbegu au miche na kutunza bustani na miti ya matunda.— The Ministry of Healing, 193 . ChS 129.3

Katika huduma kwa maskini kuna uwanja mpana wa huduma kwa wanawake na wanaume pia. Mpishi mwenye ufanisi (au stadi), mtunza-nyumba, mshona nguo, muuguzi,—msaada wa wote unahitajika. Wacha wanakaya maskini wafundishwe jinsi ya kupika, kutengeneza na kukarabati nguo zao wenyewe, jinsi ya kuuguza wagonjwa, jinsi ya kutunza nyumba ipasavyo. Waache wavulana na wasichana wafundishwe kikamilifu stadi fulani ya kazi yenye manufaa.— **The Ministry of Healing, 194 . ChS 129.4**

**Alika Watu kwa Ajili ya Mikutano ya Injili**

Kuna mambo mengi ambayo watu wanaweza kufanya ikiwa tu wataweka akili yao katika kufanya kazi. Kuna wengi ambao hawataenda kanisani kusikia Ukweli ukihubiriwa. Kwa juhudi binafsi sahili na hekima, watu hawa wanaweza kushawishika kuelekeza miguu yao kwenye nyumba ya Mungu. Usadikisho unaweza kukaza akilini mwao mara ya kwanza

wanaposikia hotuba kuhusu Ukweli wa sasa. Ikiwa ushawishi wako unakataliwa, wewe usikate tamaa. Vumilia hadi mafanikio yalete taji kwenye juhudi zako.— **The Review and Herald, Juni 10, 1880 . ChS 130.1**

### Kukusanyika Kwenye Shule ya Sabato

Kazi nyingine ambayo wote wanaweza kushiriki ni kukusanya watoto na vijana katika shule ya Sabato. Vijana wanaweza kwa njia hii kufanya kazi kwa ufanisi kwa ajili ya Mwokozi mpendwa. Wanaweza kuunda mazingira yenye kuleta hatima ya roho. Wanaweza kufanya kazi kwa ajili ya kanisa na ulimwengu ambayo kiwango na ukuu wake hakitajulikana kamwe duniani hapa, hadi siku ya mahesabu ya mwisho, wakati "Vema" itakapotamkwa kwa wale wema na waaminifu.— **The Review and Herald, Juni 10 , 1880 . ChS 130.2**

### Kwa Kalamu na Sauti

Kwa kalamu na sauti tangazeni kwamba Yesu yu hai ili kufanya maombezi kwa ajili yetu (Waebrania 7:25). Unganeni na Mtendakazi Mkuu na Bora, mfuatilieni Mkombozi anayejikana nafsi Yake, kupitia hija Yake ya upendo alipoishi hapa duniani.— **The Review and Herald, Januari 24, 1893 . ChS 130.3**

Wengine watafanya kazi kwa njia moja na wengine kwa njia nyingine, kama Bwana atakavyowaita na kuwaongoza. Lakini wote wanapaswa kujitahidi pamoja, wakitafuta kukamilishana na kuifanya kazi hiyo yote kuwa kamilifu. Kwa kalamu na sauti wanadamu wanapaswa kumfanyia kazi Mungu.
**—Shuhuda kwa Kanisa 9:26. ChS 130.4**

Kristo aliyesulubiwa—zungumzia mada hii, uombee, uiimbe, na itavunja -vunjaa mioyo na kuvutia mioyo.
**—Shuhuda kwa Kanisa 6:67. ChS 130.5**

Kalamu ni nguvu mikononi mwa watu wanaohisi Ukweli ukiwaka juu ya madhabahu ya mioyo yao, na ambao wana bidii ya akili kwa Mungu, iliyosawazishwa na uamuzi mzuri. Kalamu, iliyochoviwa katika chemchemi ya Ukweli safi, inaweza kutuma miale ya nuru kwenye pembe za giza za dunia, ambapo itaakisi miale yake kwa

—

kurudi nyuma, ikiongeza nguvu mpya, na kutoa nuru iliyoongezeka kutawanywa kila mahali.— Life Sketches, 214.

Wahudumu wetu hawapaswi kutoa nguvu zao zote kwenye kuhubiri mahubiri au hotuba, na kuacha kazi imalizikie hapo. Wanapaswa kuwafundisha washiriki wa kanisa jinsi ya kushika na kuendeleza kwa mafanikio  tawi hili la kazi [mawasiliano ya kimishenari au kuandika barua za kimishenari], ambayo ni  trakti na vijuzuu vyetu na jamii ya wamishenari kama gurudumu ndani ya gurudumu (Ezekiel 10:10). Mwendo wa gurudumu hili la ndani huhifadhi utendaji mzuri na wenye nguvu wa gurudumu lile la nje. Ukiacha gurudumu hili la ndani liache kutenda kazi, na matokeo yataonekana katika maisha na utendaji uliopungua katika trakti na jamii ya wamishenari-chama cha wamishenari.— **The Review and Herald, Juni 10, 1880 . ChS 130.6**

Usichoke na kazi ya umishenari ya kukesha daima na kuchunga hatari na magumu yote. Hii ni kazi ambayo nyote mnaweza kushiriki kwa mafanikio, ikiwa tu mtaungana na Mungu. Kabla ya kuandika barua za uchunguzi, daima inua moyo wako kwa Mungu katika maombi ili uweze kufanikiwa

katika kukusanya baadhi ya matawi ya mwitu ambayo yanaweza kupandikizwa kwenye mzabibu wa kweli, na kuzaa matunda kwa utukufu wa Mungu. Wote ambao kwa mioyo ya unyenyekevu wanashiriki katika kazi hii, watakuwa wakijielimisha wenyewe kwa bidii kama watenda kazi katika shamba la mizabibu la Bwana.— **The Review and Herald, Juni 10, 1880 . ChS 131.1**

## SURA YA 11 — KAZI YA UMISHENARI WA TIBA -Medical Missionary Work

### Kazi ya Umuhimu wa Kwanza

Wakati wa huduma Yake, Yesu alitumia wakati mwingi zaidi kuponya wagonjwa kuliko kuhubiri.— **The Ministry of Healing,**

—

**19 . ChS 132.1**

Kazi ya umishenari wa tiba, itafungua milango mingi, mbele ya mwanamatengenezo wa kweli. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:62.ChS 132.2**

Kazi ya kweli ya umishenari wa tiba ni injili katika vitendo. **—Shuhuda kwa Kanisa 8:168.ChS 132.3**

Kazi ya umishenari wa tiba, ni kazi ya uanzishaji wa injili kwenye eneo jipya. Katika huduma ya Neno na katika kazi ya umishenari wa tiba injili inapaswa kuhubiriwa na kutekelezwa kwa vitendo (kutendwa).— **The Ministry of Healing, p. 144 . ChS 132.4**

Mwokozi wa ulimwengu alitumia muda na kazi nyingi zaidi ili kuponya walioteswa na magonjwa yao kuliko kuhubiri. Amri Yake ya mwisho kwa mitume Wake, wawakilishi Wake hapa duniani, ilikuwa ni kuweka mikono juu ya wagonjwa ili wapate nafuu (Marko 16:18). Bwana atakapokuja, atawasifu wale ambao wamewatembelea wagonjwa na kudaidia mahitaji ya watu wanaoteseka.**—Shuhuda kwa Kanisa 4:225.ChS 132.5**

Bwana Amepanga kazi ya umishenari wa tiba itayarishe njia au daraja, kwa ajili ya uwasilishaji wa Ukweli unaookoa kwa wakati huu, naam, kutangazwa kwa ujumbe wa malaika wa tatu.

Muundo huu ukifikiwa, ujumbe hautafichwa wala maendeleo yake hayatazuiwa (disaini hii au Modeli hii itakapofikiwa katika mikakati ya kufikia watu kwa injili, ujumbe utakuwa nje nje na wazi na hakuna mtu atazuia injili kufikia watu). —
**Shuhuda kwa Kanisa 6:293.ChS 132.6**

Kwanza kutana na mahitaji halisi ya muda mfupi, na ya kidunia kwenye maisha ya watu wahitaji na kisha uwaondolee uhitaji huo wa kimwili, shida na mateso, na hapo utapata njia ya kukanyagia iliyo wazi kwenye moyo, mahali ambapo unaweza kupanda mbegu nzuri za wema na dini (daraja la kuvukia). —
**Shuhuda kwa Kanisa 4:227. ChS 132.7**

Hakuna kitakachotoa kwa watu nguvu kubwa ya kiroho na ongezeko kubwa la bidii na kina cha hisia kuliko kutembelea na kuhudumia wagonjwa na watu waliovunjika mioyo, kuwasaidia kuona nuru na kufuinga imani yao juu ya Yesu.—**Shuhuda kwa Kanisa 4:75, 76.ChS 132.8**

**Mfano wa Bwana Mwenyewe**

Kristo, Tabibu Mmishenari mkuu, Ndiye mfano wetu. Maneno haya yameandikwa kumhusu Yeye "Naye alikuwa akizunguka Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya Ufalme, na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu." Mathayo 4:23. Yeye Aliponya wagonjwa na kuihubiri Injili. Katika huduma Yake, uponyaji na kuhubiri injili viliunganishwa pamoja. Leo hii, hivi viwili, havipaswi kutenganishwa.
**— Shuhuda kwa Kanisa 9:170, 171. ChS 133.1**

Watumishi wa Kristo wanapaswa kufuata mfano Wake. Alipokuwa akienda mahali hadi mahali, aliwafariji walioteseka na kuwaponya wagonjwa. Kisha akaweka mbele yao zile Kweli
Kuu kuhusu Ufalme Wake. Leo hii Ndiyo Kazi ya wafuasi Wake.
.— **Christ's Object Lessons,** ChS 133.2

Mfano wa Kristo lazima ufuatwe na wale wanaodai kuwa wana

Wake. Leteni afueni kwenye mahitaji ya kimwili ya wanadamu wenzenu, na shukrani zao zitavunja vizuizi na kuwawezesha kuifikia mioyo yao. Zingatieni sana jambo hili kwa dhati na bidii. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:127.**ChS 133.3

Hasa kwa wale ambao ni wamishenari wa tiba, hawa wanapaswa kudhihirisha kwa roho, maneno, na tabia kwamba wanamfuata Kristo Yesu, Mfano wa mbingu/Kiungu wa juhudi za kimishenari na za tiba-au ukarimu usio na ubinafsi). —**Shuhuda kwa Kanisa 7:127.**ChS 133.4

**Unganisha Umishenari wa Tiba na Huduma ya Injili**

Injili na kazi ya umishenari wa tiba vinapaswa kusonga mbele pamoja. Injili inapaswa kuunganishwa na kanuni za matengenezo ya Kweli ya afya. Ukristo unapaswa kuletwa katika maisha ya vitendo/utendaji. Kazi ya dhati, bidii na, kamili na ya kina ya matengenezo inapaswa kufanywa. Dini ya Kweli ya Biblia ni upendo wa Mungu kwa mwanadamu aliyeanguka. Watu wa Mungu wanapaswa kusonga mbele katika njia zilizonyooka ili kuvutia mioyo ya wale wanaotafuta Ukweli, wanaotamani kutenda sehemu yao ifaavyo katika enzi hii yenye bidii nyingi. Tunapaswa kuwasilisha kanuni za matengenezo ya afya mbele ya watu, tukifanya yale yote tuwezayo ili kuwaongoza wanaume na wanawake kuona umuhimu wa kanuni hizi, na kuzitekeleza. —**Shuhuda kwa Kanisa 6:379**.ChS 133.5

Ni mpango wa Mungu kwamba tutafanya kazi kama wanafunzi walivyofanya kazi. Uponyaji wa kimwili unafungamana na agizo la injili. Katika kazi ya injili, mafundisho na uponyaji hayapaswi kutenganishwa kamwe.— **The Ministry of Healing, p. 141 . ChS 133.6**

Kazi ya **umishenari wa tiba** na **huduma ya injili** ni mikondo/chaneli ambayo Mungu hutafuta kumimina ugavi endelevu wa wema Wake. Hivi vitu viwili, vinapaswa kuwa kama mto wa uzima kwa ajili ya unyweshaji/umwagiliaji wa kanisa Lake.— **The Bible Echo, Agosti 12, 1901 . ChS 133.7**

Hebu wachungaji/wahudumu wetu, ambao wamepata uzoefu katika kuhubiri Neno, wajifunze jinsi ya kutoa tiba rahisi/sahili na kisha wafanye kazi kwa akili kama wainjilisti wamishenari wa tiba. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:172.ChS 134.1**

Mwinjilisti anapoenda kutoka mahali hadi mahali kuuza vitabu, atapata watu wengi ambao ni wagonjwa. Anapaswa kuwa na ujuzi wa vitendo wa sababu za ugonjwa, na anapaswa kuelewa jinsi ya kutoa matibabu rahisi, ili apate kuwapa afueni wale wanaoteseka. Zaidi ya hayo, anapaswa kuomba kwa imani na usahili kwa wagonjwa, akiwaelekeza kwa Tabibu mkuu. Anapotembea hivyo na kufanya kazi pamoja na Mungu, malaika wanaomtumikia huwa karibu naye, wakimpa njia ya kufikia mioyo. Ni uwanja mpana jinsi gani wa juhudi za umishenari uliopo mbele ya wahubiri waaminifu, wainjilisti wa vitabu waliojiweka wakfu; atapata baraka iliyoje katika utendaji wa uadilifu katika kazi yake!— The Southern Watchman, Novemba 20, 1902 **( Pacific Union Recorder, Novemba 20, 1902 ). ChS 134.2**



Kila mfanyakazi wa injili anapaswa kuhisi kwamba utoaji wa mafundisho katika kanuni za maisha yenye afya, ni sehemu ya kazi yake aliyopangiwa na Mungu. Kuna hitaji kubwa la kazi hii, na ulimwengu uko wazi kwa ajili ya kulipokea.— The Ministry of

—

Healing, p. 147 . ChS 134.3

Mkono wa Kuume wa Ujumbe

**Tena na tena nimeagizwa kwamba kazi ya umishenari wa tiba ni kubeba uhusiano sawa na kazi ya ujumbe wa malaika watatu ambao ndiyo kiganja na mkono kutoka kwenye mwili. Chini ya Uongozi wa Kichwa cha Kiungu/mbinguni vyote vinapaswa kufanya kazi kwa umoja katika kuandaa njia kwa ajili ya kuja kwa Kristo. Mkono wa kuume wa mwili wa ile Kweli unapaswa kuwa na utendaji kila wakati, ukifanya kazi kila mara, na Mungu atauimarisha. Lakini mkono haupaswi kufanywa kuwa mwili. Wakati huo huo mwili haupaswi kusema kwa mkono: "mimi Sina haja na wewe." Mwili unahitaji mkono ili kufanya kazi hai na ya juhudi kali (aggressive). Vyote viwili, mwili na mkono vina kazi yao iliyoteuliwa na Mungu, na kila kimoja kitapata hasara kubwa ikiwa kitafanya kazi bila ya kingine. —Shuhuda kwa Kanisa 6:288.ChS 134.5**

**Kazi ya umishenari wa tiba inapaswa kufanywa. Lakini hii ni sehemu moja tu ya kazi ambayo inapaswa kutimizwa, na haipaswi kufanywa kuwa ndio yote katika yote. Inapaswa kuwa kazi ya Mungu, kamavile mkono ulivyo kwa mwili. —Shuhuda kwa Kanisa 8:160.ChS 134.6**

## Ushirikiano wa Kiungu

—

Kristo anahisi ole wa kila anayeteseka. Pepo wachafu wanaporarua sura ya mwanadamu, Kristo anahisi laana. Wakati homa inapochoma mkondo wa maisha, Yeye huhisi uchungu. Naye Yuko tayari kabisa kuwaponya wagonjwa yao sasa, kama vile alipokuwa mbashara hapa duniani, uso kwa uso na watu. Watumishi wa Kristo ni wawakilishi Wake, mikondo ya kufanya kazi Yake. Yeye Anatamani atumie nguvu Zake za uponyaji kupitia kwao.— **The Desire of Ages, p. 823, 824 . ChS 135.1**

Kupitia watumishi Wake, Mungu anapanga kwamba wagonjwa, wasiobahatika au watu waliopata majanga na shida, na wale waliopagawa na pepo wachafu, waisikie sauti Yake. Kupitia mawakala Wake ya kianadamu Anatamani kuwa mfariji, kwa namna ambayo ulimwengu haujui.— **The Ministry of Healing, p . ChS 135.2**

Kristo anashirikiana na wale ambao hujihusisha na kazi ya umishenari wa tiba. —
Shuhuda kwa Kanisa 7:51.**ChS 135.3**

Bwana alitenda kupitia kwao. Popote walipoenda, wagonjwa waliponywa, na maskini walihubiriwa injili.— **The Acts of the Apostles, p. 106 . ChS 135.4**

Kristo hayuko tena katika ulimwengu huu katika mwili, akipita katika miji na vijiji, akiwaponya watu mgonjwa; bali Ametuagiza sisi kuiendeleza kazi ya umisenari wa tiba, ambayo Yeye aliianzisha. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:168. ChS 135.5**

## Kazi ya Kila Kanisa

Kuna ujumbe kuhusu matengenezo ya afya unaopaswa kubebwa katika kila kanisa. —
**Shuhuda kwa Kanisa 6:370. ChS 135.6**

Kazi ya umishonari wa tiba inapaswa kuwa sehemu ya kazi ya kila kanisa katika nchi yetu. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:289.ChS 135.7**

Tumefika wakati ambapo kila mshiriki wa kanisa anapaswa kuchukua kazi ya umishenari wa tiba. **—Shuhuda kwa Kanisa**

—

**7:62.ChS 135.8**

Kazi ya matengenezo ya afya ni njia ya Bwana kupunguza mateso na taabu katika ulimwengu wetu na kulitakasa kanisa Lake. Wafundishe watu kwamba wanaweza kutenda kama mkono wa msaada/kusaidia wa Mungu kwa kushirikiana na Mwalimu mkuu katika kurejesha afya za watu za kimwili na kiroho. Hii kazi ina muhuri wa mbinguni na itafungua milango kwa ajili ya kuingia kwa Kweli zingine za thamani. Kuna nafasi kwa wote kufanya kazi ambao wataishikilia kazi hii kwa akili mahiri-akili zenye akiil. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:112, 113.ChS 135.9**

Kuna nyakati za dhoruba mbele yetu, lakini tusitamke hata neno moja la kutoamini au kukatisha tamaa. Na tukumbuke kwamba tunabeba ujumbe wa uponyaji kwa ulimwengu uliojaa roho zinazougua kwa dhambi.— **Special Testimonies Series B, No. 8, p. 24 . ChS 136.1**

Kazi hii, ikifanywa ipasavyo, itaokoa maskini wengi wenye dhambi ambao wametelekezwa na makanisa. Wengi wasio wa imani yetu wanatamani msaada uleule

—

ambao Wakristo wana wanawajibika kuutoa. Ikiwa watu wa Mungu wangeonyesha kupendezwa kikweli na jirani zao, wengi wangefikiwa na Kweli za pekee za wakati huu. Hakuna kitu kitakachoweza kutoa tabia kwa kazi Mungu, kama kuwasaidia watu pale walipo. Huenda maelfu leo wangeshangilia ujumbe huo ikiwa wale wanaodai kumpenda Mungu na kushika amri Zake wangefanya kazi kama Kristo alivyofanya kazi. Wakati kazi ya umishenari wa tiba inapowapata wanaume na wanawake kuja kwenye ujuzi unaookoa wa Kristo na Ukweli Wake, pesa na kazi ya bidii inaweza kuwekezwa ndani yake kwa usalama, kwa kuwa ni kazi ambayo itadumu. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:280.ChS 136.2**

Hebu watu wetu waonyeshe kuwa wana nia yenye utendaji hai katika kazi ya umishenari wa tiba. Hebu wajiandae kwa kuwa watu watu wenye kunufaisha, kwa kusoma vitabu ambavyo vimeandikwa katika mafundisho yetu katika njia hii. Vitabu hivi vinastahili umakini na kuthaminiwa zaidi ya jinsi vilivyopokelewa. Mengi ambayo wote wanapaswa kuelewa, kwa kuwa ni ya kunufaisha watu yameandikwa kwa kusudi maalum la kufundisha kanuni za afya. Wale ambao hujifunza na kutekeleza kanuni hizi watabarikiwa sana, kimwili na kiroho. Kuelewa falsafa ya afya itakuwa kinga dhidi ya maovu mengi ambayo yanaendelea kuongezeka. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:63. ChS 136.3**

Nimeagizwa kwamba kazi ya umishenari wa tiba itagundua katika kina kirefu cha uharibifu, wanadamu ambao, ingawa wamejitolea wenyewe kwa tabia zisizo na kiasi, na zisizofaa, wataitikia aina sahihi ya kazi. Lakini wanahitaji kutambuliwa na kutiwa moyo. Juhudi thabiti, zenye uvumilivu, na za dhati zitahitajika ili kuwainua. Hawa hawawezi kujirejesha wenyewe. Wanaweza wasikie wito wa Kristo, lakini masikio yao ni mazito sana yasiweze kupokea maana yake; macho yao yamepofuka sana wasiweze kuona lolote jema ambalo liko kwaajili yao. Wamekufa katika makosa na dhambi. Lakini hata hawa hawapaswi kutengwa na karamu ya injili. Wanapaswa kupokea mwaliko: "Njooni." Ingawa wanaweza kujisikia kutostahili, Bwana

—

asema: "Walazimishe kuingia." Sikiliza udhuru au visingizio vyovyote. Kwa upendo na fadhili washike sawa. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:279, 280.ChS 136.4**

Wale wanaochukua aina hii ya kazi wanapaswa kwenda wakiwa tayari kwa kazi ya umishenari wa tiba. Walio wagonjwa na wanaoteseka wanapaswa kusaidiwa. Wengi ambao kazi hii ya rehema imefanyika kwao watasikia na kuyakubali Maneno ya uzima.
—Shuhuda kwa Kanisa 9:34.**ChS 137.1**

Ni nani anayejiandaa kushika mpini wa kazi hii ya umishenari wa tiba kwa uelewa? Kwa kazi hii, akili za wale wanaokuja kwenye vituo vyetu vya tiba wataongozwa kwa Kristo na kufundishwa kuunganisha udhaifu wao na nguvu Zake. Kila mtendakazi anapaswa kuwa na uelewa mzuri na ufanisi. Halafu kwa hali ya juu na pana anaweza kuwasilisha Ukweli kama ulivyo katika Yesu. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:70.ChS 137.2**

Hebu kazi ya Bwana isonge mbele. Hebu umisheonari wa tiba na kazi ya elimu zisonge mbele. Nina hakika kwamba huu ndio upungufu wetu mkubwa—watendakazi walio dhati, wenye bidii, wanaojitolea, wenye akili mahiri na wenye uwezo. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:168, 169. ChS 137.4**

Hebu watendakazi wachukue kanuni hai za matengenezo ya afya katika jamii ambazo kwa kiwango kikubwa hawazijui kanuni hizi. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:118.ChS 137.5**

Nimeagizwa kuwaambia wakufunzi wa matengenezo ya afya: Songa mbele. Ulimwengu unahitaji kila nukta ya ushawishi mnaoweza kuwa nao ili kurudisha nyuma wimbi la ole wa maadili. Hebu wale wanaoufundisha ujumbe wa malaika wa tatu wasimame kweli kwa rangi zao. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:113. ChS 137.6**

## Mpango Mkubwa wa Tiba

Bwana atazipatia Sanitarium zetu ambazo kazi yake tayari imeshaanzishwa fursa ya kushirikiana Naye katika kusaidia mbegu mpya inayochipua. Kila taasisi mpya inapaswa kuzingatiwa kama ndugu msaidizi katika kazi kubwa ya kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu. Mungu amezipatia Sanitarium zetu fursa ya kuweka katika utekelezaji kazi ambayo itakuwa kama jiwe hisia lililojaa uhai, likikikua na likiwa linavingirishwa na Mkono usioonekana. Hebu Jiwe hili la ajabu liwekwe katika mjongeo. **— Shuhuda kwa Kanisa 7:59.ChS 137.6**

## Kazi ya Kitaasisi

Migahawa ya afya na vyumba vya tiba/matibabu vinapaswa kuanzishwa (Hygenic restaurants na Sanitarium). Jitihada zetu katika nyanja hii zinapaswa kujumuisha vituo vingi vya watalii na mapumziko, kwenye fukwe za bahari. Kama sauti ya Yohana Mbatizaji ilivyosikika nyikani, "Tengenezeni njia ya Bwana," ndivyo sauti ya wajumbe wa Bwana inapaswa kusikiwa katika vituo vingi vya watalii na maeneo ya kutalii kando ya bahari.**— Shuhuda kwa Kanisa 7:55, 56.ChS 138.1**

Nimepewa nuru kwamba katika miji mingi ni vyema kwamba migahawa ya afya iunganishwe na vyumba vya tiba sahili. Hivi viwili vinaweza kushirikiana katika kushikilia kanuni sahihi. Kuhusiana na haya wakati mwingine inashauriwa kuwa na vyumba ambavyo vitatumika kwa kupumzikia wagonjwa

—

wanaokuja. Taasisi hizi zitatumika kupata walengwa/wateja kwaajili ya vituo vya Sanitarium vilivyopo katika nchi. — **Shuhuda kwa Kanisa 7:60.ChS 138.2**

Bwana ana ujumbe kwa ajili ya miji yetu, na ujumbe huu tunapaswa kuutangaza katika mikutano yetu ya makambi na katika mikutano yetu ya hadhara pia kupitia machapisho yetu. Kwa kuongezea hili, migahawa inayozingatia kanuni za afya inapaswa kuanzishwa katika miji, na kupitia kwa hiyo, ujumbe wa kuwa na kiasi utatangazwa. Mikakati inapaswa kuwekwa katika kufanya mikutano inayounganisha wateja wanaokuja kwenye migahawa yetu. Kadri inavyowezekana, hebu vyumba vitolewe, ambavyo wadau wanaweza kualikwa kutoa mihadhara juu ya sayansi ya afya na mwenendo wa Kikristo, mahali ambapo wanaweza kupokea maagizo juu ya utayarishaji wa chakula bora cha afya, kisichokobolewa au kusindikwa na juu ya masomo mengine muhimu. — **Shuhuda kwa Kanisa 7:115. ChS 138.3**

Wale wanaokuja kwenye migahawa yetu wanapaswa kupatiwa vitu vya kusoma. Usikivu wao unapaswa kuvutwa katika machapisho yetu juu ya kiasi na matengenezo ya lishe, na vipeperushi vinavyoshughulikia masomo ya Kristo, watu wapewe haya machapisho. Mzigo

wa kusambaza machapisho haya ya kusoma unapaswa kufanywa na watu wetu wote. Wote wanaokuja wapewe kitu cha kusoma. Inawezekana kwamba wengi hawatayasoma machapisho hayo, lakini wengine kati ya wale unaowawelea makala hizi mikono mwao, wanaweza kuwa wanatafuta nuru. Watasoma na kujifunza kile unachowapa, kisha watawapatia wengine. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:116.ChS 138.4**

Nimeagizwa kuwa moja ya sababu kuu kwa nini migahawa inayozingatia kanuni za afya na vyumba vya tiba inapaswa kuanzishwa katika vituo vya miji mikubwa ni kwamba kwa njia hii umakini wa watu wakuu wa mji, wale wanaoongoza watavutwa katika ujumbe wa Malaika Watatu (wa tatu). Kwa kugundua kuwa migahawa hii inaendeshwa kwa njia tofauti kabisa na njia ambayo migahawa ya kawaida husimamiwa, watu wenye akili mahiri wataanza kuhoji sababu za tofauti ya njia za kuendesha shuguli na biashara, na watachunguza kanuni ambazo zinatuongoza kutoa chakula bora. Kwa hivyo wataongozwa katika ujuzi wa ujumbe kwa wakati huu. **— Shuhuda kwa Kanisa 7:122, 123. ChS 139.1**

**Shule za Upishi**

Nimeagizwa kuhamasisha uendeshaji wa shule za upishi katika maeneo yote ambapo kazi ya umishenari wa tiba inaendeshwa. Kila motisha ya kuwaongoza watu kufanya matengenezo lazima iwekwe mbele yao. Hebu mwanga mwingi kadri iwezekanavyo uangaze juu yao. Wafundishe watu kufanya kila maboresho wanayoweza, katika utayarishaji wa chakula, na uwatie moyo kuwagawia wengine yale wanayojifunza.— **Gospel Workers, 362, 363 . ChS 139.2**

Shule za upishi zinapaswa kuanzishwa (mafunzo ya mapishi). Watu wanapaswa kufundishwa jinsi ya kuandaa chakula kizuri cha afya, kisichosindikwa wala kukobolewa. Wanapaswa kuoneshwa hitaji la kuacha vyakula visivyofaa. Lakini hatupaswi kamwe kutetea watu kukaa kwa njaa kwaajili ya lishe hafifu (no

—

starvation). Inawezekana kuwa na lishe bora, yenye virutubisho bila kutumia chai nyeusi ya China, kahawa, na chakula cha nyama. Kazi ya kufundisha watu jinsi ya kuandaa lishe ambayo ni ya afya, yenye vyakula visivyokobolewa wala kusindikwa na ya kupendeza kwa ladha ni ya umuhimu mkubwa. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:112.ChS 139.3**

## Ujumbe wa Wakati

Siwezi kuwasisitizia kwa uzito wa kutosha washiriki wote wa kanisa letu kuliko hivi, wale wote ambao ni wamishenari wa Kweli, wote wanaoamini ujumbe wa malaika wa tatu, wote wanaoigeuza miguu yao kutoka kwenye Sabato, wanapaswa kuzingatia ujumbe wa sura ya hamsini na nane ya Isaya (Isaya 58). Kazi ya rehema, ukarimu, wema na fadhila, waliyopewa watu katika sura hii ni kazi ambayo Mungu anahitaji watu Wake waifanye kwa wakati huu. Ni kazi aliyoiweka Yeye mwenyewe. Hatujaachwa katika shaka juu ya mahali ambapo ujumbe huo unahusu, na wakati wa utimizo wake uliowekwa alama, kwa kuwa twasoma hivi: “Na watu wako watapajenga mahali palipokuwa ukiwa; utaiinua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka; na, Mwenye kurejeza njia za kukalia." Mstari wa 12. **ChS 139.2**

Kumbukizi/kumbumbu ya Mungu, Sabato ya siku ya saba, ishara ya kazi Yake katika kuumba ulimwengu, imehamishwa na mtu wa dhambi-mwana wa uasi. Watu wa Mungu wana kazi maalum ya kufanya katika kutengeneza mbomoko/mvunjiko ambao umefanywa katika

sheria Yake; na kadiri tunavyokaribia mwisho, ndivyo kazi hii inavyokuwa ya haraka zaidi. Wote wanaompenda Mungu wataonyesha kwamba wanabeba ishara Yake kwa kushika amri Zake. Hao ndio warejeshaji wa njia za kukaa ndani. Bwana asema hivi: "Kama ukigeuza mguu wako usiiache Sabato, usifanye anasa yako katika siku Yangu takatifu, na kuiita Sabato siku ya furaha; . . . ndipo utakapojifurahisha katika Bwana; Nami nitakupandisha mahali palipoinuka duniani." Mistari 13, 14. Hivyo kazi ya umishenari wa kweli wa tiba , na inafungamanishwa na kushika amri za Mungu bila kutenganishwa, ambapo Sabato inatajwa kwa njia mahususi, kwa kuwa ndiyo iliyo kuu. ukumbusho wa kazi ya uumbaji ya Mungu. Utunzaji Wake unafungamanishwa na kazi ya kurudisha sura ya kimaadili ya Mungu ndani ya mwanadamu. Hii ndiyo huduma ambayo watu wa Mungu wanapaswa kuiendeleza mbele, kwa wakati huu. Huduma hii ikifanywa ipasavyo, italeta baraka tele kwa kanisa. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:265, 266.ChS 139.4**

## SURA YA 12 UINJILISTI WA BIBLIA

### Wazo Kutokea Mbinguni

Mpango wa kufanya usomaji wa Biblia, (darasa la Biblia),

—

ulikuwa ni wazo lililozaliwa mbinguni (Bible Study). Kuna wengi, wanaume na wanawake, ambao wanaweza kushiriki katika tawi hili la kazi ya umishenari. Watenda kazi wanaweza kukuzwa ambao watakuwa watu hodari wa Mungu. Kwa njia ya kazi hii, Neno la Mungu limetolewa kwa maelfu; na watendakazi wanaletwa katika mawasiliano binafsi na watu wa mataifa na lugha zote. Biblia inaletwa katika familia, na Kweli zake takatifu huja moyoni kwenye dhamiri. Wanaume wanahamasishwa kusoma, kuchunguza, na kujihukumu/kujichunguza wenyewe, na lazima wawe na msimamo wenye wajibu wa kupokea, au kukataa nuru ya Bwana. Mungu hataruhusu kazi hii ya thamani Kwake kwenda bila thawabu. Yeye Ataivika taji kwa mafanikio kila jitihada ya unyenyekevu inayofanywa kwa Jina Lake.— **Gospel Workers, p. 192 . ChS 141.1**

Kazi yetu imewekewa alama na Baba yetu wa mbinguni. Tunapaswa kuzichukua Biblia zetu na kwenda kuuonya ulimwengu. Tunapaswa kuwa mikono ya usaidizi ya Mungu katika kuokoa roho--njia ambazo upendo Wake unapitia siku baada ya sikuna kutiririka kwa watu wanaoangamia. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:150.ChS 141.2**

## Wito wa Uhakika

Wengi wataitwa shambani mwa Bwana, kufanya kazi nyumba kwa nyumba, wakitoa mafundisho ya Biblia na kuomba pamoja na walio na shauku. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:172.ChS 141.3**

Watendakazi wengi wanapaswa kutenda sehemu yao, kufanya kazi ya nyumba kwa nyumba na kuisoma Biblia katika familia. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:141.ChS 141.4**

Wanawake waliowekwa wakfu wanapaswa kushiriki katika kazi ya Biblia, nyumba kwa nyumba. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:120, 121.ChS 141.5**

Ikiwa tunafuata nyayo za Kristo, ni lazima tukaribia wale wanaohitaji huduma yetu. Ni lazima tufungue Biblia kwa uelewa wa watu, tuwasilishe madai ya sheria ya Mungu, tusome ahadi kwa wanaositasita, tuwaamshe wasiojali, na wazembe, tuwatie nguvu watu walio dhaifu.— **Gospel Workers, p. 336 . ChS 141.6**

Katika uzoefu wa Filipo na Mkushi imewasilishwa kazi ambayo kwayo Bwana anawaita watu Wake. Mkushi anawakilisha tabaka kubwa ambalo linahitaji wamishenari kama Filipo, wamishenari ambao wataisikia sauti ya Mungu na kwenda kule anakowatuma. Wapo watu ulimwenguni ambao wanasoma Maandiko, lakini hawawezi kuelewa maana yake. Wanaume na wanawake ambao wana maarifa juu ya Mungu wanahitajika kulielezea neno kwa roho hizi. **—Shuhuda kwa Kanisa 8:58, 59.ChS 142.1**

Miongoni mwa washiriki wa makanisa yetu kunapaswa kuwa na kazi zaidi ya nyumba kwa nyumba katika kuisoma Biblia kwa pamoja katika nyumba hizo. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:127.ChS 142.2**

Hebu watenda kazi waende nyumba kwa nyumba, wakiifungua Biblia kwa watu. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:123.ChS 142.3**

Katika majimbo mengi kuna makazi ya watu wenye stadi na bidii ya kazi, wakulima wenye hali nzuri kimaisha na kifedha, ambao hawajaupata Ukweli wa leo. Maeneo kama haya yanapaswa kufanyiwa kazi. Hebu Washiriki wetu walei wachukue

aina hii ya huduma. Kwa kuazimisha au kuuza vitabu, kwa kusambaza vijizuu na machapisho, na kwa kuifungua Biblia na kusoma pamoja, washiriki wetu wanaweza kufanya kazi kwa kiwango kikubwa sana kwa majirani zao wenyewe. Wakiwa wamejazwa na upendo kwa roho za watu, wanaweza kuutangaza ujumbe kwa nguvu kubwa kiasi cha kuwaongoa wengi. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:35.ChS 142.4**

**Mandhari ya Kuvutia**

Mamia kwa maelfu walionekana wakizitembelea familia na kulifunua mbele yao Neno la Mungu. Mioyo ilisukwa-sukwa na kusandikishwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, na roho ya uongofu wa kweli ikadhihirishwa. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:126.ChS 142.5**

Watendakazi wawili wa Biblia walikuwa wameketi katika familia. Wakiwa na Biblia iliyofunguliwa mbele yao, walimwasilisha Bwana, Yesu Kristo kama Mwokozi anayesamehe dhambi. Maombi ya dhati yalitolewa kwa Mungu, na mioyo ikalainishwa na kutiishwa kwa ushawishi wa Roho wa Mungu. Maombi yao yalitamkwa kwa upya na nguvu. Kadri Neno la Mungu lilivyofafanuliwa, niliona kwamba, nuru laini, ang’avu iliyaangazia Maandiko, na nikasema, kwa upole: “Nenda barabarani na mipakani,

ukawashurutishe kuingia ndani, ili nyumba Yangu ipate kujaa. "Luka 14:23. — **Shuhuda kwa Kanisa 9:35. ChS 142.6**

Kuna wengi wanaosoma Maandiko ambao hawawezi kuelewa maana yake ya Kweli. Ulimwenguni kote wanaume na wanawake wanakodolea mbingu kwa shauku. Maombi na machozi na maswali hupanda juu kutoka kwa roho zinazotamani nuru, neema, na Roho Mtakatifu. Wengi wako kwenye ukingo wa ufalme wa Mungu, wakingoja tu kukusanywa.— **The Acts of the Apostles, 109 . ChS 143.1**

**Maandalizi kwa Ajili ya Kazi**

Wafuasi wa Yesu hawakutani na akili na mapenzi ya Mungu ikiwa wanaridhika kukaa katika ujinga wa kutolijua Neno Lake. Watu wote wanapaswa kuwa wanafunzi wa Biblia. Kristo aliwaamuru wafuasi Wake: "Mwayachunguza Maandiko, kwa maana mnadhania mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndio yanayonishuhudia." Petro anatuhimiza:" Bali mtakaseni Bwana Mungu mioyoni mwenu; muwe tayari daima kumjibu kila mtu anayekuuliza sababu ya tumaini lililo ndani yako kwa upole na kwa hofu." **—Shuhuda kwa Kanisa 2:633, 634.**

Wale ambao wameongoka kweli kweli lazima wawe na akili mahiri zaidi katika uelewa wao wa Maandiko, ili waweze kunena Maneno ya nuru na wokovu kwa wale walio gizani, wanaoangamia katika dhambi zao. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:121.**

Tunapaswa kutoa onyo la mwisho la Mungu kwa wanadamu, na jinsi gani bidii yetu katika kujifunza Biblia inavyopaswa kuwa kubwa, na ari yetu katika kueneza nuru! Hebu kila nafsi iliyopokea nuru ya Bwana itafute kuitoa hiyo nuru kwa wengine. Hebu watenda kazi waende nyumba kwa nyumba, wakiwafungulia watu Biblia, wakisambaza machapisho, wakiwaambia wengine juu ya nuru ambayo imebariki nafsi zao wenyewe.— **Gospel Workers, 353 . ChS 143.4**

Kazi nzuri yenye msawaziko, inaweza kufanywa vizuri zaidi

—

pale shule ya mafunzo kwa watendakazi wa Biblia inapokuwa inaendeshwa. Wakati mikutano ya hadhara inaendelea, ikiunganishwa na shule hii ya mafunzo au utume wa mijini kwa watendakazi wenye uzoefu, wenye uelewa wa kina wa kiroho ambao wanaweza kuwapa watendakazi wa Biblia maelekezo, na ambao wanaweza pia kuungana kwa moyo wote katika juhudi za mahubiri ya hadhara yanayoendelea. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:111.**

**Siri ya Mafanikio**

Leta udhati na bidii katika maombi yako, katika usomaji wako wa Biblia, na katika mahubiri yako, ili uweze kuacha mguso moyoni mwa watu kwamba zile Kweli takatifu unazowasilisha kwa wengine ni uhalisia ulio hai kwako wewe binafsi. Chochote unachomfanyia Yesu, tafuta kwa nguvu zako zote kukifanya kwa dhati na bidii. Usijisikie kamwe kwamba umefikia kiwango cha juu zaidi, na kwa hivyo huwezi kupanda juu zaidi Weka akili yako kwenye kazi, ili uweze kuwasilisha Ukweli kwa namna ya kuwavutia. Chukua sehemu zenye kupendeza zaidi za Maandiko ambazo unaweza kuleta mbele yao, njoo moja kwa moja kwenye pointi au kipengele husika, usizunguke-zunguke, na

utafute kukaza fikira na mioyo yao, na kuwafundisha katika njia za Bwana.— **The Review and Herald, Julai 26, 1887 . ChS 144.1**

Kazi kubwa inaweza kufanywa kwa kuiwasilisha Biblia kwa watu kama inavyosomeka tu. Lipelekeni Neno la Mungu kwenye mlango wa kila mtu, sisitizeni Kauli Zake kwa uwazi juu ya dhamiri ya kila mtu, rudieni kwa wote, Amri ya Mwokozi: "Yachunguzeni Maandiko." Washaurini watu waichukue Biblia kama ilivyo, waombe mwangaza wa Bwana, halafu, wakati nuru inapong'aa, waukubali kila mwale wa nuru ya thamani kwa furaha na kuyapokea na kukaa matokeo yake bila woga. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:388. ChS 144.2**

## Kazi ya Shangwe

Ni kazi ya shangwe kuwafunulia wengine Maandiko. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:118.ChS 144.3**

Fungua Maandiko kwa mtu aliye gizani, na usilalamike kwa uchovu na ukosefu wa nia na shauku kwa sababu ya Ukweli. Moyo wako utaamshwa kwa nafsi zinazohangaika, na shangwe katika ushahidi wa imani itajaa ndani ya moyo wako, nawe utajua kwamba "atiaye maji atanywesha yeye mwenyewe."— **The Review and Herald, Machi 13, 1888 . ChS 144.4**

# SURA YA 13 HUDUMA YA UCHAPISHAJI

## Kazi ya Umuhimu wa Kwanza

Ikiwa kuna kazi moja iliyo muhimu zaidi kuliko nyingine, ni ile ya kupeleka machapisho yetu mbele ya watu wote, na hivyo kuwaongoza kuyachunguza Maandiko. Kazi ya umishonari—kutambulisha machapisho yetu katika familia, kuzungumza, na kusali pamoja nao na kwa ajili yao—ni kazi nzuri.— **The Colporteur Evangelist, 80 . ChS 145.1**

—

Hebu kila Muadventista wa Sabato ajiulize, “Nifanye nini ili kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu?” Kristo alikuja katika ulimwengu huu kutoa ujumbe huu kwa mtumishi Wake ili wawape makanisa. Ujumbe huu unapaswa kutangazwa kwa kila taifa, kabila, lugha, jamaa na watu. Tuutoe vipi ujumbe huu? Ugawaji wa machapisho yetu ni njia mojawapo ambayo kwayo ujumbe unapaswa kutangazwa. Hebu kila muumini atawanye majarida, makala, vipeperushi na vitabu vyenye ujumbe kwa wakati huu. Wauzaji/wainjilisti wa vitabu wanahitajika ambao wataenda kusambaza machapisho yetu kila mahali.— **The Southern Watchman, Januari 5, 1904 . ChS 145.2**

Makala, na vitabu (machapisho) ni njia ya Bwana kuweka daima ujumbe kwa wakati, mbele ya watu. Katika kuzitia nuru na kuzithibitisha nafsi katika ile Kweli machapisho yatafanya kazi kubwa zaidi kuliko ile inayoweza kukamilishwa na huduma ya Neno pekee. Wajumbe wa kimya ambao wamewekwa katika nyumba za watu kupitia kazi ya mwinjilisti wa vitabu, wataimarisha huduma ya injili kwa kila njia; kwa maana Roho Mtakatifu atawavutia watu wasomapo vitabu hivyo, kama vile anavyovutia akili za wale wanaosikiliza kuhubiriwa kwa Neno. Huduma hiyo hiyo ya malaika huhudhuria vitabu

vilivyo na Ukweli kama ambavyo huhudhuria kazi ya mchungaji anayehubiri. — **Shuhuda kwa Kanisa 6:315, 316.ChS 145.3**

Hebu kazi ya uinjilisti wa vitabu nyumba kwa nyumba, isiachwe idhoofike. Acheni vitabu vyenye nuru juu ya Ukweli uliopo viwekwe mbele ya wengi. Wenyeviti wetu wa konferensi/majimbo zetu na wengine katika nyazifa za kuwajibika wana wajibu wa kufanya katika suala hili. —**The Southern Watchman, April 25, 1905.ChS 145.4**

Ulimwengu unapaswa kupokea nuru ya Ukweli kupitia huduma ya kueneza injili ya Neno katika vitabu vyetu na majarida. Machapisho yetu yanapaswa kuonyesha kwamba mwisho wa mambo yote umekaribia.— **The Colporteur Evangelist, 100 . ChS 146.1**

Mungu anawaita watu Wake kutenda kama watu walio hai, na wasiwe watu goigoti, wazembe, wavivu na wasiojali. Ni lazima tupeleke machapisho kwa watu kuwahimiza wayapokee na kuyakubali. —**The Southern Watchman, April 25, 1905.ChS 146.2**

Machapisho yetu sasa yanapanda mbegu ya injili, na ni chombo kinacholeta roho nyingi kwa Kristo kama Neno lililohubiriwa kibwetani. Makanisa mapya yameinuliwa kama matokeo ya mzunguko wa machapisho. Katika kazi hii kila mfuasi wa Kristo anaweza kutenda sehemu.— **The Review and Herald, Juni 10, 1880 . ChS 146.3**

Mjumbe kutoka mbinguni alisimama katikati yetu, na alizungumza maneno ya onyo na maelekezo. Alitufanya tuelewe wazi kwamba injili ya ufalme ni ujumbe ambao ulimwengu unaangamia kwa kukosa na kwamba ujumbe huu, upo, nao kama ulivyo katika machapisho yetu ambayo tayari yamechapishwa na yale ambayo yako tayari kutolewa baadae, unapaswa kusambazwa kati ya watu walio karibu na walio mbali. — **Shuhuda kwa Kanisa 9:67.ChS 146.4**

Kazi ya vitabu inapaswa kuwa njia ya haraka ya kutoa nuru

—

takatifu ya Ukweli wa leo kwa ulimwengu. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:69.ChS 146.5**
Shetani ana shughuli nyingi katika idara hii ya kazi yake, akieneza machapisho ambayo yanashusha chini maadili na kutia sumu akili za vijana. Machapisho ya kikafiri yametawanyika kote nchini. Kwa nini kila mshiriki wa kanisa asifurahie kwa kina, kutuma machapisho ambayo yatainua akili za watu, na kuleta Ukweli moja kwa moja mbele yao? Karatasi na vipeperushi hivi ni kwa ajili ya nuru ya ulimwengu, na mara nyingi vimekuwa chombo katika kuongoa roho za watu— **The Review and Herald, Juni 10, 1880 . ChS 146.6**

Ni kana kwamba tumelala usingizi kuhusu kazi inayoweza kukamilishwa kwa kuenezwa kwa fasihi iliyotayarishwa vizuri. Hebu sasa, kwa tutumie kwa hekima magazeti na vitabu, tulihubiri Neno kwa nguvu iliyoazimiwa, ili ulimwengu upate kuelewa ujumbe ambao Kristo alimpa Yohana kwenye kisiwa cha Patmo.— **The Colporteur Evangelist, 101 . ChS 146.7**

Washiriki wa kanisa, waamke juu ya umuhimu wa usambazaji wa machapisho yetu, na watoe muda zaidi kwa kazi hii. Weka katika nyumba za watu karatasi, machapisho, vipeperushi, na vitabu ambavyo vitahubiri injili katika mistari yake kadhaa. Hakuna wakati wa kupotea.

—

Hebu wengi wajitoe wenyewe kwa hiari na bila ubinafsi kwa kazi ya kuhubiri, na hivyo kusaidia kutoa onyo ambalo linahitajika sana. Kanisa litakapoanza kazi yake iliyoagizwa na Mungu, litatoka nje "katika uzuri kama mwezi, angavu kama jua, na la kutisha kama jeshi lenye bendera." (Wimbo Ulio Bora 6)— **The Southern Watchman, Novemba 20, 1902 ( Pacific Union Recorder, Novemba 20, 1902). 1902 ). ChS 147.1**

Nuru ya Ukweli inamwaga miali yake mikali juu ya ulimwengu kupitia juhudi za kimishenari. Vyombo vya habari na viwanda vya uchapishaji ni nyenzo ambayo huwafikia wengi ambao wasingeweza kufikiwa kwa juhudi za wachungaji. —Shuhuda kwa Kanisa 5:388.**ChS 147.2**

Usiku wa kujaribiwa unakaribia kuisha. Shetani anatenda kwa uwezo wake mkuu kwa sababu anajua kwamba wakati wake ni mfupi. Adhabu ya Mungu iko juu ya ulimwengu kuwaita wote waijuao Kweli wajifiche katika ufa wa Mwamba na kuutazama utukufu wa Mungu. Ukweli haupaswi kufungwa mdomo sasa. Kauli za wazi lazima zitolewe. Ukweli unaodumu lazima usemwe, katika vipeperushi, makala na majarida, na hivi lazima vitawanywe kama majani ya wakati wa kupukutisha au baridi. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:231.ChS 147.3**

Wainjilisti wa vitabu wa nyumba kwa nyumba wanahitajika ili kuchukua kazi ya kubeba wajumbe hawa wa kimya wa Ukweli kwa watu, - wainjilisti wa vitabu ambao wanahisi mzigo kwa nafsi, na ambao wanaweza kusema maneno kwa wakati kwa wale wanaotafuta nuru. Wengine wanaweza kusema, "Mimi si mchungaji; Siwezi kuwahubiria watu," Huenda usiweze kuhubiri, lakini unaweza kuwa mwinjilisti, ukihudumia mahitaji ya wale unaokutana nao; unaweza kuwa mkono wa msaada wa Mungu, ukifanya kazi kama wanafunzi walivyofanya kazi; unaweza kuwauliza wale unaokutana nao ikiwa wanampenda Bwana Yesu.— **The Southern Watchman, Novemba 20, 1902 ( Pacific Union Recorder, Novemba 20, 1902 ).**
**ChS** 147.4

### Nyumba za Uchapishaji Mawakala Wenye Ufanisi

Waadventista wa Sabato wamechaguliwa na Mungu kama watu wa kipekee, waliotengwa na ulimwengu. Kwa hekima kubwa ya kisu cha Ukweli, Yeye amewakata kutoka katika machimbo ya ulimwengu na kuwaleta katika muunganiko Naye. Amewafanya kuwa wawakilishi Wake na amewaita kuwa mabalozi Wake katika kazi ya mwisho ya wokovu. Tunu/utajiri mkubwa zaidi wa Ukweli uliowahi kukabidhiwa kwa wanadamu, maonyo mazito na ya kutisha kuwahi kutumwa na Mungu kwa mwanadamu, yamekabidhiwa kwao ili waupatie ulimwengu; na katika kufanikisha kazi hii nyumba zetu za uchapishaji ni miongoni mwa wakala wenye ufanisi zaidi. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:138. ChS 147.5**

Kazi yetu ya uchapishaji ilianzishwa kwa mwongozo wa Mungu na chini ya usimamizi Wake maalum. Iliundwa kutimiza kusudi maalum. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:138.ChS 148.1**

Na kwa kiwango kikubwa kupitia nyumba zetu za uchapishaji inapaswa kutimizwa kazi ya yule malaika mwingine anayeshuka kutoka mbinguni akiwa na nguvu kubwa na ambaye huangaza dunia kwa utukufu wake. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:140. ChS 148.2**

Ninalazimika kuziambia nyumba zetu za chapishaji: “Inueni kiwango, inueni juu zaidi.

Utangazeni ujumbe wa malaika Yule wa tatu; ili upate kusikiwa na ulimwengu wote. Hebu na ionekane kuwa 'hawa ndio wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu.' Ufunuo 14:12. Hebu machapisho yetu yatoe ujumbe kama ushuhuda kwa ulimwengu wote."—**Shuhuda kwa Kanisa 9:61. ChS 148.3**

### Kupanua Kazi ya Uchapishaji

Ninyi mnaouamini Ukweli wa leo, amkeni. Ni jukumu lenu sasa kuleta mali zote zinazowezekana kusaidia wale wanaoulewa Ukweli ili kuutangaza. Sehemu ya pesa zinazopatikana kutokana na mauzo ya machapisho yetu inapasa kutumiwa kuongeza miundombinu ya uchapishaji mingine zaidi, kwa ajili ya kuzalisha machapisho mengi zaidi yatakayofungua macho ya vipofu na kukatua ardhi ngumu ndani ya mioyo, ambayo ilikuwa bado kulimwa. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:62.ChS 148.4**

Miaka kadhaa iliyopita Bwana alinipa maagizo maalumu kwamba majengo yanapaswa kujengwa katika maeneo mbalimbali ya huko Marekani, Ulaya, na nchi zingine kwaajili ya uchapishaji wa vitabu mbalimbali vyenye nuru ya Ukweli wa sasa. Alitoa maelekezo kwamba kila juhudi inapaswa kufanywa katika kutuma ulimwenguni kutoka katika mitambo ya uchapaji ujumbe wa mwaliko na wa onyo. Baadhi watafikiwa na machapisho yetu ambao wasilingefikiwa kwa njia nyingine yoyote. Kutoka katika vitabu vyetu na makaratasi, miali angavu inapaswa kuangaza ili kuutia nuru ulimwengu kwa Ukweli wa sasa. **—Shuhuda kwa Kanisa 8:87.ChS 148.5**

Nimeonyeshwa kwamba machapisho yetu yanapaswa kuchapishwa katika lugha mbalimbali na kutumwa katika kila nchi iliyostaarabika, kwa gharama yoyote. Je, pesa ina thamani kwa wakati huu, kwa kulinganisha na thamani ya nafsi? Kila dola katika pesa zetu, inapaswa kuzingatiwa kama ya Bwana, sio yetu; na kama amana ya thamani kutoka kwa Mungu kwetu; siyo ya kupotezwa kwa ajili ya anasa zisizo na maana, bali kutumika kwa uangalifu katika kazi ya Mungu, katika kazi ya kuwaokoa wanaume na wanawake kutoka katika uharibifu.— **Life Sketches,**

—

p . ChS 149.1

Neno lililochapishwa la Ukweli linapaswa kutafsiriwa katika lugha tofauti-tofauti na kupelekwa hadi miisho ya dunia. — **Shuhuda kwa Kanisa 9:26.ChS 149.2**

Machapisho haya yanapaswa kutafsiriwa katika lugha nyingi, maana injili inapaswa kuhubiriwa kwa wote ulimwenguni. Kwa kila mtendakazi Kristo anaahidi ufanisi wa Bwana Mwenyewe, ambao utafanya kazi Yake iwe na mafanikio. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:34.ChS 149.3**

Machapisho yetu yanapaswa kwenda kila mahali. Hebu yatolewe kwa lugha nyingi. Ujumbe wa malaika wa tatu unapaswa kutolewa kupitia chombo hiki na kupitia kwa mwalimu aliye hai. Ninyi mnaoamini U kweli kwa wakati huu, amkeni.— **The Colporteur Evangelist, 101 . ChS 149.4**

Wengi wa Watu wa Mungu wanapaswa kupeleka machapisho yetu kwenye maeneo ambayo ujumbe wa malaika wa tatu haujatangazwa. Vitabu vyetu vinapaswa kuchapishwa katika lugha nyingi mbalimbali. Kwa kutumia vitabu hivi, Watu wanyenyekevu, na waaminifu wanapaswa kwenda kama wainjilisti wa vitabu wanaotembea nyumba kwa nyumba,

wakiipeleka Kweli kwa wale ambao kamwe wasingeipata nuru. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:33, 34.ChS 149. 5**

Kutoka mji hadi mji, kutoka nchi hata nchi, wanapaswa kubeba machapisho yenye ahadi ya ujio wa Mwokozi hivi karibuni. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:34.ChS 149.6**

**Nimeonyeshwa kwamba machapisho yamekuwa yakifanya kazi juu ya akili za watu fulani katika nchi nyingine tayari, kwa kubomoa kuta za ubaguzi na ushirikina. Nilionyeshwa wanaume na wanawake wakijifunza kwa shauku sana karatasi za makala mbalimbali na kurasa chache za trakti juu ya Ukweli wa sasa. Walisoma ushahidi wa ajabu sana na ulio mpya kwao, watu hawa walifunua Biblia zao kwa shauku kubwa na mpya, na mada za Ukweli ambazo zilikuwa giza kwao ziliwekwa wazi, hasa nuru kuhusu Sabato ya amri ya nne. Walipokuwa wakichunguza Maandiko ili kuona kama mambo hayo ndivyo yalivyo, nuru mpya iliangaza juu ya ufahamu wao, kwa kuwa malaika walikuwa wakizunguka-zunguka juu yao, na kukazia akilini mwao zile Kweli zilizo katika machapisho, walivyokuwa wakisoma.ChS 149.7**

**Niliwaona wakiwa wameshika magazeti na vijitabu kwa mkono mmoja, na Biblia kwenye mkono mwingine, huku mashavu yao yakiwa yamelowa machozi; na kusujudu mbele za Mungu kwa maombi ya dhati, na ya unyenyekevu, ili kuongozwa katika Kweli yote,—jambo lile lile ambalo Roho amekuwa akiwafanyia kabla hawajamwita. Na Kweli ilipopokelewa mioyoni mwao, na wakauona mnyororo upatanifu kwenye Ile Kweli, Biblia kwao kilikuwa kitabu kipya; waliikumbatia Kweli mioyoni mwao kwa shangwe yenye shukrani, huku nyuso zao zote zikiwaka kwa furaha na shangwe takatifu. ChS 150.1**

Hawa hawakuridhika tu na kufurahia nuru wenyewe, na walianza kufanya kazi kwa ajili ya wengine. Wengine walijitoa dhabihu sana kwa ajili ya Kweli na kuwasaidia ndugu waliokuwa gizani.

—

Kwa hiyo njia ilitayarishwa ii kufanya kazi kubwa katika ugawaji wa trakti na karatasi katika lugha nyinginezo.— **Life Sketches, 214, 215 . ChS 150.2**

## Fursa za Usambaji Huru

Hebu maandishi yasambazwe kwa busara kwenye treni, barabarani, mitaani na kwenye meli kubwa zinazopita baharini, na kupitia barua.— **Gospel Workers, 353 . ChS 150.3**

Katika siku hizi za kusafiri, fursa za kukutana na wanaume na wanawake wa tabaka zote, na wa mataifa mengi, ni kubwa zaidi kuliko siku za Israeli. Njia za usafiri zimeongezeka mara elfu. Mungu ameandaa njia kwa jinsi ya kustaajabisha. Wakala wa matbaa ya uchapishaji, pamoja na vifaa vyake vingi, iko kwa amri yetu. Biblia, na machapisho katika lugha nyingi, vinavyotangaza Ukweli kwa wakati huu, viko karibu nasi-mikononi mwetu, na vinaweza kubebwa upesi katika kila sehemu ya ulimwengu.— **Gospel Workers, 352 . ChS 150.4**

Hebu vipeperushi na magazeti, karatasi na vitabu, viende kila upande. Beba pamoja nawe, popote uendapo, kifurushi cha vipeperushi vilivyochaguliwa, ambavyo unaweza kutoa kadiri unavyopata fursa. Uza unachoweza, na uwakopeshe au uwape kama hali inaweza kuonekana kuhitaji. Matokeo muhimu yatafuata.— **The Review and Herald, Juni 10, 1880 . ChS 151.1**

Nimeoneshwa kuwa hatufanyi wajibu wetu katika usambazaji wa machapisho madogo madogo. Kuna roho nyingi za uaminifu ambazo zinaweza kuletwa kuukubali Ukweli kwa njia hii peke yake. Kama kwenye kila nakala ya vipeperushi hivi kutakuwa na tangazo la machapisho yetu na maeneo yanakoweza kupatikana, hii itaongeza usambazaji wa machapisho makubwa na magazeti ya *Review*, *Instructor* na *Reformer*. Hivi vipeperushi vidogo vyenye kurasa nne, nane, au kumi na sita vinaweza kutolewa kwa wingi, kwa gharama ndogo tu, kutoka kwenye mfuko uliotokana na michango ya wale ambao kazi iko moyoni. Unapomwandikia rafiki unaweza kuambatanisha

—

kipeperushi kimoja au zaidi bila kuongeza gharama ya posta. Unapokutana na watu kwenye magari, kwenye mashua, au kwenye hali ambayo wanaonekana kuwa na sikio la kusikia, unaweza kuwapatia kipeperushi. —Shuhuda kwa Kanisa 1:551, 552.**ChS 151.2**

**Tafuta kusajili Watu**

Akina dada wanaweza kufanya kazi kwa ustadi katika kupata watu kujiandikisha kwa ajili ya majarida yetu ya kila mwezi, kwa njia hii wakileta nuru mbele ya watu wengi.— **The Review and Herald, Juni 10, 1880 . ChS 151.3**

Sasa tunapewa majaliwa makubwa kwa ajili ya kueneza Kweli; lakini watu wetu hawako tayari kufanyia kazi fursa na fadhila walizopewa. Katika kila kanisa hawaoni na kuhisi umuhimu wa kutumia uwezo wao kuokoa roho. Hawatambui jukumu lao la kutafuta na kusajili wateja wa majarida, pamoja na magazeti yetu ya afya, na kutambulisha vitabu vyetu, makala na majarida. —Shuhuda kwa Kanisa 4:391.**ChS 151.4**

**Kuuza Vitabu**

Wengi wana huzuni na kukata tamaa, dhaifu katika imani na uaminifu. Hebu wafanye jambo fulani kusaidia mtu fulani aliye na uhitaji zaidi kuliko wao wenyewe, na watakuwa na nguvu katika nguvu za Mungu. Wajishughulishe na kazi nzuri ya kuuza vitabu vyetu. Hivyo watasaidia wengine, na uzoefu utakaopatikana utawapa uhakikisho wa kwamba wao ni mkono wa msaada wa Mungu. Wanapomsihi Bwana awasaidie, Yeye atawaongoza kwa wale wanaotafuta nuru. Kristo atakuwa karibu nao, akiwafundisha nini cha kusema na kufanya. Kwa kuwafariji wengine, wao wenyewe watafarijiwa.— **The Colporteur Evangelist, 40 . ChS 151.5**

**Kazi Katika Miji**

Tunaishi katika wakati ambapo kazi kubwa inapaswa kufanywa. Kuna njaa katika nchi kwa ajili ya injili safi, na mkate wa uzima utatolewa kwa roho zenye njaa. Hakuna nafasi nzuri zaidi ya kufanya kazi hii kuliko ile inayotolewa kwa mpelekaji wa vitabu aliyewekwa wakfu, naam mwinjilisti wa vitabu. Maelfu ya vitabu vyenye nuru yenye thamani ya Kweli ya sasa vyapaswa kuwekwa katika nyumba za watu katika majiji yetu makubwa.— **The Southern Watchman, Novemba 20, 1902 ( Pacific Union Recorder, Novemba 20, 1902 ).**
**ChS 152.1**

**Kweli za Biblia zenye baraka na zinazookoa nafsi zimechapishwa katika kurasa zetu. Kuna wengi ambao wanaweza kusaidia katika kazi ya kuuza majarida yetu. Bwana anatuita sisi sote kutafuta kuokoa roho zinazopotea. Shetani yuko kazini kuwadanganya hata walio wateule, na sasa**

—

**ni wakati wetu wa kufanya kazi kwa bidii. Vitabu na vijizuu vyetu vinapaswa kuletwa mbele za watu; injili ya Ukweli wa leo inapaswa ipelekwe kwenye miji yetu bila kuchelewa. Je, hatutaamka kwa ajili majukumu yetu? —Shuhuda kwa Kanisa 9:63. ChS 152.2**

**Machapisho ya Afya**

Wapekelekaji wa vitabu wapaswa kuangazia wale wanaowatembelea kuhusiana na machapisho yetu ya afya, wakiwaambia kuhusu maagizo muhimu yaliyomo katika magazeti haya kuhusu utunzaji wa wagonjwa na tiba/matibabu ya magonjwa magonjwa mbalimbali. Waambie kuwa maagizo haya, wanapojifunza, na kuyafanyia mazoezi, yataleta afya kwa familia. Eleza jinsi ilivyo muhimu kwa kila familia kuelewa sayansi ya maisha. Zielekeze akili zao kwa Yeye aliyeumba mwili kwa jinsi ya ajabu Naye ameuweka kwenye utaratibu na mjongeo endelevu. Waambie kwamba ni sehemu yetu kushirikiana na Mungu, tukitunza kwa hekima vitivyo vyetu na viungo vyetu vyote. **ChS 152.3**

Utunzaji sahihi wa mwili ni jukumu kubwa, na uhitaji maarifa yenye akili mahiri ili kujua sehemu zake na jinsi zinavyofanya kazi (fiziolojia). Waambie kwamba Mungu anavunjiwa heshima, watu wanapoendekeza kutosheleza hamu, tamaa na uchu wa chakula, mwanadamu anapotumia vibaya utaratibu wa mwili wake, anaulazimisha ufanye kazi yake kwa unyonge na kwa shida. Waambie kwamba vitabu vya kuuzwa ulivyo navyo, vinatoa maagizo muhimu sana kuhusu afya, na kwamba kwa kufuata maagizo haya, mateso mengi na pia pesa nyingi zinazotumiwa kulipia gharama za madaktari, zitaokolewa. Waambie kwamba katika vitabu hivi kuna ushauri ambao hawawezi kupata kutoka kwa tabibu wao wakati wa ziara fupi wanazofanya (Kinga ni bora kuliko kuponya).— The Southern Watchman, Novemba 20, 1902 **( Pacific Union Recorder, Novemba 20, 1902 ). ChS 152.4**

Vijana watakapoanza kazi ya kuhubiri kwa uinjilisti wa vitabu, wakiwa wamejawa na hamu kubwa ya kuwaokoa wanadamu wenzao, wataona roho zikiongoka. Kutokana na kazi yao, mavuno yatavunwa kwa Bwana. Kisha waende kama wamishenari ili kueneza Ukweli wa sasa, wakiomba kila mara kwa ajili ya kuongezeka kwa nuru na maarifa, ili waweze kujua jinsi ya kusema maneno kwa majira yake, kwa wale waliochoka. Wanapaswa kuboresha kila fursa ya kufanya tendo la wema, wakikumbuka kwamba kwa kutenda hivyo, wao wanafanya shuguli kwa ajili ya Bwana.... Katika kazi yao wanapaswa daima kuchukua baadhi ya vitabu vya afya pamoja nao; kwa maana matengenezo ya afya ni mkono wa kuume wa ujumbe.— **The Southern Watchman, Januari 15, 1903 . ChS 153.1**

## Sambaza bila Ubaguzi

Kuna sehemu nyingi ambamo sauti ya mhudumu haiwezi kusikika, mahali panapoweza kufikiwa tu kwa machapisho,—vitabu, magazeti, na vipeperushi ambavyo vimejaa Kweli za Biblia

ambazo watu wanahitaji. Maandishi yetu yanapaswa kusambazwa kila mahali. Kweli inapaswa kupandwa kando ya maji yote; kwa maana hatujui ni ipi itafanikiwa, hii au ile. Katika maamuzi yetu yenye makosa tunaweza kufikiria kuwa si jambo la hekima kuwapa machapisho wale ambao hawangekubali Kweli kwa urahisi zaidi. Hatujui jinsi matokeo mazuri ya kutoa kikaratasi kilicho na Ukweli wa sasa yatakavyokuwa.— **The Southern Watchman, Januari 5, 1904 . ChS 153.2**

### Thamini Kila Kipande cha Chapisho

Katika muujiza wa kulisha umati wa watu kwa mikate na samaki wachache, chakula kiliendelea kuongezeka, kwa kadiri kilivyopitishwa kutoka kwa Kristo hadi kwa wale waliokipokea. Ndivyo itakavyokuwa katika usambazaji wa maandishi yetu. Kweli ya Mungu, inapopitishwa kwa watu, itakuwa inazidi kuongezeka sana. Na kama ilivyokuwa kwa wanafunzi, chini ya uongozi wa Kristo, walipokusanya vipande hivyo vya mabaki ya mikate, ili chochote kisipotee, ndivyo tunapaswa kuthamini kila kipande cha maandishi kilicho na Ukweli kwa wakati huu. Hakuna awezaye kukadiria ushawishi ambao hata ukurasa uliochanika, ulio na Kweli za ujumbe wa malaika wa tatu unavyoweza kuwa nao, juu ya moyo wa mtu fulani anayetafuta Ukweli.— **The Southern Watchman, Januari 5, 1904 . ChS 153.3**

### Kuanzisha Amana-Stoo ya kuweka Vitabu

Katika kila sehemu muhimu kunapaswa kuwa na hazina ya machapisho (ABC nk). Na mtu ambaye anathamini Kweli anapaswa kuonesha nia ya kuweka vitabu hivi mikononi mwa wote watakaosoma. **—Shuhuda kwa Kanisa 1:473. ChS 154.1**

### Malaika Huandaa Njia

Niliona kwamba kazi ya Ukweli wa sasa inapaswa kuhusisha maslahi ya wote. Uchapishaji wa Ukweli ni mpango uliowekwa na Mungu kama njia ya kuonya, kufariji, kukaripia, kuhimiza, kuhamasisha au kusadikisha wote ambao wajumbe wa kimya wasio na sauti wanaweza kuwafikia. Malaika wa Mungu wana sehemu ya kufanya katika kuiandaa mioyo kwa ajili ya utakaso, kwa Ukweli uliochapishwa, ili waweze kujitayarisha kwa matukio mazito yaliyo mbele yao. **—Shuhuda kwa Kanisa 1:590. ChS 154.2**

## SURA YA 14 UHURU WA KIDINI (Religious Liberty)

### Ombi Linalofaa

Daudi aliomba, "Wakati umewadia wa Wewe kufanya kazi, Bwana, kwa maana wameibatilisha sheria Yako." Maombi haya hayajapungua umuhimu na nguvu yake, hata kwa wakati huu.

Ulimwengu umepotoka kutoka kwa Mungu, na hali yake ya uasi wa sheria inapaswa kuogopesha na kushtua moyo, na kuwaongoza wote walio waaminifu kwa Mfalme mkuu kufanya kazi kwa ajili ya matengenezo. Mamlaka ya upapa imefikiria kubadili sheria ya Mungu kwa kuweka Sabato ya uwongo badala ya ile ya Yehova; na katika ulimwengu wote wa kidini sabato ya uwongo inaheshimiwa, huku ile Sabato ya Kweli ikikanyagwa-kanyagwe chini ya miguu michafu, isiyo mitakatifu**….** **ChS 155:1**

—

Ni juu ya kipengele cha sheria ya Mungu ndipo ulipo msukosuko mkubwa wa mwisho kuhusu pambano kati ya Kristo na malaika Zake na Shetani na malaika zake litakuja, na litakuwa na maamuzi yenye hitimisho kwa ulimwengu wote.... Wanadamu walio katika nyadhifa za kuwajibika kama viongozi wa serikali nk hawatapuuzia tu na kuidharau Sabato wenyewe, lakini dharau itatoka kwenye uongozi wa kiroho, kwenye mimbari za makanisa, viongozi wa kiroho, watawaambia watu kuitunza siku ya kwanza ya juma, wakiwasihi watu kuenenda na mapokeo na desturi kwa niaba ya taasisi hii iliyobuniwa na mwanadamu (sabato ya uongo). Watawaelekeza watu kwenye misiba juu ya nchi kavu na baharini—kwa dhoruba za upepo, mafuriko, matetemeko ya ardhi, uharibifu wa moto—na kusema majanga hayo yanaonyesha kutopendezwa kwa Mungu, kwa sababu siku ya Jumapili haitunzwi kwa utakatifu. Misiba hii itaongezeka zaidi na zaidi, janga moja litafuata kwenye visigino vya majanga mengine; na wale wanaoibatilisha sheria ya Mungu wataelekeza kwa wale wachache wanaoshika Sabato ya amri ya nne kama ndio wale wanaoleta ghadhabu juu ya ulimwengu. Uongo huo ni mbinu ya Shetani ili kuwanasa watu wasiokuwa waangalifu, wale wasiochukua tahadhari kujua kwamba kuna hatari mbele.— **The Southern Watchman, Juni 28, 1904 . ChS 155.2**

**Matukio Yanayokuja**

—

Watu wetu wamechukuliwa kuwa wasio na umuhimu, kiasi kwamba hawawezi kutambuliwa, lakini mabadiliko yatakuja. Ulimwengu wa Kikristo sasa unafanya harakati ambayo lazima itawaleta watu wanaozishika amri kujulikana zaidi. Daima kuna tabia ya mwanadamu kuweka nadharia na mafundisho ya uongo, yenye asili kutoka kwa mwanadamu mwenyewe, kama mbadala wa kuchukua nafasi ya Ukweli wa Mungu. Harakati zinafanywa na kuwekwa kwenye msingi/miguuni ili kuziweka utumwani dhamiri za wale ambao wangekuwa waaminifu kwa Mungu. Mamlaka za kutunga sheria zitakuwa dhidi ya watu wa Mungu. Kila nafsi itajaribiwa. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:546.ChS 155.3**

Wanadamu watainuka na kutekeleza kwa ukali sheria ambazo ziko kinyume cha sheria ya Mungu (zitakuwa kavukavu). Ijapokuwa wana bidii katika kutekeleza amri zao wenyewe, watageuka kutoka katika Ukweli wazi wa "Hivi ndivyo asemavyo Bwana." Wakiinua siku ya mapumziko ya uwongo/feki, watatafuta kuwalazimisha watu kuidharau sheria ya Yehova, nakala ya tabia Yake. Ingawa hawana hatia ya kufanya makosa yoyote, Watumishi wa Mungu wataachiliwa ili kuteseka, kudhalilishwa na kunyanyaswa na wale ambao, wakiongozwa na roho wa Shetani, wamejawa na husuda na ubaguzi wa kidini.- **—Shuhuda kwa Kanisa 9:229.ChS 156.1**

Mamlaka za kidini, wakijidai kuungana na mbingu kwa maneno ya mdomo tu, na huku kudai kuwa na sifa za mwana-kondoo, wataonyesha kwa matendo yao kwamba wana moyo wa joka na kwamba wanachochewa na kudhibitiwa na Shetani. Wakati unakuja ambapo watu wa Mungu watahisi mkono wa mateso kwa sababu wanashika siku takatifu ya saba. Shetani amesababisha mabadiliko ya Sabato kwa matumaini ya kutekekeleza makusudi yake dhidi ya mipango ya Mungu. Anatafuta kufanya amri za Mungu kuwa na nguvu kidogo duniani kuliko sheria za binadamu. Mwana wa kuasi (mtu wa dhambi), ambaye alifikiria kubadili nyakati na sheria, na ambaye amewahi siku zote kuwatesa watu

—

wa Mungu, atasababisha sheria zitungwe zinazolazimisha ushikaji wa siku ya kwanza ya juma. Lakini watu wa Mungu wanapaswa kusimama imara kwa ajili yake. Na Bwana atafanya kazi kwa niaba yao, akionesha wazi kwamba Yeye ni Mungu wa miungu. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:229, 230.ChS 156.2**

Kila aibu, kudhalilishwa, lawama, na ukatili ambao Shetani angeweza kuchochea mioyo ya wanadamu kubuni, umetembelewa juu ya wafuasi wa Yesu. Na itatimizwa tena kwa namna ya alama; kwa maana moyo wa kimwili bado una uadui na sheria ya Mungu, wala hautazitii amri Zake. Ulimwengu haupatani tena na kanuni za Kristo leo kama ilivyokuwa katika siku za mitume. Chuki ileile iliyosababisha kilio. "Msulubishe! msulubishe!" chuki ile ile iliyosababisha mateso ya wanafunzi, ingali inafanya kazi kwa watoto wa kuasi. Roho ile ile ambayo katika Enzi za Giza iliwatupa wanaume na wanawake gerezani, uhamishoni, na kifoni, ambapo walipata mateso makali ya Baraza la Kuhukumu Wazushi, ambalo lilipanga na kutekeleza mauaji ya Mtakatifu Bartholomayo, na kuwasha moto huko Smithfield, bado inafanya kazi na nishati ya kansa mbaya katika mioyo isiyozaliwa upya. Historia ya Ukweli imewahi kuwa kumbukumbu ya mapambano kati ya mema na mabaya. Utangazaji wa injili daima unaendelezwa mbele katika ulimwengu huu katika uso wa upinzani, hatari, hasara, na mateso.— **The Acts of the Apostles, 84, 85 . ChS 156.3**

—

Kanisa la masalio litaletwa katika majaribu na dhiki kuu. Wale wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu watahisi hasira ya joka na majeshi yake. Shetani anahesabu ulimwengu kuwa raia na mali yake, amepata udhibiti wa makanisa yaliyoasi; lakini hapa kuna kundi dogo linaloupinga ukuu wake. Kama angeweza kuwafuta watu kutoka duniani, ushindi wake ungekuwa kamili. Kama alivyoyashawishi mataifa ya kipagani ili kuwaangamiza Israeli, ndivyo, katika siku za usoni atazichochea nguvu mbaya za dunia kuwaangamiza watu wa Mungu. Wote watatakiwa kutoa utii kwa amri za wanadamu kwa kukiuka sheria ya Mungu. Wale ambao watakuwa waaminifu kwa Mungu na wajibu watasalitiwa, watatishwa, watalaaniwa, na kupigwa marufuku. Watasalitiwa "na wazazi na ndugu, na jamaa, na marafiki." Luka 21:16. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:231.ChS 157.1**

Wakati hauko mbali ambapo mtihani utakuja kwa kila nafsi. Utunzaji wa sabato ya uwongo utasisitizwa juu yetu. Shindano litakuwa kati ya amri za Mungu na amri na mapokeo ya wanadamu. Wale ambao wamejisalimisha hatua kwa hatua kwa matakwa ya kidunia, na kufuata desturi za kidunia, basi watajisalimisha kwa mamlaka hiyo, badala ya kujinyenyekeza wenyewe kwa dhihaka, matusi, kutishiwa kufungwa, na kifo. Wakati huo dhahabu itatenganishwa na takataka...…. Nyota nyingi ambazo tumependezwa nazo kwa mng'ao wake zitatoweka gizani. Wale ambao wamejivika mapambo ya Patakatifu, lakini hawajavaa haki wa Kristo, wakati huo wataonekana katika aibu ya uchi wao wenyewe.—
**Prophets and Kings, 188 . ChS 157.2**

Kuna matarajio mbele yetu ya mgogoro endelevu, katika hatari ya kufungwa gerezani, kupoteza mali, na hata maisha yenyewe, katika kutetea sheria ya Mungu, ambayo imebatilishwa na sheria za wanadamu. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:712.**

Wakati unaenda kasi ambapo wale wanaosimama katika kutetea Ukweli watajua kwa uzoefu nini maana ya kushiriki katika mateso ya Kristo. Mkandamizaji mkuu anaona kwamba ana

muda mfupi tu wa kufanya kazi, kwamba hivi karibuni atapoteza uwezo wake juu ya mwanadamu na nguvu zake kuchukuliwa kutoka kwake, na anafanya kazi kwa uovu na udanganyifu wote wa udhalimu ndani yao wanaopotea. Ushirikina na makosa yanaikanyaga Kweli, haki na usawa. Kila nguvu ambayo inapinga Ukweli inaimarika.— The Southern Watchman, Oktoba 31, 1905 **( The Review and Herald, May 29, 1900 ). ChS 157.4**

Kazi ambayo kanisa limeshindwa kuifanya wakati wa amani na ustawi, litalazimika kuifanya katika hali ya kutisha na yenye kukatisha tamaa, ya dharura, na isiyo ya kirafiki. Maonyo kwamba kufanana na dunia kumenyamazisha au kuzuia lazima yatokee chini ya upinzani mkali kutoka kwa maadui wa imani. Na wakati huo tabaka la mambo ya juu juu, na la kihafidhina (conservative), ambalo ushawishi wake umedidimiza maendeleo ya kazi kwa uhakika, wataikana imani na kuchagua msimamo wao pamoja na maadui zao hadharani, ambao huruma zao zimekuwa zikiwatunza kwa muda mrefu. Waasi hawa wataonyesha uadui mkali kabisa, wakifanya yote katika uwezo wao kuwakandamiza na kuwachafua ndugu zao wa zamani na kuleta hasira dhidi yao. Siku hiyo iko mbele yetu. Washiriki wa kanisa mmoja mmoja watajaribiwa na kuthibitishwa. Watawekwa katika mazingira ambayo

watalazimika kutoa ushuhuda kwaajili ya Ukweli. Wengi wataitwa kuzungumza mbele ya mabaraza na katika mahakama za haki, pengine kila mmoja peke yake au wakiwa wengi zaidi. Uzoefu ambao ungewasaidia katika dharura hii wamepuuza kuukamata, na roho zao zinaelemewa na majuto kwa fursa zilizopotea na nafasi walizozipuuza. **— Shuhuda kwa Kanisa 5:463.ChS 158.1**

Ulimwengu huu wa Kiprotestanti leo, unaona katika kundi dogo la watunza kama Mordekai kwenye malango. Tabia na mwenendo wake vilidhirisha jinsi anavyoiheshimu sheria ya Mungu, jambo hili hukemea vikali wale ambao wameikanyaga Sabato ya Bwana na kushindwa kumheshimu; mgeni asiyealikwa ni lazima aondoshwe katika njia. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:450. ChS 158.2**

Shetani ataamsha ghadhabu yake dhidi ya wanyenyekevu wachache ambao kwa dhamiri yao wamekataa kukubali mila na mapokeo yenye upotoshaji maarufu. Watu wenye hadhi na sifa mbalimbali watajiunga na waasi wa sheria ya Mungu, na watu waovu ili kupeana mashauri ya namna ya kupambana dhidi ya watu wa Mungu. Utajiri, na wale watu wanaofikirika kuwa wana akili mahiri sana (genius), vitaungana/zitaungana kuwafunika kwa dharau. Watawala wanaonyanyasa, watumishi mbalimbali shambani mwa Bwana, pamoja na washiriki wa kanisa watafanya njama dhidi yao wazishikao Amri za Mungu. Kwa sauti na kalamu, kwa kujisifu, vitisho, na kejeli, watatafuta namna ya kuipindua imani yao. Kwa uwakilishi wa uongo na kusihi Kwa hasira watachochea tamaa mbaya za watu. Kwa sababu hawana "imeandikwa" kuleta dhidi ya watetezi wa Sabato ya Biblia, wataamua kutekeleza sheria za ukandamizaji ili kuchochea ukosefu wa Neno Takatifu. Ili kupata umaarufu, wadau, ulinzi, wabunge watakubali matakwa ya sheria ya Jumapili. Wale wanaomcha Mungu hawawezi kukubali taasisi ambayo inakiuka amri za Mungu hivyo watajiondoa. Kwenye uwanja huu wa vita kutakuwapo na mzozo mkubwa wa mwisho ambao ni pambano kati ya Ukweli na uongo. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:450, 451.**

—

**ChS 158.3**

**Mateso ni Muhimu**

Walipotawanywa na mateso, walienda wakiwa wamejawa na bidii ya umishenari. Walitambua wajibu wa utume wao. Walijua kwamba walishikilia mikononi mwao mkate wa uzima kwa ajili ya ulimwengu wenye njaa; nao walisukumwa na upendo wa Kristo kuumega mkate huu kwa wote waliokuwa na uhitaji.— **The Acts of the Apostles, p. 106 . ChS 159.1**

Mungu anamaanisha kuwa Ukweli unaojaribu utaletwa mbele na utafanywa kuwa mada ya uchunguzi na majadiliano, hata ikiwa ni kwa dharau inayowekwa juu yake. Mawazo ya watu lazima yafadhaishwe/yakorogwe. Kila pambano, laumu, na kashfa, litakuwa njia ambazo Mungu atatumia kuchochea uchunguzi, maswali, hoja na kuamsha akili ambazo vinginevyo zingelala.
**—Shuhuda kwa Kanisa 5:453. ChS 159.2**

**Kwanini Mateso Yanakawia/Kusinzia**

Mtume Paulo anatangaza kwamba "wote wapendao kuishi utauwa katika Kristo Yesu watateswa." Kwa nini basi, kwamba mateso yanaonekana kwa kiwango kikubwa

kusinzia? Sababu pekee ni kwamba, kanisa limeendana na viwango vya ulimwengu hivyo kufanana zaidi na ulimwengu, ndiyo maana haliamshi upinzani. Dini iliyopo katika siku zetu sio ya tabia safi na takatifu iliyotia alama imani ya Kikristo katika siku za Kristo na mitume Wake. Ni kwa sababu tu ya roho ya maafikiano na dhambi, kwa sababu Kweli zile kuu za Neno la Mungu hazizingatiwi sana, kwa sababu kuna utauwa mdogo sana katika kanisa, hivyo Ukristo unaonekana kupendwa sana na ulimwengu. Hebu kuwe na uamsho wa imani na nguvu wa kanisa la kwanza, na roho ya mateso itafufuliwa, na moto wa mateso utawashwa tena.— **The Great Controversy, 48 . ChS 159.3**

### Sehemu Tatu za Muungano wa Mateso

Kupitia makosa mawili makubwa, kutokufa kwa roho na utakatifu wa Jumapili, Shetani atawaleta watu chini ya madanganyo yake. Wakati kutokufa kwa roho kunaweka msingi wa Imani ya Umizimu, utakatifu wa Jumapili, unajenga uhusiano wa huruma na Rumi. Waprotestanti wa Marekani watakuwa mstari wa mbele katika kunyoosha mikono yao katika korongo ili kuushika mkono wa umizimu; watafikia kuzimu ili kushikana mikono na mamlaka ya Kirumi; na chini ya ushawishi wa muungano huo wenye sehemu tatu, nchi hii itafuata hatua za Rumi katika kukanyaga haki za dhamiri.— **The Great Controversy, 588 . ChS 160.1**

### Tukio la Mwisho la Kuigiza (last drama)

Kuingizwa kwa sheria za wanadamu kama mbadala wa sheria ya Mungu, kuinuliwa, kwa mamlaka ya kibinadamu, ya Jumapili badala ya Sabato ya Biblia, ni tukio la mwisho katika mchezo wa kuigiza (drama). Wakati uingizwaji huu wa sheria za mwanadamu kama mbadala wa sheria ya Mungu, utakapokuwa wa ulimwengu wote, Mungu atajifunua Mwenyewe. Atatokea kwa utukufu kuitikisa sana dunia. Atatoka katika kiti Chake kuwaadhibu wakazi wa ulimwengu kwa uovu wao, na nchi itadhihirisha damu yake na haitawafunika tena waliouawa. — **Shuhuda kwa Kanisa 7:141.ChS 160.2**

—

Wakati taifa letu litakapotupilia mbali kanuni za serikali yake (kukanusha), hata kutunga sheria ya Jumapili, Uprotestanti katika tendo hili utaungana na upapa; hakitakuwa kitu kingine zaidi ya kutoa uhai kwa ubabe na dhuluma ambayo kwa muda mrefu imekuwa ikitazama kwa hamu fursa yake ya kuibuka tena kwenye udhalimu hai. —Shuhuda kwa Kanisa 5:712.**ChS 160.3**

Kwa amri inayoshinikiza/inayolazimisha kwa nguvu taasisi ya upapa kukiuka sheria ya Mungu, taifa letu litajiondoa kabisa kutoka kwenye haki/uadilifu. Wakati Uprotestanti utakaponyosha mkono wake kuvuka korongo/ghuba ili kushika mkono wa nguvu ya Kirumi, utakapoamua kufikia shimo la kuzimu ili kuunganisha mikono yake na umizimu, wakati, chini ya ushawishi wa muungano huu wa pande tatu, nchi yetu itakataa/itakanusha kila kanuni za Katiba yake kuwa kama serikali ya Kiprotestanti na ya jamhuri, na itatoa fursa ya kusambaza uongo wa upapa na udanganyifu wake, basi tufahamu kwamba wakati umefika wa Shetani kufanya kazi yake vyema na kwa jinsi ya ajabu na ule mwisho utakuwa umekaribia.Shuhuda kwa Kanisa 5:712.**ChS 160.4**

*Huu si wakati wa watu wa Mungu kuweka upendo wao katika hazina zao ulimwenguni*. Si muda mrefu, kama ilivyokuwa kwa wanafunzi wa awali, tutalazimika kutafuta kimbilio

katika sehemu zenye ukiwa, faragha na zilizotengwa. Kama ilivyokuwa ishara wakati wa kuzingirwa kwa Yerusalemu na majeshi ya Kirumi kwa Wakristo wa Uyahudi kukimbia, ndivyo basi kwa upande wa kanisa letu Amri ya kutekeleza sabato ya kipapa itakavyokuwa ilani kwetu. Huu utakuwa ni wakati wa kuondoka katika miji mikubwa, matayarisho ya kuishi katika sehemu ndogo za nyumba zilizotengwa katikati ya milima. —**Shuhuda kwa Kanisa 5:464, 465. ChS 161.1**

## Wengi Vipofu wa Macho

Kuna wengi, hata miongoni mwa wale wanaohusika katika harakati hii ya utekelezaji wa ushinikizaji wa Jumapili, ambao wamepofushwa macho kuona matokeo ambayo yatafuatia hatua hii. Hawaoni kwamba wanafanya mgomo ulio moja kwa moja dhidi uhuru wa kidini. Kuna wengi ambao hawajawahi kuelewa madai ya Sabato ya Biblia na msingi wa uongo, ambao utaratibu wa Jumapili umewekwa juu yake. —**Shuhuda kwa Kanisa 5:711.ChS 161.2**

## Majukumu na Wajibu wa Watu wa Mungu

Bendera ya Ukweli na uhuru wa kidini iliyoinuliwa juu na waanzilishi wa kanisa la injili na mashahidi wa Mungu wakati wa karne ambazo zimepita tangu wakati huo, katika pambano hili la mwisho, imekabidhiwa mikononi mwetu. Wajibu wa zawadi hii kuu upo kwa wale ambao Mungu amewabariki kwa ujuzi wa Neno Lake. Tunapaswa kupokea Neno hili kama mamlaka kuu duniani na mbinguni. Tunapaswa kutambua serikali ya mwanadamu kama agizo la uteuzi wa Mwenyezi Mungu, na kufundisha utiifu kwake kama jukumu takatifu, ndani ya nyanja yake halali. Lakini pale madai yake yanapopingana na madai ya Mungu, ni lazima tumtii Mungu kuliko wanadamu (Matendo 5:29). Neno la Mungu lazima litambuliwe kuwa juu ya sheria zote za wanadamu. Agizo "Bwana asema hivi" halipaswi kuwekwa kando kwa ajili ya "Kanisa linasema hivi" au "Hivi ndivyo serikali inavyosema." Taji la Kristo inapaswa kuinuliwa juu ya taji za wenye mamlaka duniani.— **The Acts of the Apostles, 68, 69 . ChS 161.3**

—

Sisi kama watu hatujamaliza kazi ambayo Mungu ametukabidhi. Hatuko tayari kwa suala ambalo litaletwa na ushinikizaji na utekelezaji wa sheria ya Jumapili. Ni jukumu letu, tunapoona dalili za hatari inayokaribia, kuamka kwa kuchukua hatua. Hebu mtu awaye yote asiketi akiwa ametulia tuli, akingojea mabaya; akijifariji kwa kuamini kwamba kazi hii lazima iendelee kwa sababu unabii umeitabiri, na kwamba Bwana atawahifadhi watu Wake. Sisi hatufanyi mapenzi ya Mungu ikiwa tunakaa kimya, bila kufanya lolote ili kuhifadhi uhuru wa dhamiri. Maombi ya dhati, yenye matokeo/ufanisi yanapaswa kupaa mbinguni ili msiba huu uweze kuahirishwa hadi tuweze kukamilisha kazi ambayo imepuuzwa kwa muda mrefu. Hebu kuwe na sala ya dhati na bidii zaidi, na kisha tufanye kazi kupatana na sala zetu. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:713, 714.ChS 162.1**

Ni jukumu letu kufanya yote yaliyo ndani ya uwezo wetu kuepusha hatari inayoashiria na kutishia kuja. Tunapaswa kujitahidi kuondoa ubaguzi uliopo miongoni mwetu na kujiweka kwenye nuru iliyo sawa, mbele za watu (ili kuelewa Ukweli). Tunapaswa kuleta mbele yao maswali halisi yanayohusika katika hili suala, na hivyo kujiweka katika hali sahihi ya kupinga kunakofaa na kwa ufanisi zaidi dhidi ya hatua za kuzuia uhuru wa dhamiri. —

—

**Shuhuda kwa Kanisa 5:452. ChS 162.2**

Wakati Mungu ametupa nuru inayoonesha hatari zilizo mbele yetu, tunawezaje kusimama bila lawama machoni pake ikiwa tutapuuza kuweka kila juhudi katika uwezo wetu kuileta mbele za watu? Je, tunaweza kuridhika kuwaacha watu wakutane na suala hili muhimu bila kuonywa? **—Shuhuda kwa Kanisa 5:712.ChS 162.3**

Wakati Wanamatengenezo wa Kitaifa walipoanza kuhimiza hatua za kuzuia uhuru wa kidini, viongozi wetu walio mstari wa mbele walipaswa kuwa hai kwa hali hiyo na walipaswa kufanya kazi kwa bidii ili kupinga jitihada hizi. Siyo kwa utaratibu wa Mungu kwamba nuru imezuiliwa kutoka kwa watu wetu - Ukweli huu wa sasa ambao watu waliuhitaji kwa wakati huu. Siyo wachungaji wetu wote wanaotoa ujumbe wa malaika watatu wanaoelewa kwa hakika kile kinachojumuisha ujumbe huo. Vuguvugu la Matengenezo ya Kitaifa limechukuliwa na wengine kuwa la umuhimu mdogo sana kiasi kwamba hawajaweka umakini na kulizingatia sana na hata wamehisi kwamba kwa kufanya hivyo watakuwa wakitoa muda kwa masuala tofauti na ujumbe wa malaika watatu. Bwana awasamehe ndugu zetu kwa kuutafsiri hivyo ujumbe wenyewe wa wakati huu. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:715.ChS 162.3**

Tumekuwa tukisubiri kwa miaka mingi kwa sheria ya Jumapili kutungwa katika nchi yetu; na, kwa kuwa sasa harakati iko juu yetu, tunauliza: Je, watu wetu watafanya wajibu wao katika suala hili? Je, hatuwezi kusaidia katika kuinua kiwango na kuwaita mbele wale wanaojali haki na fursa/upendeleo wao wa kidini? Wakati unakaribia upesi ambapo wale wanaochagua kumtii Mungu badala ya wanadamu watafanywa kuhisi mkono wa uonevu. Je, basi tutamdharau Mungu kwa kunyamaza huku amri Zake takatifu zikikanyagwa chini ya miguu Yake? Wakati ulimwengu wa Kiprotestanti kwa mtazamo wake ukiikubali Rumi, hebu tuamke kuelewa hali hiyo na kutazama shindano lililo mbele yetu katika mwelekeo wake halisi. Hebu walinzi sasa wapaze sauti zao na

—

kutoa ujumbe ambao ni Ukweli uliopo kwa wakati huu. Hebu tuwaoneshe watu mahali tulipo katika historia ya unabii na tutafute kuamsha roho ya Uprotestanti wa Kweli, tukiamsha ulimwengu upate hisia ya thamani ya fursa za uhuru wa kidini ambazo umezifurahia kwa muda mrefu sana. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:716.ChS 163.1**

Watu wa nchi yetu wahitaji kuamshwa ili kupinga ushawishi wa adui huyo wa hatari zaidi kuelekea uhuru wa kiraia na wa kidini.— **The Spirit of Prophecy 4:382 . ChS 163.2**

Je, tuketi tukiwa tumekunja mikono tu, na tusifanye lolote katika mgogoro huu? ... Mungu atusaidie kuamka kutoka katika usingizi ambao umening'inia juu yetu kwa miaka mingi.— **The Review and Herald, Desemba 18, 1888 . ChS 163.3**

### Mwenendo wa Busara Kufuata

Kuziasi sheria za Jumapili kutaimarisha tu mateso ya wakereketwa wa mambo ya kidini wanaotafuta kuyatekeleza. Msiwape nafasi ya kuwaita ninyi kuwa ni wavunja sheria. Ikiwa wataachwa kushika hatamu kwa watu wasiomwogopa Mungu wala mwanadamu, uimarikaji wao punde utapoteza nguvu, na wataona kuwa hakuna maana wala haifai kwao kuwa

—

wakali kuhusiana na utunzaji wa Jumapili. Endeleeni katika kazi yenu ya umisionari, mkiwa na Biblia zenu mikononi mwenu, na adui ataona kwamba amelifanya kusudi lake mwenyewe kuwa baya zaidi. Mtu yeyote hapokei alama ya mnyama kwa sababu anaonesha kwamba anatambua hekima ya kulinda amani kwa kujiepusha kufanya kazi zile ambazo zingelimletea mzozo, na kufanya kazi wakati huohuo ya umuhimu wa juu zaidi. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:232.**ChS 163.4

Tunapoitumia Jumapili kwa kazi ya umishionari, mjeledi utaondolewa mikononi mwa watu wakereketwa ambao wangefurahi kuwadhalilisha Waadventista wa Sabato. Wanapoona tunajitoa wenyewe siku ya Jumapili katika kuwatembelea watu na kuyafungua Maandiko kwao, watajua kwamba haina maana kwao kujaribu kuzuia kazi yetu kwa kutunga sheria za Jumapili. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:232, 233.** ChS 164.1

Jumapili inaweza kutumika kwa kuendeleza kazi mbalimbali ambazo zitatimiza mengi kwa ajili ya Bwana. Katika siku hii, mikutano ya ndani na nje inaweza kufanyika na hata kwenye majumba madogo. Kazi ya nyumba kwa nyumba inaweza kufanywa. Wale wanaoandika wanaweza kuitumia siku hii kuandika makala zao. Inapowezekana, hebu mikutano ya dini ifanyike katika siku ya Jumapili. Hakikisheni kuwa mikutano hii inakuwa ya kuvutia sana. Imbeni nyimbo nzuri za uamsho kwa unyofu, na hubirini kwa nguvu na uhakika juu ya upendo wa Mwokozi. Hubirini juu ya kiasi na juu uzoefu wa dini ya Kweli. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:233.**ChS 164.2

Hebu walimu katika shule zetu waitoe Jumapili kwa ajili ya juhudi za kimishenari. Niliagizwa kuwa wakifanya hivyo wataweza kuyashinda makusudi ya adui. Hebu walimu wawachukue wanafunzi pamoja nao kufanya mikutano kwa wale ambao hawaujui Ukweli. Hivyo watafanikisha mengi zaidi ya njia nyingine yoyote. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:233.**ChS 164.3

—

**Ushindi wa Kweli**

Kushuku na kutilia mashaka kunaweza kuchukulia madai ya sheria ya Mungu kwa mzaha, dhihaka, na kukanusha (skepticism). Roho ya ulimwengu inaweza kuwachafua na kuwaambukiza wengi na kuwatawala wachache; sababu ya Mungu inaweza kushikilia msingi wake tu kwa juhudi kubwa na dhabihu ya daima; lakini mwishowe Ukweli utashinda kwa utukufu.— Prophets and Kings, 186 . ChS 164.4

Katika kufunga kazi ya Mungu duniani, kiwango cha sheria Yake kitainuliwa tena. Dini ya uwongo inaweza kutawala na kushamiri, uovu ukaongezeka, upendo wa wengi unaweza kupoa, msalaba wa Kalvari upotee machoni pake, na giza, kama maumivu ya kifo, kuenea duniani kote; nguvu nzima ya mkondo maarufu inaweza kugeuzwa dhidi ya Ukweli; njama baada ya njama zinaweza kufanywa kuwapindua watu wa Mungu; lakini katika saa ya hatari kubwa zaidi, Mungu wa Eliya atainua vyombo vya kibinadamu vya kutoa ujumbe ambao hautanyamazishwa. Katika miji ya nchi, yenye watu wengi, na mahali ambapo watu wamefikia hatua kubwa zaidi katika kusema dhidi ya Aliye Juu zaidi, sauti ya kemeo kali itasikika. Kwa ujasiri watu walioteuliwa na Mungu watashutumu muungano wa kanisa na ulimwengu. Kwa bidii watawaita wanaume na

—

wanawake wageuke kutoka kwenye ushikaji/utunzaji wa taasisi iliyobuniwa na wanadamu na kuelekea kwenye ushikaji wa Sabato ya kweli.— Prophets and Kings, 186, 187 . ChS 165.1

## Nuru Katika Giza

Miongoni mwa wakaaji wa dunia, waliotawanyika katika kila nchi, kuna wale ambao hawajampigia goti Baali. Kama nyota za mbinguni, zinavyoonekana vyema usiku tu, waaminifu hao watang'aa wakati giza litaifunika dunia na giza kuu la watu. Katika Afrika ya kipagani, katika nchi za Kikatoliki za Ulaya na Amerika ya Kusini, katika China, katika India, katika visiwa vya bahari, na katika pembe zote za giza za dunia, Mungu ana akiba ya anga ya wateule ambayo bado inaangaza katikati ya giza, ikifunua waziwazi kwa ulimwengu ulioasi nguvu igeuzayo ya utii kwa sheria Yake Mungu. Hata sasa watu hawa waaminifu, wanaonekana katika kila taifa, kati ya kila lugha na jamaa; na katika saa ya uasi wa imani mkubwa zaidi, wakati jitihada kuu ya Shetani inapofanywa kusababisha “wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru na watumwa,” kupokea, chini ya adhabu ya kifo, ishara ya utii kwa siku ya mapumziko isiyo ya Kweli (sabato ya uongo). Waaminifu hao, “wasio na lawama na wasio na hatia, wana wa Mungu, bila lawama,” ‘watang’aa kama mianga katika ulimwengu. Kadiri usiku unavyozidi kuwa mweusi ndivyo watakavyoangaza kwa uzuri zaidi. —Manabii na Wafalme, 188, 189.**ChS 165.2**

Dhoruba ya mateso na unyanyasaji itakapotujia kwa ukali, kondoo wa Kweli watasikia sauti ya Mchungaji wa Kweli. Jitihada za kujikana nafsi, zitawekwa ili kuokoa watu waliopotea, na wengi ambao wamepotea kutoka kwenye zizi watarudi kumfuata yule Mchungaji Mkuu.. —Australian The Signs of the Times, January 26, 1903, Supplement. **ChS 166.2**

## Ulinzi wa Bwana

Lakini ingawa mzozo haukomi, hakuna anayeachwa ahangaike peke yake. Malaika huwasaidia na kuwalinda wale wanaotembea kwa unyenyekevu mbele za Mungu. Mungu wetu hatamfanyia hiana au kumsaliti yule mwenye kumtegemea Yeye. Watoto Wake wanapomkaribia kwa ajili ya ulinzi dhidi ya uovu, kwa huruma na

—

upendo Yeye atanyanyua kiwango dhidi ya adui (Isaya 59:19). Msiwaguse, Anasema; kwa maana hao ni Wangu. Nimewachora kwenye vitanga vya mikono Yangu.— Prophets and Kings, 571 . ChS 166.2

Mbingu iko karibu sana na wale wanaoteseka kwa ajili ya haki. Kristo anabainisha maslahi yake na maslahi ya watu Wake waaminifu; Yeye Anateseka katika nafsi ya watakatifu Wake; na anayewagusa wateule Wake humgusa Yeye. Nguvu zilizo karibu za kukomboa kutokana na madhara ya kimwili au fadhaa na dhiki, ziko karibu pia kuokoa kutoka katika uovu mkubwa zaidi, na kufanya iwezekane kwa mtumishi wa Mungu kudumisha utimilifu wake chini ya hali zote.— Prophets and Kings, 545 . ChS 166.3

Wakati fulani Bwana anaweza kuonekana kuwa amesahau hatari za kanisa Lake, na kuumizwa kwake na adui zake. Lakini Mungu hajasahau. Hakuna kitu katika ulimwengu huu kinachopendwa sana na moyo wa Mungu kama kanisa lake. Si mapenzi Yake kwamba sera za kilimwengu ziharibu rekodi ya kanisa. Yeye Hawaachi watu Wake washindwe na

majaribu ya Shetani. Yeye Atawaadhibu wale wanaomwakilisha vibaya, lakini Atakuwa Mwenye rehema kwa wote wanaotubu kwa unyoofu.— Prophets and Kings, 590 . ChS 166. 4

## SURA YA 15 KUKUSANYA MAVUNO

### Tatizo linalofadhaisha

Kwa miaka mingi swali la kutatanisha limekuwa mbele yetu: Tunawezaje kupata fedha zinazotosheleza kusaidia utume ambao Bwana ametangulia mbele yetu ili kuufungua? Tunalisoma wazi agizo la injili; na la utume, pote katika maeneo ya nyumbani na ya nchi za kigeni, huwasilisha mahitaji yao. Viashiria, na mafunuo chanya ya mibaraka na majaliwa ya Mungu, huungana nasi katika kutuhimiza kufanya haraka kazi ambayo inatakiwa kufanywa. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:114. ChS 167.1**

### Mpango Wenye Mafanikio

Mojawapo ya mipango mipya ya kuwafikia wasioamini ni kampeni ya Kukusanya Sadaka ya Mavuno kwa ajili ya utume (ingathering offering). Kwenye maeneo mengi katika miaka michache iliyopita, hii imeonekana kuleta mafanikio na baraka kwa wengi, na kuongeza mtiririko wa fedha katika hazina ya misheni. Kwa vile wale ambao si wa imani yetu wamefahamishwa na maendeleo ya ujumbe wa malaika wa tatu katika nchi za kipagani, huruma zao zimeamshwa, na wengine wametafuta kujifunza zaidi juu ya Ukweli ambao una nguvu kubwa kama hiyo, ya kubadilisha mioyo na maisha. Wanaume na wanawake wa tabaka zote wamefikiwa, na Jina la Mungu limetukuzwa. —**Manuscript 2, "Consecrated Efforts to Reach Unbelievers," June 5, 1914. ChS 167.2**

Wengine wanaweza kutilia shaka usahihi wa kupokea zawadi kutoka kwa watu wasioamini. Hebu watu hao wajiulize: "Ni nani

—

mmiliki halisi wa ulimwengu wetu? Nyumba zake na mashamba yake ni ya nani, na hazina zake za dhahabu na fedha?” Mungu ana vingi vilivyosheheni katika ulimwengu wetu, na ameweka mali Yake mikononi mwa wote, watiifu na wasiotii. Yeye Yuko tayari kusogeza mioyo ya watu wa kidunia, hata waabudu sanamu, ili watoe vingi vyao, kwa ajili ya kutegemeza kazi Yake; na atafanya hivi punde tu watu Wake watakapojifunza kuwaendea watu hawa kwa hekima na kuelekeza usikivu wao kwa yale ambayo ni fursa kwao kufanya. Ikiwa mahitaji ya kazi ya Bwana yangewekwa wazi kwa nuru ifaayo mbele ya wale walio na uwezo na ushawishi, watu hawa wangeweza kufanya mengi kuendeleza kazi ya Ukweli wa sasa. Watu wa Mungu wamepoteza fursa nyingi ambazo wangejinufaisha nazo, kama hawangechagua kusimama huru na ulimwengu.— **The Southern Watchman, Machi 15, 1904 . ChS 167.3**

Bwana bado anasonga juu ya mioyo ya wafalme na watawala kwa niaba ya watu Wake. Wale wanaofanya kazi kwa ajili Yake wanapaswa kujinufaisha wenyewe kwa msaada ambao Yeye huwahamasisha watu kutoa kwa ajili ya kuendeleza kazi Yake. Mawakala

ambao kupitia kwao karama hizi huja, wanaweza kufungua njia ambazo kwazo nuru ya Ukweli itatolewa kwa nchi nyingi zenye giza. Watu hawa wanaweza wasiwe na huruma na kazi ya Mungu, wasiwe na imani katika Kristo, wasiwe na ujuzi na Neno Lake; lakini zawadi zao hazipaswi kukataliwa kwa sababu hiyo.— **The Southern Watchman, Machi 15, 1904 . ChS 168.1**

Bwana ameweka mali Yake mikononi mwa makafiri na pia Waumini; wote wanaweza kurudi Kwake walio Wake kwa ajili ya kufanya kazi ambayo ni lazima ifanywe kwa ajili ya ulimwengu ulioanguka. Maadamu tuko katika ulimwengu huu, maadamu Roho wa Mungu anashindana na watoto wa wanadamu, basi ni hakika kuwa sisi tutapokea upendeleo na kutoa upendeleo kwa watu. Tunapaswa kuupa ulimwengu nuru ya Ukweli, kama inavyofunuliwa katika Maandiko; nasi twapaswa kupokea kutoka kwa ulimwengu kile ambacho Mungu husukuma mioyo yao kutoa kwa ajili ya kazi Yake.— **The Southern Watchman, Machi 15, 1904 . ChS 168.2**

Ingawa sasa, ulimwengu unakaribia kuwa chini ya milki ya watu waovu, ulimwengu wote, pamoja na mali na hazina zake, ni wa Mungu. "Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana. (Hagai 2)" "Fedha ni Yangu, na dhahabu ni Yangu, asema Bwana wa majeshi." “Kila mnyama wa mwituni ni Wangu, na ng’ombe juu ya milima elfu. Nawajua ndege wote wa milimani; na wanyama wa porini ni Wangu. Kama ningekuwa na njaa, nisingekuambia; kwa maana ulimwengu ni Wangu, na vyote viujazavyo.” Laiti Wakristo wangetambua kikamilifu zaidi na zaidi kwamba ni pendeleo lao na wajibu wao, huku wakithamini kanuni sahihi, kutumia kwa faida kila fursa inayotumwa na mbingu kwa ajili ya kuendeleza ufalme wa Mungu katika ulimwengu huu.— **The Southern Watchman, Machi 15, 1904 . ChS 168.3**

### Mawaidha kwa Watenda kazi

Kwa wote wanaokaribia kuanza kazi ya pekee ya umishenari wakiwa na karatasi iliyotayarishwa kutumika katika kampeni ya

—

sadaka ya mavuno (ingathering offering), ningesema: Iweni na bidii na uadilifu katika jitihada zenu; Ishini chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Ongeza+ kila siku katika uzoefu wako wa Kikristo. Wale walio na uwezo wa pekee na wafanye kazi kwa ajili ya watu wasioamini katika nyadhifa za juu na katika nafasi za chini za maisha. Tafuta kwa bidii roho zinazopotea. Loo, fikiria hamu kubwa aliyo nayo Kristo kuwaleta kwenye zizi Lake tena wale waliopotea! Lindeni roho kama wale wanaopaswa kutoa hesabu. Katika kazi ya umishenari ya kanisa lako na ujirani wako, acha nuru yako iangaze katika miale iliyo wazi, nuru thabiti hivi kwamba hakuna mtu anayeweza kusimama katika hukumu, na kusema, "Kwa nini hukuniambia kuhusu Ukweli huu? Kwa nini hukuijali nafsi yangu?" Kisha na tuwe na uadilifu na bidii katika ugawanyaji wa fasihi ambazo umetayarishwa kwa uangalifu ili kutumiwa miongoni mwa wale wasio wa imani yetu. Hebu na tuitumie vyema kila fursa ili kukamata usikivu wa watu wasioamini. Hebu tuweke maandishi katika kila mkono utakaoyapokea. Na tujiweke wakfu kwa ajili ya tangazo la ujumbe huu, "Itengenezeni njia ya Bwana, nyosheni njia kuu ya Mungu wetu nyikani."— **Manuscript 2, "Jitihada Zilizowekwa wakfu za Kuwafikia Wasioamini," Juni 5, 1914 . ChS 169.1**

**Yaliyo Muhimu Kwa Ajili ya Mafanikio**

Katika kufuata mpango wowote ule unaoweza kuwekwa katika utendaji wa kuwapelekea wengine maarifa ya Ukweli wa sasa, na wa majaliwa ya ajabu yanayohusiana na kuendeleza kusudi la Mungu, na tujiweke wakfu kikamilifu kwa Yeye ambaye tunataka kuliinua Jina Lake. Pia tuombe kwa dhati na bidii kwa ajili ya wale tunaotarajia kuwatembelea, kwa imani iliyo hai inayowaleta, mmoja baada ya mwingine, katika uwepo wa Mungu. Bwana anajua mawazo na makusudi ya mwanadamu, na jinsi anavyoweza kutuyeyusha mioyo yetu kwa urahisi! Jinsi Roho Wake, kama moto, anavyoweza kuutiisha moyo wa jiwe la gumegume! Jinsi anavyoweza kuijaza roho kwa upendo na huruma nyororo! Jinsi awezavyo kutupa neema za Roho Wake Mtakatifu, na kutufanya sisi tufaekuingia na kutoka, katika kufanya kazi kwa ajili ya nafsi!— **Manuscript 2, "Jitihada Zilizowekwa wakfu za Kuwafikia Wasioamini," Juni 5, 1914 . ChS 169.2**

Kazi ya Bwana inaweza kupokea upendeleo mkubwa zaidi kuliko inavyopokea sasa, ikiwa tungewafikia wanadamu kwa hekima, tukiwafahamisha kazi, na kuwapa nafasi ya kufanya yale ambayo ni fursa yetu kuwashawishi kufanya kwa ajili ya maendeleo yake. Ikiwa sisi, kama watumishi wa Mungu, tungechukua mwenendo wa hekima na busara, mkono Wake mzuri ungetufanikisha katika jitihada zetu.— **The Southern Watchman, Machi 15, 1904 . ChS 170.1**

Ikiwa wote wanaojishugulisha na kazi ya Bwana wangetambua jinsi ambavyo mengi hutegemea uadilifu na mawazo yenye hekima, ufanisi mkubwa zaidi ungehudhuria jitihada zao. Kupitia hali ya kukosa ujasiri, kuona aibu na kurudi nyuma mara nyingi tunashindwa kupata kile ambacho kinaweza kupatikana kama haki yetu, kutoka kwa mamlaka zilizopo. Mungu atatufanyia kazi, tunapokuwa tayari kufanya yale tuwezayo na tunapaswa kufanya kwa upande wetu.— **The Southern Watchman, Machi 15, 1904 . ChS 170.2**

—

**Utume wa Nyumbani Dhidi ya Utume wa Kigeni**

Kazi ya umishenari ya nyumbani itasonga mbele zaidi katika kila njia wakati roho ya ukarimu zaidi, ya kujinyima, kujikana nafsi, na ya kujitolea itakapodhihirika kwa ajili ya usitawi wa utume katika nchi za kigeni; kwa maana ustawi wa kazi ya nyumbani unamtegemea kwa kiasi kikubwa Mungu, juu ya mvuto wa kutafakari wa kazi ya kiinjilisti inayofanywa katika nchi za mbali. Ni katika kufanya kazi kwa bidii ili kupeana mahitaji ya kazi ya Mungu ndipo tunaleta roho zetu katika uhusiano na Chanzo cha nguvu zote. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:27. ChS 170.3**

Mfanyabiashara wa Kiamerika ambaye alikuwa Mkristo mwenye dhati na mwenye bidii, katika mazungumzo na mfanyakazi mwenzake alisema kwamba yeye mwenyewe alifanya kazi kwa ajili ya Kristo masaa ishirini na nne ya siku. "Katika mahusiano yangu yote ya kibiashara," alisema, najaribu kumwakilisha Bwana na Mwalimu wangu. Nikiwa na nafasi, najaribu kuwavuta wengine Kwake. Siku nzima ninafanya kazi kwa ajili ya Kristo. Na usiku, nikiwa nimelala, nina mtu anayenifanyia kazi huko Uchina." Aliongeza hivi katika

maelezo: "Katika ujana wangu nilipani kwenda kama mmishenari katika watu wa mataifa tofauti. Lakini baada ya kifo cha baba yangu ilinibidi nirithi biashara yake ili kusaidia familia yangu kujipatia riziki. Sasa, badala ya mimi kwenda mwenyewe huko nchi za kigeni, nilijishughulisha na mambo mengine, na ninamsaidia mmishenari (sponsa). Katika mji x wa jimbo hilo la Uchina, mfanyakazi wangu yuko kazini. Na kwa hivyo, hata nilalapo, kupitia mwakilishi wangu, bado ninafanya kazi kwa ajili ya Kristo." **ChS 170.4**

Je, hakuna Waadventista Wasabato ambao watafanya vivyo hivyo? Badala ya kuwaweka wahudumu kazini kwa ajili ya makanisa ambayo tayari yanaijua Kweli, hebu washiriki wa makanisa wawaambie watenda kazi hawa: “Nendeni mkafanye kazi kwa ajili ya roho zinazoangamia gizani. Sisi wenyewe tutaendeleza ibada za kanisa. tutaendeleza mikutano, na, kwa kudumu ndani ya Kristo, tutadumisha maisha ya kiroho. Tutafanyia kazi roho zinazotuzunguka, na tutatuma maombi yetu na karama zetu ili kuwategemeza watenda kazi katika mashamba yenye uhitaji zaidi na ukiwa. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:29, 30. ChS 171.1**

## Mfano Unaostahili

Yule mjane maskini aliyetupa senti zake mbili katika hazina ya Bwana hakujua alichokuwa akifanya. Mfano wake wa kujitoa dhabihu, umetenda na kurudisha mwitikio kwa maelfu ya mioyo katika kila nchi na katika kila zama. Mfano huu, umeleta kwenye hazina ya Mungu zawadi kutoka kwa wale walio juu na walio chini, matajiri na maskini. Umesaidia kuendeleza misheni, kkuanzisha hospitali, kulisha wenye njaa, kuwavisha walio uchi, kuponya wagonjwa, na kuhubiri injili kwa maskini. Watu wengi wamebarikiwa kupitia tendo lake lisilo la ubinafsi. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:310.**

## Masomo Kutokana na Uzoefu wa Nehemia

Katika miaka iliyopita, nimezungumza kwa kupendelea mpango wa kuwasilisha kazi yetu ya utume na maendeleo yake mbele ya marafiki na majirani zetu, na nimerejelea mfano wa Nehemia. Na

sasa ninatamani kuwahimiza ndugu na dada zetu wajifunze upya uzoefu wa mtu huyu wa sala na imani na uamuzi wa busara, ambaye alifanya ujasiri kumwomba rafiki yake, Mfalme Artashasta, msaada wa kuendeleza masilahi ya Mungu.—. **Manuscript 2, “Jitihada Zilizowekwa wakfu za Kuwafikia Wasioamini,” Juni 5, 1914 . ChS 171.3**

*Njia Zilizoombwa Kutoka Kwa Wale Wanaoweza Kutoa* —Watu wa maombi wanapaswa kuwa watu wa kutenda. Wale ambao wako tayari na tayari, watapata njia na njia za kufanya kazi. Nehemia hakutegemea kutokuwa na uhakika. Njia alizokosa aliomba kutoka kwa wale walioweza kutoa.— **The Southern Watchman, Machi 15, 1904 . ChS 171.4**

*Ujasiri kwa Ajili ya Kazi Hiyo Ulikuja Kupitia Nguvu* —Nehemia na Artashasta walisimama uso kwa uso,—mmoja mtumishi wa jamii iliyokandamizwa, yule mwingine mfalme wa milki kuu ya ulimwengu. Lakini kubwa zaidi kuliko tofauti ya cheo ilikuwa umbali wa kimaadili uliowatenganisha. Nehemia alikuwa ametii mwaliko wa Mfalme wa

wafalme, “Na azishike nguvu zangu, Afanye amani nami, naye atafanya amani nami.” Ombi la kimya-kimya ambalo alituma mbinguni lilikuwa lile lile alilokuwa ametoa kwa majuma mengi, kwamba Mungu afanikishe ombi lake. Na sasa, akipata ujasiri katika wazo la kwamba alikuwa na Rafiki, mjuzi na muweza yote, kufanya kazi kwa niaba yake, mtu wa Mungu alimjulisha mfalme shauku yake ya kuachiliwa kwa muda kutoka ofisi yake katika nyumba ya kifalme, na kwa mamlaka. ili kupajenga mahali pa Yerusalemu palipoharibiwa, na kuyafanya tena kuwa mji wenye nguvu na wenye ulinzi. Matokeo muhimu kwa mji na taifa la Kiyahudi yalitegemea ombi hili. “Na,” asema Nehemia, “mfalme akanipa, kama mkono mwema wa Mungu wangu ulivyokuwa juu yangu.”— **The Southern Watchman, Machi 8, 1904 . ChS 172.1**

*Kuandikishwa Rasmi* —Kwa kuwa ombi lake [Nehemia] kwa mfalme lilikuwa limepokelewawa vyema, alitiwa moyo kuomba msaada kama uliohitajiwa ili kutimiza mipango yake. Ili kutoa hadhi na mamlaka kwa misheni yake, na vile vile kutoa ulinzi katika safari, alipata msindikizaji wa kijeshi. Akapata barua za kifalme kwa maliwali wa majimbo ya ng'ambo ya Eufrati, nchi ambayo itampasa kupita katika njia yake kwenda Yudea; na alipata, pia, barua kwa mlinzi wa msitu wa mfalme katika milima ya Lebanoni, ikimuelekeza kuandaa mbao ambazo zingehitajika kwa ajili ya ukuta wa Yerusalemu na majengo ambayo Nehemia alipendekeza kujenga. Ili kusiwe na nafasi ya kulalamika kwamba alikuwa amepitcaxxvui tume wake, Nehemia alikuwa mwangalifu kupata mamlaka na mapendeleo aliyopewa, yaliyofafanuliwa waziwazi.— **The Southern Watchman, Machi 15, 1904 . ChS 172.2**

Barua za kifalme kwa magavana wa majimbo katika njia yake, zilimletea Nehemia mapokezi ya heshima na msaada wa haraka. Na hakuna adui aliyethubutu kumdhulumu ofisa aliyekuwa analindwa na mamlaka ya mfalme wa Uajemi na kushughulikiwa

—

sana na watawala wa majimbo. Safari ya Nehemia ilikuwa salama na yenye ufanisi.— **The Southern Watchman, Machi 22, 1904 . ChS 172.3**

*Kukumbana na Vizuizi* —Hata hivyo, kuwasili kwake Yerusalemu, pamoja na kuhudhuria kwa walinzi wa kijeshi, kuonyesha kwamba alikuwa amekuja kwa kazi fulani muhimu, kulichochea wivu na chuki ya maadui wa Israeli. Makabila ya makafiri yaliyokaa karibu na Yerusalemu hapo awali yalikuwa yamejiingiza kwenye uadui wao dhidi ya Wayahudi kwa kuwarundikia kila tusi na madhara ambayo walithubutu kuwaletea. Waliotangulia katika kazi hii mbaya walikuwa machifu fulani wa kabila hizi, Sanbalati Mwahoroni, Tobia Mwamoni, na Geshemu Mwarabu; na kuanzia wakati huu viongozi hao walitazama kwa jicho la wivu mienendo ya Nehemia, na kujitahidi kwa kila njia katika uwezo wao kuzuia mipango yake na kuzuia kazi yake.— **The Southern Watchman, Machi 22, 1904 . ChS 173.1**

Walijaribu kusababisha mgawanyiko miongoni mwa watenda kazi kwa kupendekeza mashaka na kuamsha kutoamini juu ya mafanikio yao. Pia walidhihaki juhudi za wajenzi,

wakatangaza biashara kuwa haiwezekani, na kutabiri kushindwa kwa fedheha Wajenzi
kwenye ukuta walipata upinzani mkali zaidi. Walilazimika kulinda daima dhidi ya njama za wapinzani wao wasio na usingizi. Wajumbe wa adui walijaribu kuharibu ujasiri wao kwa kusambaza taarifa za uongo; njama ziliundwa kwa visingizio mbalimbali vya kumvuta Nehemia katika taabu zao; na Wayahudi wenye mioyo ya uwongo walipatikana tayari kusaidia kazi ya hila.... Wajumbe wa adui, waliodai urafiki, walichangamana na wajenzi, wakipendekeza mabadiliko katika mpango huo, wakitafuta kwa njia mbalimbali kugeuza usikivu wa wafanyakazi, kusababisha kuchanganyikiwa na kufadhaika, na kuamsha hali ya kutoaminiana na kutia shaka.— **The Southern Watchman, Aprili 12, 1904 . ChS 173.2**

*Vizuizi Vilevile Wanakabili Viongozi Leo* —Jaribio la Nehemia limerudiwa katika historia ya watu wa Mungu wakati huu. Wale wanaofanya kazi katika njia ya ukweli watapata kwamba hawawezi kufanya hivi bila kusisimua hasira ya maadui zake. Ingawa wameitwa na Mungu kwa kazi ambayo wanashiriki, na njia yao imeidhinishwa Naye, hawawezi kuepuka lawama na dhihaka. Watashutumiwa kuwa wenye maono, wasiotegemeka, walaghai, wanafiki, kitu chochote, kwa ufupi, ambacho kitalingana na kusudi la adui zao. Mambo matakatifu zaidi yatawakilishwa katika nuru ya kejeli ili kuwafurahisha wasiomcha Mungu. Kiasi kidogo sana cha kejeli na akili duni, iliyounganishwa na husucxdkvaii, husuda, uasherati, na chuki, inatosha kuamsha furaha ya mdhihaki mbaya. Na hawa wenye kiburi wenye kiburi hunoa ujanja wao kwa wao, na kutiana moyo katika kazi yao ya kufuru. Dharau na dhihaka kwa hakika ni chungu kwa asili ya mwanadamu; lakini lazima zivumiliwe na wote walio wa kweli kwa Mungu. Hivyo ni kanuni ya Shetani kugeuza nafsi kutoka katika kufanya kazi ambayo Bwana ameweka juu yao.— **The Southern Watchman, Aprili 12, 1904 . ChS 173.3**

*Kukusanya Majeshi Waliokata Tamaa* —Kwa usiri na ukimya,

—

Nehemia alikamilisha mzunguko wake wa kuta. Anatangaza, “Wala mashehe hawakujua nilikokwenda, wala nilivyotenda; wala sijawaambia Wayahudi, wala makuhani, wala wakuu, wala mashehe, wala watu wengine waliokuwa wakiifanya kazi hiyo. Katika uchunguzi huu mchungu hakutaka kuvutia usikivu wa marafiki au maadui, isije msisimko ukatokezwa, na ripoti kuwekwa katika mzunguko ambazo zinaweza kushindwa, au angalau kuzuia, kazi yake. Nehemia alitumia muda uliosalia wa usiku kwa maombi; asubuhi lazima kuwe na jitihada ya dhati ya kuwaamsha na kuwaunganisha watu wa nchi yake waliokata tamaa na waliogawanyika.— **The Southern Watchman, Machi 22, 1904 . ChS 174.1**

Ingawa Nehemia alipewa utume wa kifalme uliohitaji wakaaji washirikiane naye katika kujenga upya kuta za mji, alichagua kutotegemea matumizi tu ya mamlaka. Afadhali alitaka kupata imani na huruma ya watu, akijua vyema kwamba muungano wa mioyo na mikono ulikuwa muhimu kwa mafanikio katika kazi kubwa ambayo alikuwa ameifanya. ChS 174.2

Alipowaita watu pamoja siku ya pili yake, aliwasilisha hoja zilizokusudiwa kuamsha nguvu zao zilizokuwa zimelala na kuunganisha idadi yao iliyotawanyika Na baada ya kuliweka jambo hilo kikamilifu mbele yao, akionyesha kwamba alikuwa ameungwa mkono na mamlaka iliyounganishwa. wa mfalme wa Uajemi na Mungu wa Israeli, Nehemia aliwauliza watu moja kwa moja swali kama wangechukua fursa ya pindi hiyo nzuri, na kuinuka pamoja naye na kuujenga ukuta. Ombi hili lilikwenda moja kwa moja kwenye mioyo yao; udhihirisho wa neema ya Mbinguni kwao ulizitia aibu hofu zao. Kwa ujasiri mpya walipaza sauti kwa sauti moja, “Haya! Na tuondoke tukajenge.”— **The Southern Watchman, Machi 29, 1904 . ChS 174.3**

Nguvu takatifu na tumaini kuu la Nehemia ziliwasilishwa kwa watu. Waliposhika roho, walipanda kwa muda hadi kiwango cha maadili cha kiongozi wao. Kila mmoja, katika nyanja yake mwenyewe, alikuwa aina ya Nehemia; na kila mmoja akamtia nguvu na kumtegemeza ndugu yake katika kazi hiyo.— **The Southern Watchman, Machi 29, 1904 . ChS 175.1**

*Makuhani wa Israeli Miongoni mwa Watu wa Kwanza Kuitikia* — Miongoni mwa watu wa kwanza kupata roho ya Nehemia ya bidii na bidii walikuwa makuhani wa Israeli. Kutokana na nafasi ya ushawishi waliyokuwa nayo, wanaume hawa wangeweza kufanya mengi kuzuia au kuendeleza kazi. Ushirikiano wao tayari mwanzoni kabisa ulichangia c.x.xv.i ii
sio kidogo katika mafanikio yake. Ndivyo inavyopaswa kuwa katika kila kazi takatifu.
Wale wanaochukua nafasi za ushawishi na wajibu katika kanisa, wanapaswa kuwa wa kwanza katika kazi ya Mungu. Wakihama kwa kusitasita, wengine hawatahama hata kidogo. Lakini “bidii yao itawachochea wengi sana.” Nuru yao inapowaka sana, mienge elfu moja itawashwa kwenye mwali huo.— **The Southern Watchman, Aprili 5, 1904 . ChS 175.2**

—

*Nehemia Akiwa Mpangaji* —Watu kwa ujumla walikuwa na moyo mmoja na nafsi moja ya uzalendo na utendaji wenye uchangamfu. Watu wenye uwezo na ushawishi walipanga matabaka mbalimbali ya wananchi kuwa makampuni, kila kiongozi akijifanya kuwajibikia uwekaji wa sehemu fulani ya ukuta. Lilikuwa jambo la kupendeza sana kwa Mungu na malaika kuona makundi yenye shughuli nyingi yakifanya kazi kwa upatano juu ya kuta zilizobomoka za Yerusalemu, na ilikuwa sauti ya shangwe kusikia kelele za vyombo vya kazi tangu mapambazuko ya mapema zaidi "mpaka nyota zikaonekana. "— **The Southern Watchman, Aprili 5, 1904 . ChS 175.3**

*Onyesho la Uongozi wa Kweli* —Bidii na nguvu za Nehemia hazikupungua, kwa kuwa sasa kazi ilikuwa imeanza. Hakukunja mikono yake, akihisi kwamba anaweza kuuacha mzigo ule. Kwa uangalifu usiochoka alisimamia kazi mara kwa mara, akiwaelekeza wafanyakazi, akibainisha kila kizuizi, na kuandaa kila dharura. Ushawishi wake ulisikika kila mara katika upana wote wa maili hizo tatu za ukuta. Kwa maneno ya wakati ufaao aliwatia moyo wenye hofu, akaidhinisha wenye bidii, au kuwaamsha wale waliozembea.

Na tena alitazama kwa jicho la tai mienendo ya adui zao, ambao nyakati fulani walikusanya kwa mbali na kufanya mazungumzo ya dhati, kana kwamba walikuwa wakipanga njama mbaya, na kisha kuwasogelea wafanya kazi, walijaribu kugeuza fikira zao na kuzuia kazi. **ChS 175.4**

Ijapokuwa jicho la kila mtenda kazi mara nyingi huelekezwa kwa Nehemia, akiwa tayari kutii ishara hata kidogo, jicho lake na moyo wake vimeinuliwa kwa Mungu, Mwangalizi mkuu wa kazi yote, yeye aliyeiweka katika moyo wa mtumishi Wake kujenga. Na imani na ujasiri vinapoimarika moyoni mwake, Nehemia anapaza sauti, na maneno yake, yanayorudiwa-rudiwa na kurudiwa, yasisimua mioyo ya wafanyakazi katika mstari huo wote, "Mungu wa mbinguni, atatufanikisha!"— **The Southern Watchman, Aprili 5, 1904 . ChS 176.1**

Nehemia na watenda kazi wenzakee hawakurudi nyuma kutokana na magumu, au kujitetea kutokana na kujaribu huduma. Wala usiku wala mchana, hata kwa muda mfupi wa kusinzia, hawakuvua mavazi yao, au hata kuweka kando silaha zao. "Basi mimi, na ndugu zangu, na watumishi wangu, na watu wa walinzi walionifuata, hatukuvua hata nguo zetu hata mmoja; kila mtu alikwenda kuteka maji akichukua silaha yake."— **The Southern Watchman, Aprili 26 1904 . ChS 176.2**



*Kupinga Ushawishi Katika Kila Vuguvugu la Kidini* —Wengi wa wakuu na watawala wa Israeli pia walitimiza wajibu wao kwa uungwana; lakini kulikuwa na wachache, wakuu Watekoi, ambao "hawakutia shingo zao kazini mwa bwana wao." Ingawa wajenzi waaminifu wametajwa kwa heshima katika kitabu cha Mungu, kumbukumbu ya watumishi hao wavivu inatiwa aibu, na kutolewa kama onyo kwa vizazi vyote vijavyo. **ChS 176.3**

Katika kila vuguvugu la kidini kuna wengine ambao, ingawa hawawezi kukana kwamba ni kazi ya Mungu, watajiweka kando, wakikataa kufanya juhudi zozote za kuiendeleza. Lakini katika biashara za kukuza masilahi yao ya ubinafsi, wanaume hawa mara

—

nyingi ndio wafanyikazi wenye bidii na wenye nguvu. Ilikuwa vyema kukumbuka ile rekodi iliyowekwa juu, kitabu cha Mungu, ambamo nia zetu zote na kazi zetu zimeandikwa— kile kitabu ambacho ndani yake hakina upungufu, hakuna makosa, na ambacho kutoka kwake tunapaswa kuhukumiwa. Huko kila fursa iliyopuuzwa ya kufanya utumishi kwa Mungu itaripotiwa kwa uaminifu, na kila tendo la imani na upendo, hata liwe la unyenyekevu jinsi gani, litakumbukwa milele.— **The Southern Watchman, Aprili 5, 1904 . ChS 176.4**

**Wito Kwa Ajili ya Nehemia wa Leo**

Kuna hitaji la akina Nehemia katika kanisa leo,—sio wanaume wanaoweza kuomba na kuhubiri tu, bali wanaume ambao maombi na mahubiri yao yanaimarishwa kwa kusudi thabiti na la shauku. Kozi inayofuatwa na mzalendo huyu wa Kiebrania katika kutimiza mipango yake ni ile ambayo bado inapaswa kupitishwa na mawaziri na wanaume wakuu.

Wakishaweka mipango yao, wanapaswa kuiwasilisha kwa kanisa kwa namna ambayo itawafanya wapendezwe na kushirikiana nao. Hebu watu waelewe mipango na washiriki kazi hiyo, nao watakuwa na nia ya kibinafsi katika usitawi wake. Mafanikio ya kuhudhuria jitihada za Nehemia yanaonyesha kile ambacho sala, imani, na hatua ya hekima na yenye nguvu itatimiza. Imani iliyo hai itachochea kutenda kwa nguvu. Roho inayoonyeshwa na kiongozi itaonyeshwa kwa kiasi kikubwa na watu. Ikiwa viongozi wanaodai kuamini kweli zile takatifu, muhimu ambazo zitaujaribu ulimwengu kwa wakati huu, hawaonyeshi bidii ya kuwatayarisha watu kusimama katika siku ya Mungu, lazima tutarajie kanisa kuwa wazembe, wavivu na wa kujifurahisha. -enye upendo.— **The Southern Watchman, Machi 29, 1904 . ChS 177.1**

**SURA YA 16 —VUGUVUGU ZA UPANUZI WA KANISA**

**Mpango wa Kimungu**

Si kusudi la Mungu kwamba watu Wake waanzishe koloni au kukaa pamoja katika makundi makubwa. Wanafunzi wa Kristo ni wawakilishi wake duniani, na Mungu anakusudia kwamba watawanyike kote juu ya nchi, katika miji midogo, miji mikubwa, na vijiji, kama nuru katikati ya giza la ulimwengu. **—Shuhuda kwa Kanisa 8:244.**

Mpango wa kufanya koloni, au kuhamia kutoka maeneo tofauti ambapo kunanguvu kidogo au ushawishi kidogo, na kuzingatia ushawishi wa wengi katika eneo moja, ni kuondoa taa kutoka mahali ambapo Mungu angeitaka iangaze. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:633.**

Kama kanisa la Kristo lingetimiza kusudi la Bwana wetu, nuru ingeangaziwa juu ya wote wakaao katika giza na katika eneo na uvuli wa mauti. Badala ya kukusanyika pamoja na kukwepa kuwajibika na kubeba msalaba, washiriki wa kanisa wangetawanyika

—

katika nchi zote, wakiacha nuru ya Kristo iangaze kutoka kwao, wakifanya kazi kama alivyofanya kwa ajili ya wokovu wa roho, na hii “injili ya ufalme. ” ingebebwa upesi hadi ulimwenguni pote.— **Thoughts From the Mount of Blessing, 42, 43 . ChS 178.3**

Ndugu na dada, kwa nini kuelea juu ya makanisa? Jifunzeni mfano wa kondoo aliyepotea, na nendeni kama wachungaji wa kweli, mkimtafuta aliyepotea aliye katika jangwa la dhambi. Okoa wanaoangamia.— **The Review and Herald, Desemba 12, 1893 . ChS 178.4**

Washiriki walei wa makanisa yetu wanaweza kukamilisha kazi, ambayo kwa hadi sasa, wameianza kidogo sana. Asiwepo mtu atakayehamia sehemu mpya kwa ajili ya manufaa ya kidunia tu; bali palipo na fursa ya kupata riziki, hebu familia zilizo na msingi mzuri katika ukweli ziingie, familia moja au mbili katika sehemu, wakifanya kazi kama wamisionari. Wanapaswa kuhisi upendo kwa ajili ya roho, mzigo wa kutenda kazi kwa ajili yao, na wanapaswa kuchunguza kujua jinsi ya kuwaleta katika Kweli. Wanaweza

kugawanya machapisho yetu, kufanya mikutano katika nyumba zao, kufahamiana na majirani zao, na kuwaalika waje kwenye mikutano hii. Hivyo wanaweza kuiruhusu nuru yao kuangaza katika matendo mema. **—Shuhuda kwa Kanisa 8:245.**

Ndugu ambao wanataka kubadilisha eneo lao, wanaoutazama utukufu wa Mungu, na kuhisi wajibu binafsi uko juu yao kuwatendea mema wengine, kufaidika na kuokoa roho ambazo Kristo hakuwazuilia maisha Yake ya thamani, wanapaswa kwenda katika miji na vijiji ambako kuna nuru kidogo au hakuna kabisa na wanapoweza kutoa huduma ya kweli na kuwabariki wengine kwa bidii na uzoefu wao. Wamisionari wanatakiwa kwenda katika miji na vijiji na kuinua kiwango cha Kweli, ili mashahidi wa Mungu watawanyike kote nchini, ili nuru ya Kweli iweze kupenya ambako bado haijafikia, na kiwango cha Kweli kiinuliwe ambako hakijulikani bado. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:115.**

Hakuna kitu kitakachoamsha bidii ya kujitolea na kupanua na kuimarisha tabia ya kushiriki katika kazi kwa ajili ya wengine. Wengi wanaojiita Wakristo, katika kutafuta uhusiano wa kanisa, wanajifikiria wao wenyewe tu. Wanatamani kufurahia ushirika wa kanisa na utunzaji wa kichungaji. Wanakuwa washiriki wa makanisa makubwa na yenye ufanisi, na wanaridhika kufanya kidogo kwa ajili ya wengine. Kwa njia hii wanajinyang'anya wenyewe baraka zenye thamani zaidi. Wengi wangefaidika sana kwa kujitolea makundi yao yenye kupendeza na yenye kuleta urahisi. Wanahitaji kwenda mahali ambapo nguvu zcxaxoxi zitatolewa katika kazi ya Kikristo, na wanaweza kujifunza kubeba madaraka.— **The Ministry of Healing, p. 151 . ChS 179.2**

Kuna maelfu ya mahali pa kuingia ambapo kiwango cha ukweli hakijawahi kuinuliwa, ambapo tangazo la ukweli halijapata kusikika katika Amerika. Na kuna maelfu ambao wanaweza kuingia katika shamba la mavuno ambao sasa hawana kazi ya kidini, na kwa sababu hiyo, wanakwenda kulemaza njia yao ya

—

kwenda mbinguni, wakionyesha shaka yao kama wao ni Wakristo. Hitaji lao ni muungano muhimu na Yesu Kristo. Ndipo inaweza kusemwa kuwahusu, “Ninyi ni watenda kazi pamoja na Mungu.” Nataka kuwaambia wengi, Mnangoja mtu awapeleke shambani na kuwafanyisha kazi, au alete shamba la mizabibu kwenu, ili msipate usumbufu katika kazi. Utasubiri bure. Ukiinua macho yako, utaona mavuno yameiva, tayari kwa mundu, kwa njia yo yote utakayotazama; utapata kazi karibu na mbali. Lakini Kristo atasema juu ya wangapi katika hukumu, “Watumishi wema na waaminifu”? Nafikiri jinsi malaika wanapaswa kuhisi kuona mwisho unakaribia, na wale wanaodai kuwa na ujuzi wa Mungu na Yesu Kristo ambaye Yeye amemtuma, hukusanyika pamoja, kutawala, na kuhudhuria mikutano, na kujisikia kutoridhika ikiwa hakuna mahubiri mengi. kunufaisha nafsi zao na kulitia nguvu kanisa, huku wakiwa hawafanyi lolote kihalisi Ikiwa matarajio yao ya
kidunia, ya kifedha hayafanikiwi kwa kuhamia maeneo ambayo ukweli haujatangazwa, au ambako kumekuwako lakini kumeta kwa nuru. , je, hawatakuwa wakifanya tu kazi ambayo Yesu amefanya ili kuwaokoa?— **The General Conference Daily Bulletin, Februari 4, 1893 , 131. ChS 179.3**

Tunaona uhitaji mkubwa wa kazi ya umishonari kupeleka kweli si kwa nchi za kigeni tu, bali kwa wale walio karibu nasi. Karibu nasi kuna miji na miji ambayo hakuna juhudi zinazofanywa kuokoa roho. Kwa nini familia zinazojua ukweli wa sasa zisikae katika miji na vijiji hivi, ili kuweka pale kiwango cha Kristo, wakifanya kazi kwa unyenyekevu, si kwa njia yao wenyewe, bali katika njia ya Mungu, kuleta nuru mbele ya wale wasio na ujuzi? yake? **ChS 180.1**

Kanisa litakapokuwa na roho ya ujumbe kwa kweli, watatupa nguvu zao zote katika kazi ya kuokoa roho ambazo Kristo amezifia. Wataingia kwenye nyanja mpya. Wengine ambao si wahudumu waliowekwa wakfu watakuwa watenda kazi pamoja na Mungu katika kuyatembelea makanisa, na kujaribu kuyatia nguvu yale yaliyosalia, yaliyo tayari kufa. Kutakuwa na watu wa kawaida ambao watahamia mijini na mijini, na katika sehemu zinazoonekana kuwa nje ya njia, ili waweze kuacha nuru ambayo Mungu amewapa, iwaangazie wengine. Wengine ambao watakutana nao hawataonekana kuwa somo wenye kutegemeka zaidi, lakini swali pekee lapaswa kuwa, Je, watapatana na Kristo? Je, watakuwa washirika wa roho yake, ili kwamba mvuto wao, katika kanuni na kielelezo, utoe vivutio vya yule Mwanzilishi wa ukweli na haki? **ChS 180.2**

Mahali ambapo ukweli haujulikani, akina ndugu ambao wamezoea kazi hiyo wanaweza kuajiri jumba, au mahali pengine pa kufaa pa kukutanikia, na kuwakusanya pamoja wote
cx x xi i
wanaokuja. Kisha wawa f u n dishe watu kwa haki. Hawahitaji kuhubiri, bali wachukue
Biblia, na kumwacha Mungu aseme moja kwa moja kutoka ~~kat~~ika Neno Lake. Ikiwa kuna idadi ndogo tu iliyopo, wanaweza kusoma "Bwana asema hivi," bila gwaride kubwa au msisimko; soma tu na kueleza ukweli sahili wa injili, na kuimba na kusali pamoja nao.— **The Review and Herald, Septemba 29, 1891 .** **ChS 181.1**

**Ibrahimu Mfano Unaofaa**

—

Haikuwa jaribu jepesi ambalo lilileletwa juu ya Ibrahimu, dhabihu isiyo ndogo ambayo ilitakiwa kutoka kwake. Kulikuwa na mahusiano yenye nguvu ya kumfunga kwa nchi yake, jamaa zake, na nyumba yake. Lakini hakusita kutii wito huo. Hakuwa na swali la kuuliza kuhusu Nchi ya Ahadi,—kama udongo ulikuwa na rutuba, na hali ya hewa yenye afya; kama nchi ina mazingira mazuri, na ingemudu fursa za kukusanya mali. Mungu alikuwa amesema, na mtumishi wake lazima atii; mahali pa furaha zaidi duniani kwake palikuwa mahali ambapo Mungu angemtaka awepo. **ChS 181.2**

Wengi bado wanajaribiwa kama vile Ibrahimu. Hawasikii sauti ya Mungu ikisema moja kwa moja kutoka mbinguni, lakini Yeye huwaita kwa mafundisho ya Neno Lake na matukio ya utoaji huu. Wanaweza kuhitajika kuacha kazi ambayo inaahidi utajiri na heshima, kuacha mashirika ya kupendeza na yenye faida, na kujitenga na jamaa, kuingia kwenye kile kinachoonekana kuwa njia ya kujinyima, shida, na dhabihu. Mungu ana kazi kwa ajili yao ya kufanya; lakini maisha ya raha na ushawishi wa marafiki na jamaa yangezuia ukuzaji wa sifa muhimu sana kwa utimilifu wake. Anawaita mbali na mvuto

na usaidizi wa kibinadamu, na kuwaongoza kuhisi hitaji la msaada Wake, na kumtegemea Yeye pekee, ili aweze kujidhihirisha kwao. **ChS 181.3**

Nani yuko tayari kwa wito wa Providence kukataa mipango inayopendwa na mashirika yanayofahamika? Ni nani atakayekubali majukumu mapya na kuingia katika nyanja zisizojaribiwa, akifanya kazi ya Mungu kwa mioyo thabiti na iliyo tayari, kwa ajili ya Kristo akihesabu hasara Zake tena? Yeye atakayefanya hivyo ana imani ya Ibrahimu, naye atashiriki pamoja naye ule “uzito wa milele uzidio kuwa mwingi sana,” ambao “mateso ya wakati huu wa sasa hayastahili kulinganishwa nao.”— Patriarchs and Prophets. 126, 127 . ChS 181.4

## Unafanya Nini Hapa?

Mengi hutegemea shughuli isiyokoma ya wale walio wa kweli na waaminifu; na kwa sababu hii Shetani huweka kila jitihada iwezekanayo ili kuzuia kusudi la kimungu litakalotekelezwa kupitia kwa watiifu. Anawafanya wengine wapoteze utume wao wa juu na mtakatifu, na kuridhika na anasa za maisha haya. Anawaongoza kutulia kwa raha, au, kwa ajili ya manufaa makubwa zaidi ya kidunia, kuwaondoa kutoka mahali ambapo wanaweza kuwa na uwezo wa kufanya mema. Wengine anawafanya wakimbie kwa kukatishwa tamaa na kazi, kwa sababu ya upinzani au mnyanyaso. Lakini wote hao wanachukuliwa na Mbingu kwa huruma nyingi. Kwa kila mtoto wa Mungu ambaye sauti yake adui wa roho ilikuwa imefaulu kunyamazisha, swali linashughulikiwa, "Unafanya nini hapa?" Nilikuamuru uende ulimwenguni kote na kuhubiri injili, kuwatayarisha watu kwa ajili ya siku ya Mungu. Kwa nini uko hapa? Ni nani aliyekutuma?— Manabii na Wafalme, 171, 172 . ChS 182.1



Kuhusu familia, kama watu binafsi, swali linaulizwa, "Unafanya nini hapa?" Katika makanisa mengi kuna familia zilizofundishwa

—

vyema kweli za Neno la Mungu, ambazo zinaweza kupanua wigo wa uvutano wao kwa kuhamia mahali penye uhitaji wa huduma wanayoweza kutoa.— Prophets and Kings, 172 . ChS 182.2

**Wito Kwa Familia za Kikristo?**

Familia za wamisionari zinahitajika ili kukaa mahali pasipokuwa na watu. Hebu wakulima, wafadhili, wajenzi na wenye ujuzi wa sanaa na ufundi mbalimbali waende kwenye mashamba yaliyosahaulika, waimarishe ardhi, waanzishe viwanda, wajiandalie makazi duni, na wasaidie jirani zao.— **The Ministry of Healing, 194. ChS 182.3**

Mungu anaziita familia za Kikristo kwenda katika jamii zilizo katika giza na makosa, na kufanya kazi kwa hekima na kwa uvumilivu kwa ajili ya Bwana. Ili kuitikia wito huu inahitaji kujitoa nafsi. Wakati wengi wanasubiri kila kikwazo kuondolewa, roho zinakufa bila tumaini na bila Mungu duniani. Wengi, wengi sana ,kwa ajili ya kutafuta manufaa ya kidunia, kwa ajili ya kutafuta kupata ujuzi wa kisayansi, watajiweka katika maeneo yenye magonjwa na kuvumilia shida na ufukara. Wako wapi walio tayari kufanya hivi kwa ajili ya kuwaambia wengine juu ya Mwokozi? Wako wapi wanaume na wanawake

ambao watakwenda kwenye maeneo yanayohitaji injili, ili wawaelekeze walio gizani kwa Mkombozi? **—Shuhuda kwa Kanisa 9:33.**

Kuna familia nzima ambazo wanaweza kuwa wamishionari, wakijihulisha na kazi ya binafsi, wakifanya kazi kwa bidii kwa ajili ya Bwana kwa mikono yenye shughuli nyingi na akili imara, wakibuni mbinu mpya kwa ajili ya mafanikio ya kazi Yake. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:40.**

Ikiwa familia zingeishi mahali penye giza duniani, mahali ambapo watu wamefunikwa na giza la kiroho, na kuacha nuru ya maisha ya Kristo iangaze kupitia kwao, kazi kubwa ingetimizwa. Hebu na Waanze kazi yao kwa utulivu, usio na bugudha, bila kuchota fedha za makoferensi hadi kazi iwe kubwa kiasi kwamba hawawezi kuisimamia bila msaada wa wachungaji. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:442.**

**Upandikizaji Unahitaji Wenye Hekima**

Tayarisha na watendakazi kwenda kwenye njia kuu na njia njia. Tunahitaji wapanda- vitalu (transplant nursery) wenye busara ambao watapandikiza miti katika maeneo mbalimbali na kuisaidia ili iweze kukua. Ni wajibu chanya kwa watu wa Mungu kwenda katika maeneo ya nje na mbali. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:118.**

Washiriki wengi wa makanisa yetu makubwa hawafanyi lolote unapolinganisha. Wangeweza kutimiza kazi nzuri ikiwa, badala ya kukusanyika pamoja, wangetawanyika katika sehemu ambazo bado hazijafikiwa na ukweli. Miti iliyopandwa kwa karibu sana haistawi. Hupandikizwa na mtunza bustani, ili ipate nafasi ya kukua na isidumae na kuwa dhaifu. Sheria iyo hiyo ingefanya kazi vizuri kwa makanisa yetu makubwa. Wengi wa washiriki wanakufa kiroho kwa kukosa kazi hii hii. Wanakuwa dhaifu na kukosa ufanisi. Kama wangehamishwa, wangekuwa na nafasi ya kukua wakiwa na nguvu na juhudi. **— Shuhuda kwa Kanisa 8:244.**

**Uhakika wa Matokeo**

—

Ikiwa washiriki walei wa kanisa wataamka kufanya kazi wanayoweza kuifanya, wakienda vitani kwa nia na gharama yao wenyewe, kila mmoja akiona ni kiasi gani anachoweza kutimiza katika kuvuta roho kuja kwa Yesu, tutaona wengi wakiacha safu za Shetani na kusimama chini ya bendera ya Kristo. Kama watu wetu watatenda kulingana na nuru inayotolewa katika Maneno haya machache ya maagizo, bila shaka tutauona wokovu wa Mungu. Uamsho wa ajabu utafuata. Wenye dhambi wataongoka, na roho nyingi zitaongezeka kanisani. **—Shuhuda kwa Kanisa 8:246.**

Washiriki wetu wa kanisa wanapaswa kuona shauku kubwa katika utume wa nyumbani na nchi za kigeni. Mibaraka mikubwa itakuja kwao kadri wanavyo fanya jitihada za kujitoa kafara ili kupanda kiwango cha Kweli katika eneo jipya. Fedha iliyowekezwa kwa ajili ya kazi hii italeta faida kubwa. Waongofu wapya, wakifurahia nuru waliyoipokea kutoka katika Neno. kwa upande wao watatoa mali zao kwa ajili ya kuipeleka nuru ya Ukweli kwa wengine. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:49.**

Katika maeneo ambayo hali ni ya kuchukiza na ya kukatisha tamaa kiasi kwamba wafanyakazi wengi wanakataa kwenda huko, mabadiliko bora na ya kushangaza yanaweza kuletwa na juhudi za washiriki walei waliojitoa. Wafanyakazi hawa wanyenyekevu watatimiza mengi kwa sababu wanaweka juhudi yenye uvumilivu, isiyochoka, bila kutegemea nguvu za kibinadamu, bali za Mungu, ambaye huwapatia kibali Chake. Kiasi cha mema ambayo watendakazi hawa hukamilisha hakitajulikana kamwe katika ulimwengu huu. **—Shuhuda kwa Kanisa 7:22, 23.**

**Masomo Kutokana na Kushindwa kwa Israel ya Kale**

Waisraeli walipoingia Kanaani, hawakulitimiza kusudi la Mungu kwa kumiliki nchi yote. Baada ya kufanya ushindi kwa sehemu, walitulia ili kufurahia matunda ya ushindi wao. Katika kutokuamini kwao na kupenda raha walikusanyika katika sehemu zilizokwisha kutekwa, badala ya kusonga mbele ili kuchukua maeneo mapya. Hivyo wakaanza kumwacha Mungu. Kwa kushindwa kwao kutimiza kusudi Lake walifanya isiwezekane Kwake kutimiza ahadi Yake ya baraka kwao. Je, kanisa la leo halifanyi jambo lilo hilo? Ulimwengu mzima mbele yao ukiwa na hitaji la injili, wale wanaojulikana kuwa Wakristo hukusanyika mahali ambapo wao wenyewe wanaweza kufurahia manufaa ya injili. Hawahisi umuhimu wa kumiliki maeneo mapya, wakipeleka ujumbe wa wokovu katika maeneo ya mbali. Wanakataa kutimiza agizo la Kristo: "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Je, wana hatia kidogo kuliko lilivyokuwa kanisa la Kiyahudi? **—Shuhuda kwa Kanisa 8:119.**

—

**Kufuatisha Nyayo za Kimungu**

Wengi wanahisi kwamba lingekuwa fursa kubwa kutembelea matukio ya maisha ya Kristo duniani, kutembea pale Alipokanyaga, kutazama ziwa ambalo alipenda kufundisha, na vilima na mabonde ambayo macho Yake mara nyingi yalitulia. Lakini hatuhitaji kwenda Nazareti, Kapernaumu, au Bethania, ili tutembee katika hatua za Yesu. Tutapata nyayo zake kando ya kitanda cha wagonjwa, katika mashimo ya umaskini, katika vichochoro vilivyosongamana vya mji mkuu, na katika kila mahali ambapo kuna mioyo ya wanadamu inayohitaji kufarijiwa. Kwa kufanya kama Yesu alivyofanya alipokuwa duniani, tutatembea katika hatua zake.**— The Desire of Ages, p. 640 . ChS 186.1**

Yesu alifanya kazi ili kuondoa kila kisa cha mateso alichoona. Alikuwa na pesa kidogo za kutoa, lakini mara nyingi alijinyima chakula ili kuwasaidia wale walioonekana kuwa wahitaji zaidi kuliko Yeye. Ndugu zake walihisi kwamba ushawishi Wake ulienda mbali

sana kupingana na wao. Alikuwa na busara ambayo hakuna hata mmoja wao alikuwa nayo, au alitamani kuwa nayo. Walipozungumza kwa ukali na maskini, watu walioshushwa hadhi, Yesu aliwatafuta hawa, na kuwaambia maneno ya kutia moyo. Kwa wale waliokuwa na uhitaji Angewapa kikombe cha maji baridi, na angeweka kwa utulivu mlo Wake mwenyewe mikononi mwao. Alipowaondolea mateso, kweli Alizofundisha zilihusishwa na matendo Yake ya rehema, na hivyo zilikumbukwa.— **The Desire of Ages, 86, 87 . ChS 186.2**

**Kuidhinisha**

Wafuasi wa Kristo wanapaswa kufanya kazi kama Yeye. Tunapaswa kuwalisha wenye njaa, kuwavisha walio uchi, na kuwafariji wanaoteseka na kuteswa. Tunapaswa kuwahudumia waliokata tamaa, na kutia moyo tumaini kwa wasio na tumaini. Na kwetu pia ahadi itatimizwa, “Haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakuwa nyuma yako.”— **The Desire of Ages, 350 . ChS 186.3**

Wale ambao wamejishughulisha na kazi hii ya usaidizi ya Kikristo wamekuwa wakifanya kile ambacho Bwana anatamani kufanywa, na Amekubali kazi zao. Yale ambayo yamefanywa katika mstari huu ni kazi ambayo kila Mwadventista Wa Sabato anapaswa kuhurumia kwa moyo wote na kuyakubali, na kuyashikilia kwa bidii. Kwa kupuuza kazi hii ambayo iko ndani ya mipaka yao wenyewe, kwa kukataa kubeba mizigo hii, kanisa linakutana na hasara kubwa. Kama kanisa lingechukua kazi hii jinsi walivyopaswa kufanya, ingekuwa njia ya kuokoa roho nyingi.—**Shuhuda kwa Kanisa 6:295**. Vipawa vyake vyote vinapaswa kutumika katika kuwabariki wanadamu, katika kuwaondolea mateso na wahitaji. Tunapaswa kuwalisha wenye njaa, kuwavisha walio uchi, kuwatunza wajane na yatima, kuwahudumia walio na shida na kukandamizwa. Mungu hakumaanisha kamwe kwamba taabu iliyoenea ulimwenguni inapaswa kuwepo. Hakumaanisha kamwe kwamba mtu mmoja awe na wingi wa anasa za maisha, wakati

—

watoto wa wengine walilie mkate. Njia zaidi na zaidi ya mahitaji halisi ya maisha imekabidhiwa kwa mwanadamu kufanya mema, kubariki ubinadamu. Bwana asema, “Uzeni mlivyo navyo, mtoe sadaka. Uwe “tayari kusambaza, tayari kuwasiliana.” "Ufanyapo karamu, waite maskini, viwete, viwete, vipofu." “Zifungueni vifungo vya uovu,” “zifungueni mizigo mizito,” “waacheni walioonewa waende zao huru,” “vunje kila nira.” “Wape wenye njaa mkate wako,” “walete maskini waliotupwa nyumbani kwako.” “Unapomwona aliye uchi, ... mfunike.” “Iridhishe nafsi iliyoteswa.” “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Haya ni maagizo ya Bwana. Je, kundi kubwa la wanaodai kuwa Wakristo wanafanya kazi hiyo?— **Christ’s Object Lessons, 370, 371 . ChS 187.2**

Matendo mema ni tunda ambalo Kristo anatutaka tuzae: maneno ya upole, matendo ya ukarimu, ya kuwahurumia na kuwajali masikini, wahitaji, walio na shida. Wakati unapohurumia mioyo iliyolemewa na kukatishwa tamaa kwa huzuni, wakati mkono unanyooshwa kwa wahitaji, wakati walio uchi wanavikwa, mgeni anakaribishwa kwenye

kiti sebuleni kwako na anapewa nafasi moyoni mwako, malaika wanasogea karibu zaidi, na kila ombi lililoelekezwa mbinguni hujibiwa. Kila tendo la haki, huruma, na ukarimu huleta nyimbo mbinguni. Baba kutoka kwenye kiti chake cha enzi huwaona wale wanaofanya matendo haya ya huruma, na amewawekea alama kwa ajili ya hazina Zake za thamani zaidi. "Nao watakuwa Wangu, asema Bwana wa majeshi, katika siku ile nitakapotengeneza vito vyangu." Kila tendo la huruma kwa wahitaji, wanaoteswa, huchukuliwa kana kwamba limetendwa kwa Yesu. Unaposaidia maskini, unahurumia walio taabika na wanaodhulumiwa, na kuwa rafiki wa yatima, unakuwa umejisogeza karibu katika uhusiano na Yesu. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:25.**

Kazi ya kuwakusanya wenye uhitaji, walioonewa, wanaoteseka, wasio na kitu, ndiyo kazi yenyewe ambayo kila kanisa linaloamini Ukweli kwa wakati huu linapaswa kuwa likifanya tangu zamani. Yatupasa kuonyesha huruma nyororo ya Msamaria katika kupeana mahitaji ya kimwili, kuwalisha wenye njaa, kuwaleta maskini waliotupwa nje ya nyumba zetu, kukusanya kutoka kwa Mungu kila siku neema na nguvu ambazo zitatuwezesha kufika kwenye vilindi vya wanadamu. huzuni na kuwasaidia wale ambao hawawezi kujisaidia wenyewe. Katika kufanya kazi hii tunayo nafasi nzuri ya kumweka wazi Kristo aliyesulubiwa. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:276.**

Wengi wanashangaa kwa nini maombi yao hayana uhai, imani yao ni dhaifu sana na yenye kuyumba-yumba, cxxxvii uzoefu wao wa Kikristo wenye giza na usio na uhakika. Je! sisi si hatukufunga wanasema, na "kutembea kwa huzuni mbele ya Bwana wa majeshi?" Katika sura ya hamsini na nane ya Isaya (58) Kristo ameonyesha jinsi hali hii ya mambo inaweza kubadilishwa. Anasema: "Je! hii si ndiyo saumu niliyoichagua? Kufungua vifungo vya uovu, na kulegeza kamba za ubaya, na kuwaacha huru walioonewa, na kuvunja kila nira? Je! mwenye njaa, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako, umwonapo

—

mtu aliye uchi, umfunike; wala usijifiche kutoka kwa ndugu/jamaa zako ? Mistari ya 6, 7. Hiki ndicho kichocheo ambacho Kristo ameagiza kwa ajili ya nafsi iliyokata tamaa, yenye mashaka, na inayotetemeka. Hebu wenye huzuni, waendao kwa huzuni mbele za Bwana, wainuke na kumsaidia mtu yule anayehitaji msaada. **— Shuhuda kwa Kanisa 6:266.**

Utukufu wa mbinguni uko katika kuwainua walioanguka, kuwafariji walio na huzuni. Na popote Kristo anapokaa ndani ya mioyo ya wanadamu, atafunuliwa vivyo hivyo. Popote inapotenda, dini ya Kristo itabariki. Popote inapofanya kazi, kuna mwangaza.— **Christ's Object Lessons, 386 . ChS 188.3**

Yule mjane wa Sarepta akamgawia Eliya tonge; na kwa kurudi, maisha yake na ya mtoto wake yalihifadhiwa. Na kwa wote ambao, katika wakati wa majaribu na kutaka, huwapa huruma na usaidizi wengine wenye uhitaji zaidi, Mungu ameahidi baraka kuu. Hajabadilika. Nguvu zake si ndogo sasa kuliko katika siku za Eliya.— Prophets and Kings, 131, 132 . ChS 188.4

Upendo wa Kristo, unaodhihirishwa katika huduma isiyo na ubinafsi, utakuwa na

ufanisi zaidi katika kumrekebisha mtenda mabaya kuliko upanga au mahakama ya haki. Haya ni muhimu ili kutia hofu kwa mvunja sheria, lakini mishonari mwenye upendo anaweza kufanya zaidi ya hili. Mara nyingi moyo ambao unakuwa mgumu chini ya karipio utayeyuka chini ya upendo wa Kristo. — **The Ministry of Healing, p . ChS 189.1**

**Kukumbukwa**

Katika vyama vyetu vyote ikumbukwe kwamba katika uzoefu wa wengine kuna sura zilizofungwa kutoka kwa macho ya kibinadamu. Kwenye kurasa za kumbukumbu kuna historia za kusikitisha ambazo zinalindwa kwa utakatifu kutoka kwa macho ya udadisi. Hapo yanasimama mapigano marefu, magumu na hali ngumu, labda shida katika maisha ya nyumbani, ambayo siku baada ya siku hudhoofisha ujasiri, ujasiri, na imani. Wale wanaopigana vita vya maisha katika hali ngumu sana wanaweza kuimarishwa na kutiwa moyo na uangalifu mdogo unaogharimu tu jitihada ya upendo. Kwa watu kama hao, kushika mkono kwa nguvu na kusaidia kwa rafiki wa kweli kuna thamani zaidi kuliko dhahabu au fedha. Maneno ya wema yanakaribishwa kama tabasamu la malaika. ChS 189.2

Kuna umati wa watu wanaohangaika na umaskini, wanalazimika kufanya kazi kwa bidii kwa ujira mdogo, na wanaoweza kupata lakini mahitaji duni ya maisha. Kazi ngumu na kunyimwa, bila matumaini[cxxxviii] ya mambo bora, hufanya mzigo wao kuwa mzito sana. Wakati maumivu na ugonjwa huongezwa, mzigo ni karibu hauwezekani. Wakiwa wametunzwa na kudhulumiwa, hawajui waelekee wapi kupata nafuu. Wahurumie katika majaribu yao, maumivu yao ya moyo, na kukatishwa tamaa. Hii itakufungulia njia ya kuwasaidia. Zungumza nao juu ya ahadi za Mungu, sali pamoja nao na kwa ajili yao, uwatie moyo na tumaini.— **The Ministry of Healing, p. 158 . ChS 189.3**

Kuna wengi ambao maisha ni mapambano chungu; wanahisi upungufu wao, na wana huzuni na wasioamini; wanafikiri hawana kitu cha kushukuru. Maneno ya fadhili, sura ya huruma, maneno

—

ya shukrani, yangekuwa kwa wengi walio na shida na upweke kama kikombe cha maji baridi kwa nafsi yenye kiu. Neno la huruma, tendo la fadhili, lingeinua mizigo ambayo iko juu ya mabega yaliyochoka. Na kila neno au tendo la fadhili lisilo na ubinafsi ni wonyesho wa upendo wa Kristo kwa wanadamu waliopotea.—**Thoughts From the Mount of Blessing, 23 . ChS 189.4**

**Panua Mkono wa Msaada**

Dhambi ni uovu mkubwa kuliko ubaya wote, na ni juu yetu kumhurumia na kumsaidia mwenye dhambi. Lakini si wote wanaweza kufikiwa kwa njia ile ile. Kuna wengi wanaoficha njaa ya nafsi zao. Hawa wangesaidiwa sana na neno nyororo au ukumbusho mzuri. Kuna wengine walio na uhitaji mkubwa zaidi, lakini hawajui. Hawatambui ufukara wa kutisha wa nafsi. Umati wa watu wamezama katika dhambi hivi kwamba wamepoteza hisia ya uhalisi wa milele, wamepoteza mfano wa Mungu, na ni vigumu kujua kama wana roho za kuokolewa au la. Hawana imani kwa Mungu wala

tumaini kwa mwanadamu. Mengi ya haya yanaweza kufikiwa tu kupitia matendo ya fadhili zisizopendezwa. Mahitaji yao ya kimwili lazima kwanza yashughulikiwe. Ni lazima walishwe, kusafishwa, na kuvikwa kwa adabu. Wanapoona uthibitisho wa upendo wako usio na ubinafsi, itakuwa rahisi kwao kuamini katika upendo wa Kristo. ChS 190.1

Kuna wengi wanaokosea, na wanaona aibu yao na upumbavu wao. Wanaangalia makosa na makosa yao mpaka wanasukumwa karibu na kukata tamaa. Nafsi hizi hatupaswi kuzipuuza. Wakati mtu anapaswa kuogelea dhidi ya mkondo, kuna nguvu zote za mkondo zinazomrudisha nyuma. Hebu mkono wa usaidizi unyooshwe kwake kama ulivyokuwa mkono wa Kaka kwa Petro aliyekuwa akizama. Zungumza naye maneno yenye tumaini ambayo yataimarisha ujasiri na kuamsha upendo.— **Christ's Object Lessons, p . ChS 190.2**

Kwa nafsi iliyochoka kwa maisha ya dhambi, lakini bila kujua ni wapi pa kupata kitulizo, wasilisha Mwokozi mwenye huruma. Kumshika mkono, kumwinua, kuzungumza naye maneno ya ujasiri na matumaini. Msaidie kuushika mkono wa Mwokozi.— **The Ministry of Healing, p. 168 . ChS 190.3**

## Ukarimu Wajibu wa Kikristo

Kazi yetu katika ulimwengu huu ni kuishi kwa faida ya wengine, kubariki wengine, kuwa wakarimu; na mara kwa mara inaweza kuwa kwa usumbufu tu kwamba tunaweza kuwaburudisha wale ambao wanahitaji sana utunzaji wetu na faida ya jamii yetu na majumba yetu. Wengine huepuka mizigo hii ya lazima. Lakini mtu fulani ni lazima aibebe; na kwa sababu ndugu kwa ujumla hawapendi kukaribisha wageni, na hawashiriki kwa usawa katika majukumu haya ya Kikristo, wachache ambao wana mioyo iliyo tayari, na ambao kwa furaha hufanya kesi za wale ambao wanahitaji msaada kuwa yao wenyewe, basi hutingwa na mizigo. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:645.**

"Msisahau kuwakaribisha wageni; kwa maana kwa njia hii

—

wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua." Maneno haya hayajapoteza nguvu zake zozote kupitia kupita kwa wakati. Baba yetu wa mbinguni bado anaendelea kuweka katika njia ya watoto Wake fursa ambazo ni baraka katika kujificha; na wale wanaoboresha fursa hizi hupata shangwe kubwa.— Prophets and Kings, 132 . ChS 191.2

**Mchakato wa Upimaji**

MUNGU hutahini na kututhibitisha kwa matukio ya kawaida ya maisha. Ni vitu vidogo vinavyodhihirisha kurasa za moyo. Ni kwa kutilia makini vilivyo vidogo, matukio madogo mbalimbali,na kujali/wema katika mambo ya kawaida ya maisha, ndiyo ambako huleta jumla ya maisha ya furaha; Na ni kwa kupuuzia kutia moyo, kutoa maneno ya upendo na kujali wengine katika maisha ndiyosababu ya huzuni kubwa. Itafahamika mwishoni kuwa kujikana nafsi kwa wema na furaha ya wale wanaotuzunguka itatengeneza mchango mkubwa wa kumbukumbu mbinguni. **—Shuhuda kwa Kanisa**

**2:133.**

Niliona kuwa ni majaliwa ya Mungu kwamba wajane na yatima, vipofu, viziwi, viwete, na watu wenye matatizo ya namna mbalimbali, wamekuwa wakiwekwa katika uhusiano wa Kikristo ulio wa karibu kwa kanisa Lake; kwa ajili ya kuwathibitisha watu Wake na kuboresha tabia yao ya Kweli. Malaika wa Mungu wanatazama kuona namna tunavyoshughulika na watu hawa ambao wanahitaji huruma yetu, upendo, na ukarimu wa kweli usio na ubinafsi. Hili ni jaribio la Mungu kwa tabia yetu. Kama tunayo dini ya kweli ya Biblia tutahisi kuwiwa kuonesha upendo, utu wema, na ukaribu ni kwa ajili ya Kristo kwa niaba ya ndugu zake; na tunaweza kufanya kwa kiwango kikubwa kuonesha shukrani yetu kwa upendo Wake usiopimika kwetu tulipokuwa wenye dhambi tusiostahili neema Yake, kwa kuonesha ukaribu wa hali ya juu na upendo usio na ubinafsi kwa wale ambao ni ndugu zetu na walio wahitaji zaidi kuliko sisi. **—Shuhuda kwa Kanisa 3:511.**

## Fumbo

Kanuni mbili kubwa za sheria ya Mungu ni upendo mkuu kwa Mungu na upendo usio na ubinafsi kwa jirani zetu. Amri nne za kwanza na zile sita za mwisho zimeshikiliwa kwa, au zinachomoza, kutoka katika kanuni hizi mbili. Kristo alielezea kwa mwanasheria nani aliyekuwa jirani yake katika kielelezo cha mtu ambaye alikuwa anasafiri toka Yerusalemu kwenda Yeriko na kuanguka kati ya wezi na wakamnyang'anya na kumpiga na kumwacha karibu na kufa. Kuhani na mlawi walimwona mtu huyu akiteseka, lakini mioyo yao haikuonesha mwitikio kwa mahitaji yake. Wakamkwepa kwa kupita kando. Msamaria akapita njia ile, na alipoona hitaji la msaada kwa yule msafiri hakuhoji kwamba alikuwa ndugu yake au raia mwenzake au wa imani yake; bali alikwenda kufanya kazi ya kumsaidia aliyekuwa akiteseka kwa sababu kulikuwa na kazi iliyotakiwa kufanywa. Akamhudumia vizuri mno kwa kadiri alivyoweza, akampandisha juu ya punda wake, na kumpeleka katika nyumba ya wageni na kumpatia yaliyokuwa mahitaji ya yule mtu kwa gharama yake mwenyewe. Yesu

akasema, msamaria huyu, alikuwa jirani kwa yule aliyeanguka katikati ya wanyang'anyi. Mlawi na kuhani wanawakilisha tabaka katika kanisa ambalo linaonesha kutojali kwa wale wanaohitaji huruma na msaada toka kwao. Hili tabaka pasipo kujali wadhifa wao katika kanisa, ni wavunjaji wa amri. Msamaria anawakilisha tabaka ambalo ni wakarimu wa Kweli pamoja na Kristo na wanaoiga mfano Wake katika kutenda mema. **—Shuhuda kwa Kanisa 3:511-513.**

## SURA YA 18

## MKUTANO YA MAKAMBI MSAADA KATIKA HUDUMA YA KIKRISTO

### Umuhimu

Mkutano wa kambi ni mojawapo ya mawakala muhimu katika kazi yetu. Ni mojawapo ya mbinu bora zaidi za kukamata usikivu wa watu. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:31.**

Katika kazi yetu tumeshangazwa kujua jinsi ya kuvunja vizuizi vya ulimwengu na ubaguzi, na kuleta mbele ya watu Ukweli wa thamani ambao una maana kubwa sana kwao. Bwana ametuagiza kwamba mkutano wa kambi ni mojawapo ya nyenzo muhimu kwa ajili ya kukamilisha kazi hii. **— Shuhuda kwa Kanisa 6:31, 32.**

### Lengo

Ni nini lengo la kukusanyika pamoja? Je! Ni kumfahamisha Mungu, kumuelekeza kwa kumwambia yote tuyajuayo kwa maombi? Tunakutana pamoja ili kujengana na kubadilishana mawazo na hisia, kukusanya nguvu, nuru, na ujasiri kwa kufahamishana na wengine matumaini na matamanio; na kwa sala zetu za dhati za kutoka moyoni, zinazotolewa kwa imani, tunapata kiburudisho na nguvu kutoka kwa chanzo cha nguvu zetu. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:578.**



Na mikutano yetu ya kambi ina kitu kingine, matayarisho kwa hili. Wanapaswa kukuza maisha ya kiroho kati ya watu wetu wenyewe. Ulimwengu kwa hekima yake haumjui Mungu. Ulimwengu hauwezi kuona uzuri, uzuri, wema, utakatifu wa Ukweli wa mbingu. Na ili watu waweze kuelewa hili, lazima kuwe na njia ambayo itakuja ulimwenguni. Kanisa limeundwa njia hiyo. Kristo anajidhihirisha kwetu ili tupate kumdhihirisha kwa wengine. Kupitia kwa watu Wake inapasa kudhihirishwa utajiri na utukufu wa kipawa Chake kisichoneneka. Mungu amekabidhi mikononi mwetu kazi takatifu zaidi, na tunahitaji kukutana pamoja ili

—

kupokea mafundisho, ili tuweze kufaa kufanya kazi hii. Tunahitaji kuelewa ni sehemu gani ambayo sisi binafsi tutaitwa kutenda katika kuijenga kazi ya Mungu duniani, katika kutetea sheria takatifu ya Mungu (Amri Kumi), na kumwinua Mwokozi kama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." Yohana 1:29. Tunahitaji kukutana pamoja na kupokea mguso wa Bwana, ili tuweze kuelewa kazi yetu nyumbani. —Shuhuda kwa Kanisa 6:32, 33.

Ukiendeshwa vizuri, mkutano wa makambi ni shule ambapo wachungaji, wazee, na mashemasi wanaweza kujifunza kufanya kazi kamilifu zaidi kwa ajili ya Bwana. Inapaswa kuwa shule ambapo washiriki wa kanisa, wazee kwa vijana, wanapewa nafasi ya kujifunza njia ya Bwana kwa ukamilifu zaidi, mahali ambapo waumini wanaweza kupata elimu ambayo itawasaidia kuwasaidia wengine. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:49.**

Kuhusianisha na mikutano yetu ya makambi katika miaka iliyopita, watumishi wa Mungu wameboresha fursa nyingi za thamani za kuwafundisha watu wetu kwa mbinu

za vitendo za kuwasilisha Kweli zinazookoa za ujumbe wa malaika wa tatu kwa marafiki zao na wale wanaokutana nao. Wengi wamefundishwa jinsi ya kufanya kazi kama wamishionari wanaojitegemeza katika jumuiya zao za nyumbani. Wengi wamerudi nyumbani kutoka kwenye hii mikusanyiko ya mwaka na kufanya kazi kwa bidii na akili zaidi kuliko hapo awali. Ingempendeza Mungu ikiwa zaidi ya mafundisho haya ya vitendo yangetolewa kwa washiriki wa kanisa ambao huhudhuria mikutano ya makambi yetu, kuliko mara zote ilivyotolewa katika miaka iliyopita. Wafanyakazi wetu kwa ujumla na kaka na akina dada zetu katika kila konferensi wanapaswa kukumbuka kwamba mojawapo ya malengo ya mikusanyiko yetu ya kila mwaka ni kwamba wote wapate ujuzi wa mbinu za vitendo za kazi ya binafsi ya umishionari. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:81**.

Katika baadhi ya konferensi zetu viongozi wamesita kuzitambulisha mbinu hizi za maelekezo ya kiutendaji. Wengine kwa asili wana mwelekeo wa kuhubiri badala ya kufundisha. Lakini kwenye hafla kama za mikutano yetu ya makambi ya kila mwaka hatupaswi kamwe kupoteza fursa ya kuwafundisha waumini jinsi ya kufanya kazi ya umishonari kwa vitendo mahali watakapoweza kuishi. —**Shuhuda kwa Kanisa 9:82.**

### Ufafanuzi wa Kivitendo wa Mbinu za Kimisionari

Kwa kushiriki katika kazi katika mkutano wa makambi, wote wanaweza kuwa wanajifunza jinsi ya kufanya kazi kwa mafanikio katika makanisa yao ya nyumbani. — **Shuhuda kwa Kanisa 6:4 9.**



Katika baadhi ya mikutano yetu ya kambi mashirika yenye nguvu ya wafanyakazi yamepangwa waende jijini na viunga vyake ili kugawanya machapisho na kuwaalika watu kwenye mikutano. Kwa njia hii mamia ya watu walipatikana kuwa wahudhuriaji katika nusu ya mwisho ya mkutano ambao vinginevyo hawakuwa na wazo hata kidogo kulihusu. —**Shuhuda kwa Kanisa 6:36.**

Kisha tunaweza kwenda kwenye mkutano wa makambi si

kupokea tu, bali kutoa. Kila mtu ambaye ni mshiriki wa upendo wa msamaha wa Kristo, kila mtu ambaye ametiwa nuru na Roho wa Mungu na kuongoka kwenye Ukweli, atahisi kwamba kwa ajili ya baraka hizi za thamani ana deni kwa kila nafsi ambayo anakutana nayo. Wale walio wanyenyekevu moyoni Bwana atawatumia kufikia roho ambazo wahudumu waliowekwa rasmi hawawezi kuzikaribia. Watasukumwa kunena maneno ambayo yanafunua neema ya wokovu ya Kristo. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:43.**

Tunapofuata mipango inayotokana na Bwana "sisi ni watenda kazi pamoja na Mungu." Vyovyote nafasi yetu ilivyo,-- iwe wanyeviti/marais wa konferensi, watumishi, walimu,wanafunzi, au washiriki wa kawaida,--tunawajibishwa na Bwana kwa kufanyia kazi kikamilifu fursa za kuwaangazia wale wanaohitaji Ukweli wa sasa. Na moja ya wakala mkuu aliyemtakasa kwa matumizi yetu ni kurasa zilizochapishwa. Katika shule zetu na sanitariamu, katika makanisa yetu ya nyumbani/mahalia, na hasa katika mikutano yetu ya kila mwaka ya makambi, lazima tujifunze kutumia kwa busara wakala

huyu wa thamani. Kwa bidii ya uvumilivu,watendakazi waliochaguliwa lazima wawaelekeze watu wetu jinsi ya kuwaendea wasioamini katika kwa ukarimu, njia ya ushindi na jinsi ya kuweka mikononi mwao maandishi ambayo Ukweli wa sasa umo ukiwa umetolewa kwa uwazi na nguvu. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:86, 87.**

Kazi katika mikutano yetu ya kambi inapaswa kuendeshwa, si kulingana na usanifu wa mwanadamu, bali kufuatisha namna ya utendaji kazi wa Kristo. Washiriki wa kanisa wanapaswa kuvutwa kufanya kazi. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:120.**

**Sifa Pekee ya Mikutano ya Makambi Kukaribia Mwisho wa Wakati**

Nimeonyeshwa kuwa mikutano yetu ya makambi ni ya kuongeza hamu na mafanikio. Tunapokaribia mwisho, nimeona kwamba katika mikutano hii kutakuwa na kuhubiri kidogo na kujifunza Biblia zaidi. Kutakuwa na vikundi vidogo vidogo duniani kote vikiwa na Biblia zao mikononi mwao, na vikundi mbalimbali vinavyoongoza katika mafunzo ya huru kutoka katika mazungumzo ya Maandiko. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:87.**

**Hasara Kubwa ya Kubakia Mbali**

Mikutano yetu ya kambi hupangwa na hufanyika kwa gharama kubwa. Watendakazi wa Mungu wanaotetea Ukweli usiopendwa, wanafanyakazi kupita kiasi kwenye mikusanyiko hii mikubwa ili kubeba ujumbe wa rehema kutoka kwa Mkombozi aliyesulubiwa kwa wenye dhambi maskini walioanguka. Kupuuza au kutendea ujumbe huu bila kujali ni kupuuza huruma ya Mungu na sauti Yake ya onyo na kusihi. Kukosekana kwako kwenye mikutano hii kumeathiri sana ustawi wako wa kiroho. Umekosa nguvu ambayo ungeweza kupata hapo kwa kusikiliza Neno la Mungu linalohubiriwa, na kujichanganya na waumini wa Ukweli. **—Shuhuda kwa Kanisa 4:115.**

—

Si jambo dogo kwa familia kusimama kama wawakilishi wa Yesu, wakishika sheria ya Mungu katika jamii isiyoamini. Tunatakiwa kuwa nyaraka hai zinazojulikana na kusomwa na watu wote. Msimamo huu unajumuisha majukumu ya kutisha. Ili kuishi katika nuru, lazima uje mahali nuru inang'aa. Ndugu K, kwa dhabihu yoyote ile, anapaswa kuhisi kuwa chini ya wajibu wa heshima wa kuhudhuria, pamoja na familia yake, angalau mikusanyiko ya kila mwaka ya wale wanaopenda Ukweli. Ingemtia nguvu yeye na wao, na kuwafaa kwa majaribio na wajibu. Sio vizuri kwao kupoteza fursa ya kushirikiana na wale wa imani sawa; kwani Ukweli hupoteza umuhimu wake katika akili zao, mioyo yao huacha kuangazwa na kuhuishwa na ushawishi wake wa kutakasa, na hupoteza hali ya kiroho. Hawajatiwi nguvu na Maneno ya mhubiri aliye hai. Mawazo ya kidunia na biashara za ulimwengu zinaendelea kutumia akili zao kuwatenga na masomo ya kiroho. **— Shuhuda kwa Kanisa 4:106.**

Hebu wale wote wanaoweza, wahudhurie mikutano hii ya kila mwaka. Wote wanapaswa kuhisi kuwa Mungu anataka hili kwao. Ikiwa hawatachangamkia upendeleo ambao

ameutoa ili kwamba wawe imara ndani na nguvu ya neema Yake, watadhoofika na kudhoofika zaidi, na watapunguka na kupunguka zaidi shauku yao yote ya kujiwekwa wakfu kwa Mungu. Njooni Ndugu na Dada kwenye mikutano hii mitakatifu ili kumtafuta Yesu. Atakuja kwenye sikukuu. Atakuwepo na atafanya kwa ajili yako yale yote ambayo unataka kuyafanywa. Mashamba yako hayapaswi kuzingatiwa kwa uthamani mkubwa kuliko maslahi ya roho. Hazina zote ulizo nazo, ziwe za thamani kiasi gani hazitaweza kukununulia amani na matumaini, ambayo itakuwa faida isiyo na kikomo, ikiwa itakugharimu yote uliyonayo na taabu na mateso ya maisha. Hisia imara ya mambo ya umilele na moyo ulio tayari kutoa vyote kwa Kristo ni baraka za thamani zaidi kuliko utajiri na raha zote na utukufu wa ulimwengu huu. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:575, 576.**



## Chapter 19—NYUMBANI ENEO LA KIGENIThe Home-Foreign Field Kazi Iliyo Sawa kwa Umuhinu na

—

**Ile Katika Maeneo ya Kigeni**

Amkeni, amkeni, ndugu na dada zangu, na muingie katika maeneo huko Marekani yale ambayo hayajawahi kufanyiwa kazi. Baada ya kutoa kitu kwa ajili ya maeneo ya ugenini, usifikiri kuwa wajibu wako umekwisha. Kuna kazi ya kufanywa katika maeneo ya ugenini, lakini kuna kazi ya kufanywa ndani ya Marekani ambayo pia ni muhimu sana. Katika miji ya Marekani kuna watu karibu wa kila lugha. Hawa wanahitaji nuru ambayo Mungu ameitoa kwa kanisa Lake. —Shuhuda kwa Kanisa 8:36.

Wakati mipango inafanywa ya kuwaonya wakazi wa mataifa mbalimbali katika nchi za mbali, mengi lazima yafanywe kwa niaba ya wageni waliofika kwenye fukwe za nchi yetu wenyewe. Roho zilizo China hazina thamani zaidi kuliko roho zilizo ndani ya uvuli wa milango yetu. Watu wa Mungu wanapaswa kufanya kazi kwa uaminifu katika nchi za mbali, kadiri usimamizi wake unavyoweza kufungua njia; nao pia wanapaswa kutimiza wajibu wao kuelekea wageni wa mataifa mbalimbali katika majiji na vijiji na wilaya za maeneo yaliyo karibu.— **The Review and Herald, Julai 25, 1918 ( The Review and Herald, Oktoba 29, 1914 ). ChS 199.2**

Katika Jiji la New York, Chicago, na katika vituo vingine vikuu vya idadi ya watu, kuna sehemu kubwa zaidi ya kigeni—makundi ya mataifa mbalimbali, na yote hayajaonywa. Miongoni mwa Waadventista Wasabato kuna bidii kubwa—na sisemi kwamba kuna mengi sana—ya kufanya kazi katika nchi za kigeni; lakini ingempendeza Mungu ikiwa bidii ifaayo ingeonyeshwa kufanya kazi katika miji iliyo karibu. Watu wake wanahitaji kusonga kwa busara. Wanahitaji kuanzisha kazi hii katika miji kwa bidii kubwa. Watu waliowekwa wakfu na wenye talanta wanapaswa kutumwa katika miji hii na kuanza kufanya kazi. Madarasa mengi ya Watenda kazi yanapaswa kuungana katika kufanya jitihada hizi za kuwaonya watu.— **The Review and Herald, Julai 25, 1918 ( The Review and Herald, Oktoba 29, 1914 ). ChS 199.3**

**Fursa ya Kimbingu Ilyotumwa**

Katika nchi yetu wenyewe kuna maelfu ya mataifa yote, na lugha, na watu wajinga na washirikina, wasio na ujuzi wa Biblia au mafundisho yake matakatifu. Mkono wa Mungu ulikuwa katika kuja kwao Amerika, ili waweze kuletwa chini ya ushawishi wenye nuru wa ile kweli iliyofunuliwa katika Neno Lake, na kuwa washiriki wa imani Yake yenye kuokoa.— **The Review and Herald, Machi 1, 1887 . ChS 200.1**

Mungu katika uangalizi Wake amewaleta watu kwenye malango yetu, na kuwasukuma, kana kwamba, mikononi mwetu, ili wapate kujifunza kweli, na kustahili kufanya kazi ambayo hatukuweza kufanya katika kupata nuru kwa watu wa lugha nyingine. **— The Review and Herald, Julai 25, 1918 ( The Review and Herald, Oktoba 29, 1914 ). ChS 200.2**

Wengi wa wageni hawa wako hapa katika uangalizi wa Mungu, ili wapate nafasi ya kuisikia kweli kwa wakati huu, na kupokea matayarisho yatakayowafaa kurejea katika nchi zao wenyewe wakiwa wabeba wa nuru ya thamani inayoangaza moja kwa moja kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu. **— Pacific Union Recorder, Aprili 21, 1910 ( North Pacific Union Gleaner,**

—

Aprili 13, 1910 ). ChS 200.3

Manufaa makubwa yangekuja kwa ajili ya kazi ya Mungu katika maeneo ya mbali, ikiwa jitihada za uaminifu zingefanywa kwa ajili ya wageni katika miji ya nchi yetu. Miongoni mwa wanaume na wanawake hao kuna baadhi ya watu ambao, baada ya kuukubali ukweli, hivi karibuni wangeweza kufaa kufanya kazi kwa ajili ya watu wao wenyewe katika nchi hii na katika nchi nyinginezo. Huenda wengi wakarudi mahali walipotoka, wakiwa na tumaini la kupata marafiki wao kwenye kweli. Wangeweza kuwatafuta watu wa jamaa zao na majirani, na kuwajulisha maarifa wa ujumbe wa malaika wa tatu.— The Review and Herald, Oktoba 29, 1914 . ChS 200.4

**Upuuziaji wa Kivivu**

Kumekuwa na upuuziaji wa kivivu na kutokuamini kwa uhalifu miongoni mwetu kama watu, jambo ambalo limetuzuia tusifanye kazi ambayo Mungu ametuachia tuifanye

katika kuruhusu nuru yetu iangaze kwa mataifa mengine.— **Life Sketches, p . ChS 200.5**

Nimeonyeshwa kwamba, kama watu, tumekuwa tukilala usingizi kuhusu wajibu wetu kuhusu kupeleka nuru mbele ya mataifa mengine.— **Life Sketches, p. 212 . ChS 200.6**

Hatuendi sambamba na uangalizi ulio wazi wa Mungu. Yesu na malaika wako kazini. Kzi hii inaendelea, huku tukiwa tumesimama tuli na kuachwa nyuma. Ikiwa tungefuata uangalizi ulio wazi wa Mungu, tunapaswa kuwa wepesi kutambua kila fursa, na kutumia vyema kila manufaa tunayoweza kufikia, kuruhusu nuru ipanuke na kuenea kwa mataifa mengine.— **Life Sketches, 212, 213 . ChS 201.1**

**Strengthen the Hands of the Workers**

Mungu angependezwa kuona mengi zaidi yakitimizwa na watu Wake katika uwasilishaji wa ukweli kwa wakati huu kwa wageni wa Amerika, kuliko ambavyo imefanywa huko nyuma. Hebu tuimarishe mikono ya Mzee Olsen [Mzee OA Olsen wakati huo alikuwa katibu mkuu wa Idara ya Mambo ya Nje ya Amerika Kaskazini ya Koferensi Kuu.] na wasaidizi wake katika kazi. Hebu tusiwaruhusu kuhangaika peke yao, wakiwa na posho kidogo tu kwa ajili ya mateso ya kazi yao kubwa.— **The Review and Herald, Oktoba 29, 1914 . ChS 201.2**



Mzee Olsen alituambia pia kuhusu mwanzo wenye kutia moyo miongoni mwa Waitalia,
Waserbia, Warumi, Warusi, na mataifa mengine kadhaa. Tunafurahi pamoja naye katika yote ambayo yamefanywa, na bado mioyo yetu ilihuzunishwa na ufahamu kwamba mengi ambayo yangeweza kufanywa yameachwa bila kutekelezwa kwa sababu ya ukosefu wa mbinu. Tunatumai kwamba mkutano maalum ... unaofanywa katika makanisa yetu yote huko Amerika, utawawezesha ndugu zetu walio na idara hii inayosimamia kufanya kazi ya ujasiri zaidi katika miji mikubwa ya nchi. Hivyo wengi waweza kuvutwa kwenye safu zetu, na kutoka miongoni

—

mwa hao waweza kuwa watenda kazi waliositawi wanaoweza kutangaza ujumbe kwa wale wa taifa lao wenyewe katika nchi yetu wenyewe na katika mataifa mengine ya dunia.— **The Review and Herald, Oktoba 29, 1914 . ChS 201.3**

## SURA YA 20 — KUWAFIKIA MATAJIRI NA WATU MAARUFU Reaching The Wealthy And Influential

### Wasipuuzwe

Kuna kazi ya kufanya kwa matajiri. Wanahitaji kuamshwa kwa wajibu wao kama wale waliokabidhiwa karama za mbinguni. Wanahitaji kukumbushwa kwamba lazima watoe hesabu kwa Yeye ambaye atawahukumu walio hai na wafu. Tajiri anahitaji kazi yako katika upendo na hofu ya Mungu. Mara nyingi sana anaamini katika utajiri wake, na

hahisi hatari yake. Macho ya akili yake yanahitaji kuvutiwa na mambo yenye thamani ya kudumu.— **Christ’s Object Lessons, p . ChS 202.1**

Wale wanaosimama juu duniani kwa ajili ya elimu, mali, au wito wao, ni nadra sana kushughulikiwa kibinafsi kuhusiana na masilahi ya nafsi. Watenda kazi wengi Wakristo wanasitasita kukaribia matabaka haya. Lakini hii haipaswi kuwa. Ikiwa mtu angezama, tusingesimama karibu na kumwona akiangamia kwa sababu alikuwa wakili, mfanyabiashara, au hakimu. Ikiwa tungeona watu wakikimbia juu ya mteremko, tusingesita kuwahimiza warudi, haijalishi nafasi au wito wao. Wala tusisite kuwaonya watu juu ya hatari ya nafsi. Hakuna hata mmoja anayepaswa kupuuzwa kwa sababu ya ujitoaji wao unaoonekana kwa mambo ya kiulimwengu.— **Christ's Object Lessons, 230, 231 . ChS 202.2**

Tunapaswa kuwa na taabu ya nafsi kwa ajili ya wale walio mahali pa juu; tunapaswa kuwatolea mwaliko wenye fadhili wa kuja kwenye karamu ya ndoa.— **The Southern Watchman, Machi 15, 1904 . ChS 202.3**

Bwana anahitaji kwamba watu wenye pesa waongoke na kutenda kama msaada Wake katika kuwafikia wengine. Anatamani kwamba wale wanaoweza kusaidia katika kazi ya matengenezo na urejeshaji waione nuru iliyo ya thamani ya Ukweli na kugeuzwa tabia na kuongozwa kutumia mali zao walizokabidhiwa katika utumishi Wake. Bwana huwataka wawekeze mali alizowaazima, katika kutenda mema, katika kufungua njia kwa ajili ya injili kuhubiriwa kwa watu wa tabaka zote za karibu na za mbali. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:114.**



Wale walio wa vyeo vya juu zaidi vya jamii wanapaswa kutafutwa kwa shauku kubwa na heshima ya kindugu. Watu katika maisha ya biashara, katika nyadhifa za juu za uaminifu, watu walio na uwezo mkubwa wa uvumbuzi na ufahamu wa kisayansi, watu mahiri,

—

waalimu wa injili ambao akili zao hazijaitwa kwenye kweli maalum kwa wakati huu, - hawa wanapaswa kuwa wa kwanza kusikia wito. Kwao mwaliko lazima utolewe.— **Christ's Object Lessons, p. 230 . ChS 203.1**

Makosa yamefanywa kwa kutotafuta kuwafikia wachungaji/wahudumu na watu wa tabaka za juu na Ukweli. Watu wasio wa imani yetu wameepukwa sana. Ingawa hatupaswi kushirikiana nao ili kupokea msaada wao, kuna watu wanyoofu kila mahali ambao tunapaswa kuwafanyia kazi kwa uangalifu, kwa hekima, na kwa akili, waliojawa na upendo kwa nafsi zao. Mfuko unapaswa kuanzishwa ili kuelimisha wanaume na wanawake kufanya kazi kwa matabaka haya ya juu, hapa na katika nchi zingine. **— Shuhuda kwa Kanisa 5:580, 581.**

**Sifa Maalum za Watenda kazi**

Baadhi wanafaa hasa kufanya kazi kwa matabaka ya juu. Hawa wanapaswa kutafuta hekima kutoka kwa Mungu ili kujua jinsi ya kuwafikia watu hawa, wasiwe na maarifa ya kawaida tu, bali kwa juhudi binafsi na imani iliyo hai ili kuwaamsha wapate mahitaji ya

nafsi, ili kuwaongoza kwenye maarifa ya ukweli kama ilivyo katika Yesu.— **Ministry of Healing, 213 . ChS 203.3**

Hebu wale wanaofanya kazi kwa matabaka ya juu wajitwike wenyewe heshima ya kweli, wakikumbuka kuwa malaika ni wenzao. Hebu waweke hazina ya akili na moyo iliyojaa, “Imeandikwa.”— **The Ministry of Healing, 215 . ChS 203.4**

Katika kila juhudi ili kufikia tabaka ya juu, mtenda kazi wa Mungu anahitaji imani yenye nguvu. Mionekano inaweza kuonekana kuzuia; lakini katika saa yenye giza kuu kuna nuru juu.— **The Acts of the Apostles, 242 . ChS 203.5**

Mungu anawaita watenda kazi waaminifu, wanyenyekevu, ambao wataipeleka injili kwenye tabaka za juu zaidi.— **The Acts of the Apostles, 140 . ChS 203.6**

**Matokeo Yamehakikishwa**

Kuna miujiza ya kufanywa katika wongofu wa kweli,—miujiza ambayo sasa haitambuliki. Watu wakuu wa dunia hii hawako nje ya uwezo wa Mungu wa ajabu. Ikiwa wale ambao ni watenda kazi pamoja Naye watakuwa watu wa fursa, wanaofanya wajibu wao kwa ujasiri na uaminifu, Mungu atawaongoa watu wanaochukua nafasi za kuwajibika, watu wenye akili na ushawishi. Kupitia nguvu za Roho Mtakatifu wengi
watakubali kanuni za k im ungu. Wakiongolewa kupitia ukweli, watakuwa wakala

mkononi mwa Mungu ili kuwasilisha nuru. Watakuwa na mzigo maalum kwa nafsi nyingine za tabaka hili lililopuuzwa. Muda na pesa vitawekwa ~~wak~~fu kwa kazi ya Bwana, na ufanisi mpya na nguvu zitaongezwa kwa kanisa.— **The Acts of the Apostles, 140 . ChS 204.1**

Wengi walio katika nafasi za juu za kijamii wana uchungu wa moyo, na wagonjwa wa ubatili. Wanatamani amani ambayo hawana. Katika safu za juu kabisa za jamii kuna wale ambao wana njaa na kiu ya wokovu. Wengi wangepokea msaada ikiwa watenda kazi wa Bwana wangewafikia binafsi, kwa njia ya fadhili, moyo

—

uliofanywa mwororo na upendo wa Kristo.— **Christ's Object Lessons, p . ChS 204.2**

Wengi wa wasomi wakubwa na wakuu wa serikali, watu mashuhuri zaidi ulimwenguni, katika siku hizi za mwisho watageuka kutoka kwenye nuru, kwa maana ulimwengu kwa hekima haumjui Mungu. Hata hivyo, watumishi wa Mungu wanapaswa kuboresha kila fursa ya kuwajulisha watu hao kweli. Wengine watakiri kutojua kwao mambo ya Mungu, na watachukua mahali pao wakiwa wanafunzi wanyenyekevu miguuni pa Yesu, Mwalimu Mkuu.— **The Acts of the Apostles, 241-242 . ChS 204.3**

## Watu Matajiri wa Nyakati za Biblia

Mwethiopia huyo alikuwa mtu wa cheo kizuri na mwenye ushawishi mkubwa. Mungu aliona kwamba wakati wa kuongoka, angewapa wengine nuru aliyopokea, na angetumia ushawishi mkubwa katika kupendelea injili. Malaika wa Mungu walikuwa wakimfikia

mtafutaji huyu wa nuru, na alikuwa akivutwa kwa Mwokozi. Kwa huduma ya Roho Mtakatifu, Bwana alimleta kwenye uhusiano na mtu ambaye angeweza kumwongoza kwenye nuru.— **The Acts of the Apostles, p . ChS 204.4**

Wakati Wayahudi walipokuwa wakijaribu kuliangamiza kanisa hilo changa, Nikodemo alikuja mbele katika utetezi wake. Akiwa hana tahadhari tena na kuuliza maswali, alihimiza imani ya wanafunzi, na alitumia mali yake kusaidia kutegemeza kanisa la Yerusalemu na katika kuendeleza kazi ya injili. Wale ambao katika siku nyingine walikuwa wamemheshimu, sasa walimdharau na kumtesa; na akawa masikini katika mali ya dunia; lakini hakusitasita katika kulinda imani yake.— **The Acts of the Apostles, 105 . ChS 205.1**

## SURA YA 21 NYUMBA KITUO CHA MAFUNZO YA KIMISIONARI

### Yenye Umuhimu wa Kwanza

Nyumba ndiyo shule ya kwanza ya mtoto, na ni hapa ambapo msingi unapaswa kuwekwa kwa ajili ya maisha ya utumishi.— **The Ministry of Healing, 400 . ChS 206.1**

Biashara/shuguli kubwa na ya kwanza ya maisha yako ni kuwa mmishonari nyumbani.
**—Shuhuda kwa Kanisa 4:138.**



Urejeshwaji na kuinuliwa kwa ubinadamu huanzia nyumbani. Kazi ya wazazi ni msingi wa kila mmoja.... Ustawi wa jamii, mafanikio ya kanisa, ustawi wa taifa hutegemea ushawishi wa nyumbani.— **The Ministry of Healing, 349 . ChS 206.3**

Kadiri roho ya huduma ya kweli inavyoenea nyumbani ndivyo itakavyokuzwa kikamilifu katika maisha ya watoto. Watajifunza kupata shangwe katika utumishi na kujitolea kwa manufaa ya wengine.— **The Ministry of Healing, p. 401 . ChS 206.4**

—

Hebu wazazi wasisahau kazi kubwa ya utume ilio mbele yao nyumbani. Kwa kila mama kumekabidhiwa jukumu takatifu kutoka kwa Mungu kwa ajili ya watoto. "Mchukue mwana huyu, na binti huyu," Mungu asema, "na umfundishe kwa ajili Yangu. Mpatie tabia iliyotengenezwa kwa mfano wa ikulu, ili ipate kung'aa katika nyua za Bwana milele." Nuru na utukufu unaong'aa kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu huwa juu ya mama mwaminifu anapojaribu kuwaelimisha watoto Wake ili kupinga mivuto ya uovu.
**—Shuhuda kwa Kanisa 9:37.**

Kazi yetu kwa Kristo ni kuanza na familia nyumbani. Elimu ya vijana inapaswa kuwa ya utaratibu tofauti na ile iliyowahi kutolewa huko nyuma. Maslahi yao yanadai kazi nyingi zaidi kuliko walizopewa. Hakuna eneo la umishonari lililo muhimu kuliko hili. Kwa kanuni na mfano wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao kufanya kazi kwa ajili ya wale ambao hawajaongoka. Watoto wanapaswa kuelimishwa ili waweze

kuwahurumia wazee na wanaoteseka na watatafuta kupunguza mateso ya maskini na wenye dhiki. Wafundishwe kuwa na bidii katika kazi ya umishonari; na tangu miaka yao ya kwanza kujinyima na kujitolea kwa ajili ya mema ya wengine na kuendeleza kazi ya Kristo kunapaswa kufundishwa, ili wawe watenda kazi pamoja na Mungu. Lakini wakijifunza kufanya kazi ya Kweli ya umishonari kwa ajili ya wengine, lazima kwanza wajifunze kufanya kazi kwa ajili ya wale walio nyumbani, ambao wana haki ya asili katika ofisi zao za upendo. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:429.**

Ni lazima kaya zetu ziwe na utaratibu, na jitihada za bidii lazima zifanywe ili kuvutia kila mshiriki wa familia katika shughuli za umisionari. Ni lazima tutafute kuhusisha huruma za watoto wetu katika kazi ya bidii kwa ajili ya wale ambao hawajaokolewa, ili wafanye yote wawezayo nyakati zote na mahali pote kumwakilisha Kristo.— **The Review and Herald, Julai 4, 1893 . ChS 207.1**

## Kumbukumbu za Malaika

Wanaume waliooa wakiingia kazini, wakiwaacha wake zao wawatunze watoto nyumbani, mke na mama anafanya kazi kubwa na muhimu kikamilifu kama afanyavyo mume na baba. Ingawa mmoja yuko katika shamba la umishonari, yule mwingine ni mmishonari wa nyumbani, ambaye mahangaiko na masumbuko na mizigo yake mara nyingi huwa mikubwa kupita ile ya mume na baba. Kazi yake ni ya taadhima na muhimu—kufinyanga akili na kutengeneza tabia za watoto wake, kuwafunza kwa manufaa hapa na kuwafaa kwa maisha yajayo, yasiyoweza kufa. Mume katika eneo la wazi la umisionari anaweza kupokea pongezi na heshima za watu, huku mfanyakazi wa nyumbani asipate sifa ya kidunia kwa ajili ya kazi yake. Lakini ikiwa anafanya kazi kwa manufaa ya familia yake, akitafuta kuwatengenezea tabia zao kwa Kielelezo kitakatifu, malaika anayerekodi huandika jina lake kama mmoja wa wamisionari wakuu zaidi ulimwenguni. Mungu haoni mambo kama vile maono yenye ukomo ya mwanadamu

—

yanavyoona. —**Shuhuda kwa Kanisa 5:594.**

## Watoto Kushiriki Mizigo ya Kiroho na Kimwili

Wote wanaweza kufanya kitu. Katika kujaribu kujiwekea udhuru, wengine wanasema: “Majukumu yangu ya nyumbani, watoto wangu, wanadai muda wangu na mali yangu.” Wazazi, watoto wako wanapaswa kuwa mkono wako wa kusaidia, wakiongeza nguvu na uwezo wako wa kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Watoto ni washiriki wachanga wa familia ya Bwana. Wanapaswa kuongozwa kujiweka wakfu kwa Mungu, ambaye wao ni Wake kwa uumbaji na kwa ukombozi. Wanapaswa kufundishwa kwamba nguvu zao zote za mwili, akili, na roho ni Zake. Wanapaswa kufundishwa kusaidia kwa njia mbalimbali za huduma isiyo na ubinafsi. Usiruhusu watoto wako kuwa vizuizi. Pamoja nawe watoto wanapaswa kushiriki mizigo ya kiroho na ya kimwili. Kwa kuwasaidia wengine wanaongeza furaha yao na manufaa yao binafsi. — **Shuhuda kwa Kanisa 7:63.**

## Mvuto wa Nyumba Unaofika Mbali

Familia ya Kikristo yenye utaratibu mzuri ni hoja yenye nguvu inayounga mkono ukweli wa dini ya Kikristo, hoja ambayo kafiri hawezi kuipinga. Wote wanaweza kuona kwamba kuna ushawishi unaofanya kazi katika familia unaoathiri watoto, na kwamba Mungu wa Abrahamu yuko pamoja nao. Ikiwa nyumba za wanaodai kuwa Wakristo zingekuwa na utii unaofaa wa kidini, zingetokeza uvutano mkubwa kwa ajili ya wema. Kwa hakika wangekuwa “nuru ya ulimwengu.”— Patriarchs and Prophets, 144 . ChS 208.1

Utume wa nyumba huenea zaidi ya wanachama wake wenyewe. Nyumba ya Kikristo inapaswa kuwa somo halisi, kwa ajili ya kuonyesha ubora wa kanuni za kweli za maisha. Mfano kama huo utakuwa na nguvu kwa ulimwengu. Nguvu zaidi kuliko mahubiri yoyote yanayoweza kuhubiriwa ni mvuto wa makao ya kweli juu ya mioyo na maisha ya wanadamu. Vijana wanapotoka katika nyumba kama hiyo, mambo ambayo wamejifunza yanatolewa. Kanuni bora za maisha huletwa katika kaya nyingine, na ushawishi unaoinua hufanya kazi katika jamii.— **The Ministry of Healing, p. 352 . ChS 208.2**

Ushahidi mkubwa zaidi wa nguvu ya Ukristo unaoweza kuwasilishwa kwa ulimwengu ni familia iliyo na utaratibu mzuri na yenye nidhamu. Hili litautetea Ukweli kuliko kitu kingine kiwezavyo kufanya, kwa kuwa ni shahidi hai mwenye nguvu ya vitendo juu ya moyo. **—Shuhuda kwa Kanisa 4:304.**

Mungu anapanga kwamba familia za dunia zitakuwa mfano/uwakilishi wa familia ya mbinguni. Nyumba za Kikristo, zilizoanzishwa na kuendeshwa kwa mujibu wa mpango wa Mungu, ni miongoni mwa wakala Wake wenye ufanisi zaidi kwa ajili ya malezi ya tabia ya Kikristo na kwa ajili ya kuendeleza kazi Yake. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:430.** Nyanja yetu ya ushawishi inaweza kuonekana kuwa finyu, uwezo wetu ni mdogo, fursa zetu chache, upatikanaji wetu mdogo; bado uwezekano wa ajabu ni wetu kupitia utumiaji sahihi ya fursa za nyumba zetu wenyewe. Ikiwa

—

tutafungua mioyo na nyumba zetu kwa kanuni takatifu za maisha, tutakuwa mikondo ya mikondo ya nguvu za uzima. Kutoka kwa nyumba zetu kutatiririka vijito vya uponyaji, kuleta uhai, na uzuri, na kuzaa matunda ambapo sasa ni utasa na upungufu.— **The Ministry of Healing, p. 355 . ChS 209.1**

### Kuchagua Bendera ya Kaya

Nilimwona Shetani akiweka bendera yake katika kaya za wale wanaodai kuwa wateule wa Mungu, lakini wale wanaotembea kwenye nuru wanapaswa kutambua tofauti kati ya bendera nyeusi ya adui na kiwango cha Kristo kilicho na damu. **— Shuhuda kwa Kanisa 4:200.**

### Umuhimu wa Madhabahu ya Familia

Ewe unayedai kwamba unampenda Mungu, mbebe Yesu mahali popote uendapo; na kama wazee wa zamani, jenga madhabahu ya Bwana popote utakapopiga, utakapoweka

hema yako. Matengenezo katika heshima hii yanahitajika, matengenezo ambayo yatakuwa ya kina na mapana. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:320, 321.**

Shetani hufanya kila juhudi katika kuwatoa watu kwa Mungu, Hufanikiwa katika kusudi lake pale maisha ya kiroho yanapofunikwa na masumbufu ya maisha haya, pale azamishapo mawazo ya watu katika shughuli za kimaisha hata hawana muda wa kusoma Biblia zao kuomba kwa faragha na kuendelea kutoa sadaka za sifa na shukrani mbele ya madhabahu ya kuteketeza asubuhi na jioni. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:426.**

Hebu ibada ya familia iwe ya kupendeza na ya kuvutia. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:335.**

Wanapaswa kufundishwa kuheshimu saa ya maombi, wanatakiwa kuamka asubuhi kwaajili ya kushiriki ibada (maombi ya asubuhi). **—Shuhuda kwa Kanisa 5:424.**

Watoto wanahitaji dini yenye kuvutia, si ya kuchukiza. Saa ya ibada ya familia inapaswa kufanywa kuwa saa ya furaha zaidi ya siku. Hebu usomaji wa Maandiko uchaguliwe vyema na rahisi; waache watoto washiriki kuimba; na maombi yawe fupi, na zielekee sawasawa**.— The Southern Watchman, Juni 13, 1905 ( The Review and Herald, Machi 18, 1902 ). ChS 210.1**

Katika bodi ya familia na madhabahu ya familia wageni wanakaribishwa. Majira ya maombi huweka hisia Zake kwa wale wanaopokea burudani, na hata ziara moja inaweza kumaanisha kuokoa rochlio kutoka kwa kifo. Kwa kazi hii Bwana hufanya hesabu, akisema: "Mimi nitalipa." **—Shuhuda kwa Kanisa 6:347.**

Watoto wanapaswa kufundishwa kuheshimu na kujali saa ya maombi. Kabla ya kuondoka nyumbani kwa kazi, familia yote inapaswa kuitwa pamoja, na baba, au mama kama babahayupo, anapaswa kusihi kwa bidii kwa Mungu ili awadumishe mchana. Njoo kwa unyenyekevu na moyo uliojaa huruma na hisia za majaribu na hatari mbele yenu na watoto wenu; kwa imani uwafunge juu ya madhabahu, na kusihi kwa ajili ya uangalizi wa

—

Bwana. Malaika wanaohudumu watawalinda watoto ambao wamejitolea kwa Mungu. Ni jukumu la wazazi wa Kikristo, asubuhi na jioni, kwa maombi ya dhati na imani ya kudumu, kutengeneza uzio juu ya watoto wao. Wanapaswa kuwafundisha kwa uvumilivu, kwa fadhili na bila kuchoka kuwafundisha jinsi ya kuishi ili kumpendeza Mungu. **—Shuhuda kwa Kanisa 1:397-398.**

Abrahamu, “rafiki ya Mungu,” alituwekea kielelezo kinachofaa. Yake yalikuwa maisha ya maombi. Popote alipopiga hema lake, karibu nayo kuliwekwa madhabahu yake, akiita watu wote waliokuwa katika kambi yake wapate dhabihu ya asubuhi na ya jioni. Hema lake lilipoondolewa, madhabahu ilibaki. Katika miaka iliyofuata, kulikuwa na wale kati ya Wakanaani wazururaji ambao walipokea maagizo kutoka kwa Abrahamu; na kila mmoja wao alipofika kwenye madhabahu ile, alimjua ni nani aliyekuwepo kabla yake; na alipokwisha kusimamisha hema lake, akatengeneza madhabahu, na hapo akamwabudu Mungu aliye hai.— Patriarchs and Prophets, 128 . ChS 210.4

—

## SURA YA 22

## MAOMBI NA MKUTANO WA KIMISIONARI

### Siri ya Ombi Lenye Mafanikio

Kujengwa kwa ufalme wa Mungu kunacheleweshwa au kusukumwa mbele kulingana na kutokuwa mwaminifu au uadilifu wa mawakala ya kibinadamu. Kazi inazuiwa na kushindwa kwa mwanadamu kushirikiana na Mungu. Watu wanaweza kuomba, "Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike duniani kama huko mbinguni; lakini wakishindwa kutekeleza maombi haya maishani mwao, maombi yao hayatakuwa na matunda. —**Shuhuda kwa Kanisa 6:437, 438.**

Mbingu zote zinawatazama wakaao duniani. Malaika na Mungu wa mbinguni wanawatazama wale wanaodai kuwa Wakristo, na kupima mazoezi yao ya ibada.— **Australasian Signs of the Times, Juni 22, 1903 ( The Review and Herald, Juni 5, 1894 ). ChS 211.2**

### Kuifanya Mikutano Ivutie

Hebu mkutano wa wamisionari ufanywe kuwa ni wa kuwafundisha watu jinsi ya kufanya kazi ya umisionari.— **An Appeal to Our Churches in Behalf of Home Missionary Work, 11 . ChS 211.3**

cliji

Maombi yetu na mikutano ya kijamii inapaswa kuwa misimu ya msaada maalum na kutia moyo. Kila mmoja ana kazi ya kufanya ili kufanya mikusany~~iko~~ hii iwe ya kuvutia na yenye faida iwezekanavyo. Hili linaweza kufanywa vyema zaidi kwa kuwa na uzoefu mpya kila siku katika mambo ya Mungu, na kwa kutosita kusema juu ya upendo Wake katika mikusanyiko ya watu Wake. Ikiwa hamruhusu giza au kutoamini kuingia mioyoni mwenu, halitaonekana wazi katika mikutano yenu.— **The Southern Watchman, Machi 7, 1905 . ChS 211.4**

Mikutano yetu inapaswa kufanywa kuwa ya kuvutia sana. Inapaswa kufunikwa na angahewa lenyewe la mbinguni. Kusiwe

—

na hotuba ndefu, kavu na sala ndefu ya kupangwa kwa ajili tu ya kusogeza muda au ili kujaza muda na vitu vya kufanya. Wote wanapaswa kuwa tayari kutenda sehemu yao kwa kulinda wakati, na wajibu wao unapokamilika, mkutano unapaswa kufungwa. Hivyo shauku/matamanio ya mkutano yatahifadhiwa hadi mwisho. Hii ni sadaka kwa Mungu ibada inayokubalika. Utumishi Wake unapaswa kufanywa kuwa wa kuvutia na usiruhusiwe kupungua hadi kuwa mtindo usio na uhai/mkavu. Ni lazima tuishi kwa ajili ya Kristo dakika kwa dakika, saa kwa saa, na siku kwa siku; ndipo Kristo atakaa ndani yetu, na tunapokutana pamoja, upendo Wake utakuwa mioyoni mwetu, ukibubujika kama chemchemi jangwani, kuwaburudisha wote, na kuwafanya wale walio karibu na kuangamia, kuwa na shauku ya kunywa maji ya uzima.**—Shuhuda kwa Kanisa 5:609.**

Usifikirie kwamba unaweza kuamsha usikivu mwingi wa vijana kwa kwenda kwenye mkutano wa kimisionari na kuhubiri hubiri refu. Panga njia zinazoleta mvuto wa

kuamsha wa moja kwa moja. Wiki hadi wiki vijana wanapaswa kuleta ripoti zao, wakieleza kile ambacho wamejaribu kufanya kwa ajili ya Mwokozi, na mafanikio yao yamekuwaje. Ikiwa mkutano wa kimisionari ungefanywa kuwa kipindi ya kuleta ripoti kama hizo, usingekuwa usio na mguso/mvuto, wenye kuchosha, na usiopendeza. Ungekuwa wa kuvutia, na usingekuwa na ukosefu wa mahudhuria.— **Gospel Workers, 210, 211 . ChS 212.1**

Imani inapomshika Kristo, Ukweli utaleta furaha moyoni, na huduma za dini hazitakuwa zenye kuchosha na zisizovutia. Mikutano yenu ya kijamii, ambayo sasa imefugwa na isiyo na roho, itahuishwa na Roho Mtakatifu; kila siku mtakuwa na wingi wa uzoefu mnapoishi ukristo mnaoutangaza. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:437.**

**Ushuhuda wa Mtu Binafsi**

Kama wafuasi wa Kristo tunapaswa kufanya maneno yetu kuwa msaada na kutiana moyo katika maisha ya Kikristo. Zaidi sana kuliko sisi, tunahitaji kuzungumza juu ya sura zenye thamani za uzoefu wetu.— **Christ's Object Lessons, 338 . ChS 212.3**

Kanisa linahitaji uzoefu mpya, ulio hai wa washiriki ambao wana ushirika wa muda wote na Mungu. Ushuhuda mkavu, uliochakaa, uliovunda na maombi, bila udhihirisho wa Kristo ndani yao, sio msaada kwa watu. Ikiwa kila mtu anayedai kuwa mtoto wa Mungu angejazwa na imani na mwanga na uzima, ni ushahidi wa ajabu jinsi gani ungetolewa kwa wale wanaokuja kusikia Ukweli! Na ni roho ngapi zinaweza kuvutwa kwa Kristo!
**—Shuhuda kwa Kanisa 6:64.**

Kukiri kwetu kwa uaminifu Wake ni wakala mteule wa Mbinguni kwa ajili ya kumdhihirisha Kristo kwa ulimwengu. Yatupasa kukiri neema Yake kama ilivyodhihirishwa kupitia watakatifu wa kale; lakini kile ambacho kitakuwa na matokeo zaidi ni ushuhuda wa uzoefu wetu wenyewe. Sisi ni mashahidi wa Mungu tunapofunua ndani yetu utendaji wa nguvu ambayo ni ya kimungu. Kila mtu ana maisha tofauti na wengine wote, na uzoefu unaotofautiana kimsingi na wao. Mungu anatamani

—

kwamba sifa zetu zipae Kwake, zikiwa zinatambulika kwa sifa ya mtu binafsi. Utambuzi huu wa thamani kwa sifa ya utukufu wa neema Yake, yanapoungwa mkono na maisha kama ya Kristo, yana nguvu isiyozuilika, inayofanya kazi kwa ajili ya wokovu wa roho.— **The Ministry of Healing, p. 100** **ChS 213.1**

**Kusifu na Kushukuru**

Kumsifu Mungu kwa utimilifu na unyofu wa moyo ni wajibu sawa na maombi. Tunapaswa kuonyesha kwa ulimwengu na kwa mawakala wote wa mbinguni kwamba tunathamini upendo wa ajabu wa Mungu kwa wanadamu walioanguka, na kwamba tunatazamia baraka kubwa zaidi na tena kubwa zaidi kutoka kwa utimilifu Wake usio na kikomo. Baada ya umwagwaji pekee wa Roho Mtakatifu, furaha yetu katika Bwana na

ufanisi wetu katika utumishi Wake ungeongezeka sana kwa kusimulia wema Wake na kazi Zake za ajabu kwa niaba ya watoto Wake. Mazoezi haya yanarudisha nyuma nguvu za Shetani. Yanaondoa roho ya manung'uniko na malalamiko, na mjaribu hupoteza

msingi. Hupalilia sifa hizo za tabia ambazo zitawafaa wakaaji duniani kwa ajili ya makao ya mbinguni. Ushuhuda kama huo utakuwa na ushawishi kwa wengine. Hakuna njia zenye matokeo zaidi zinazoweza kutumika ili kuleta nafsi kwa Kristo.—**Christ's Object Lessons, 299, 300 . ChS 213.2**

Bwana anatamani sisi tutaje wema Wake na kueleza juu ya nguvu Zake. Anaheshimiwa kwa usemi wa sifa na shukrani. Anasema, "Atoaye dhabihu za kushukuru, Ndiye anayenitukuza." Watu wa Israeli, walipokuwa wakisafiri nyikani, walimsifu Mungu kwa nyimbo takatifu. Amri na ahadi za Bwana ziliwekwa kwa muziki, na wakati wote wa safari hizi ziliimbwa na wasafiri walioelekea nchi ya kigeni. Na katika Kanaani, walipokutana kwenye karamu zao takatifu, kazi za ajabu za Mungu zilipaswa kusimuliwa, na shukrani za kupendeza zilitolewa kwa jina Lake. Mungu alitaka maisha yote ya watu Wake yawe ya sifa.—**Christ's Object Lessons, 298, 299 . ChS 213.3**

## Sera ya Hatari

Wengine, wakiogopa kuwa watapoteza hazina ya kidunia, wanapuuza maombi na kujikusanya kwa pamoja kwa ajili ya kumwabudu Mungu, ili wapate muda zaidi wa kujitolea kwenye mashamba yao au biashara zao. Wanaonyesha kwa matendo yao kuwa ni katika ulimwengu gani wameweka matarajio ya juu zaidi. Wanatoa kafara ya fursa kidini, ambayo ni muhimu kwa maendeleo yao ya kiroho, kwa mambo ya maisha haya na kushindwa kupata ujuzi wa mapenzi ya Mungu. Wanakosa kukamilisha tabia ya Kikristo na hawakifiki kipimo cha Mungu. Wanafanya masilahi yao ya muda ya kidunia kuwa ya kwanza, na kumwibia Mungu wakati ambao wangepaswa kutumia kwa huduma Yake. Watu kama hao Mungu huwaweka alama, na watapokea laana badala ya baraka.
**—Shuhuda kwa Kanisa 2:654.**

## Ahadi Inayofariji

Mungu atawakumbuka wale waliokutana pamoja na kulifikiria

—

Jina Lake, na atawaepusha na moto mkubwa. Watakuwa kama vito vya thamani machoni Pake. — **Shuhuda kwa Kanisa 4:107.**

## SURA YA 23 — SEHEMU MBALIMBALI ZA KAZI YA UMISIONARI

### Kuwatazama Vipofu

Malaika wanatumwa kuwahudumia watoto wa Mungu walio vipofu kimwili. Malaika wanalinda hatua zao na kuwaokoa kutoka katika hatari elfu, ambazo, pasipo wao kujua, zinawazingira njiani. **—Shuhuda kwa Kanisa 3:516.**

Hatasikiliza sala ya watu Wake na ili hali yatima, wasio na baba, viwete, vipofu, na wagonjwa wanapuuzwa miongoni mwao. **—Shuhuda kwa Kanisa 3:518.**

Kama wapo katika kanisa wale ambao wangelisababisha vipofu kujikwaa, wanapaswa kuhukumiwa kwa haki; kwa kuwa Mungu ametufanya sisi kuwa walezi wa vipofu, wanaoteseka, wajane, na wasio na baba. Jiwe la kujikwaa linalotajwa katika Neno la Mungu halimaanishi kisiki kinachowekwa mbele ya miguu ya kipofu ili kumsababisha apate kujikwaa, bali lina maana kubwa zaidi ya hiyo. Linamaanisha jambo lolole linaloweza kufanywa na kuumiza mvuto wa ndugu yao aliye kipofu, kutenda kinyume na maslahi yake, au kukwamisha ustawi wake. **—Shuhuda kwa Kanisa 3:519.**

Kipofu ana matatizo ya kushindwa kufikia kila upande kutokana na kukosa kwake uwezo wa kuona. Moyo huo ambao hauna huruma na haujali unapomwona kipofu akipapasa-papasa njiani katika ulimwengu na kumweka gizani, ni mgumu mno na unapaswa kulainishwa kwa neema ya Mungu. **—Shuhuda kwa Kanisa 3:521.**

### Kuwajali Yatima

Hadi mauti itakapomezwa kwa kushinda, kutakuwa na yatima wanaotakiwa kutunzwa, ambao watateseka kwa njia nyingi zaidi ya moja ikiwa huruma na fadhili zenye upendo za washiriki wa kanisa letu hazitumiki kwa ajili yao. Bwana anatuambia, “kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako.” Ukristo lazima utoe huduma ya baba na mama kwa hawa wasio na

—

makazi. Huruma kwa mjane na yatima inayodhihirishwa katika maombi na matendo, itakumbukwa mbele za Mungu, ili kupewa thawabu wakati ujao.— **The Review and Herald, Juni 27, 1893 . ChS 215.5**

Unaposaidia maskini, unahurumia walio taabika na wanaodhulumiwa, na kuwa rafiki wa yatima, unakuwa umejisogeza karibu katika uhusiano na Yesu. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:25.**
Wapo yatima wanaoweza kutunzwa; lakini wengi hawatathubutu kufanya kazi hiyo; kwa maana inahusisha kutenda zaidi kuliko wanavyoweza kufanya, kwa kuwaacha lakini muda mfupi wa kujifurahisha wenyewe. Lakini Mfalme atakapofanya uchunguzi, watu hawa wasiofanya lolote, wasio na uhuru, na wenye ubinafsi ndipo watajifunza kwamba mbinguni ni kwa ajili ya wale ambao wamekuwa watenda kazi, wale ambao wamejikana wenyewe kwa ajili ya Kristo. Hakuna maandalizi ambayo yamefanywa kwa ajili ya wale ambao wamewahi kuchukua uangalifu huo wa pekee katika kujipenda na kujiangalia wenyewe. Adhabu ya kutisha ambayo Mfalme aliwatishia wale walio kwenye mkono Wake wa kushoto, katika kesi hii, sio kwa sababu ya uhalifu wao mkubwa.

Hawahukumiwi kwa mambo waliyofanya, bali kwa yale ambayo hawakufanya. Hawakufanya mambo hayo ambayo Mbingu iliwapa kufanya. Walijifurahisha wenyewe, na wanaweza kuchukua sehemu yao pamoja na watu wanaojifurahisha wenyewe.— **The Review and Herald, Agosti 16, 1881 . ChS 216.2**

Kuna yatima ambao Kristo amewaagiza wafuasi Wake wapokee kama amana kutoka kwa Mungu. Mara nyingi sana haya hupitwa kwa kupuuzwa. Wanaweza kuwa chakavu, wasiojulikana, na wanaonekana katika kila njia zisizovutia; hata hivyo ni mali ya Mungu. Wamenunuliwa kwa bei, na ni wa thamani machoni Pake kama sisi. Wao ni washiriki wa nyumba kuu ya Mungu, na Wakristo kama wasimamizi/mawakili Wake wanawajibika kwa ajili yao. "Roho zao," Anasema, "nitawataka mkononi mwako."— **Christ's Object Lessons, 386, 387 . ChS 216.3**

Bwana anamwita kila mshiriki wa kanisa ufanya wajibu wako kwa yatima hawa. Hata hivyo, msiwafanyie kazi kwasababu tu ya wajibu, bali kwa sababu mnawapenda, na Kristo alikufa ili kuwaokoa. Kristo amenunua roho hizi zinazohitaji utunzaji wako, na Yeye anatarajia uzipende kama vile Yeye ambavyo amekupenda wewe katika dhambi na upotovu wako.— **The Review and Herald, Juni 27, 1893 . ChS 216.4**

Hatasikiliza maombi ya watu Wake na ili hali yatima, wasio na baba, viwete, vipofu, na wagonjwa wanapuuzwa miongoni mwao. **—Shuhuda kwa Kanisa 3:518.**

Kuna uwanja mpana mbele ya wote watakaomtumikia Bwana katika kuwatunza watoto na vijana hawa wasio na marafiki, wakiwaweka katika nafasi nzuri kwa ajili ya malezi ya tabia iliyo sawa, ili wapate kuwa watoto wa Mungu. Kuna watoto ambao hawajaahidiwa wanaohitaji kuangaliwa; wengi ambao pengine wangekua katika ujinga, na kujiingiza katika vyama vinavyoongoza kwenye maovu na uhalifu, wanaweza kuletwa katika mazingira mazuri, na chini ya uangalizi wa Kristo wapate kuokolewa kwa Kristo. Kazi

—

hii kwa wengine itahitaji juhudi na kujikana nafsi na dhabihu; lakini ni dhabihu gani ndogo tunayoweza kufanya, kwa kulinganisha na zawadi kuu ya Mungu ya Mwana wake wa pekee? Mungu ametupa upendeleo wa kuwa watenda kazi pamoja Naye.— **The Review and Herald, Juni 27, 1893 . ChS 217.2**

**Jamii ya Watu Weusi**

Kuna uwanja mzuri sana katika nchi hii, eneo kubwa ambalo halijafanyiwa kazi. Jamii ya watu weusi, wanaofikia idadi ya maelfu kwa maelfu, inavutia wema na huruma ya kila muumini wa Kristo aliye wa kweli na wa vitendo. Watu hawa hawaishi katika nchi ya kigeni, wala hawazisujudii sanamu za miti na mawe. Wanaishi miongoni mwetu, na tena na tena, kupitia shuhuda za Roho Wake, Mungu ametoa wito wa usikivu wetu kwao, akituambia kwamba hapa kuna wanadamu waliopuuzwa. Uwanja huu mpana upo mbele yetu bila kufanyiwa kazi, ukitaka nuru ambayo Mungu ametupa kwa dhamana. — **Shuhuda kwa Kanisa 8:205.**

Kuta za utengano zimejengwa kati ya wazungu na weusi. Kuta hizi za ubaguzi zitabomoka zenyewe, kama zilivyofanya kuta za Yeriko, wakati Wakristo watakapolitii Neno la Mungu, ambalo linawaamuru upendo wa hali ya juu kwa Muumba wao na upendo usio na upendeleo kwa jirani zao.... Hebu kila kanisa ambalo washiriki wake wanadai kuamini ukweli kwa wakati huu, litazame jamii hii iliyopuuzwa, iliyokandamizwa, ambayo kwa sababu ya utumwa imenyimwa nafasi ya kufikiri na kutenda wenyewe.— **The Review and Herald, Desemba 17, 1895 . ChS 217.4**

Tujiweke kufanya kazi kwa ajili ya watu wa Kusini. Tusiridhike kwa kutazama tu, kwa kufanya tu maazimio ambayo kamwe hayatekelezwi; lakini na tufanye jambo fulani kwa moyo wote kwa Bwana, ili kupunguza dhiki ya ndugu zetu weusi.— **The Review and Herald, Februari 4, 1896 . ChS 218.1**

Jina la mtu mweusi limeandikwa katika kitabu cha uzima kando ya mzungu. Wote ni wamoja katika Kristo. Kuzaliwa, kituo, utaifa, au rangi haiwezi kuwainua au kuwashusha watu. Tabia humtengeneza mtu. Ikiwa mtu mwekundu, Mchina, au Mwafrika anatoa moyo wake kwa Mungu kwa utii na imani, Yesu anampenda hata zaidi kwa ajili ya rangi yake. Anamwita ndugu yake mpendwa sana.— **The Southern Work, 8** , iliyoandikwa **Machi 20, 1891. ChS 218.2**

Siku inakuja ambapo wclavifiialme na watu wakuu wa dunia wangefurahi kubadilishana mahali na Mwafrika mnyenyekevu zaidi ambaye ameshikilia tumaini la injili.— **The Southern Work, 8 , iliyoandikwa Machi 20, 1891. ChS 218.3**

Mungu hajali tu kidogo roho za jamii ya Waafrika ambazo zinaweza kupatikana ili kumtumikia, kuliko alivyoijali Israeli. Anahitaji zaidi watu Wake kuliko walivyojitoa kwa ajili Yke kazi ya umisionari miongoni mwa watu wa Kusini wa tabaka zote, na hasa jamii ya watu weusi. Je, sisi hatuko chini ya wajibu mkubwa zaidi wa kufanya kazi kwa ajili ya watu weusi kuliko wale ambao

—

wamependelewa zaidi? Ni nani aliyewaweka watu hawa utumwani? Ni nani aliyewaweka katika ujinga?... Ikiwa jamii inashushwa hadhi, ikiwa ni wenye kuchukiza kwa tabia na tabia, ni nani aliyewafanya hivyo? Je, hakuna mengi kutokana na wao kutoka kwa watu weupe? Baada ya kutenda kosa kubwa namna hii, je, jitihada za bidii hazipaswi kufanywa ili kuwainua? Ukweli lazima upelekwe kwao. Wana roho za kuokoa kama sisi pia.— **The Southern Work, 11, 12 , iliyoandikwa Machi 20, 1891. ChS 218.4**

**Matengenezo ya Kiasi**

Kati ya wote wanaodai kuhesabiwa miongoni mwa wanokubali kiasi, Waadventista Wasabato wanapaswa kusimama katika safu za mbele.— **Gospel Workers, 384 . ChS 218.5**

Katika suala la kiasi, chukua msimamo wako bila kuyumbayumba. Iweni imara kama mwamba.— **Gospel Workers, 394 . ChS 219.1**

Tuna kazi ya kufanya kulingana na kanuni za kiasi kando na ile ya kuzungumza hadharani. Ni lazima tuwasilishe kanuni zetu katika vipeperushi na katika karatasi zetu. Ni lazima tutumie kila njia iwezekanayo ya kuwaamsha watu wetu kwenye wajibu wao ili kujihusisha na wale wasiojua ukweli. Mafanikio ambayo tumepata katika kazi ya umisionari yamelingana kikamili na jitihada za kujinyima na za kujidhabihu ambazo tumefanya. Bwana peke yake ndiye anayejua ni kiasi gani tungetimiza ikiwa kama watu tungejinyenyekeza mbele Zake, na kutangaza ukweli wa kiasi kwa njia iliyo wazi na iliyonyooka.— **Gospel Workers, p. 385 . ChS 219.2**

Suala la kuwa na kiasi ni kupokea ukubali ulioamuliwa kutoka kwa watu wa Mungu. Kutokuwa na kiasi ni kujitahidi kupata umahiri; tamaa ilikithiri, na machapisho yanayoshughulikia matengenezo ya afya yanahitajika sana. Maandishi yanayohusiana na jambo hili ni mkono wa msaada wa injili, unaoongoza nafsi kutafuta Biblia kwa ufahamu bora wa ukweli. Ujumbe wa onyo dhidi ya uovu mkuu wa kutokuwa na kiasi unapaswa usikike; na ili hili lifanyike, kila Mtunza Sabato anapaswa kusoma na kutekeleza maagizo yaliyomo katika majarida yetu ya afya na vitabu vyetu vya afya. Nao wanapaswa kufanya zaidi ya hili: wanapaswa kufanya jitihada za bidii za kusambaza machapisho haya miongoni mwa majirani zao.— **The Southern Watchman, Novemba 20, 1902 ( Pacific Union Recorder, Novemba 20, 1902 ). ChS 219.3**

Toa wito kamili wa kua[c]c[lix]ha, ukiwasihi kwamba pesa ambazo wangetumia kwa ajili ya vileo, tumbaku, au anasa, zitolewe kwa ajili ya kusaidia wagonjwa, maskini, au kwa ajili ya kuwafundisha watoto na vijana kwa manufaa ya ulimwengu.— **The Ministry of Healing, 211 . ChS 219.4**

### Umuhimu wa Juhudi za Kufuatilia

Kama matokeo ya uwasilishaji wa Ukweli katika mikutano mikubwa, roho ya utafiti inaamshwa, na ni muhimu hasa

kwamba shauku hizi zifuatiliwe kwa kazi ya binafsi. Wale wanaotamani kuichunguza Kweli wanahitaji kufundishwa kujifunza Neno la Mungu kwa bidii. Mtu lazima awasaidie kujenga juu ya msingi wa uhakika. Katika wakati huu muhimu katika uzoefu wao wa kidini, ni muhimu jinsi gani watendakazi wa Biblia walioelekezwa kwa hekima huja kuwasaidia na kuwafungulia katika uelewa wao hazina za nyumba ya Neno la Mungu. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:111.**

Wasaa wa thamani umepotea. Maoni yaliyotolewa hayakufuatwa. Ingelikuwa bora kama shauku isingeamshwa; kwa kuwa usadikisho ukipingwa mara na kushindwa, ni vigumu sana kuvutia akili tena kwa Kweli. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:118.**

**Uwakili wa Matumizi**

Katika namna zetu zote za matumizi tunapaswa kujitahidi kulitimiza kusudi Lake Yeye aliye Alfa na Omega wa juhudi zote za Mkristo. **— Shuhuda kwa Kanisa 9:49.**

Pesa ina thamani kubwa, kwa sababu inaweza kufanya vizuri sana. Mikononi mwa watoto wa Mungu ni chakula cha wenye njaa, kinywaji cha wenye kiu, na nguo kwa walio uchi. Ni ulinzi kwa walioonewa, na njia ya msaada kwa wagonjwa. Lakini pesa haina ya thamani zaidi kuliko mchanga, isipokuwa pale tu inapotumiwa katika kuandaa mahitaji ya maisha, kuwabariki wengine, na kuendeleza kazi ya Kristo.— **Christ's Object Lessons, p. 351 ChS 220.3**

Mungu Mwenyewe aliianzisha mipango ya kuiendeleza kazi Yake, na amewapa watu Wake mali za ziada, ili atakapoita kwa ajili ya msaada waweze kuitika kwa kusema: "Bwana mali yako imepata mali nyingine." **—Shuhuda kwa Kanisa 9:58.**

Pesa haiwezi kubebwa katika maisha yajayo; haihitajiki hapo; lakini matendo mema yaliyofanywa katika kuleta roho kwa Kristo yanapelekwa kwenye nyua za mbinguni. Lakini wale ambao kwa ubinafsi wanatumia zawadi za Bwana juu yao wenyewe, wakiwaacha viumbe wenzao wenye uhitaji bila msaada, na bila kufanya lolote kuendeleza kazi ya Mungu duniani, wanamvunjia heshima Muumba wao. Kumuibia Mungu kumeandikwa kinyume na majina yao katika vitabu vya mbinguni.— **Christ's Object Lessons, 266 . ChS 220.5**

Je, ni thamani gani ya pesa kwa wakati huu, kwa kulinganisha na thamani ya roho? Kila dola ya uwezo wetu inapaswa kuzingatiwa kama ya Bwana, sio yetu; na kama amana ya

clx

thamani kutoka kwa Mungu kwetu; si kupotezwa kwa ajili ya anasa zisizo na maana, bali kutumika kwa uangalifu katika kazi ya Mungu, katika kazi ya kuwaokoa wanaume na wanawake kutoka katika uharibifu.— **Life Sketches, p . ChS 220.6**

Je, kazi ya umisionari inayopaswa kufanywa katika ulimwengu wetu si ya umuhimu wa kutosha kuamuru ushawishi na usaidizi wetu? Je! hatupaswi kujikana wenyewe na kila ubadhirifu, na kuweka karama zetu katika hazina ya Mungu, ili ukweli upelekwe katika nchi nyingine, na kwamba utume wa nyumbani uweze

—

kudumishwa? Je, kazi hii haitapata kibali cha Mbinguni? Kazi ya siku hizi za mwisho haijaungwa mkono na urithi mkubwa, au kukuzwa na ushawishi wa ulimwengu. Imedumishwa na karama ambazo zilikuwa ni matokeo ya kujinyima, ya roho ya kujitolea. Mungu ametupa upendeleo wa kuwa washiriki pamoja na Kristo katika mateso Yake hapa, na ameandaa kwamba tuwe na cheo cha urithi katika dunia iliyofanywa upya.— The Review and Herald, Desemba 2, 1890 . ChS 221.1

Nilioneshwa kuwa malaika wa kurekodi hufanya rekodi ya uaminifu ya kila toleo lililowekwa wakfu kwa Mungu na kuwekwa kwenye hazina na mwisho wa hazina hizo zilizotolewa. Jicho la Mungu hutambua kila senti iliyotolewa kwa kazi Yake, na utayari au kusita kwa mtoaji. Nia ya kutoa pia huandikwa. Hao wanaojitoa mhanga, wanaojitolea kumrudishia Mungu vitu ambavyo ni Vyake, kama anavyotaka kwao, watalipwa kulingana na matendo yao. Ingawa mali zilizowekwa wakfu zitatumiwa vibaya, na hivyo zisitimize lengo ambalo Mtoaji alikuwa nalo kichwani.    utukufu wa

Mungu na wokovu wa roho-- Wale ambao walitoa dhabihu hiyo kwa uaminifu wa roho, na jicho likiwa limekita kwaajili ya utukufu wa Mungu, hawatapoteza thawabu yao. — **Shuhuda kwa Kanisa 2:518, 519.**

Kila fursa ya kumsaidia ndugu aliye na shida, au kusaidia kazi ya Mungu katika kueneza Ukweli, ni lulu ambayo unaweza kuituma mapema na kuiweka katika benki ya mbinguni kwa utunzaji ulio salama. Mungu anakujaribu na kukuthibitisha. Amekuwa akikupa baraka Zake kwa mkono wa ukarimu na sasa anaangalia kuona ni matumizi gani unayoyatumia, kuona ikiwa utawasaidia wale wanaohitaji msaada na ikiwa utahisi thamani ya roho na ufanye kile unachoweza na mali ambazo amekukabidhi. Kila fursa kama hiyo iliyoboreshwa huongeza hazina yako ya mbinguni. — **Shuhuda kwa Kanisa 3:249, 250.**

**Kumbukumbu za Kimbingu**

Malaika huweka kumbukumbu ya uaminifu wa kazi ya kila mtu, —**Shuhuda kwa Kanisa 1:198.**

Kila tendo la upendo, kila neno la fadhili, kila sala kwa niaba ya wanaoteswa na walioonewa, inawekwa katika kumbukumbu mbele ya kiti cha enzi cha milele na kuwekwa kwenye rekodi ya kutokuharibika ya mbinguni. —**Shuhuda kwa Kanisa 5:13**



**3.**

Mbinguni inatolewa taarifa ya kila jitihada yenye mafanikio kwa upande wetu ya kuondoa giza na kueneza maarifa wa Kristo kotekote. Tendo linaposimuliwa mbele za Baba, shangwe husisimka kwa jeshi lote la mbinguni.— **The Acts of the Apostles, p. 154 . ChS 222.3**

Malaika wametumwa kuwa wasaidizi wetu. Wanapita katikati ya dunia na mbingu, wakiwa wamebeba juu taarifa ya matendo ya wanadamu.— **The Southern Watchman, Aprili 2, 1903 . ChS 222.4**

Ilikuwa vyema ... kukumbuka rekodi iliyowekwa juu, -kitabu

kile ambacho hakina makosa, hakina makosa, na ambayo kutoka kwayo watahukumiwa. Hapo kila nafasi iliyopuuzwa ya kufanya huduma kwa Mungu imeandikwa; na huko pia, kila tendo la imani na upendo hukumbukwa milele.— Prophets and Kings, 639 . ChS 222.5

## Chapter 24— SIFA ZA HUDUMA YA KIKRSTO YENYE MAFANIKIO

### Ufanisi

Kutokuwa na majukumu na uzembe sio ucha Mungu. Tunapotambua kwamba tunamfanyia Mungu kazi tutakuwa na shauku ya juu sana kuliko tuliyowahi kuwa nayo hapo awali ya utakatifu wa huduma ya kiroho. Utambuzi huu utaweka maisha na umakini na nguvu ya kudumu katika utekelezaji wa kila wajibu. **—Shuhuda kwa**

**Kanisa 9:150.**

Muda unadai ufanisi mkubwa na kujiweka wakfu wa kina.Aah!, nimejaa jambo hili hata ninamlilia Mungu: “Simamisha, na uwatume haraka wajumbe waliojazwa kwa ufahamu wa wajibu wao, wajumbe ambao mioyoni mwao ibada ya sanamu ya nafsi, ambayo ndio msingi wa dhambi zote, imesulubishwa. —Shuhuda kwa Kanisa 9:27.

Kazi iliyowekwa kwa wanafunzi ingehitaji ufanisi mkubwa; kwa maana wimbi la uovu lilikuwa kubwa na lenye nguvu dhidi yao.— **The Acts of the Apostles, 31 . ChS 223.3**

**Usemi Ufaao**

Utamaduni ufaao na utumiaji wa nguvu za usemi unahusiana na kila mstari wa kazi ya Kikristo. Tunapaswa kujizoeza kusema kwa sauti za kupendeza, kutumia lugha safi na sahihi, na maneno yenye fadhili na adabu.— **Christ’s Object Lessons, 336 . ChS 223.4**

Kila mhudumu na kila mwalimu anapaswa kukumbuka kwamba anawapa watu ujumbe unaohusisha maslahi ya milele. Kweli iliyosemwa itawahukumu katika siku kuu ya hesabu ya mwisho. Na kwa baadhi ya roho namna ya mwenye kufikisha ujumbe itaamua kuupokea au kuukataa. Kisha neno lisemwe hivyo kwamba litavutia ufahamu na kuuvutia moyo. Linapaswa kusemwa polepole, kwa uwazi, na kwa taadhima, lakini kwa bidii yote ambayo umuhimu wake unadai.— **Christ's Object Lessons, p . ChS 223.5**

Unapotafuta kuwavuta wengine[clxii] ndani ya mduara wa upendo Wake, hebu usafi wa lugha yako, kutokuwa na ubinafsi wa huduma yako, furaha ya mwenendo wako, vishuhudie nguvu ya neema Yake.— **The Ministry of Healing, p 156 . ChS 224.1**

Kila Mkristo ameitwa kuwajulisha wengine utajiri wa Kristo usiochunguzika; kwa hivyo atafute ukamilifu katika usemi. Anapaswa kuwasilisha neno la Mungu kwa njia ambayo itawasadikisha wasikilizaji. Mungu hajapanga kwamba mikondo

—

Yake ya kibinadamu chakavu. Si mapenzi Yake kwamba mwanadamu adharau au kudhalilisha mkondo wa mbinguni unaotiririka kupitia kwake hadi ulimwenguni.— **Christ's Object Lessons, p 336. ChS 224.2**

Wataelimishwa katika subira, fadhili, ukarimu, na msaada. Watajizoeza adabu ya kweli ya Kikristo, wakikumbuka kwamba Kristo, mtendakazi mwenza wao, hawezi kukubali maneno au hisia zenye ukali, zisizo za fadhili. Maneno yao yatatakaswa. Nguvu ya usemi itachukuliwa kuwa talanta yenye thamani, ambayo itawawezesha kufanya kazi ya juu na takatifu.— **Gospel Workers, p 97 . ChS 224.3**

**Ukuaji wa Kiakili**

Ukuaji wa kiakili ndicho kile tunachohitaji sisi kama wanadamu, na ndicho tunachohitaji ili kukidhi matakwa ya wakati huu. — **Shuhuda kwa Kanisa 4:414.**

Hatupaswi kuingia katika kazi ya Bwana hovyo ovyo na kutarajia mafanikio. Bwana anahitaji watu wenye akili, watu wanafikiri. Yesu anatoa wito kwa watendakazi pamoja

Naye, sio wafanya makosa. Mungu anataka watu wenye fikra sahihi na wenye akili kufanya kazi kubwa inayohitajika kwa wokovu wa roho. **—Shuhuda kwa Kanisa 4:67.**

Baadhi wanahitaji kufunza akili kwa kuifanyia mazoezi. Wailazimishe akili kufikiri. Wakati wanapomtegemea mtu fulani kufikiri kwa ajili yao, kutatua magumu yao, wakikataa kuishugulisha akili kwa tafakari, kutokuwa na uwezo wa kukumbuka, basi kuangalia mbele udunia ndani ya kanisa na kutofautisha kutaendelea. Juhudi lazima ifanywe na kila mmoja kuelimsha akili. **—Shuhuda kwa Kanisa 2:188.**

Mungu hataki tutosheke na akili za kivivu, zisizo na nidhamu, mawazo yasiyofaa, na kumbukumbu zisizofaa.— **The Counsels to Parents, Teachers, and Students, 506 . ChS 224.7**

Watu wa Mungu lazima wawe na bidii katika kusoma, wawe na bidii katika kupata maarifa, bila kupoteza hata saa moja. Kupitia juhudi ya kudumu wanaweza kupanda hadi kufikia kiwango chochote kile cha ukuu kama Wakristo, kama watu wenye mamlaka na ushawishi. **—Shuhuda kwa Kanisa 4:411.**

Acha tu nyakati hizo zitunzwe.... Muda uliotumika katika kusafiri; ... nyakati za kungoja chakula, kungoja wale ambao wamechelewa kuweka miadi, - ikiwa kitabu kingewekwa karibu, na vipande hivi vya wakati viliboreshwa katika kusoma, kusoma, au kufikiria kwa uangalifu, ni nini kisichoweza kuwa. yametimizwa!— **Christ's Object Lessons, p. 343, 344 . ChS 225.2**



Kusudi thabiti, tasnia yenye kuendelea, na uchumi makini wa wakati, utawezesha watu kupata maarifa na nidhamu ya kiakili ambayo itawastahilisha kwa karibu nafasi yoyote ya ushawishi na manufaa.— **Christ's Object Lessons, p. 334 . ChS 225.3**

Wanaume katika nafasi za uwajibikaji wanapaswa kuboreka kila wakati. Haipaswi kutia nanga juu ya uzoefu wa zamani na kuhisi kuwa sio lazima kuwa wafanyikazi wa kisayansi. Mwanadamu,

ingawa ni mnyama dhaifu zaidi kati ya viumbe vya Mungu wakati anakuja ulimwenguni, na mpotovu zaidi katika asili yake, hata hivyo ana uwezo wa kuendelea kila wakati. Anaweza kuangaziwa na sayansi, kupongezwa na fadhila, na anaweza kuendelea katika hadhi ya kiakili na kimaadili, hadi kufikia ukamilifu wa akili na usafi wa tabia lakini chini kidogo kuliko ukamilifu na usafi wa malaika. **—Shuhuda kwa Kanisa 4:93.**

Wale ambao wangekuwa watenda kazi pamoja na Mungu lazima wajitahidi kwa ukamilifu wa kila kiungo cha mwili na ubora wa akili. Elimu ya kweli ni maandalizi ya nguvu za kimwili, kiakili na kimaadili kwa ajili ya kutekeleza kila wajibu; ni mafunzo ya mwili, akili, na roho kwa ajili ya huduma ya kiungu. Hii ndiyo elimu itakayodumu hadi uzima wa milele.— **Christ's Object Lessons, p. 330 . ChS 225.5**

Mafundi mitambo/makanika, wanasheria, wachuuzi, watu wa biashara na madai yote, hujielimisha ili waweze kuwa magwiji/wataalamu katika biashara zao. Je! Wafuasi wa Kristo wanapaswa kuwa na akili ndogo, na wakati wanadai kuwa wanahusika katika

huduma Yake wasijue njia na nyenzo za kutumia? Shuguli/biashara ya kupata uzima wa milele iko juu ya kila jambo la kidunia. Ili kuongoza roho kwa Yesu lazima kuwe na maarifa ya asili ya mwanadamu na utafiti wa akili ya mwanadamu. Tafakari ya kina na maombi makini yanahitajika kujua jinsi ya kuwafikia wanaume na wanawake juu ya mada kuu ya Ukweli. **—Shuhuda kwa Kanisa 4:67.**

**Heshima ya Kikristo na Upole**

Ukosefu wa hadhi ya Kweli na usafishwaji wa Kikristo katika safu za watunza-Sabato ni dhidi yetu kama watu na hufanya Ukweli ambao tunadai kuwa nao uonekane mbaya. Kazi ya kuelimisha akili na adabu inaweza kuendelezwa kwa ukamilifu. Ikiwa wale wanaodai Ukweli hawataboresha sasa upendeleo na nafasi zao za kukua hadi kufikia kimo kamili cha wanaume na wanawake katika Kristo Yesu, hawatakuwa na heshima kwa sababu ya Ukweli, hapatakuwa na heshima kwa Kristo. **—Shuhuda kwa Kanisa 4:358, 359.**

Hakikisha unadumisha heshima ya kazi kwa maisha yenye mpangilio mzuri na mazungumzo ya kimungu. Usiogope kamwe kuinua kiwango cha juu sana Ukorofi na ukali wote lazima uondolewe kwetu. Heshima, uboreshaji, adabu ya Kikristo, lazima zipendwe. Jilinde dhidi ya kuwa wa harara na kukosa utambuzi. Usizikubali sifa kama hizo kuwa fadhila; maana Mungu hawafikirii hivyo. Jitahidi kuacha hassira kwa chochote kisivyo cha lazima.— **The Review and Herald, Novemba 25, 1890 . ChS 226.2**

Kuna ulazima mkubwa zaidi kwamba wanaume na wanawake walio na ujuzi wa mapenzi ya Mungu wajifunze kuwa wafanyakazi wenye mafanikio katika kazi Yake. Wanapaswa kuwa watu wenye kipaji, wenye ufahamu, wasio na mng'aro wa nje wa udanganyifu na uvutano mzito wa walimwengu, bali ule usafishaji na uungwana wa Kweli ambao una harufu ya mbinguni, na ambao kila Mkristo

—

atakuwa nao ikiwa ni mshiriki wa asili ya Uungu. **—Shuhuda kwa Kanisa 4:358.**

Tuna ukweli mkuu na matumaini ambayo yaliwahi kutolewa kwa ulimwengu wetu, na imani kuu zaidi; na tunataka kuwakilisha hili katika tabia yake iliyotukuka kwa ulimwengu. Hatutaki kuchukulia mtazamo huo kana kwamba tunapita katika ulimwengu tukiomba msamaha wa ulimwengu kwa sababu tunathubutu kuamini ukweli huu wa thamani na mtakatifu; bali tunataka kutembea kwa unyenyekevu pamoja na Mungu, na kujiendesha kana kwamba sisi tu watoto wa Mungu Aliye juu, na, ingawa ni vyombo dhaifu, kana kwamba tunashughulikia masomo ya maana sana na ya kuvutia, ya juu zaidi na yaliyotukuka zaidi kuliko mandhari yoyote ya kidunia. .— **The Review and Herald, Julai 26, 1887 . ChS 226.4**

Mtenda kazi wa roho anahitaji kujitolea, uadilifu, akili, tasnia, nguvu, na busara. Kuwa na sifa hizi, hakuna mtu anayeweza kuwa duni; badala yake atakuwa na ushawishi wenye kuamuru kwa wema.— **Gospel Workers, 111 . ChS 227.1**

Watu walio tayari kufundishwa namna njema ya kuwafikia watu na familia wanapaswa kuwa kazini. Mavazi yao yapaswa kuwa nadhifu, lakini si ya fasheni za fahari zinazonasa macho ya watu, na tabia zao zisiwe zenye kukera watu. Kuna hitaji kubwa la adabu ya Kweli miongoni mwetu sisi wanadamu. Hili linapaswa kukuzwa na wote ambao wataifanya kazi ya kimisionari. —**Shuhuda kwa Kanisa 4:391, 392.**

**Ukweli**

Hakupaswi kuwa na maisha ya kuigiza (feki) kwa wale wenye ujumbe wa thamani na mtakatifu walioitiwa kuubeba. Ulimwengu unawaangalia Waadventista Wasabato kwa sababu unajua kitu kuhusu ushuhuda wao wa imani na ubora wao wa hali ya juu, na unapowaona wale ambao hawaishi kulingana na ushuhuda/Kukiri kwao, huwatazama kwa kuwadharau. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:23.**

Watu wanaweza kuwa na vipawa bora, uwezo mzuri, sifa nzuri; lakini kasoro moja, dhambi moja ya siri iliyoendekezwa, itathibitisha kwa mhusika kile ambacho mbao/ubao ulioliwa na mchwa/minyoo hufanya kwa meli - maafa mabaya na uharibifu!
**—Shuhuda kwa Kanisa 4:90.**

Paulo aliikuwa pamoja na angahewa la mbinguni. Wote walioshirikiana naye walihisi ushawishi wa muungano wake na Kristo. Uhakika wa kwamba maisha yake mwenyewe yalionyesha kweli aliyotangaza, ulitoa nguvu yenye kusadikisha kwa mahubiri yake. Hapa ndipo penye nguvu ya [clxv] ukweli. Ushawishi ambao haujasomwa, usio na fahamu wa maisha matakatifu ni mahubiri yenye kusadikisha zaidi yanay~~ow~~eza kutolewa kwa ajili ya Ukristo. Mabishano, hata yasipojibika, yanaweza kuibua upinzani tu; lakini kielelezo cha kimungu kina nguvu ambayo haiwezekani kupinga kabisa.— **Gospel Workers, 59 . ChS 227.5**

Tabia ya kweli haijaundwa kutoka nje, na kuvaa; hutoka ndani. Ikiwa tunataka kuwaelekeza wengine katika njia ya haki, kanuni za uadilifu lazima ziwekwe ndani ya mioyo yetu wenyewe.

Ukubali wetu wa imani unaweza kutangaza nadharia ya dini, lakini ni uchamungu wetu wa vitendo ambao unashikilia neno la ukweli. Uhai wenye uthabiti, mazungumzo matakatifu, uadilifu usioyumba, roho tendaji, ya ukarimu, kielelezo cha kimungu,—hizi ndizo njia ambazo kupitia hizo nuru hupitishwa kwa ulimwengu.— **The Desire of Ages, 307 . ChS 228.1**

Maombi, maonyo, na maneno ya mdomoni ni matunda ya bei ndogo sana (bei che!), ambayo mara nyingi huambatanishwa na kazi; lakini matunda ambayo hudhihirishwa kwa kutenda matendo mema, katika kuwajali wahitaji, yatima, na wajane, ni matunda yaliyo ya kweli/dhati, na kwa kawaida huota kwenye mti mzuri. —Shuhuda kwa Kanisa 2:24.

**Ujasiri**

Mungu kwa ujumla hafanyi miujiza ili kuendeleza ukweli Wake. Ikiwa mkulima atapuuza kulima udongo, Mungu hafanyi muujiza wowote ili kupinga matokeo ya

hakika. Anafanya kazi kulingana na kanuni kuu zilizojulishwa kwetu, na ni sehemu yetu kukomaa mipango ya hekima, na kuweka katika utendaji njia ambayo Mungu ataleta matokeo fulani. Wale ambao hawafanyi juhudi yoyote iliyoamuliwa, lakini wanangojea tu Roho Mtakatifu awashurutishe kutenda, wataangamia gizani. Hupaswi kukaa kimya na kutofanya lolote katika kazi ya Mungu.— **The Southern Watchman, Desemba 1, 1903 ( The Review and Herald, RH Septemba 28, 1897 ). ChS 228.3**

Baadhi ya wanaoshiriki katika utumishi wa kimisionari ni dhaifu, hawana ujasiri, hawana roho, wamevunjika moyo kwa urahisi. Wanakosa msukumo. Hawana sifa hizo chanya za tabia zinazowapa uwezo wa kufanya jambo fulani,—roho na nguvu zinazowasha shauku. Wale ambao wangeshinda mafanikio lazima wawe na ujasiri na matumaini. Wanapaswa kusitawisha si tu sifa za kupita kiasi bali pia wema wenye kutenda.— **Gospel Workers, p. 290 . ChS 228.4**

Bwana anahitaji Watenda kazi ambao watasukuma ushindi wa msalaba wa Kristo.— **The Review and Herald, Mei 6, 1890 . ChS 228.5**

Sio kwa maneno baridi, yasiyovutia ujumbe huu unapaswa kutolewa, bali ni kwa maneno dhahiri, thabiti, yenye kusisimua. **—Shuhuda kwa Kanisa 8:16.**

Wanenaji wenye maneno fasaha na ya kuvutia hawahitajiki kutoa ujumbe huu. Ukweli katika ukali Wake wote lazima usemwe. Watu wa vitendo wanahitajika - watu ambao watafanya kazi kwa bidii, nguvu isiyokoma kwa ajili ya utakaso wa kanisa na onyo la ulimwengu. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:187.**

Mungu hawatumii wavivu katika kazi yake; anataka wafanyakazi wenye fikra, wema,wenye upendo na bidii. **—Shuhuda kwa Kanisa 4:411.**

**Dhamira**

Wale walio katika huduma ya Mungu lazima waonyeshe uhuishaji

hai na dhamira katika kazi ya kuleta roho. Kumbuka kwamba kuna wale ambao wataangamia isipokuwa sisi kama vyombo vya Mungu tufanye kazi kwa dhamira ambayo haitashindwa wala kukata tamaa. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:418.**

Ametupa kazi kubwa ya kufanya. Hebu tuifanye kwa usahihi na kwa kudhamiria. Hebu tuonyeshe katika maisha yetu kile ambacho Kweli imetufanyia. **—Shuhuda kwa Kanisa 6:418.**

## Bidii

Ni ari ya Kikristo yenye bidi indio inayohitajika, ari itakayoonyeshwa kwa kufanya kitu. Wote ni lazima sasa wafanye kazi nafsini mwao wenyewe, na watakapokuwa na Yesu miyoni mwao, watamdhihirisha kwa wengine. Ni hakika kuwa nafsi iliyompokea Yesu haiwezi ikanyamazishwa isitangaze habari za Yesu kwa watu wengine. Hii ni sawa na kutokuweza kuzuia maporomoko ya maji ya mto Niagara yanapotiririka. **—Shuhuda**

**kwa Kanisa 2:233.**

Kila mtu anayemkubali Kristo kuwa Mwokozi wake binafsi atatamani upendeleo wa kumtumikia Mungu. Akitafakari kile mbingu imemfanyia, moyo wake unasukumwa na upendo usio na kikomo na shukrani ya kuabudu. Ana hamu ya kuonyesha shukrani kwa kutumia uwezo wake katika utumishi wa Mungu. Anatamani sana kuonyesha upendo wake kwa Kristo na mali yake aliyoinunua. Anatamani kazi ngumu, taabu, dhabihu.— **The Ministry of Healing, 502 . ChS 229.7**

Kuna uwanja mpana kwa akina Martha, pamoja na bidii yao katika kazi ya kidini yenye bidii. Lakini hebu wakae kwanza pamoja na Mariamu miguuni pa Yesu. Hebu bidii, upesi, na nguvu zitakaswe kwa neema ya Kristo; basi maisha yatakuwa nguvu isiyoweza kushindwa kwa wema.— **The Desire of Ages, p. 525 . ChS 230.1**

Kwa Jina la Bwana, na uvumilivu usiochoka na bidii isiyokoma ambayo Kristo alileta ndani ya watumishi wake, tunapaswa kuipeleka mbele kazi ya Bwana. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:25.**

Tunahitaji kuvunja mazoea ya kazi yetu ya kidini. Tunafanya kazi ulimwenguni, lakini hatuonyeshi shughuli na bidii ya kutosha. Ikiwa tungekuwa na bidii zaidi, watu wangesadikishwa juu ya Ukweli wa ujumbe wetu. Kukosa ushawishi na mazoea ya huduma yetu kwa Mungculxvhiiufukuza roho nyingi za tabaka la juu, zinazohitaji kuona bidii ya kina, ya dhati, iliyotakaswa. —Shuhuda kwa Kanisa 6:417.

## Subira

Lakini kuwa mfanyakazi mwenza na Yesu, unapaswa kuwa na uvumilivu wote kwa wale ambao unawafanyia kazi, sio kudharau urahisi wa kazi, bali ukiangalia matokeo yaliyobarikiwa. Wakati wale ambao unawafanyia kazi hawakidhi akili yako, mara nyingi husema moyoni mwako: “Waache waende; hawastahili kuokoa.” Je! Vipi kama Kristo angewatendea watu masikini waliotengwa

—

katika namna inayofanana? Alikufa ili kuokoa wenye dhambi duni wasio na furaha, na ikiwa unafanya kazi kwa roho ile ile na kwa njia ile ile iliyooneshwa na mfano wa Yeye ambaye unamfuata, ukiacha matokeo kwa Mungu, huwezi kamwe katika maisha haya kupima kiwango cha mema uliyotimiza. — **Shuhuda kwa Kanisa 4:132.**

Fanya kazi bila kujali, kwa upendo, kwa uvumilivu, kwa wote ambao unakutana nao. Usioneshe kutokuwa na subira. Usiseme neno moja lisilofaa. Hebu Upendo wa Kristo uwe ndani ya mioyo yenu, sheria ya wema midomoni mwenu. **—Shuhuda kwa Kanisa 9:41.**

**Umahiri**

Wale wanaojisalimisha kabisa kwa Mungu wataweka fikira na maombi na busara iliyowekwa wakfu katika kazi zao.— **The Signs of the Times, Mei 29, 1893 . ChS 230.6**

Ikiwa mtu ana busara, ubunifu, kazi, stadi na shauku, atafanikiwa katika biashara ya muda, na sifa zile zile, zilizowekwa wakfu kwa kazi ya Mungu, zitathibitisha kuwa na ufanisi maradufu; kwa kuwa nguvu ya Bwana itajumuishwa na juhudi ya mwanadamu. **—Shuhuda kwa Kanisa 5:276.**

Katika kazi ya kushinda nafsi, busara kubwa na hekima zinahitajika. Mwokozi kamwe hakukandamiza ukweli, lakini Alitamka daima kwa upendo. Katika kujamiiana Kwake na wengine, Alitumia busara kubwa zaidi, na Alikuwa daima mpole na mwenye kufikiria. Hakuwa mkorofi, hakuzungumza neno kali bila sababu, hakutoa maumivu yasiyo ya lazima kwa roho nyeti. Hakushutumu udhaifu wa kibinadamu. Yeye bila woga alishutumu unafiki, kutoamini, na uovu, lakini machozi yalikuwa katika sauti Yake alipokuwa akitamka makemeo Yake makali. Hakufanya ukweli kuwa mkatili, lakini alidhihirisha huruma ya kina kwa wanadamu. Kila nafsi ilikuwa ya thamani machoni pake. Alijibeba kwa hadhi ya kimungu; lakini aliinama kwa huruma nyororo na kujali kwa kila mshiriki wa familia ya Mungu. Aliona ndani ya wote, roho ambao ulikuwa utume Wake kuokoa.— **Gospel Workers, p. 117 . ChS 231.2**

Wengine hukimbia kwa harara zenye msukumo, japo ni roho zenye uaminifu, baada ya wajibu wao kutolewa, zitagharimu wale ambao hawapo nasi kwa njia ya ghafla sana, na kufanya Ukweli, ambao tunapenda waupokee, uwachukize. "Watoto wa ulimwengu huu wana busara katika kizazclixvciiihao kuliko watoto wa nuru." Wafanyabiashara na wanasiasa hujifunza kwa adabu. Ni sera yao kujifanya wavutie iwezekanavyo. Wanasoma kutoa hotuba na tabia zao ili wawe na ushawishi mkubwa juu ya akili za wale wanaowahusu. Wanatumia maarifa na uwezo wao kwa ustadi iwezekanavyo ili kupata kitu hiki. **— Shuhuda kwa Kanisa 4:68.**

Ujumbe huu lazima uweze kutolewa; lakini ingawa ni lazima utolewe, tunapaswa kuwa waangalifu tusiwalazimishe na kuwakusanya watu na kuwahukumu wale ambao hawana nuru

